

**NIDHAMU  
YA KIJAMII  
KATIKA  
UISLAMU**

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا - وَآتُوا الْيَتَامَى أَمْوَالَهُمْ وَلَا تَتَبَدَّلُوا الْخَيْثَرَ بِالْطَيْبِ وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَهُمْ إِلَى أَمْوَالِكُمْ إِنَّهُ كَانَ حُوبًا كَبِيرًا - وَإِنْ خَفْتُمْ أَلَا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَى فَانكِحُوهَا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَتَّشِينَ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ فَإِنْ خَفْتُمْ أَلَا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلِكْتُ أَيْمَانَكُمْ ذَلِكَ أَدْنَى أَلَا تَعُولُوا - وَآتُوهُنَّا النِّسَاءَ صَدَقَاتِهِنَّ نَحْلَةً فَإِنْ طَبِنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِئًا مَرِيئًا - وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَاماً وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا وَاكسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا - وَابْتَلُوا الْيَتَامَى حَتَّى إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ فَإِنْ آتَسْتُمْ مِنْهُمْ رُشْدًا فَادْفِعُوهَا إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَنْ يَكْبِرُوا وَمَنْ كَانَ غَنِيًّا فَلَا يُسْتَعْفِفُ وَمَنْ كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ بِالْمَعْرُوفِ فَإِذَا دَفَعْتُمُ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ فَأَشْهُدُوهَا عَلَيْهِمْ وَكَفَى بِاللَّهِ حَسِيبًا (النِّسَاءُ: 1 - 6)

Aya ya ufunuzi.

Utangulizi katika nidhamu ya kijamii.

Mwanamke na mwanamume.

Athari ya mtazamo wa mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke.

Kupanga mahusiano baina ya mwanamke na mwanamume  
Maisha Khassa.

Ufaradhi wa kuwatenganisha wanaume na wanawake katika  
Maisha ya kiislamu.

Kumtizama mwanamke.

Sio wajibu juu ya mwanamke muislamu kufinika uso wake.

Mwanamke na mwanamume mbele ya majukumu ya kisharia.

Kazi za mwanamke.

Ndoa.

Walioharamishwa katika wanawake.

Wake wengi.

Ndoa za Mtume (saaw).

Maisha ya ndoa.

Kumwaga nje (AZL).

Talaka.

Nasaba (uhusiano.)

La'ana (lia'an).

Usimamizi wa baba (WALI).

Ulezzi wa mtoto (kafala).

Kuunga jamaa (silat ar-rahim).

### Utangulizi

Wengi katika watu hukosa kwa kuita nidhamu zote za maisha (nidamu ya jamii) na tamko hilo ni makosa. Kwa sababu nidhamu ya maisha ni bora kutamkwa (nidhamu za mujtamaa) kwani kihakika ni nidhamu za mijtamaa kwani hupangilia mahusiano ambayo husimama kati ya watu ambao wanaishi katika mujtamaa maalum bila ya kujali mkusanyiko wao au tofauti yao. Na mkusanyiko sio wenyewe kungaliwa bali huangaliwa mahusiano tu na mpaka hapa imekua ni nyangi na tofauti kwa muelekeo kuzidi uhusiano na kutofautiana na imekusanya uchumi na utawala na siasa na elimu, na adhabu ya wahalifu, na maamiliano na ushuhuda na yasiyokua hayo. Kwa hivyo kuita (nidamu ya kijamii) haikulekea, wala haiambatani nayo. Mbali na hayo kwani neno jamii ni sifa ya nidhamu, basi hamna budi nidhamu hii iwe imewekwa kwa ajili ya kutatua matatizo yanayotokeza kutokamana na mjumuiko huu au kwa mahusiano yanatokamana na mjumuiko. Na mjumuiko wa mwanamume kwa mwanamume, na mwanamke kwa mwanamke haihitaji nidhamu kwa sababu haitokamani kwayo matatizo wala haitokamani nayo mahusiano yanayohitajia nidhamu. Bali inahitajia usimamizi wa maslahi baina yao kwa nidhamu, kwa maumbile yao wanaoishi katika nchi moja hata lau kama hawajakusanyika. Ama mjumuiko wa wanaume kwa nidhamu, nayo kwayo hutokamana uhusiano unahitajia usimamizi kwa nidhamu, kwa hivyoitakua ni bora kuitwa mjumuiko huu nidhamu ya kijamii, kwa sababu ndio inayopanga kiuhakika mjumuioko baina mwanamume na mwanamke, na hupangilia mahusiano yanaopatikana na mjumuiko huo.

Kwa hivyo nidhamu ya kijamii imefungika katika nidhamu ambayo hubainisha mpangilio wa mjumuiko wa mwanamke kwa mwanamume na mwanamume kwa mwanamke na inapanga mahusiano ya mwanamke kwa mwananmume na mwanamke kwa mwanamume yanayopatikana na mjumuiko wao, wala sio maslahi ya katika mujtamaa, na hubainisha vitanzu vya mahusiano hayo. Kwa hivyo biashara ya manamke pamoja na mwanamume, na mwanamume pamoja na mwanamke ni katika nidhamu za mujtamaa, wala sio katika nidhamu ya kijamii. Kwa sababu haiingii katika nidhamu ya kiuchumi. Ama kukatazwa (kua) faragha baina mwanamume na mwanamke, au ni wakati upi mwanamke anamiliki talaka yake au ni wakati upi mwanamke atakua ana haki ya kulea mtoto, kwani hayo yote ni katika nidhamu ya kijamii ni: - nidhamu ambayo inapanga mjumuiko wa mwanamke kwa mwanamume, na mwanamume kwa mwanamke na inapangilia uhusiano ambayo yanaotokamana katia yao kwa mijumuiko yao wao, kiila kitanzu cha mahusiano hayo.

Zilichanganyikiwa fahamu za watu na zaidi waislamu kwa nidhamu ya kijamii katika uislamu mchafuko mkubwa, na kuwa mbali na ufahamu kwa uhakika wa kiislamu kwa kua mbali na fikra zake na hukmu zake na wakawa ni wenye kukosa kikamilifu na anaonelea ni katika haki hzo za mwanamke kukaa faragha na mwanamume vile anavotaka na kutoka nje anaonesha uchi wake na kwa mavazi anayotaka yeye. Na kati yao waliokosa klilla aina ya kosa anaona sio katika haki za mwanamke kufanya biashara au kulima wala kujumuka na wanaume kabisa na wanaona kua mwili mzima wa mwanamke ni tupu ikiwemo katika hayo uso wake na vitengele vyake vya mikono. Na ikawa kwa kukosa huku na kuharibika kwa tabia na kuganda katika kufikiria, na kutokamana nayo kuharibika upande wa kijamii na wasiwasi katika familia za kiislamu vya kuzidi kwa kulalamika na kutotosheka juu ya viungo vya jamii na kuzidi mizozano na migongano kati ya watu wake (jamii). Na zikazuka hisia kwa haja ya kuleta jamii pamoja na kudhamini utulivu wake zimejaa katika nafsi/ roho za waislamu wote.

Utafiti ukaanza ili kutatua matatizo hayo ya khatari zikiwashughulisha akili za wengi, na majaribio mengi tofauti tofauti yallidhihiri ya kutibu. Mengi yakaandikwa ambayo yanafafanua tiba ya kijamii, na kuingizwa marekebisho mengi juu ya kanuni za sheria za makoti, na nidhamu za uchaguzi. Na wengi wakajaribu kutabikisha rai zao juu ya watu wao katika wake na madada, na mabanati, na kukaingizwa katika nidhamu za vyuo marekebisho katika upande wa mchanganyiko wa waume na wake. Na hivi ndivyo ilivyodhihiri majaribio hayo kwa mwelekeo huo na mifano hiyo. Na lakini wote hao na huwa hawakufikia kutibu, wala hawakuongokewa na nidhamu, wala hawakupata katika walioyahisi katika kurekebisha kwa namna ye yote ile. Kwa sababu yamefichika kwa waislamu wengi jambo la mahusiano ya jinsi mbili mke na mume. Na wakawa hawajui namna ambayo hushirikiano nayo jinsi mbili hizi, ili ipate ummah kutengea kwa ushirikiano huu, na wakawa wajinga na fikra za uislamu na hukmu zake ambazo zahusiana na mjumuiko mwanamume kwa mwanamke, kiasi ambacho wakawa wanashindana na wanajadiliana katika yanayohusu namana ya kutatua na wakawa mbali katika kuelewa ukweli wake, mpaka ikazidi wasiwasi na balaa katika hali ya majaribio yao, na ikawa katika mijitamaa dhiki na kutishia juu ya ummah wa kiislamu, kwa sifa zake bora za kipekee. Na zikaogopewa kwa majumba ya kiislamu, kupoteza asili ya kiislamu na kwa jamii ya kiislamu kupotewa na maadili ya fikra za kiislamu na kuwambali na kujua uweza wa hukmu zake na rai zake.

Ama sababu ya kuchafuka fikra na kupotoka katika fahamu ya sawa, inaregea kwa vita vikali ambavyo walitupiga nazo hadhara ya kimagharibi na wakatawala fikra zetu na hisia zetu kikamilifu na zikabadilisha fahamu zetu na hisia zetu kikamilifu na zikabadilisha fahamu zetu juu ya uhai na vipimo vyetu kwa vitu ambavyo vilikua zimeshikamana na nafsi zetu mfano ghera yetu juu ya uislamu na kutukuza matukufu yetu. Na ikawa ushindi ni hadhara ya kimagharibi juu yetu iliokusanya nyanja zote za kimaisha na ikiwemo upande huu wa kijamii.

Na hayo yalikua wakati hadhara ya kimagharibi ilipodhihiiri muundo wake wa kimada na thamani yake ya kimada na kupofua macho ya wengi. Na wakaanza kuiga muudno wa kimada na wakajaribu kuchukua hadhara hii kwa sababu vitu vya kimada ni dalili ya maendeleo vimeundwa na watu wa hadhara hii wanoilingania kwake. Na kwa hivyo wakawa wanajaribu kuiga hadhara ya kimagharibi billa ya kupambanua tofauti baina ya hadhara hii ya kimagharibi na baina vitu vya kimadania, na billa ya kujuu kua hadhara inamaanisha mkusanyiko wa fahamu juu ya uhai na ni njia maalum katika maaisha. Na madania ni vitu vya mada vinavyoshikika ambavyo hutumia kwa mbinu na vyombo katika maisha billa ya kuangalia ufahamu wa uhai na njia ya kimagharibi imesimama juu ya msingi ambao unagongana na msingi wa hadhara ya kiislamu, na kua unatofautiana na hadhara ya kiislamu katika mtazamo wa uhai na katika ufahamu wa mafanikio (saada) ambayo mwanaadam hukimbilia ili kufikia. Na hawakubainisha kwa umma muhali wa kuchukua hadhara ya kimagharibi, na kua haiwezekani kuchukua hadhara hii kwa kikundi chochote cha umma wa kiislamu katika biladi yejote na itaendelea kubakia kikundi hiki ni sehemu ya umma wa kiislamu au itaendelea kubakia na sifa ya kikundi cha kiislamu.

Na kwa kutolewa kiini cha tofauti baina ya hadhara ya kiislamu na hadhara ya kimagharibi likawapelekea kuchukua na kuiga. Na ikawa wengi katika waislamu wakajaribu kuhamia hadhara ya kimagharibi bila ya kuufahamu mfano wa kutoa nakala kitabu aliejifunga juu ya kuchora manenop na herufi. Na wakawa baadhi yao kuiga hadhara ya kimagharibi kwa kuchukua ufahamu wakena vipimo vyake bila ya kuzingatia sababu na natija ya fahamu hizi na vipimo hivi. Na wakaona hawa na wale kua katika mujtamaa wa kimagharibi husimama mwanamke pamoja na mwanamume bila tofauti yejote baina yao na bila kujali yatakayo patikana kwa hayo Katika natija. Na wakaona kwa mwanamke wa kimagharibi amedhihirishwa yeje na vitu vya kimadania na pia yeje amedhiohirisha vitu vya kimadania na wakamuiga au wakajaribu kumuiga, bila ya

kudhihirika kua vitu hivi vinaafikiana na hadhara ya kimagharibi na ufahamu wake juu ya uhai, na mtazamo wake, nawala haukulaliani na hadhara ya kiislamu na ufahamu wake juu ya uhai na mtazamo wake. Na bila ya kupiglia mahisabu yoyote kwa yale yatakayopatikana kwa vitu hivi ambavyo vimedhihiri na mambo yaliodhihirishwa nayo. Naam walioyaona hayo na wakafikiri kua hamna budi mwanamke wa kiislamu kusimama karibu na mwanamume katika mujtana katika mikusanyiko bila ya kujali natija zote. Na wakaonelea kua mwanamke wa kiislamu hana budi kudhihirishwa yeze na madania ya kimagharibi bila ya kujali yatakayo patikana kwa kwa katika matatizo na mambo. Na kwa hayo wakalingania kwa kupigania uhuru wa mwanamke wa kiislamu na kumpatia yeze haki kufanya analolipenda. Na pamoja na hayo wakalingania kwa kupigania uhuru wa mwanamke wa kiislamu na kumpatia yeze haki kufanya analolipenda. Na pamoja na hayo wakalingania kuchanganyika bila ya umuhimu wowote, na wakalingania kujipamba (tabarujj) na kudhihirisha uzuri wake (zeena) na wkalingania mwanamke kusimamia utawala na wakaona kwa hayo kua ni maendeleo na ni dalili ya mwamko.

Na kilichofanya udongo kuzidiwa na maji ni kua hawa wenyewe kuihamia na kuiga waliachia nafsi zao uhuru wa binafsi kuichia kikamilifu, kiasi cha kuanana mwanamke kwa mwanamke kuona moja kwa moja bila ya umuhimu wowote na kutumia uhuru wa kibinafsi pekee, bila ya kuwepo sababu ambayo inayolazimisha kuonana huko, na bila ya kuwepo katika mjtamaa haja yeote ya mchanganyiko huo. Na ikawa kuingiliana huko baina ya jinsi hizi mbili kwa kuonana tu na kutumia uhuru wa kibinafsi tu, athari ambayo walitanguliza rai zao hizo mpaka ikafungika makutano yao mwanamume na mwanamke kwa mtazamo wa ume na uke wala sio jengine. Na ikaenea athari mbaya ya kikundi hichi kwa vikundi vingine katika mjtamaa na haikupatikana natija katika maingiliano hayo, yaani ushirikiano baina ya mwanamume na mwanamke katika mabo ya kimaisha, bali yalipatikana kutokamana nayo, kuperomoka kwa tabia, na wanawake kujipamba na

kudhihirisha uzuri wao kwa wasiokua waume wao na maharimu wao. Na yakapatikana kutokamana nayo kupotoka katika kufikiria kwa waislamu na kufisidika kwa utamu, shaka katika imani, na kubomoka katika vipimo. Na wakaifanya upande wa kijamii katika umagharibi ndio kiigizi cha kukimbiliwa, na wakaichukua mujtama wa kimagharibi ndio kipimo, bila ya kuangalia kwa undani kua mujtamaa wa kimagharibi haukatai maingiliano ya ume au uke, na wasione aibu yejote au ubaya au kupingana na njia ambayo ni wajibu kwa kufuata, au uhusiano wowote katika tabia au khatari yejote juu yake. Na bila ya kutambua kua mujtama wa khatari yejote juu yake. Bila ya kutambua kua mujtamaa wa kiislamu unapingana nayo katika mtazamo huu kupingana kimsingi, na unagongana mgongano kamili kwa sababu mujtamaa wa kiislamu huzingatia maingiliano ya ume au uke ni katika madhambi makubwa, na ukaiwekea adhabu kali nayo ni viboko au mawe, na unatabiri kwa anaetenda kwa kutengwa na mtu duni. Na unaona kua ni katika ya wazi kabisa kua hishma ni wajibu kuschungwa, na ni katika mambo ambayo hayakubali mazungumzo wala mijadala na ambayo ni wajibu kufanya bidii kuihifadhi pamoja na mali na nafsi na kua radhi kukimbilia bila ya kukubali udhuru au sababu yejote.

Naam hawakutambua wanaoiga hawo tofauti baina ya mujtamaa hizi mbili vile vile hawakutambua walicholazimishiwa juu yao na maisha ya kiislamu na kile kinacho takiwa kutoka kwa ahkamu sharii na wakaikimbilia kuiga mpaka mwanamke akavaa vazi la uhalali kwa ul;inganizi wa mwamko, na bila ya kujali kwa kujipamba na tabia ya kuchukiza. Na hivi ndivyo walivyoendelea waigaji katika kuvunja upande wa kijamii ya waislamu chini ya bendera ya kumnyanyua mwanamke na kwa hujja ya kuifanyia kazi kunyanyua ummah. Lanini hao walikua ni wachache mwanzoni, na hawa kuridhika ummah na ulinganizi huo mwanzoni. Lakini baada ya kutabikishwa nidhamu ya kiraslimali katika nchi ya kiislamu na kutokamana na makafiri wakoloni na kisha na vibaraka wao na wanaofuata katika muelekeo wao na muongozo

wao, walifaulu wachache hao kuathiri na kuwahamisha wengi katika watu wa miji na baadhi ya wakaazi wa vijijini katika kufuata njia ambayo wao walifuata . na katika kuiga hadhara ya kimagharibi mpaka kufuta ubora wa uisilamu katika miji mingi ya kiislamu bila ya tofauti baina ya istanbul caoro na wala baina ya tunis na dimishq wala baina ya karachi na baghdad wala baina quda na beirut, zote hizi zinakwenda katika njia ya kuiga hadhara ya kimagharibi.

Na ikawa ni jambo lakawaida kusimama kikundi miongoni mwa waislamu kuzigonga fikra hizi na ikawa hamna shaka kujitokeza watu flani na kwa ujumla katika biladi ya kiislamu kuzipiga vita fikra hizi, kusimama kikundi bali vikundi vinalingana uwajibu wa kumhifadhi mwanamke wa kiislamu na kuhifadhi utukufu wake katika mujtamaa, lakini bila ya kuelewa nidhamu za kiislamu na bila ya kufafanua ahkam sharia. Na wakakubali iwe maslahi kulingana na akili ndio msingi wa utafiti, na kipimo cha rai na vitu na walingania kuhifadhi desturi na ada na kulingana na kushikamana na tabia, bila ya kuelewa kua msingi ni aqeedah ya kiislamu, na kipimo ni ahkam shariah na kufikia kushikamana kiupofu kwa kumsitiri mwanamke kua ni kumnyanyasa mwanamke na asiruhusiwe yeye kutoka nje ya nyumba yake au kutekeleza mahitaji yake na yeye kusimamia mambo yake. Na wengine katika wanavyuoni kua mwanamke ana aura tano: - Aura katika swala, Aura akiwa mbele ya maharimu wake, Aura akiwa mbele ya wanaume ajnabi, Aura mbele ya wanawake waislamu, Aura akiwa mbele ya wanawake makafiri.Na kulingana na haya walilingania kwa hijab kamili ambayo itamzuia mwanamke kumuona yejote au yeye kuonekana na yeyeote. Na wakalingania kwa kumzuia katika kupewa haki ya kuchagua na kumharamishia yeye rai katika siasa, na utawala, uchumi na jamii. Na kuweka vizuizi baina yake na baina ya maisha mpaka wakafanya baadhi ya aya za Allah zimekuja kumzungumzia mwanamume. Basi mwanamke na wakapotosha hadithi za Mtume (saaw) katika kumpatia mkono mwanawake katika baiyah na hadithi zake katika aura ya mwanamke na muamala wake kwa wanawake katika uhai

kupotosha kuambatana na wanayoyataka wao kwa mwanamke, wala sivyo inavotakiwa na hukmu za mteremsha sharia na yakawa yote hayo linawaweza watu katika mbali hukmu za mteremsha sheria na kua wapofu hakika upande wakijamii katika waislam nakwa sababu hiyo hazikuweza rai zao kusimama mbele ya fikra vamizi; wala hawakuweza kuzuia mawimbi makubwa yaliokua yakuendelea; wala haikuweza kuathiri katika kunyanya upande wakijmii zakiislamu hata kidogo. Pamoja na kwamba katika ummah kulikua na maulamaa wasiopungua mujtahidina wa kwanza au watu wa madhahib katika usomi au ujuzi; na pamoja au kwamba kuna utajiri mkubwa wa kifikra wakisheria kwa waislam ambao hakuna ummah unaokaribiya kwa utajiri huo. Na pamoja na kwamba kuna vitabu vyta thamani kwa waislamu katika makataba za watu jumla na za kibinagsi; pia haikuwezekana kuleta athari yoyote au kuzuia waigaji katika uovu wao. Na katika kuwakinaisha wenge fikkra finyo kwa rai ya kiislam ambayo mujtahid ameistanbit sahihi, maadam yalikua yana kwenda kinyume wanayoyataka mwanamke awe juu yake. Na hayo kwa sababu hiyo hawana hao wenge kuiga na wenge fikra hiyo, na wanavyuoni wasomi walikua mbali wao na sifa ya mtu mwenye kufikiri. Hawakufahamu ukweli [waqiah] au hawafahamu hukmu ya Allah (swt) au hawazichukui ahkam za sheria upokezi wa kifikra, na utabikishaji wake juu ya waqia utabikishaji wakindani utakaoleta utabikishaji kamili. Na kwa ajili yahio ikaendelea mujtama katika nchi za kiislamu ikiyumba yumba kati ya fikra mbili. Fikra zilizo ganda (jumud) na kuiga (taqleed). Na ikaendelelea upande wa kijamii kuperomoka, mpaka mwanamke wakiislamu akawa amechanganyikiwa kwa hivyo alikua kati ya mwanamke waliochanganyikiwa wanao igaiga hadhara ya kimagharibi bila yakuifahamu mgongano uliopo kati yake na kati hadhara ya kiislam .na akiwa kati ya mwanamke walio ganda mawazo yao asiweze kujinufaisha nafsi yake na wala waislam hawafaidiki na juhud zake. Wayote hayo kutokana na ukosefu wa kukuchukua uislamu kifikra. Na kwa ukosefu wa kufahamu nidhamu ya kijamii katika uislam.

Kwa hivyo hamna budi kusoma nidhamu ya kijamii katika uislamu kikamilifu, wala hamna budi kuzama katika kusoma huko mpaka ijulikane tatizo na kua ni kukutana mwanamke na mwanamume, na mahusiano yanayopatikana kutokamana na kukutana huko na yale matanzu yanayopatikana kutokamana na uhusiano huo. Kwa hivyo linalotakiwa ni kutibu makutano hayo na mahusiano yanayopatikana nayo na yale matanzu yanayopatikana nayo. Na kutibu huko isiwe ni kulingana na shara'a ama akili ni kuifahamu, na kua ni suluhisho la mwanamke wa kiislamu na mwananmume muisilamu, wanaoishi kwa mtazamo maalum wa kimaisha ikiwa ni mtazamo ambaa umewajibishwa na uisilamu. Na ni juu yao wajitunge kimaisha juu ya mtazamo huu pekee, kama alivyo amrisha Allah katika Quran na Sunna, bila ya kuangalia unavyogongana na umagharibi, au kwenda kinyume waliokua nayo mababa wa mababu katika mila na desturi.

### Mwanamke Na Mwanamume

Amesema Allah SWT:

{ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَرَّةٍ وَأَنْشَئَنَاكُمْ شُعُوبًا وَجَبَّانِينَ لِتَعْارِفُوا }  
(الحجرات: 13)

“Enyi wanadamu hakika sisi tumewaumbeni nyinyi kutokamana na mwanamume mmoja na mwanamke mmoja na tukawafanya ni mataifa na makabila ili mupate kujuana” alhujrat 13 na amesema:

{ يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ مَا عَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ } (الإنفطار: 6)

“Ewe mwanadamu ni lipi linalokughuri katika kumuabudu mola wako alietukuka” infitar 6 na akasema:

{ قُتِلَ الْإِنْسَانُ مَا أَكْفَرَهُ - مِنْ أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ - مِنْ نُطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَرَهُ } { عبس : 19 - 17 }

“Amelaaniwa mwanadamu kwa anayoyakufuru- kwa kitu gani amemuumba yeye – kutokamana na tone la maji amemuumba yeye na kumsawazisha” abasa 17-19. Kwa hivyo Allah SWT amekhutubia mwanadamu kwa majukumu na kumfanya mwanadamu ndie aliekhutubiwa na majukumu kumfanya mwanadamu ndie aliekhutubiwa na majukumu. Na kumteremsha sheria kwa ajili ya mwanadamu, Allah SWT

atamfufua mwanadamu, na mwanadamu kuhisabiwa na mwanadamu kuingiziwa peponi na motoni na kufanywa mwanadamu ndie aliekalifishwa sio mwanamume wala sio mwanamke.

Na Allah swt akamuumba mwanadamu mwanamume au mwanamke katika umbile maalum tofauti na mnyama kwa hivyo mwanamke ni mwanadamu, na mwanamume ni mwanadamu, wala mmoja hatofautiani na wengine katika uwanadamu wala hatofautiani mmoja na mwengine katika chochote katika uwanadamu huu. Na amewatayarisha wote wawili kuyaingilia mahitaji yakimaisha kwa sifa za kiuwanadam. Na akawafanya wao wawili waishi katika mujtamaa mmoja. Na akafanya kuendeleza kizazi kwa mujibu wa kukutana wao wawili na kuwepo kwao katika kila mujtamaa kwa hivyo haijuzu moja kumuangalia mwengine illa kama anavyomuangalia mwengine akiwa ni mwanadamu ambae ana sifa zote za uwanadamu na mahitaji ya kimaisha, na Allah SWT amemuumba killa mmoja wao na nguvu za kivyake (taqa hayawiyah) ndio nguvu ileile ambayo amemuumbia mwengine. Na akawajaalia killa mmoja kati yao mahitaji ya kiviungo kama njaa na kiu na kukidhi haja. Na akamjaaliya kila mmoja kati yao ghariza ya kuhifadhi maisha ya ghariza ya kuendeleza kizazi na ghariza ya kuabudu. Na ndizo ghariza zile zile alioumbiwa nazo mwengine. Kila mmoja kati yao akapewa uweza wa kufikiri na ndio uweza ule ule alionao mwengine. Kwa hivyo akili alio nayo mwanamume ndio akili alio nayo mwanamke kwani Allah swt ameiuumba akili ya mwanadamu wala sio akili ya mwanamume au mwanamke.

Isipokua ghariza ya kuendeleza kizazi hata kama kuna uwezekano wa kuishibisha na mwanamume na mwanamke au na mnyama au njia nyenginezo. Na yawezekana kwa mwanamke na mwanamke au mnyama au njia nyinginezo. Na lakini haiwezekani kutekeleza malengo ambayo kwa ajili yake imeumbwa katika mwanadamu isipokua katika hali moja pekee nayo ni kushibisha mwanamume kwa mwanamke au kuishibisha

mwanamke kwa mwanamume. Kwa hivyo yamekua mahusiano ya mwanamume kwa mwanamke na mwanamke kwa mwanamume katika upande wa kijinsia wa kimaghariza ni mahusiano ya kimaumbile wala hamna jambo la kigeni ndani yake. Bali ni mahusiano ya kiasili ambayo hupatikana lengo ambalo kwa ajili yake imewekwa nao ni ghariza ya kuendeleza kizazi. Kwa hivyo yapatikana kati yao mahusiano hayo kwa njia ya kukutanisha jinsi mbili itakua ni kawaida na lakimaumbile wala hamna jambo kegeni. Bali ni jambo la kawaida kwa ajili ya kuendeleza kizazi cha mwanadamu. Isipokua kuiacha huru ghariza hii itamdhuru mwanadamu na maisha yake ya kijamii. Na lengo la kuwepo kwake ni kuzaana kwa ajili ya kuendeleza kizazi. Kwa hivyo hamna budi kufanya mtazamo wa mwanadamu kwa ghariza hii imejengeka juu ya lengo ambalo kwa ajili yake imepatikana katika mwanadamu, nalo ni kuendeleza kizazi, wala hamna tofauti katika hayo kati ya mwanamume na mwanamke. Amma raha na starehe ambayo hupatikana katika kushibisha ni katika jambo la kimaumbile lisilo na shaka, ni sawa aliangalie mwanadamu au asiliangalie. Kwa hivyo haifai kusemwa ni wajibu kuepusha mtazamo wa raha na starehe katika ghariza ya kuendeleza kizazi, kwa sababu hilo haliji katika mtazamo bali ni maumbile na lisilo na shaka, na wala haiwezekani kuepukwa, kwa sababu ni katika muhali lisilowezekana, lakini mtazamo inapatikana kutokamana na ufahamu wa mwanadamu katika kushibisha huko na lengo la kupatikana lakini kwake. Na mpaka hapa hamna budi kuleta ufahamu maalum kwa mwanadamu katika ghariza ya kundeleza kizazi, na kwa lengo la kuwepo kwake katika mwanadamu, itampelekea yeye kua na mtazamo maalum kwa yale ambayo Allah SWT ameiumba katika mwanadamu katika ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mwanamke na mwanamke kwa mwanamume, na kukuza kwake mtazamo maalum kati mwanamume na mwanamke katika mahusiano ya uume na uukeni au kwa maana nyengine mahusiano ya kijinsia, kwa namna ambayo itajengwa juu ya malengo ambayo kwa ajili yake yamewekwa nayo ni kuendeleza kizazi. Na kwa mtazamo maalum hii itapatikana kushibisha ghariza na kupatikana lengo

ambalo kwa ajili yake limekuwepo na itapatikana utulivu kwa njtamaa ambao watauchukua ufahamu huu, kupatikana kwao mtazamo wa watu yaani watu jumla katika wanaadamu katika mwanamume na mwanamke katika mahusiano uume na uukeni au kwa lugha nyengine mahusiano ya kijinsia, katika mtazamo kujengwa juu ya raha na starehe, na kuifanya raha haina starehe ni jambo la kimaumbile na hamna budi kuishibisha. Na kuufanya mtazamo umejengwa juu ya lengo ambalo kwa ajili yake ipo ghariza hiyo. Na mtazamo huu itabakia ghariza ya kuendeleza kizazi na kuisimamia hakika sura ya sawa ambayo imeumbiwa, na kumfungulia mwanadamu nafasi ya kusimamia mabo yake yote, na kufuatilia mambo yote ambayote ambayo yatamfirahisha.

Na kwa sababu hiyo imekuwa hamna budi kwa mwanadamu katika ufahamu wa kusibisha ghariza ya kuendeleza kizazi na kwa lengo la kuwepo kwake na pia hamna budi kuwepo kwa jamii za wanadamu nidhamu itakayoondosha katika nafsi uovu wa fikra ya maingiliano ya kijinsia na kuizingatia kuwa ndio pekee, na kuweka mahusiano ya ushirikiano kati ya mwanamume na mwanamke. Kwa sababu hamna kufaulu kwa jamaa ila kwa ushirikiano wao wawili, kwa kuzingatia wao ni ndugu washirikiana ushirikiano wa mapenzi na huruma. Kwa hivyo hamna budi lazima mabadiliko ya mtazamo wa jamaa kwa mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke kubadilisha kikamilifu itakaoondosha uovu wa ufahamu wa maingiliano ya kijinsia na wanaifanya ni jambo la kimaumbile na ni lazima kushibishwa na itakaondosha kufungika kwa mahisiano hayo kwa raha na starehe na kuifanya kua ni mtazamo unaolenga maslah kwa jamaa na sio mtazamo wa uume na uukeni. Na utakaosimamiwa na uch mungu sio kupenda starehe na matamanio ya roho. Mtazamo usiokanusha kwa mwanadamu kujistarehesha kwa raha ya kijinsia, lakini inaolenga kueneleza kizazi, anaafikiana na lengo bora kwa muislamu nao radhi za Allah swt.

Na zimekuja aya za Quran zinazoelezea juu ya upande wa kindoa. Yaani juu ya lengo ambalo kwa ajili yake ipo ghariza ya kuendeleza kizazi. Kwa hivyo zimekuja aya za Quran zinazoelezea kuumbwa kwa ghariza kwa asli yake ni kwa ajili ya kindoa yaani kwa ajili ya kuendeleza kizazi, yaani Alla swt ameiumba ghariza kwa ajili ya ndoa. Na yameelezewa hayo kwa namna tofauti na kwa maana tofauti ili ifanye mtazamo wa jamaa kwa mahusiano ya mwanamke kwa mwanamume umejengwa juu ya ndoa sio kwa maingiliano ya kijinsia, amesema Allah swt:

{يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً} (النِّسَاءَ - 1)

*“Enyi watu mcheni Mola wenu ambae amewaumbeni nyinyi kutokamana na nafsi moja (adam) na akaumba kutokamana na hao wawili waume wengi na wanawake”* (Annisa 1) na amesema:

{ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا فَلَمَّا تَعَشَّاهَا حَمَلَتْ حَمْلًا خَفِيفًا فَمَرَّتْ بِهِ فَلَمَّا أَتَقْلَتْ دَعَوَا اللَّهَ رَبَّهُمَا لَنِّي آتَيْتَنَا صَالِحًا لَنَكُونَنَّ مِنْ الشَّاكِرِينَ} (الأعراف: 189)

*“Ni yeye ambae amewaumbeni nyinyi kutokamana na nafsi moja na ajaalia kutokamana nayo mkewe ili apate utulivu kutokamana nayo na alipo starehe nae, alibeba mimba nyepesi na ilipokua kubwa wao wawili wakamuomba mola wao (kwa kusema) lau utatupatia (kijana mwema kwa hakika tutakua ni mionganoni mwa wanakushukuru”* (Al-araaf 189) na amesema:

{ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً} (الرعد: 38)

*“Na hakika tuliwatuma mitume kabla yako na tukawajaliya wao wake na watoto”* (Raad-38) na amesema:

{ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ بَنِينَ وَحَفَدَةً} (النحل: 72)

*“Na Allah SWT amejaalia ya kutokamana na nafsi zenu wake na akajaalia kutokamana na wake zenu watoto wa wajukuu”* (Nahl 72) na akasema:

{ وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً }  
{ الروم: 21 }

“Na katika alama zake ni kua amewaumbia nyinyi kutokamana na nafsi zenu ili mupate utulivu kwao na akajaakiya baina yenu mapenzi na huruma” rum 21.

{ فَاطِرُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا } (الشورى: 11)  
"Na amesema "muumba wa mbingu na ardhi amewajaalia wake kutokamana na nafsi zenu" (shura 11) Na amesema:

{ وَإِنَّهُ خَلَقَ الرَّوْجِينَ الذَّكَرَ وَالأنثَى - مِنْ نُطْفَةٍ إِذَا تُمْنَى } (النجم: 45-46)  
"Na kwa hakika ni yeye alieumba jozi mume na mke kutokamana na tone (manii) yanapotoka" (An-Najm 45-6) na amesema:

{ وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا } (النبا: 8).  
"Na tumewaumbieni nyinyi jozi" (Anaba 8) Kwa hivyo Allah SWT amewafunga kuumba juu ya mwanamume na mwanamke katika upande wa ndoa na kukariri hayo ili iwe mtazamo baina ya mwanmume na mwanamke yaliojengwa juu ya mahusiano ya ndoa yaani kuzaa ili kuendeleza kizazi.

Athari ya mtazamo wa mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke

Inapochemsha ghariza hutaka kushibishwa na isipochemka haitaki kushibishwa. Na ghariza inapotaka kushibishwa humsukuma mwanadamu ili aishibishe, na asipoishibisha humtia wasiwasi maadamu inachemka. Na inapotulia huondoa wasiwasi. Na wala kutoishibisha kwake haipelekei kifo, wala madhara ya kiwiliwili au ya kinafsi au ya kiakili. Bali hufungika juu ya wasiwasi na dhiki na mpaka hapa ushibishaji ya kiviungo, bali ni kushibisha kwa ajili ya utulivu na umakinifu.

Na ghariza huchemshwa na mambo mawili ya kwanza:- uhakika wa kimada na yapili ni fikra na mawazo. Na isipokuwepo moja katika hayo mawili ghariza haichemki kwani haichemki kwa msukumo wa kindani kama mahitaji ya kiviungo

bali ni msukumo wa kiinje nayo ni ukweli wa kimada na fikra. Na hayo yote hufuata juu ya ghariza ya kuabudu (gharitu at-adayyun) na ghariza ya kuendeleza kkizazi (gharizatul A-NAU) sawa kwa sawa bila ya tofauti yejote baina yao.

Na kwa kua ghariza ya kuendeleza kizazi ni kama ghariza nyenginezo, inapochemka hutaka kushibishwa na haichemki illa ukweli wa kimada au fikra. Kwa hivyo imekua ghariza ya kuendeleza kizazi inaotoka kushibishwa inawezekana kwa mwanadamu kusimamia na kuelekeza kushibishaa huku, bali yawezekana kuisarifu katika kulileta au kulizuia kuchangamsha kwenda katika mwelekeo upande wa kuendeleza kizazi. Kwa hivyo kuangalia wanawake au waqia wowote yenye mahusiano kwa ghariza ya kuendeleza kizazi huchemsha ghariza na kuifanya kutaka kushibishwa. Na pia kusoma visa vya kijinsia na kusikia hadithi za kijinsia huchemsha ghariza ya kuedeleza kizazi na kujiepusha na mawazo ya kijinsia itakua kizizi baina ya ghariza ya kuendeleza kizazi na kuchemka kwake. Kwa sababu haiwezekani kuchemka ghariza ya kuendeleza kizazi isipokua inapochemsha kwa waqia wa kimada au mawazo ya kijinsia.

Kwa hivyo iwapo mtazamo wa watu kwa mahusiano ya mwanamume na mwanamke umetawaliwa na mahusiano ya uume na uu, yaani kwa mahusiano ya kijinsia kama hali ilivyo katika mujtamaa wa kimagharibi, itakua kuleta waqia wa kimada na mawazo ya kijinsia itakayochemsha kwa wanaume na wanawake ni jambo la dharura kwa ajili ya kuchemsha ghariza ili itake kushibishwa na hupatikana utulivu kwa kushibishwa kwake. Na iwapo mtazamo wa watu juu ya mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke umejengwa juu ya lengo la kuwepo kwake ghriza hii nayo ni kuendeleza kizazi itakua kuepusha waqia wa kimada au mawazo ya kijinsia kwa mwanamume na mwanamke ni jambo ladharura katika maisha ya umma ili isipate kuchemka ghariza ili isitake kushibishwa kwani kutoshibishwa huleta wasiwasi na dhiki kwa hivyo kuzuia waqia wa kimada inayochemsha katika ndoa ni

jambo la dharura kwa ajili ya kuendeleza kizazi na kupata utulivu na raha katika kupata kushibisha wakati inapotaka. Mpaka hapa yafahamika kua mtazamo wa watu wa mahusiano wa mwanamume na mwanamke ndio unoathiri na kupeleka maisha ya watu ammah. Na imekua mtazamo wa kiraslimali na wamashariki wanaobeba mfumo wa kiraslimali na wamashariki wanaobeba mfumo wa kikomunisti juu ya mahusiano wa mwanamume na mwanamke ni mtazamo wa kijinsia wala sio mtazamo wa kuendeleza kizazi. Kwa hivyo hufanya bidii kwa kusudi kuleta waqia wa kimada na mawazo ya kijinsia kwa mwanamume na mwanamke ili kuchemsha ghariza ya kuendeleza kizazi kwa ajili ya kushibisha. Na wanonelea kutoshibisha kwake husababisha dhiki ambayo itapelelkea madhara ya kiwiliwili na kinafsi na ya kiakili kwa madai yao. Na mpaka itakua watu wa kimagharibi na ukomunisti na mujtamaa wa kimagharibi na mujtamaa wa kimagharibi na wakikomunisti zimeenea kwao fikra za kijinsia katika hekaya na mashairi navitabu na yasiokua hayo, na imeenea kwa michanganyiko ya wanaume na wanawake bila ya umuhimu wowote katika majumba na sehemu ya matambezi, na mabarabara na katika sehemu za kuogelea ba nifano yake. Kea sababu wao huzingatioa ni jambo ladharura na hufanya kusudi kulileta napia ni sehemu ya maisha yao na sehemu ya mfumo wa maisha yao.

Ama mtazamo wa waislamu ambao wanaobeba uislamu wanaoiamini itiqadi yake na hukm zake na kwa ligha nyengine mtazamo wa waislamu wa mahusiano ya mwanamume na mwanamke, ni mtazamo wa kuendeleza kizazi sio mtazamo wa mahusiano ya kijinsia na pia huzingatiwa upande wa kijinsia ni jambo lisilo na shaka katika kushibishwa kwake, lakini silo ambalo hulengwa kushibishwa. Na kwa hayo inazingatiwa uislamu kuwepo kwafikra za kijinsia kati ya watu ni jambo linalopelekea katika madhara na kuwepo kwa waqia wa kimada ambayo inachemsha ghariza ni jambo lapelekea katika ufisadi. kWa hivyo ikaja kukataza kua faragha (khulwa) baina ya mwanamume na mwanamke, na ikaja kukataza kuonesha uzuri

(tabaruj) na mapambo (zeena) kwa ajnabi, na ikawakataza wote mwanamume na mwanamke kumtazama mwengine mtazamo wa kijinsia na ikaja kufunga mipaka katika ushirikiano baina ya mwanamume na mwanmke katika maisha ya amma na ikaja kufunga mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamume na mwanamke katika hali mbili pekee nayo ni:- ndoa na vijakazi (watumwa).

Kwani Uislamu hufanya bidii ya kuweka vizuizi baina ya ghariza ya kuendeleza kizazi na kinachochemsha katika maisha ya amma na juu ya kufunga mahusiano ya kijinsia katika mabo maalum. Wakati uraslimali na ukomunisti hufanya bidii ya kuleta yatakaochemsha ghariza ya kuendela kizazi kwa ajili ya kushibisha na kuiacha katika killa jambo. Na wakati mtazamo wa uislamu kwa mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke ni kwa ajili ya kuendeza kizazi na mtazamo wakiraslimali na kikomunisti kwa mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke ni matazamo wa uume na uuake, yaani mtazamo wa kijinsia. Na tafauti baina ya mitazamo miwili na tafauti kubwa baina ya wanaoyafanya bidii wote katika uislamu na mifumo hii miwili na kwa hayo yadhihiri kwa yale ya uislamu katika mtazamo safi bora na sitara na mtazamo wa kumtuliza mwanadamu na kuendeleza kizazi chake.

Ama madai ya wamagharibi na wakomunisti kua ukandamizaji wa ghariza ya kijinsia katika mwanamume na mwanamke humsababishia mwanadamu maradhi ya kiwiliwili na ya kinafsi na ya kiakili hayo sio ukweli na ni urongo unaokwenda kinyume na uhakika. Hayo ni kwa sababu kuna tofauti kati ya ghariza na mahitaji ya viungo kwa upande wa ulazima wa kishibisha kwani mahitaji ya kiviungo kama kula na kunywa na kukidhi haja ni lazima kushibishwa na zisiposhibishwa yatapatikana madhara na pengine kupelekea mauti. Ama ghariza ya kuhifadhi maisha na ghariza ya kuabudu na ghariza ya kuendeleza kizazi hiyo si lazima kushibishwa. Na zisipo shibishwa haipatikani kwa kuto shibishwa kwake madhara yejote ya kiwiliwili au ya kiakili au ya kinafsi bali

hupatikana kwayo wasiwaso na dhiki wala sio jengine. Kwa dalili mtu anaweza kuishi umri wake wote pasi na kushibisha baadhi ya ghariza. Pamoja na hayo asipate madhara yejete na dalili ya madai yao katika madhara ya kiwiliwili na kiakili na ya kinafsi hayampati mwanadamu kwa sifa ya uwanadamu asiposhibisha ghariza ya kuendeleza kizazi bali inawapata baadhi ya watu fulani na hayo yaonesha kua hayapatikanai kimaumbile kwa mujibu wa umbile lake kwa kutoshibisha, bali hupatikana hayo kwa sababu nyenginezo sio ukandamizaji. Kwani lau apatikana kutokamana na ukandamizaji wa ghariza yangempata mwanadamu katika killa hali inaopatikana ukandamizaji kwa mujib wa maumbile ya halijapatikana kwa mwanadamu kimaumbile kutokamana nao ni kwa sababu nyenginezo sio ukandamizaji.

Huu ni kwa upande moja na kwa upande mwengine mahitaji ya kiviungo hutaka kushibishwa kimaumbile ya kindani billa ya kitu cha kuathir cha kiinje japo kua kiathiri cha kinje huathiri katika hali ya kuwepo ya njaa tofauti na ghariza kwani haitaki kushibishwa kindani pasi na kinachoathiri ya kiinje bali haichemki kindani illa cha kuathiri cha kiinje kati waqia wa kimada au mawazo ya kijinsia yenyе kuichemsha ikiwemo yanaoingia katika maana ya kiinje haichemki. Na hivi ndivyo ghariza zote zilivyo namna tofauti baina ya ghariza ya kuhifadhi maisha au ghariza ya kuabudu au ghariza ya kuhifadhi maisha ai ghariza ya kuabudu au ghariza ya kuendeleza kizazi kwa sifa zake. Kwa hivyo ikiwepo mbele ya mtu kitakacho chemsha yaani ghariza huchemka na ghariza hutaka kushibisha na ikiwa mbali nae kinachochemsha ghariza au kujishughulisha na yale ambayo ni muhimu itaondoka kiu ya kuishibisha na nafsi yake itapata utulivu tofauti na mahitaji ya kiviungo kwani inapopanda haiondoki kabisa iwapo haijashibishwa bali itaendelea mpkaka ishibishwe. Na kwa hayo yaonekana kwa uwazi kua kutoshibisha ghariza ya kuendeleza kizazi haipatikani kutokamana nayo maradhi yejete ya kiwiwilaili au ya kiakili au ya kinafsi kabisa kwa sababu ni ghariza na sio mahitaji ya kiviungo. Kwa ufupi ni kua itakapo patikana mbele ya mtu

kitakachochemsha ghariza ya kuendeleza kizazi katika waqia wa kimada au mawazo ya kijinsia. Yanaoathiri basi huenda ikachemka na kutaka kushibishwa, na isiposhibishwa atasibiwa na wasiwasi wala sio zaidi na ikiendelea wasi wasi huo ataptata dhiki. Na akijiepusha na kinachowasha ghariza ya kuendeleza kizazi zu kujishughulisha na yale yatakaomsahaulisha juu ya ghariza hii kwa yale ambayo ni muhimu wasiwasi utapata kwa ukandmizaji wa ghariza ya kijinsia wakati inachemka huleta dhiki na wasiwasi wala sio zaidi na isipochemka na yanaoichemsha hamna chochote kinachopatikana hata dhiki na wasiwasi kwa hivyo dawa yake ni kutoichemsha kwa kuweka kizuizi kati yake na kati yake kinachoathiri kwa kiasi ambacho haiwezi kushibishwa.

Na kwa haya yabainika upotofu wa mtazamo wa kimagharibi na ukomunisti ambao wamefanya mtazamo wa watu juu ya mahusiano ya mwanamume na mwanamke umebuniwa juu ya mahusiano ya uume na uuke na kufuatia upotofu wa suluhisho wa mtazamo huu kwa kuichemsha ghariza hiyo kwa mwanamume na mwanamke kwa kuweka yale yatakaochemsha katika mbinu kama mchanganyiko na ngoma (dance) na michezo na hekaya na mifano kama hayo. Vile vile yabainika ukweli wa mtazamo wa kiislamu ambao umeifanya mtazamo wa watu juu ya mahusiano ya mwanamume na mwanamke umejengwa juu ya lengo la kuwepo kwake ghariza hii nao ni kuendeleza kizazi na pia inadhihirika usawa wa suluhisho wa mtazamo huu kwa kuepusha yale yanaoichemsha katika waqia na kimada na mawazo ya kijinsia iwapo haitaweza kushibishwa kisheria kwa ndoa na vijakazi kwa hivyo uislamu pekee ndio ambao unatatta yanaopatikana na ghariza ya kuendelea kizazi katika uharibifu wa mujtamaa na watu utatuzi wa kikamilifu kwa nama ambayo itapatikana kujengea na kunyanyuka katika mjtamaa na watu.

### Kupanga mahusiano baina ya mwanamke na mwanamume

Haimanishi kua mwanamke hua anachemsha ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mwanamume na mwanamke huchemsha

ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mwanamke, na kua kuchemsha huku hamna shaka kupatikana kwake killa mwanamume anapokutana na mwanamke au mwanamke kukutana na mwanamume. Bali yamaanisha kua kiasli kila moja kati yao humpandisha mwengine kwa kukutana kwao hupatikana kwa kukutana kwa mahusiano ya kijinsia baina yao. Lakini huenda kukutana kwao, na isipande ghariza hiyo. Kama kukutana kwa ajili ya mabadilishano ya kibiashara au kusimamia shughuli za kumfanyia upasuaji mgonjwa au kuhudhrria darsasa za kielimu au mengineo. Lakini katika hali zote hizi na nyenginezo kuna uwezekano wa kupandisha ghariza ya kijinsia baina yao. Isipokua haimaanishi kuwepo kwa uwezekano wa kuwepo kwa kuipandisha, bali hupatikana kuchemka katika mwangalio kutoka kila moja kwao kwa mwengine kwa mtazamo wa ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mtazamo wa uume na uke. Kea hivyo haijuzu kumfanywa umbile la mwanamke huchemsha ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mwanamke na kua ni sababu ya kumtenganisha mwanamke na mwanamume kuwatenganisha kikamilifu, yaani haifai kufanywa kukutana kwao italeta kuchemka kwa ghariza ya kuendeleza kizazi kwa mwanamke na mwanamume na kuzuia kukutana waume na wanawake katika maisha ya ammah na bila ya kushirikiana baina yao. Bali hamna budi kukutana mwanamke na mwanamume katika maisha ammah na hamna budi kushirikiana kwao. Kwa sababu kushirikiana huku ni dharura kwa mjtamaa na kwa maisha ammah. Isipokua haiwezekani ushirikiano huu illa kwa nidhamu itakaopanga mahusiano ya kijinsia baina yao na itakaopanga mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume. Na hamna budi nadhamu hii itokamane na mtazamo juu ya mahusiano hayo baina mwanamke na mwanamume kwa mtazamo wa kuendeleza kizazi. Na kwa nidhamu hiyo yawezekana kukutana mwanamke na mwanamume katika maisha ammah na kushirikiana baina yao billa ya pingamizi yoyote.

Na nidhamu pekee inaoweza kuwahakikishia utulivu wa maisha na kupanga mahusiano ya mwanamke na mwanamume

mpangilio wa kikawaida na kua upande wa kiroho ni msingi wake mna hukm sharii ndio kipimo chake zikiwemo katika hizo hukm amabzo zitafikiwa tabia bora na, na nidhamu hii ni nidhamu ya kijamii katika uislamu. Kwa hivyo humungalia mwanadamu awe ni mwanamke au mwanamume kua ni mwanadamu ana ghariza na hisia na kasoro na pia ana akili. Na inamruhusu mwanadamu huyu kuyafurahia na mazuri ya kimaisha na pia haukumkataza yeye kuchukua fungu kubwa katika hayo. Lakini kwa namna ambayo watu na mjtamaa itahifadhika na kumpelekea mwanadamu katika kuyafikia yatakayo mtuliza mwanadamu. Na nidhamu ya kijamii katika uislamu dnio pekeenidhamu sahihi juu ya ufaradhi ya kukanusha nidhamu nyenginezo zilizoko kwa sababu nidhamu hii inaangalia ghariza ya kuendeleza kizazi kua ni ghariza ya kuendeleza kizazi cha mwanadamu. Na inapangilia mahusiano ya uume nauuke kati ya mwanamke na mwanamume mpangilio wa kindani kwa namna inafanya ghariza hii imefungwa katika njia yake ya kimaumbile inashikamana na lengo la kuumbwa kwake na Mwenyezi Mungu swt katika mwanadamu. Na kwa wakati huihu inapanga mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume na kupangilia mahusiano ya uume na uuke nisehemu ya mpagilio wa mahusiano baina yao kwa namana iatdhamini ushirikiano baina ya mwanamke na mwanamume katika kuungana kwao pamoja ushirikiano ambao itapatikana kheri kwa watu na mujtamaa wa mtu binafsi kwa wakati huo huo itahakikisha kufikia tabia bora na kufanya radhi za Allah swt dnizo zinazo kimbiliwa ili iwe usafi na uchamungu ndio ambayo itaamua njia ya mahusiano baina ya jinsi mbilihizi katika maisha yna kufanya mbinu kwa namna ya kimaisha hazigongani na njia hiyo kwa namna yoyote ile.

Kwa hivyo Uislamu umefunga mahusiano ya kijinsia yaani mahusiano ya uume na uuke kati ya mwanamume na mwanamke kwa ndoa na vijakazi. Na kuifanya killa mahusiano nje na hayo ni dhambi na inawajibisha adhabu ya hali ya juu kabisa. Na kisha kuruhusu mahusiano mengine ambayo ni katika ghariza ya kuendeleza kizazi isipokua makutano ya

kijinsia kama ubaba na umama na utoto na undugu na uami na ujomba na ikafanywa ni kizazi mahram. Na akaruhusiwa mwanamke kile alicho ruhusiwa mwanamume katika kuelekeza shughuli za kibashara na ukulima na usanii na nyenginezo katika kuhuduria darasa za ilmu na swala na kubeba ulinganizi na yasiokua hayo.

Na Uislamu ukaweka ushirikiano baina ya mwanamume na mwanamke katika mambo ya kimaisha na katika mahusiano ya watu wenyewe ni jambo liko wazi katika maamiliano yote. kwa hivyo wote ni waja wa Allah na wate wanashikamana na ya kheri na katika kumcha Allah SWT na katika kumuabudu yeye. Na zimekuja aya (za quran) kumzungumzia katika kumlingania katika uislamu bila ya kijali umbile lake mwanamume au mwanamke, amesema Allah SWT:

{ قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا } (الأعراف: 158)

“Sema enyi watu hakika mimi ni mjumbe wa Allah SWT kwenu nyinyi nyote” al araf – 158. Na amesema:

{ يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ } (النساء - 1)

“Enyi watu mcheni mola” (Nisa 1) Na zimekuja aya kuwazungumzia waumini katika kutekeleza kwa hukmu za uislamu, amesema Allah:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِبُو لِلَّهِ وَلِرَسُولِهِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحِبُّكُمْ } (الأنفال: 24)

“Enyi mlionamini muitikieni Allah na mjumbe wake wanapowaiteni katika yale yatakaowapa uhai” (Al-Anfal 24) na zimekuja aya jumla zimekusanya mwanamume na mwanamke amesema Allah SWT:

{ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ } (البقرة: 18)

“Mumefaradhishiwa juu yenu saum” (Al-Baqara 183) na akasema

{ أَقِيمُوا الصَّلَاةَ } (الأنعام: 72)

“Simamisheni swala” Annaam 72 na akasema:

{ خُذُّ مِنْ أَمْوَالِهِمْ } (التوبه: 103)

“Kuchukua katika mali yao” tauba 103 na akasema:

**{ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ } (التوبه: 60)**

“Hakika zaka ni ya mafuqara na maskini” tauba 60 na akasema:

**{ وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الْذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ } (التوبه: 34)**

“Na wale wanaorudika dhahabu na fedha” tauba- 34 na akasema:

**{ قَاتَلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِيَوْمِ الْآخِرِ } (التوبه: 29)**

“Piganeni na wale ambao hawaamini Allah SWT na siku ya mwisho” tauba 29 na akasema:

**{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَخَذُوا آبَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أُولَئِكَءِ إِنْ اسْتَحْبُوا الْكُفْرَ عَلَى إِيمَانِهِمْ } (التوبه: 23)**

“Enyi mliaoamini musiwafanye baba zenu na kaka zenu kua ni vipedenzi wakipendelea ukafiri kuliko imani” (Tauba 23) na nyenginezo katika aya kwani zote ni Ama kwa mwanamume na mwanamke, na kuyafanya kazi nayo lawezekana kuwajumuisha mwanamume na mwanamke hata yale ambayo hufanyiwa kazi na mtu binafsi kama swala. Ni dalili juu ya kuruhusu uislamu kujumuika baina ya mwanamume na mwanamkekutekeleza waliofaradhishiwa nayo katika hukmu ya yale ambayo ni juu yao kutekeleza katika matendo.

Isipokua uislamu umeweka mipaka na yakatazwa yote yanaopelekea kwa mahusiano ya kijinsia yasioruhusiwa na sheria na killa anaetoka awe ni mwanamume au mwanamke kutoka nidhamu khasa ya mahusiano ya kijinsia. Na kukanya vikali kukataza huku, na ikafanywa sitara ni jambo lawajibu na kufanya kutumia killa njia mbinu na nnamna itakaopelekea kuhifadhi ubora na tabia kua ni wajibu, kwa sababu iwapo wajib hautimu illa kupatikana kwake basi hilo pia ni wajibu “Ma la yatimu Al-wajib illa bihi fahuwa wajib” na akayafungia hayo na hukm sharia maalum na hukm hizi ni nyingi kati yake ni:-

1:- Amewaaamrisha killa mmoja wao mwanamume na mwanamke kuinamisha macho yao amesema Allah swt:  
**{ قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغْضُبُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَلِكَ أَزْكَى لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ - وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُبْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ }**  
**(النور: 30-31)**

“waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wazihifadhi tupu zao hayo ni bora kwao na hakika Allah SWT ni muelewa kwa wanaoyatenda – na waambie waumini wanawake wainamishe macho yao na wazihifadhi tupu zao” AnNur 30.

2:- Amewaaamrisha wanawake wavae vazi la hishma ambalo lasitiri sehemu zote za mapambo isipokua yaliiodhihiri. Na waninginize wavazi yao ili wasitirike nayo amesema Allah swt:  
**{ وَلَا يُبَدِّلُنَّ رِيَنَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلَيَضُرِّبُنَّ بِخُمُرِهِنَّ }** (النور: 31)

“na wasidhihirishe mapambo yao illa illa yaliiodhihiri na wavae khimar (nguo ya kichwa) mpaka juu ya vifua vyao” (An-Nur 31 na akasema

**{ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَا زَوَاجٌ كَوَافِرَ وَنِسَاءُ الْمُؤْمِنِينَ يُذْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَابِيبِهِنَّ }**  
**(الأحزاب: 59)**

“Ewe Mtume waambie wakezo na mabanati wako na wanawake waumini waninginishe juu yao majilbaba (mabuibui)” (Al-Ahzab 59) yaani wasidhihirishe sehemu za mapambo ila yaliiodhihiri isipokua uso na viganja vya mikono. Na khimar ni stara ya kichwa, na jaib ni cola ya kanzu yaani sehemu ya wazi ya kanzu shingo mpaka kifuani yaani wazifanye khimar zao juu ya mashingo yao na vifua vyao. Na idna katika jilbaba ni kuninginisha nguo mpaka chini.

3:- Amekataza mwanamke kusafiri kutoka nchi moja hadi nyengine msafara wa mchana mmoja na usiku moja illa aandamane na mahram. Amesema SAW “sio halali kwa mwanamke anaeamini Allah swt na siku ya mwisho msafara wa mchana moja na usiku moja ila aandamane na mahram wake”

4:- Amekataza faragha (khulwa) kati ya mwanamume na mwanamke ila mahram awe pamoja nae. Amesema (saaw)

“Asikae faragha mwanamume na mwanamke illa awe ni mahram wake wala asisafiri mwanamke ila pamoja na mahram akasimama mtu ana akasema mke wangu ametoka kwenda kuhiji na mimi nimeandikishwa katika vita fulani na fulani akasema (saaw) nenda na uhiji na mkeo”

5:- Amekatazwa mwanamke kutoka katika nyumba yake illa kwa idhini ya mume wake kwa sababu yeye ana haki juu yake kwa hivyo haifai yeye kutoka katika nyumba yake illa kwa idhini yake mume na anapotoka pasi na idhini akakua ameasi. Na huzingatiwa ameasi (Nashiza) na hastahiki lishe (Nafaqah) imepokewa na ibn Battah katika ahkam Annissa kutoka kwa Anas kua mtu alisafiri na akmkataza mkewe kutoka. Akawa mgonjwa babake (mke) akaomba ruhusa kwa Mtume SAW ili amtembelee babake Mtume saaw akamuambia “mche Allah na usimuasi mumeo akafa babake na akaomba ruhusa kutoka Mtume saaw kuenda kuhudhuria mazishi ya babake akamuambia “mche Allah Na Usimuaasi Mumeo” Allah swt akampa wahyi Mtume SAW “hakika mimi nimemsamehe yeye kwa kumtii mumewe”

6:- Uislamu umehimiza kwa kufanya mkusanyiko wa wanawake ni wenyе kutenganishwa na mkusanyiko na wanaume katika maisha khasa ya kibanafsi na katika misikiti na vyuo na mifano yake na kufanywa mwanamke aishi kati kati ya wanawake na mwanamume aishi katikati ya wanaume na kufanywa safu za wanaume na kufanywa maisha ya wanawake yawe pamoja na wanawake au pamoja na mahram. Kwa hivyo mwanamke atatekeleza shughuli zake jumla kama kuuza na kununua na mifano yake na kuedna baada ya kazi aishi na wanawake na wenzake au mahram wake.

7:- Umehimizia mahusiano yawe juu ya ushirikiano baina ya mwanamke na mwanamume ni mahusiano amma na sio mahusiano ya khasa kama kutembeleana kati ya wanaume ajnabi na wanawake na kutoka pamoja kimatemezi kwa sababu

makusudio ya ushirikiano huo ni kutekeleza mwanamke haki yake na maslahi yake katika uwajibu ilioko juu yake.

Na kupitia hukmu hizi Uislamu umezingira kujumuika kwa mwanamke na mwanamume ili usigeuke mjumuiko huu kuwa mjumuiko wa kijinsia na isipote mjumuioko wa ushirikiano wa kutekeleza maslahi na kutekeleza shughuli zao. Kwa hivyo umetibu mahusiano ambayo yanatokamana na maslahi ya watu binafsi wawe ni wanawake au wanaume wakati wa kujumuika kwa wanaume na wanawake, na ukatibu mahusiano yanaopatikona kwa kukutana kwa mwanamume na mwanamke, kma lishe (Nafaqah na utoto na ndoa na menginea kutibu ambako itafunga kukutana kwa mahusiano ambayo imepatikana kwa mahusiano ambayo imepatikana kwa ajili yake na kumuepusha na mahusiano kukutana kijinsia.

### Maisha Khassa

Maumbile ya maisha ya mwanadamu humfanyia yeye maisha ammah wanaoishi ndani yake watu binafsi katika mujtamaa katika khabila, au mji wa kumwekea yeye maisha maalum anaoishi yeye katika nyumba yake kati ya watu wa familia yake. Na uislamu ukaja na hukmu maalum kuhusiana na maisha hayo khasa na kusuluhisha matatizo ambayo humpata mwanadamu ndani yake awe ni mwanamume au mwanamke. Na katika hukmu zilizojitokeza zaidi ni kua imefanywa maisha yake khasa katika nyumba yake iwe chini ya usimamizi wake pekee, na wamekatazwa watu kuingia katika nyumba yake illa kwa ruhusa yake. Amesema Allah swt:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْسِفُوا وَتُشَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ. } (النور: 27)

“Enyi Mulioamini Musiingie Majumba Yasiokua Yenu Mpaka Muombe Ruhusa Na Muwasalimie Watu Wake Hayo Ni Bora Kwenu Ili Mupate Kukumbuka” (An Nur 27). Kwa hivyo Allah swt amekataza kuingia majumba illa kwa idhini ya mwenyewe na kuufanya kuoomba idhini ni kutojitambulisha na idhini ni istinas Na akasema:

**{... حَتَّىٰ تَسْتَأْنِسُوا ...} (النور: 27)**

“Mpaka muombe ruhusa” nur 27 nao ni ufupisho wa kutaka idhini kwa sababu hamna kuombaruhusa illa kwa hilo. Yaani mpaka mutake idhini kwa wenyewe. Amenukulu tabrani kua Mtume saaw aesema: “Yeyote atakae chungulia katika nyumba billa ya ruhusa ya wenyewe kwa hakika ameshaibomoa” na amenukulu Abu Daud: “mtu alimuuliza Mtume saaw nitake idhini nitkitaka kuingia kwa mamangu? Akasema ndio akasema hanawakumtumikia illa mimi jee unapendelea kumuona uchi? Akasema mtu: la akasema basi taka ruhusa kwa hivyo amekatazwa mtu yeyote kuingia nyumba isiokua yake illa kwa ruhusa ya wenyeye nyumba. Wala hamna tofauti katika hayo awe mwenye kuingia awe muislamu au asiwe muislamu. Na ijapokua uzungumzi ni kwa waislamu lakini ni kwa upande wa mwenye kutaka idhini ama majumba imekuja kwa uwazi billa ya kizuizi na ujumla amma billa ya maalum takhsis kwa imekusnya killa nyumba. Na hili liko wazi katika kuhifadhi heshiima ya nyumba na katika kutofautisha maisha khasa kwa hukm maalum, kati yake ikiwa ni kuomba ruhusa wakati wa kuingia nyumba yeyote. Na asipokuta yeyote katika nyumba na katika kutofautisha maisha khasa kwa hukm maalum kati yake ikiwa ni kuomba ruhusa na atakapo ambiwa regea basi ni wajibu kwake aregee wala haifai kwake kuingia. Amesema Allah swt:

**{ فَإِنْ لَمْ تَجْدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ وَإِنْ قِيلَ لَكُمْ ارْجِعُوهَا فَارْجِعُوهَا هُوَ أَزْكَى لَكُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ } (النور: 28)**

“Na musipokuta humo yeyote basi musiingie mpaka mupewe ruhusa na munapo ambiwa regeeni basi muregee hilo ni bora kwenu na Allahh ni mjuzi kwa munayoyatenda” (An-Nur 28) Yaani haifai kwenu kusositiza katika kutanga ruhusa, na wala asisitize katika kurahisishiwa mipaka/ sitara hijab na wala musisimame milangoni mukingoja. Na hayo yote ni katika majumba ya kukaliwa. Ama majumba yasiokaliwa hapo huangaliwa iwapo yule anaetaka kuingia kuna kitu anahitajia kwake injuzu kuingia billa ya ruhusa. Na ni nyuma zilizotengwa

katika zile ambazo ni wajibu wa kuomba ruhusa kwa anaetaka kuingia. Amesema Allah swr:

{لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَذَرُّوا بِيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَاعٌ لَكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدِونَ  
وَمَا تَكْتُمُونَ} (النور: 29)

“Sio makosa kwenu kuingia majumba yasiokaliwa ambazo ziko na munaoyahitajia na Alla ni muelewa wa yale munaoyadhihirisha na munayoyaficha” Nur 29. Na ufahamu wa kinyume (mafhum al-mukhalafah) ni kua hamuna nyinyi munachohitajia humo basi musiingia kwa hivyo kutolewa kwa majumba khasa zisizokaliwa ambazo ziko na kitu ambacho mwenye kuingia anahitajia. Na kupitia hukm za kutolewa (istithnaa) hizi zinahifadhi maisha khasa na usumbufu wa wanaobisha na hupata utulivu walioko ndani au killa alioko nje.

Huu ni upande wa wale wasio milikwa nao katika watumwa na wasiokua watoto. Ama kwa wale wao wanawamiliki na watoto ambao hawaja baleghe wao wataingia majumba billa ya ruhusa isipokua katika nyakati tatu nao ni: kabla ya swala ya alfajiri, na wakati wa mchana (dhuhur) na baada ya swala ya isha. Kwa hivyo ni wajibu kwao kuomba ruhusa katika nyakati hizi tatu, kwa sababu ni nyakati za uchi wakati huo mtu hubadilisha nguo yake kwa ajili ya kulala au anapoamka kutoka usingizini nao ni wakati wa uchi. Ama kabla ya swala ya alfajiri huo ni wakati wa kuamka kutoka usingizini na pia hubadilisha nguo za kulala kwa nguo zengine. Na wakati wa adhuhuri ni wakati wa kujinyoosha na kulala na hupatikana wakati huo kubadilisha nguo na baada ya swala ya isha ni wakati wa kulala na wakati huo hubadilisha mtui nguo za kushindia na huvaan nguo za kulalia. Kwa hivyo hizi ni nyakati za uchi ni wajibu wakati huo kuomba ruhusa wanaowamiliki katika watumwa, na watoto ambao hawaja baleghe, ama kwa nyakati zisizo kua kwa hawa aina mbili wawe wakiingia majumba katika wakati wowote wanaotaka billa ya ruhusa mpaka watoto wanapofikia umri wa kubaleghe haki yao ya kuingia huanguka na itakua ni juu yao kuomba ruhusa kama watu wengine. Amesema Allah SWT

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِيَسْتَأْذِنُكُمُ الَّذِينَ مَلَكُتُ أَيْمَانُكُمْ وَالَّذِينَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلْمَ مِنْكُمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ مِّنْ قَبْلِ صَلَاةِ الْفَجْرِ وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِّنْ الظَّهِيرَةِ وَمِنْ بَعْدِ صَلَاةِ الْعِشَاءِ ثَلَاثَ عَوْرَاتٍ لَكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ بَعْدُهُنَّ طَوَافُونَ عَلَيْكُمْ بَعْضُكُمْ عَلَى بَعْضٍ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ {النور: 58}

*“Enyi mulioamini na waombe ruhusa wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki (watumwa) na wale ambao hawajafikia umri wa kubaleghe mionganini mwenu maratatu kabla ya swala ya alfajri na wakati munapo vua nguo zenu wakati wa adhuhuri na baada ya swala ya isha nyakati tatu za uchi na sio makosa juu yenu na juu yao baada ya hapo kutembeleana baadhi yenu juu ya baadhi hivi ndivyo Allah anavobainisha aya zake na Allah ni mjuzi na mwenye hikma:- na wanapofikia watoto mionganini mwenu umri wa kubaleghe basi basi na waombe ruhusa kama walivyokua wa kiomba ruhusa kabla yao hivi ndivyo Allah anavobainisha aya zake na Allah ni mjuzi na mwenye hikma” nur 58.*

Kwa hivyo hukmu hizi zinahifadhi maisha khasa ndani ya nyumba kutokamana wanaotaka kuinguingia hamna tofauti katika hayo kati ya ajnabi na mahram wa karibu au wanasaha. Ama hukm hizi za maisha khasa za ndani mwanamke anaishi pamoja na wanawake au pamoja na maharim wake kwa sababu wao ndio ambao inafaa kwake kuwadhihirishia sehemu za mapambo yake katika viungu vyake. Katika vile vinavodhiihiri kikawaida katika maisha khasa ndani ya nyumba. Na kwa wasiokua wanawake na mahrim wake haijuzu kwake kuishi pamoja nao kwa sababu haijuzu kwake kuwadhihirishia sehemu za mapambo katika viungo vyake. Katika vile vinavyodhiihiri wakati mwanamke anapotekeleza shughuli zake za kinyumbani visivyo kua uso viganja vya mikono. Kwa hivyo maisha khasa yamefungwa juu ya wanawake mahrim na hamna tofauti baina ya wanawake waislamu na wasiokua waislamu kwani wote ni wanawake. Kwa hivyo mwanamke amekatazwa kudhihirisha viungo vyake ambavyo vinamrembesha yeeye kwa ajnabi na hakukatazwa kuvidhihirisha kwa mahrim ni dalili wazi ya kufunga maisha khasa kwa mahrim pekee yao amesema Allah swt:

{ وَقُلْ لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلِيَضْرِبْنَ بِخُمْرِهِنَّ عَلَى جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعْوَلَتِهِنَّ أَوْ أَبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعْوَلَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعْوَلَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخْوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوْ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولَئِي الْأَرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهِرُوا عَلَى عَوْرَاتِ النِّسَاءِ} (النور: 31)

“Waambieni waumini wanawake wainamishe macho yao na wahifadhi tu zao na wasidhihirishe mapambo yao illa vilivyo dhihiri na watandike khimar zao juu ya vifua vyao na wasidhihirishe mapambo yao illa kwa waume zao au babazao, au baba wa waume wao, au watoto wao au watoto wa waume zao au ndugu zao au watoto wa ndugu zao au watoto a dad zao au wanawake wenzao au wale amba waliomiliki na mikono yao ya kulia (watumwa) au wale amba wasiokua na matamanio(ya wanawake) katika wamaume au watoto amba hawaelewi tupu za wanawake” nur 31.Na wameunganishwa mahrim na watumwa amba wao wanaumiliki, na wale amba hawana matamanio ya wanawake kama wakongwe, wazimu au walio vunjwa uume au kama hao katika wale wasiokua na matamanio na ni kuhitajia wanawake kwani hao yajuzu kwao wawe katika maisha khasa na wasiokua hao katika wanaume ajnabi na iwapo katika wakaribu (aqarib) wasikua mahrim kwao wao haijuzu kua katika maisha khasa kabisa kwa sababu haijuzu kwa mwanamke kuudhihirishia sehemu za mapambo katika viungo vyake ambavyo hudhihirisha kikawaida katika nyumba yake.

Kwa hivyo kukutana wanaume ajnabi na wanawake katika maisha khasa ni haramu moja kwa moja illa katika hali ambazo mteremsha sharia amezivua kama kualikwa chakula na kuunganisha kizazi (sitatul-arham)na lazima pamoja na mwanamke awe na mahra wake na awe ni mwenye kujistiri sehemu zake zote (aura).

#### UFARADHI WA KUTENGANISHA WANUME NA WANAWAKE KATIKA MAISHA YA KIISLAMU.

Hakika maisha ya kiislamu ni maisha ya waislamu katika killa jambo lao jumla imethubutu kwa nusus za kisheria katika

quran na sunna na kua wanaume watenganishwe na wanawake iwe ni katika maisha khasa katika nyumba na mfano wake au katika maisha jumla (ammah) katika masoko na mabarabara na mifano yake. Na aina hayo ya kimaisha yamethubutu katika mkusanyiko wa ahkam shariya zinohusiano na wanaume na zinazohusiano na wanaume na zinazohusina na zinazohusiana na wanaume na zinazo husiana na wanawake na zanazo husiana na wao wawili na zimethubutu kutokamana nauzungumzi wa quran kwa wanawake kwa sifa yao kama wanawake na kwa wanaume kwa sifa yao kama waume mfano wa hayo kauli ya Allah swt:

{وَالْمُتَصَدِّقِينَ وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّانِمِينَ وَالصَّانِمَاتِ وَالْحَافِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ  
وَالذَّاكِرِينَ اللَّهُ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ} (الأحزاب: 35)

“Na wanaotoa sadaqa wanaume na wanoqtoa sadaqa wanawake na wanafunga wanaume na wanaofunga wanawake na wanahifadhi tupu zao wanaume na wanaohiofadhi tupu zao wanawake na wanaomkumbuka Allah wanaume na wanaomkumbuka Allah wanawake” (Al-Ahzab 35) Na zisizo kua hizo zilizopokewa kwa sura ya kivitenda na kwa sura kijumla klatika zama za Mtume (saaw) na katika zama zote za Uislamu.

Ama jumla ya dalili kuzifuatilia tutapata kua mteremsha sharia hakubali ushahidi wa wanawake katika uhalifu (jinayat) kwa sabauhaishi sehemu inapokithiri uhalifu na kua amefaradhisha mwanamke kuvalaa jilbabu wakati anapotaka kutoka nje ya nyumba na kufanya mwanamke yeye mzima ni aura isipokua uso wake na viganja vya mkono yake kwa wasiokua mahrim wake na kuharamishwa juu ya wanaume kuangalia aura yake (mwanamke) hata nyele zake na kukatazwa mwanamke kusafiri hata kama ni haji bila ya mahram wake na tuna kuta mteremsha sharia ameharamisha kuingia katika majumba illa kwa ruhusa na tunakuta haikufaradhishwa juu ya mwanamke swala ya jamaa wala swala ya jumaa wala jihad na yakafaradhishwa juu ya wanaume, na tunakutaa amewajibishwa juu ya mwanamke. Yote haya yaliku wakati wa Mtume saaw na

alitenganisha wanaume na wanawake na akafanya safu za wanawake katika misiki na katika swala nyuma ya saffu za wanaume na wakati wa kutoka mwanzo na baadae wanaume ili watengane wanawake na wanaume. Na katika kufundisha kwake saaw katika msiki na wanawake walisema kumuambia yeye, ewe mtume wa Allah wanaume waekua wengi kwako basi tuwekee sisi siku maalum. Kwa hivyo hukm hizi na hali na mifano yake zinaonesha katika ujumla wake juu ya mwedno wa maisha ya kiislamu na kua ni maisha hayo hutenganishwa wanume na wanawake na kutenganishwa huku kati ya wanaume na wanawake imekuja ni jumla (ammah) hamna tofauti katika hayo kati ya maisha khasa na maisha ammah. Kwani maisha ya kiislamu katika zama za Mtume saaw aliwatenganisha wanaume na wanawake kabisa katika maisha khasa na katika maisha ammah sawasawa. Na wala haziviliwi katika hayo ila yale yaliokuja na mteremsha sharia kwa kuruhusu kukutana katika maisha khasa au katika maisha ammah. Na mteremsha sheria ameruhusu mwanamke kuuza na kununua na kupokea na kutoa na akamfaradhisha juu yake hijja na akamruhusu kuhudhuria swala ya jamaa, na kupigana jihad na makafiri na kumiliki na kukuza mali yake na mengineo katika hayo alioruhusiwa. Kwa hivyo vitendo hivyo ambavyo mteremsha sharia amemruhusu mwanamke au amemfaradhishia juu yake hutizamwa iwapo kutekeleza kwake itabidi kukutana na wanaume itafaa wakati huo kukutana katika mipaka ya hukmu ya mteremsha sharia na katika mipaka ya kazi ambayo ameruhusiwa yeye nayo ni kama kuuza na kununua na kuajiri na illimu na matibabu na uuguzi na ukulima na usanii kama hayo. Kwa sababu dalili ya kumruhusu yeye au kumlazimisha yeye inajumulisha kuruhusiwa kujumuika kwa ajili yake na iwapo katika utekelezajiwake haihitaji kujumuika na wanaume kama kutembea barabarani kuenda msikitiniau sokoni au kutembelea jamii au matembezi au kama kula mwanamke na mwanamume katika hali hizi kwa sababu dalili ya kutenganisha wanaume na wanawake. Ni jumla amm na haikupokewa dalili ya kuruhusu kujumuika kati ya wanaume na wanawake Kwa mfano wa mabo hayo na sio katika yale ambayo mteremsha sharii aliquoruhusu kuyatekeleza kwa hivyo

kujumuika katika mfano wa mambo haya ni dhambi hata lau kama ni katika maisha jumla ammah kwa hivyo kutamganisha wanaume na wanawake Katika maisha ya kiislamu ni faradhi. Na kutengana huku katika maisha khasa inakua ni kutenganisha kikamilifu illa yaliovuliwa na mteremsha sheria ama katika maisha ammah kwa asli ya wanaume na wanawake ila yaliokuja na mteremsha sharia katika kuruhusu au kumlazimisha au kumpendekezea (mandub) mwanamke na utekelezaji wake inabidi kujumuika na wanume ni sawa kujumuika huku na kuwepo kuchanganyikana kama katika ibada ya hajj na kuuza na kununua.

### **KUMTIZAMA MWANAMKE**

Yeyote anaetaka kuoa mke basi inafaa kwake kumtizama bila ya kukaa Faragha nae, imesimuliwa na Tabir amesema: amesema mtume (saaw) “akiposa mmoja wenu mwanamke iwapo ataweba kuangalia kitakacho mvutia kumuoa basi afanye akasema: nikaposa mwanamke na ikawa nikijificha kumchungulia mpaka nikaona kutoka kwake kinachonivutia kumuoa yeye na nikamuoa na hamna makosa kumwangalia kwa ruhusa yake na billa ya ruhusa yake, kwa sababu mtume (ssw) alituamrisha kumuangalia kabisa (Mutlaq). Na katika hadithi ya Jabir iliotangulia na nilikua nikijificha kumchungulia”.

Isipokuwa haifai kuwa faragha naye kwa sababu mtume (saaw) alisema yoyote anaemuamini Allah na siku ya mwisho na asiwe faragha na mwanamke aliye mahram wake kwani watatu wao ni shetani “na hii ni ujumla (amm) na haikuvuliwa chochote kwani anayetaka kuposa kama vile kuvuliwa katika kuangalia. Na inafaa kuangalia sura na viganja vya mikono ya visivyokuwa hivyo. Kwa sababu kuangalia sura na viganja vya mikono na jumla (amm) imekusanya anaeposa na mwengine, kwa hivyo haimaanishi kuvuliwa kwa anyeposa, kwa hivyo yaonesha kuwa kuvuliwa imejengwa zaidi ya uso na viganja vya mikono kwa sababu mtume (saaw) amesema “kumwangalia” ni jumla inakusanya kutazama uso na vignaja vya mikono na visivyo

kuwa hivyo viwili, katika vinanavotazimisha kumjua yeye kwa lengo la kumjua kwa ajili ya kumuoa ili ampose.

Na pia Allah (swt) ameamrisha waumini kuinamisha macho yao, na kuinamisha macho yalazimu kutomwangalia mwanamume kwa mwanamke na mwanmke kwa mwanamume, na ikaja hadithi ya Jabir inayomruhusu aneposa kumuangalia mwanmke kwa hivyo itakua imevuliwa na kuinamisha macho yaani ni wajibu juu ya waumini kuinamisha macho yao ila wanaposa kwani wao kutotunga macho ili waangalie wanaowataka kuwaposa katika wanawake.

Na inaruhusiwa kwa walioana wawili kutizama mwili wote wa mwenzake kulingana alioyapokea Bahz bin Hakim kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake amesema; “Nilisema ewe mjumbe wa Allah ni kipi katika tupu zetu tufiche na ni kipi tuoneshe?” Akaniambia mimi hifadhi tupu yako ila kwa mkeo, au wale ulio wamiliki na mkono wako wa kulia (Mtumwa)

Na inajuzu kwa mwanamume kuwaangalia ambao ni mahram wake waislamu na wasiokua waislamu zaidi ya uso na viganja vya mikono katika viungo ambavyo ni sehemu ya mapambo bila ya mipaka ye yote katika viungo vyake. Kwa kuwepo kwa nass akatika bayo na nass kuiacha wazi. Amesema Allah (swt):

{... وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعْوَلَتَهُنَّ أَوْ آيَاءٍ بُعْوَلَتَهُنَّ أَوْ أَبْنَاءٍ  
بُعْوَلَتَهُنَّ أَوْ إِخْوَانَهُنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانَهُنَّ أَوْ بَنِي أَخْوَاتَهُنَّ أَوْ نِسَاءَهُنَّ أَوْ مَا مَلَكُ  
أَيْمَانُهُنَّ أَوْ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولَئِي الْإِرْبَةِ مِنْ الرِّجَالِ أَوْ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهِرُوا عَلَى  
عَوْرَاتِ النِّسَاءِ}.(النور: 31)

“Na wasidhahirishe mapambo yao ila kwa waume zao au baba zao au baba wa waume zao au watoto wao au watoto wa waume wao au ndugu zao au watoto wa ndugu zao au watoto wa dada zao au wanawake wenzao au walio milikiwa na mikono yao ya kulia au wale wasio na matamanio ya wanawake katika wanaume au watoto ambao hajaelewa tupu za wanawake”(Nur-31) kwa hivyo hawa wote wanaruhusiwa kuangalia kwa mwanamke nywele zake au shingo yake na sehemu za bangili au

mkufu au miundi yake au visivyo kuwa hivyo katika viungo ambavyo huchukuliwa ni sehemu za mapambo. Kwa sababu Allah (swt) anasema “wale wasidhihirishe kuwa hao waliaotajwa na Quran, kwao inajusu kuangalia vinavyodhiri wakati anapovaa nguo za nyumbani yaani anapokuwa na nguo za nyumbani. Amepokea shafii katika musuod yake amepokea kutoka kwa Zainab Binti Abi Salamu. “Yeye alinyonya kwa asman mke wa Subeir, akasema ikawa namuona kama babangu na alikua akiingia chumbani kwangu na nilikuwa nikichana nywele na alikuwa akishika baadhi ya nywele zangu na akisema; nilekee mimi. “Na imepokewa kuwa Abo sufiani aliingia chumbani kwa binti yake Umm Habiba mke wa Mtume (saaw) wakati alipokuwa madina ili kuufanya upya mkataba wa hudaibiyah, nikakunja tandiko la mtume (saaw) ili asipate kulikalia, na asijisitiri naye, na akamwelezea mtume (saaw) na akalikubali, na asimuamrishe ajisitiri naye, pamoja ba nwanva bu mshiriki lakini ni mahram.

Ama wasiokua mahram na wasioposa na mume hutizamwa, iwapo kuna haja ya kutizama iwe ni mwanamume kumtizama kwanamke au mwanamke kumtizama mwanamume hiyo yafaa (mubah) kwake kuangalia viungo ambavyo ni dharura tu. Na asiangalie kisichokuwa uso na viganja vya mikono, na wala ambao hawana budi kuangalia zaidi ya viungo ambavyo wameruhusiwa na mteremsah sheria nao ni kama daktari, na muuguzi na mchunguzi na mfano wake kwa wale ambao hawana budi kutizama katika Quran na mengineo, kwani imepokewa “kuwa mtume (saaw) alipotawatisha saad kwa bani qureidhah alikuwa akiwavulisha vikoi vyao”. Na imepokewa kutoka kwa Athman kuwa aliletewa mtoto ambaye aliiba akasema; (mwangalieni chini kikoi chake wakakuta bado hajaota nywele kwa hivyo hakumkata mkono) na kilikuwa kitendo hicho cha Athman kilionekana na kusikiwa na maswahaba na hakuna yejote aliemkanya.

Ama iwapo hamna haja na asiwe katika mahram katika wale ambao hawana matamanio ya mwanamke, kwake yeye inafaa tu

kuangalia uso wa mwanamke na viganja vyake vyakimikono, na ni haramu juu yake kuangalia visivyokuwa hivyo impokewa na Aisha, kuwa Asma Binti Abi Bakar alikwenda kwa mtume (saaw) akiwa amevaa nguo nyembamba, akamgeuzia mgongo mtume (saaw) naakasema; “Ewe Asma hakika mwanamke anapobaleghe haifai kwake kuonekana ila hii na hii, na akaashiria uso wake na viganja vyake vyakimikono”. Na Allah (swt) ameyavua hayo katika Quran uso na viganja vyakimikono katika kukataza kudhihirisha yale ambayo amesema Allah (swt):

{ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا } (النور: 31)

“*Na wasidhahirishe mapambo yao ila yaliodhahiri*” (Nur-31) amesema Ibn Abbas; (uso na viganja kwa mwanamke kukatazwa kudhihirisha tupu (Aurah) na kua kukatazwa kwake yaonesha kwa njia ya kujilazimisha yuu ya kukatazwa kuangalia kile ambacho amekatazwa mwanamke kukidhihiisha na kuvuliwa katika vilivyo dhihiri katika vilivyo katakزوا. Kuvidhihirisha ni kuvuliwa katika uharamu wa kuviangalia yaani kuruhusiwa kuviangalia, kwa hivyo mwanmume ajnabi kuangalia uso wa mwanamke ajnabi na viganja vyake vyakimikono, ni mwangalio wa kumuezeshakumjua kwa kacho yake na atoe ushahidi juu yake itakapobidi kuutoa, na apate kmregelea atakapoamiliana naye katika kuuza au kuajiri na apate kumtambua iwapo atamkopesha au kumlipa yeye deni au atakapomfnanisha yeye na mwanake mwengine au yanaofana na hayo. Na vilevile inafaa kwa mwanamke kumtizama mwanamume kile kisicho Quran katika mwanamume. Kwa yale yaliopokewa kutoka kwa Aisha amesema Alikuwa mtume (saaw) akinificha na shuka yake na mimi nikitizama mababashi wanacheza msikitini na siku ya Idd mtume (saaw) alipomalizakhutba ya Idd “alikwenda mpaka kwa wanawake na akawatolea mawaidha na pamoja naye aliкуwa Bilal na akawaamrisha kutoa sadaqah na hili liko wazi katika kukubali kwa mtume (saaw) kwa kuwaruhusu kuangalia wanaume. Ama asli ya kuangalia kile ambacho sio Quran ni muangalio wa Aisha kwa mahabashi wakicheza. Yaonesha juu ya kuwa aliкуwa akiangalia yale yote yaliokuwa yanadhihirika isipokuwa aurah. Kwa hivyo haikufungika kutizama hali

ilikuwa ni wazi kabisa. Na kwa sababu Amri Vin Shiaib anepokea kutoka kwa babake kuoka kwa babu yake amesema; amesema mtume (saaw) atakapomwezesha moja wenu mtumishi wake mtumwa wake au muajiriwawake basi naasitazame chini ya kitovu na juu ya magoti kwani ni Aurah, “ na yafahamika ruhusa ya kuangalia visivyokua hivyo, na ruhusa ipo wai kabisa inakusanya mwanamume na mwanamke. Ama yale yaliopokewa kutoka kwa Umm salamah amesema “nilikuwa nimeketi kwa mtume (saaw) mimi na yafwah akaomba ruhusa Ibn Maktum, akasema mtume (saaw) mujistiri naye, nikasema: ewe mtume wa Allah (swt) yeye ni kipofu hawezi kuona akasema: je na nyinyi ni vipofu na hamumuoni yeye? Hadithi hii imipokewa na Abu Daud na wengineo katika riwaya za Nabhau amesema aAn-nasai: hatujui alieipokea kutoka kwa Alabtan ila Zuhri, na akasema ibn Abdul Bar: Nahbjan hajulikani na hamna mapokezi kutoka kwake yanaojulikana isipoluwa hadithi hii inaojulikana na Zuhri pekee. Na hadithi isiojulikana ni Dhaifu na wala haijukuliwi ni hunna. Ama kile kilichopokewa kutoka kwa Jarir Bin Abdallah amesema; Nilimuuliza mtume (saaw) mwaangalio wa ghfla (fujjah) na akaniamrisha nigeuze macho yangu. Na yale yalio pokewa kutoka kwa Ali (raa) amesema; ameniambia mimi mtume (saaw) “usiandamanishe mtazamo kwa mtazamo wako ni wa kwanza na sio wa pili” kwa sababu katika hjambo la mwanamume kumuangalia mwanamke na sio katika suala la mwanamke kumtizama mwanamume. Na makusudio ya hadithi ya kwanza ni kuangalia visivyokuwa uso na viganja kwa dalili ya kufaa kuangalia kwake. Na katika hadithi ya pili ni kukatazwa kuendelea kuangalia ambayo itasababisha sholiwa na wala sio kukatazwa kuangalia tu.

Ama neno lake Allah (S.W.T):

{ قُلْ لِلّٰمُؤْمِنِينَ يَغْضُوَا مِنْ أَبْصَارِهِمْ } (النور: 30)

*“waambie waumini wanaume wainamishe macho yao”* muradi wake ni kuinamisha macho kwa yale ya haramu, na kufungika juu ya halali, wala sio kuinamisha macho kabisa, kwa dalili kuwa mteremsha sharia amefafanua kuwa maharim sio makosa

kuangalia, nywelw na miguu yao, na mwanamke ajnabi kuangaliwa uso wake na viganja vyake. Na neno ghadh Al-hasar ni kuinamisha macho amesema katika kamusi: (Ghadh – ni kugeuza).

Kwa hivyo yabainika kutokana nahayo yafaa kuangalia kwa wanaume na wanawake kila moja katika yao yale ambayo ni kati ya kitovu chake na magoti yake na uchi wa mwanamke ni mwili wake wote, isipokuwa uso wake na viganja vyake kwa hivyo shingo yake ni aurah, na nywele zake hata unywele mkona ni aurah, na uhav wa kichwa chake . Ubavu wowote ni aurah, kwa hivyo yeye mzima ni aurah isipokuwa uso wake na viganja vyake, ni aurah ni wajibu kusitiri, na dalili juu ya hayo neno la Allah (swt)

... وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا... } (النور: 31)

“*Na wala wasidhihirishe mapambo yao ila yaliодhihiri* (nur-31) na yaliодhihiri ni uso na viganja vya mikono, kwa sababu hivi ndivyo vilivyokuwa vikidhihirikatika wanawake aislamu mbele ya mtume (saaw) na akanyamazia hayo. Na kwa sababu viwili hivi ndivyo hudhihiri katika ibadah kama katika hijjah na swalah, na kwa sababu viwili hivi ndivyo vilivyokuwa vikidhihiri kikawaida katika zoma za mtume (saaw) yaani zoma za kushuka aya (Quran). Na dalili nyengine juu ya uchi wa mwanamke ni mwili wake wote isipokuwa uso wake na viganja vyake ni qauli yake (saaw). Anapo haleghe mwanamke haifai kwake kudhihirisha ila uso wake na ila zaidi ya hapa na akashika kiganja chake, na akawacha baina ya aliposhika na utumbo wa mkono mfano wa mshiko mwengine. Na akamuambia Asmaa bin Abi Bakr “Ewe Asmaa, mwanamke anapo baleghe haifai kwake kuonekana ila hii na hii na akaashiria uso wake na viganja vyake”. Kwa hivyo dalili hizi wazi kuwa mwili mzima wa mwanamke ni aurah isipokuwa uso wke na viganja vyake na kuwa ni wajibu juu ya mwanamke kusitiri uchi wake yaani kusitiri mwili wake wote isipoluwa uso wake na viganja vyake.

Ama kile aakachojsitiria nacho, kwani mteremsha sharia hakueleza vazi maalum la kusitiri aurah bali aliiachia hayo bila ya kuifungua kwa qauli “na yasidhihiri kwake yaani kutodhihirisha aurah na wasidhihirishe”, haifai kwake kudhihirisha”. Haifai kwake kuonekana kwa hivyo vazi lolote litakalo sitiri mwili wake wote isipokua uso wake na viganja vyake huzingatiwa ni sitara vovote itakavyo kuwa muundo wake, kwa hivyo nguo ndefu ni sitara na surwali ni sitara, na skati ni sitara na soksi ni sitara, kwa hivyo muundo wa vazi haukuelezwa na mteremsha sharia, kwa hivyo vazi lolote litakalositiri aurah yaani haidhihiriki kwake aurah huzingatiwa na sharia kwani sitara ya uchi, bila ya kuangalia muundo wake aina yake na idadi ya vipande vyake.

Isipokuwa mteremsha sharia ameshurutisha katika vazi liwe linasitiri ngozo, kwani amefaradhisha vazi ambalo litasitiri rangi ya ngozo, yaani linasitiri ngozi; na kile ambacho kiko juu yake katika rangi kama ni nyeupe aur nyekundu au nyeusi. Mifano yake yaani ni wajibu liwe vazi lenye kusitiri ngoi na yenye kusitiri rangi yake kwa namna ambayo haitajulikana uweupe wake katika uwekundu wake katika ukunde wake, na iwapo haitakuwa hibyo basi hazingatiwi ni sitara ya aurah, na iwapo itakuwa ni nguo nyebamba inaodhihirisha rangi ya ngozi na ijulikane uweupe wake au uekundu wake au ukunde wake hiyo haifai kuwa ni sitara ya aurah na hazingatiwi ni aurah kwa kudhihirisha kwake na isio sitiri, kwa sababu sitara haikamiliki kisheria ila kwa kusitiri ngozi kwa kusitiri rangi yake. Na dalili ni kuwa mteremsha sharia amefaradhisha kusitiri ngozi kwa kusitiri ngozi kwa namna ambayo haitajulikana rangi yake kama vile imepokewa na Aisha (raa), Ameipokea kwa Asmaa bin Abi Bake aliingia kwa mtume (saaw) na nguo nyembamba na akasema “ewe Asmaa hakika mwanamke anapo haleghe haifai kwake kuonekana ila hii na hii. Kwa hivyo (saaw) aliifanya nguo nyembamba sio ya sitara ya aurah na akaifanya ni yenye kuumbua aurah yake na kumpa mgongo and kumuamrisha kujisitiri, yaani kucaa nguo inaositiri. Na dalili juu ya hayo pia ni kama ilivyokuja katika hadithi ya Usama, wakati ye

alipomuuliza kuhusu qibtiyyah (aina ya nguo) na akamjibu yeye usoma kuwa yeye alimvisha mkewe, mtume (saaw) akamwambia “muamrishe avae ghilalah (kirinda) chini yake kwani naogopea kuwa itanesha umbile la fupa lake “ kwa sababu Qibtiyyah ni nguo nyembamba, na alipojua mtume (saaw) kuwa usoma amemvisha mkewe alimuamrisha amvishe chini ya nguo ili isibaiike ngozi yake nyuma ya Qibtiyyah na akamuambia yeye “muamrishe avae chini yake ghilalah (kirinda) kisha akaifanyia ila kwa neno lake kwani mimi naogopea kuwa itaonesha fupa lake”, yaani kama kioo inavyonyesha kilichoko nyuma yake, yaani naogopea kuwa itabanisha kwa rangi ya ngozi yake. Yaani kudhihirisha ngozi yake kwa sababu qauli yake “Tasif” ina maana ya kuelezea kudhihirisha kulichoko nyuma yake yaani kubainisha kilichoko nyuma yake, kwa hivyo qauli yake yasifu yatokamana na wasaf na wast (kubainisha heiwi ila kwa kudhihirisha kilichoko nyuma yake na sio tashkita (umbo) kwa kilichoko nyuma yake na akasema tasif na hakusema tashakil, yaani naogopea haelezea kilichoko nyuna yake kaktika fupa lake, nao ni rangi yake na sio umbo lake. Kwa hivyo hadithi hizi mbili ni dalili wazi kuwa mteremsha sharia amelazimisha kile kitakacho sitiri aurah kiwe ni chaenye kusitiri ngozi na kibainishe kilichoko nyuma yake, kwa hivyo ni wajibu juu ya mwanamke kuvaan kinachositiri aurah na nguo isiwe nyembamba yaani hailezi kilichoko nyuma yake na haibainishi kilichoko chini yake.

Hayo ni maudhui kuhusiana na kusitiri aurah, na maudhui hayo haifai kuchanganya na vazi la mwanamke katika maisha ya hadharani, wala taharuuj na baadhi ya mavazi, kwa hivyo iwapo kuna vazi linalositiri aurah kuivaa akiwa natedmbea hadharani, kwa sababu kuna nguo maalum za barabara amm ambayo imeelexewa na mteremsha shariam na wala haitoshi kuwa ni yenye kusitiri aurah, kwa hivyo surwali hata kama inasitiri aurah lakini haifai kuvaan katika maisha amm, yaani haifai kuvaliwa katika mabarabara amm, kwa sababu kuna mavazi maalum za kuvaan katika baraba amm ambao mteremsha sharia amezifaradhisha kuziva, kwa hibyo akihalifu amri ya mteremsha

sharia na akavaa nguo kinyume na vile ambavyo mteremsha sharia alivyoelezea atapata madhambi kwa sababu amewacha wajibu, kwa hivyo haifai kuchanganywa maudhui ya kusitir aurah ka maudhui ya vazi la mwanamke katika maisha ammah. Vile vile haifai kuchanganywa maudhui ya kusitiri aurah na maudhui ya tabarajj. Kwa ashi ya surwali inasitiri aurah iwapo haitakuwa nyembamba lakini haimanishi aivae mbele ya wanaume ajnabi kwa kuwa kuva a kwide anadhihirisha uzuri wake na kudhihirisha mapambo yake, na hata ni yenye kusitiri aurah lakini wakati huo atakuwa amejipamba (Tabarujj) na tabarruj imekatazwa na mteremsha sharia, hata kwa kama mwanamke ni mwenye kusitiri aurah, lakini haimaanishi kuwa inasitiri aurah na kufanywa kinachositiri aurah na kuwa haimfanyi yeye amejipambap (tabaruj). Kwa hivyo haifai ya kuchanganya maudhui ya kusitiri aurah na maudhui ya kuipamba (tabarruj) kwani kila maudhi ni tafauti na nyengine.

Ama vazi la mwanamke katika Maisha ya hadharani, yaani vazi lake katika barabara amm katika kasoko, mteremsha sharia amefaradhisha juu ya mwanamke awe na vazi atakalovaa juu ya nguo yake wakati anapotoka kwenda masokoni au katika matembezi katika mabarabarani, kwa hivyo amemfaradhishia yeye awe milaatun au milhafah (buibui) atalivaa juu ya nguo zake na kuitiririsha mpaka chini mpaki ifunike nyayo zake, na iwapo hana nguo (buibui) ataazima kwa jirani yake au rafiki yake au jamaa yake Vazi la juu, haina budi yeye awe wa Khimar (kitambara cha kichwa) au mfano wake au nguo yoyote itakayofanya kazi ya kufinika kichwa kizima, na shingo yote, na ufunuo wa guo juu ya kifua, na hiyo iwe tayari wakati anapotoka kutoka kwenda masokono, au kutembea katika mabarabara Amm, yaani vazi la juu katika maisha amah; kwa hiyo ikiwa yeye anayo mvazi haya mawili inafaa kwake kutoka katika nyumba yake kwenda masokoni au kutembea barabarani, yaani katika maisha Amm, na iwapo yeye hana mavazi hayo mawili haifai kwake kutoka kwa namna yoyote ile, kwa sababu amri ya mavazi haya mawili imkuja amm na itabakia hivyo

katika hali zote kwa sababu haikupokewa kufanyiwa khasa (takhsis) kabisa.

Ama dalili ya uwajibu wa mavazi haya mawili katika maisha amah ni wano lake Allah (s.w.t.) kuhusiana na vazi kuanzia juu:

{ وَلَيَضْرِبَنَّ بُخْمُرِهِنَّ عَلَى جُبُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهِنَّ إِلَّا لِبُعْوَلَتَهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعْوَلَتَهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعْوَلَتَهِنَّ...} (النور: 31)

“Na watandaze Khimar zao juu ya vifua vyao na wala wasidhihirishe mapambo yao illa kwa waume zao au baba zao au baba wa waume zao” (Nur-31) na kuhusiana na vazi la chini ni kauli yake Allah (s.w.t):

{ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَا زَوْاجٌ لَكَ وَبَنَاتٍكَ وَنِسَاءٍ الْمُؤْمِنِينَ يُذْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَابِيبِهِنَّ }  
(الأحزاب: 59)

“Ewe mtume waambie wake zako na mabanati zako wa wake wa waumini waniginize juu ya majilbab (buibui)” (Al-ahzab - 59) na yale aliopokea Umm Atiya amesema:”Alituamrisha mtume (s.a.a.w) ikiwa mmoja wetu hana Jalbab akasema: avue jalbab la dadake “kwa hivyo dalili hizi ni wazi katika kuonesha juu ya vazi la mwanamke katika maisha amma. Kwa hivyo Allah (s.wt) amelezea katika aya hizi mbili mavazi haya mawili ambayo amemfaradhishia mwanamke kulivaa katika misha Ammah na kuelezea kiundoni, kikamilifikijumla, na akasema kuhusiana na vazi la wanawake la juu

{... وَلَيَضْرِبَنَّ بُخْمُرِهِنَّ عَلَى جُبُوبِهِنَّ...} (النور: 31)

“Na watandaze khimari zao ya vifua vyao” (Nur-31) yaani watandaze khimar vichwani mwao, juu ya mashingo yao n avifuani mwao ili wafiche yanaodhihiri sehemu za ufunuo kanzu na ufunuo wa nguo katika shingo na vifua. Na akasema kuhusiana na vazi la wanawake la chini:

{ يُذْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَابِيبِهِنَّ...} (الأحزاب: 59)

“Waniginize juu yao majalbab yao” yaani wasitiri mavazi yao wanaoyakaa na wavae juu yake kwa ajili ya kutaka sitara watakaoivaa mpaka chini (mulat na milnafah), na akasema kuhusiana na namna ambayo itakua vazi hili:

.. وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا... } (النور: 31)

“Na wasioneshe mapambo yao illa yaliодhihiri” (Nur-31) yaani wasidhihirishe sehemu za mapambo katika viungo vyao kama masikio n avisivyokua hivyo illa yale yaliokua yakionekanwa katika maisha amah wakati wa kuteremka aya yaani katika zama za mtume (saaw) nao ni uso na viganja vya mikono. Na maelezo haya ya kindani yafahamika kwa uwazi ni yapi yale ambayo ni wajibu juu yake, na ikaja hadithi ya Umm Atiya na ikabainisha kwa uwazi uwajibu wa kua na vazi atakalovaa juu ya nuguo zake anapotaka kutoka, wakati aliposema kumuambia mtume (saaww) “Iwapo mmoja wetu hana jalbab” na Mtume (saaw) akamuambia “avae jalbab la dadake “yaani aliposema kumwambia Mtume (saaw) alumumrisha aazime nguo ya dadake ambayo ataivaa juu ya nguo yake, kwa maana nyengine asipoazima basi haifai kwake kutoka, nah ii inatilia nguvu (Qarinah) kua amri katika hadithi hii juu ya uwajibu wake, yaani ni wajibu mwanamke kuvali juu ya nguo yake anapotaka kutoka na asipovaa asitoke kutoka.

Na imeshurutishwa katika jalbab iwe inatiririka mpaka chini mpaka ifinike nyayo mbili, kwa sababu anasema Allah (s.w.t) katika aya “watiririshe juu ya jilbab zao” yaani watirishe jilbab zao kwa sababu (min) hapa sio ya usehemu bali ni ya kufafanua, yaani watiririshe sitara (mulat na mikafah) mpaka chini, na kwa sababu imepokewa kutoka Ibn umar kua amesema amesema Mtume (saaw) “Yoyote atakaetirisha nguo yake kwa kiburi Allah hatamuangalia yeye siku ya Qiyama, akasema umm Salama vipa wafanye wanawake kwa inaotirika, akasema: watiririshe shibiri (mwanzo wa vidole mpaka panapovaliwa saa) akasema: basi itaonekana nyayo zao, akasema: watiririshe dhiraa na wazidishe” hii iko wazi kua nguo ambayo atavaa juu ya nguo – (mulat na milhafan) buibui itiririke mpaka chini na mpaka isitiri nyayo zake, na iwapo zimesitirika nyayo zake kwa kuvali soksi au viatu hiyo haimaanishi kua itachukua nafasi ya kutiririsha mpaka chini na hamna haja ya kutiririsha, kwa sababu nyayo zake zimesitirika, lakini hamna budi kuwepo na jalbab ilwe linatiririka mpaka chini kwa wazi kwani ndio nguo

ya maisha ammal ambayo ni wajibu juu ya mwanamke kuvaan  
katika maisha ammah, na iwe wazi kutiririka, yaani ipatikane  
kitendo cha gauli yake Allah (swt)

{يُذْنِينَ.} (الأحزاب: 59)

“*watiririshe*” yaani watiririshe.

Na kwa haya yabainika kua ni wajibu kwa mwanamke kua  
na nguo pana atakaoivaaa juu ya nguo yake ili atoke nayo, na  
iwapo hana nguo na akataka kutoka ni juu ya aazime kwa  
dadake, yaani mwanamke Muslam atakemuazima katika nguo  
yake ambayo ataivaa juu ya nguo zake, na akikosa  
atakaemuzima basi asitoke mpaka apate nguo atakaoivaa juu ya  
nguo yake, na akitoka na nguo (za nyumbani) bila ya kuvaan  
nguo pana inaotiririka mpaka chini ya nguo yake basi atapata  
madhambi, hata lau kama amesitiri auvah yote, kwa sababu vazi  
pana linalotiririka mpaka chini mpaka kwenye uyayo mbili ni  
faradhi, atakua amekwenda kinyume na faradhi, atapata  
madhambi mbele ya Allah (Swt) na kuadhibiwa kwa upande  
wa serikali adhabu ya kuazirishwa (Taa’zeer).

Yamebakia masuala mawili katika masual ya mwanamke  
kumtazama mwanamume na mwanamume kumtizama  
mwanamke, mmoja wapo ni suala la kuwepo kwa wanaume  
ajnabi katika majumba kwa ruhusa ya wenyewe, na kuwangaalia  
wanawake wakiwa wamevaa nguo za nyumbani, kuona kwao  
baadhi ya viungo vya mwanamke zaidi ya uso na viganja viwili.  
Na la pili suala la kuwepo wanawake waiokua waislamu na hata  
baadhi ya wanawake waislamu katika mabarabara za miji, na  
wao wanadhihirisha baadhi ya vioungo vyao zaidi ya uso wa  
viganja viwili. Na masuala haya mawili yapo kivitendo na  
uhakika wa balaa zake kwa wasilamu wote, basi hamna budi  
kufafanua Huumu ya Allah (swt) kuhusiana na hayo.

Ama suala la kwanza ni kua kuna ndugu wa kiume au jamaa  
wanaoishi pamoja katika nyumba moja, na wanadhihirisha  
wanawake killa mmoja kati yao kwa mwengine nguo za  
nyumbani, na anaonesha nywele zake na shingo yake na mikono

yake na miundi yake na mifano yake katika yale yanaoonekana kwa nguo za nyumbani. Na kumuangalia yeye mashemegi zake au jamaa zake wasio mahram kama wanavomuanglia ndugu yake na babake na wasiokua hao katika mahram pamoja na kwamba shemegi yake ni ajnabi kwake kama ajnabi yoyote. Na vile vile huenda wakazuru jamaa zao wenyewe kwa wenyewe, kama watoto wa ammi na watoto wa mjomba au mifano yao katika familia wasio mahram, na kuwasalimia wanawake na wanakaa pamoja nao, na wao wakiwa katika nguo za nyumbani, na kudhihirika kwao zaidi ya uso na viganja viwili, nywele, na shingo na mikono, na miundi na vengineo, na kuamiliana na kwa muamala wa mahram. Na suala hili limeenea na waislamu wengi wameonjwa nayo na zaidi katika miji, na wengi wanadhnia kua hayo yanaruhuswa, na kukm katika hayo ni kua Allah (swt) ameharamisha kabisa kuangaliwa mwanamke kwa matamanio na kasha kuvua mapambo yaani kuanglia kwa watu aina kumi na mbili wakiwemo kama mfano wa ma'ami na wajomba, kisha kuvua katika mwanamke uso na viganja viwili kwa wanaume wote, kwa hivyo matamanio yaani kuangalia kwa matamanio ni haramu moja kwa moja illa kwa mume, na kuangalia uso na viganja viwili kwa kuangalia tu ni mubala kabisa, na kuangalia zaidi ya uso na viganja viwili ni haramu wazi illa kwa mahram ambao Allah (S.w.t) amewataja na wale ambao ni mfano wao.

Hii ni hukm sharii kuhusiana na maisha amah kama ilivyokuja katika nusus (Quran na sunnah). Ama kuhusiana na maisha ya binafsi (khasa), mteremsha sheria amemruhusu mwanamke kudhihirisha zaidi ya uso wa viganja viwili vile vinavyodhihiri kikawaida, amesema Allah (swt):

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِيَسْتَأْنِفُوكُمُ الَّذِينَ مَلَكُوتُ أَيْمَانِكُمْ وَالَّذِينَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلْمَ مِنْكُمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ مِّنْ قَبْلِ صَلَةِ الْفَجْرِ وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِّنْ الظَّهِيرَةِ وَمِنْ بَعْدِ صَلَةِ الْعِشَاءِ }  
{ النور: 58 }

*“Enyi mulioamini na waombe ruhusa wale ambao mumewamiliki (watumwa) na wale ambao hawaja baleghe katika nyinyi mata tatu, kabla ya swala ya Alfajiri, na wakati*

*munapo badilisha mavazi wakati wa adhuhuri na baada ya swala ya Isha* “(An-nur – 58). Kwa hivyo Allah (S.w.t) amewaamrisha watoto ambao hawaja baleghe na watumwa wassingie kwa mwanamke katika nyakati hizi tatu, na kisha kuwaruhusu wao kuigia katika nyakati zisizo hizi tatu, na akaendeleza kuelezea hayo kwa kauli yake (swt):

﴿ ثَلَاثُ عَوْرَاتٍ لَكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ بَعْدَهُنَّ طَوَّافُونَ عَلَيْكُمْ ﴾ {النور: 58}

“*Nyakati tatu za faragha hamna makosa kutembeleana baada ya hapo*” (Nur-58) na hili lipo wazi kua nyakati zisizo kwa hizi tatu wataingia watoto na watumwa wa wanawake kuingia kwa wanawake bila ya kuomba ruhusa, yaani wakiwa wamevalia nguo za nyumbani katika mavazi ya kawaida, na yafahamika kutokamana nayo kua mwanamke katika nyumba yake ataketi na nguo zake kama kawaida, na kudhihirisha na nguo zake hizi kwa watoto wa watumwa wake. Na kwa hayo inafaa kwa mwnamke kua ndani ya nyumba yake katika nguo zake kama kawaida na hamna shaka katika hilo. Na hatakua anapata madhambi kwa hayo kabisa, na inafaa kuonekanwa katika hali hiyo na watoto wa watumwa wake na wala hamna makosa juu yake kwa hayo, na hamna haja kwake kujisitiri na o na wal hawahitaji ruhusa katika kuingia, na mfano wa watumwa ni watumishi ambao wanatumika katika nyumba hata kama ni wanaume ajnabi, kwa sababu aya imetoa illa (sababu ya kisheria) kuingia mtumwa bila ya kuomba ruhusa kwa sababu wao huingia na kutoka kwa kusema

﴿ ... طَوَّافُونَ عَلَيْكُمْ بَعْضُكُمْ عَلَى بَعْضٍ ... ﴾ {النور: 58}

“*Kuzunguka katika kuhudumiana badhi yenu baadhi nyengine*” yaani wao wanaingia na kutoka kwenu, yaani wakiwazungia nyinyi nah ii ni illa (sababu ya kisheria) iliyopo katika watumwa na ipo kwa watumishi, na killa ambao ni mgano wa, na kwa hivyo mwnamke katika maisha yake khasa sio wajibu juu yake kusitiri zaidi ya uso na mikono, katika vinavyodhishiri kawaida isipokua akiwa uchi au nusu uchi yaani illa katika hali tatu au nyakati tatu.

Ama wasiokua katika wale aliowavua Allah (swt) katika hao yaani wasio watoto na watumwa kwa sababu Allah (swt) amebainisha hokum yao katika maisha khasa, kwa amewataka wao waombe ruhusa amesema (s.w.t):

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْتِسُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا }  
(النور: 27)

“Enyi mulioamini musiingie majumba yasiokua yenu mpaka muombe rurhusa na musalimie wenyewe” (Nur- 27). Kwa akafaradhisha muislamu kuomba ruhusa kwa kueleza na neon Istinaas (kuomba ruhusa) wakati anapotaka kuingia kwa nyumba isiokua yake na mathum yake ni kua anapotaka kuingia katika nyumba yake asiombe ruhusa. Na sababu ya kuteremka (sababu Nuzul) ya ayah hii ni kua mwanamke katika Ansar alisema ewe mtume wa Allah mimi hua katika nyumba yangu katika hali ambayo sipendi nionekanwe na yoyote sio mzazi wala mtoto na babangu huja na kuingia kwangu. Na pia hawachi jamaa zangu wanaingia kwangu na mimi niko katka hali hiyo nifanye nini, na ikateremka aya ya kuomba ruhusa. Kwa hivyo ikipimwa sababu nuzul hii kwa matamshi yake na ufahamu wake yaonesha kua suala kuhusiana na maisha khasa hamna suala la kusitiri qurah na kutositiri aurah. Bali ni suala la kua na nguo za nyumbani anazokua nazo nyumbani, hakuamrishwa mwanamke kutokua katika hali hali hiyo, na hakuamrishwa kujisitiri, bali amewaamrishwa wanau;me kuomba ruhusa katika hali hiyo omaisha khasa na hamna tofauti awe ni mahram au asiekua mahram, wala hamna tofauti kati ya wanawake na wanaume, kwa hivyo baba na Ajnabi ni sawa, na mwanamume na mwanamke ni sawa, na hakucaa katika ho illa watoto na watumwa na watumishi, kwa hayo maisha ya mwanamume na mwanamke na mkewe katika nyumba ambayo kuna mwanamume mwengine au wanawake, hokum yake ni moja kama ya ndugu na baba pamoja ajnabi na mahram ni sawa, kwa hivyo hamna makosa kwa mwanamke kudhinisha katika maisha khasa, na ni juu ya mwanamume kuomba ruhusa anapotaka kuingia katika nyumba isio yake.

Ama mwanamume kumuangalia mwanamke katika hali hii hilo ni jambo jengine linalohusiana na kuangalia iwe ni katika maisha khasa au mengineo, na Allah (s.w.t) ameharamisha kwa wasiokua maharim kuagalia zaidi ya uso wa viganja viwili na kumruhusu hayo mahram, akamuamrisha (ajnabi) kuinamisha macho kwa zaidi y uso na viganja viwili, na kumsamehe kilichoonekanwa bilal ya kulaza jicho, ama haramu ni kuangalia zaidi ya uso na viganja viwili, na kuinamisha macho kwa zaidi ya hayo ni gauli yake (swt):

} قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَعْضُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ { (النور: 30)

“waambie waumini wanaume wainamishe macho yao”(Nur-30). Na mukusudio kwa dalili ya kuruhusiwa kuangalia viwili hivyo. Na katiak Bukhari “amesema Said bin Abil Hassan kumwambia Hassan “Wanawake wasiokua waarabu (ajam) wanadhihirisha vifua vyao na vichwa vyao akasema: (Inamisha macho) na katika hadithi ya kukataza kukaa katika mabarabara amesema: “Inamisha macho” yaani wanawake katika barabara huenda wakawa wanadhihirisha zaidi ya uso na viganja viwili, na kuifanya ni kuangalia kwa kusudi, ama kungalia kwa kutokusudia haikuhamishwa, na hakuamrisha kuwacha bali amearisha kuinamisha macho kwa kusema:

} ... يَعْضُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ ... { (النور: 30)

“Wanaimishe maco ya” (Nur-30) na neno “MIN” ni ya sehemu yaani wainamishe sehemu ya macho yao yaani sehemu ya kuangalia na ufahamu wake ruhusa ya kuangalia kiwa kuinamisha nao ni muangilio wa kawaida usio kusudiwa.

Na kwa hayo inafaa kuishi mtu pamoja na jamaa zake, ni ni sawa katika hayo mahrim na wasiokua maharim yaani baba na ndugu na mtoto wa Ammi, na wala sio makosa kwa mwamke kujitokeza na nguo za kikawaida kwa wanaoishi katika nyumba moja pamoja na mumewe na kakake, na ni juu ya mwanamume anaeishi katika hiyo nyumba kuinamisha macho yake, yaani hamna makosa juu yake kwa muangilio wa kawaida kumuangalia mwanamke akiwa na nguo za kikawaida isipokua katika hali tatu, yaani isipokua hali ambazo zinakua katika hali tatu.

Hayo nikuhusu wanaoishi katika nyumba moja, ama kwa wanaoingia numba kutoka nje wawe ni jamaa au wasiwe jamaa ni sawa wawe ni mahram au wasiwe mahram ni juu yao wote kuomba ruhusa bila ya kubgua. Ama mahram hatajisitiri mwanamke kwa inafaa kwa kuangalia mapambo yaani aurah. Ama wasiokua mahram ni juu ya mwanamke kujisitiri nao yaani asidhirishe mbele yao illa uso na viganja viwili. Na asipofanya haya na akaendelea katika nguo zake za kawaida basi amefanya madhambi, ama kwa mwanamume ni juu yake kuinamisha macho na sio zaidi. Na tofauti ya anaezuru kutoka nje ya nyumba na mkazi wake ni kua mkazi wa nyumba sio juu yake kuomba ruhusa kwa sababu ni nyumba yake, na sio lazima kwa mwanamke kujisitiri kwa sababu ni kwake, na sio lazima kwa mwanamke kujisitiri kwa sababu yuko katika maisha khasa. Ama kwa anaezuru Allah (swt) amemfaradhishia yeye kuomba ruhusa na ni juu ya mwanamke asiwe katika nguo zake za kinyumbani illa akiwa ni mahram wake, yaani ni juu yake kujisitiri kwa dalili ya sababu ya kuteremka aya. Na iwapo ataingia kwake yoyote hana budikuomba ruhusa iwe ni mahram au asiwe mahram, na kuombwa ruhusa ni uwajibu wa kujisitiri kwa askiekua mahram.

Ama suala pili ni tangu uvamizi wa hadhara ya kimaghari na kutawala biladi za waislamu kwa nidhamu za ukafiri wamekua wanawake wasio waislamu kwa nidhamu za ukafiri wamekua wanawake wasio waislamu wanatoka nusu uchi: Wanadhirisha vifua, migongo na nywele na mikono na miundi miwili na wamekua baadhi ya wanawake waislamu wanawaiga na wanatoka kwenda sokoni katika hali hiyo mpaka imekua ni vigumu kwa mtu kutafautisha kati ya mwanamke muislamu na asie muislamu hali ya kua anakweda sokoni au amesimama dukani katika maelewano ya kununua. Na wanaume waislmau wanaoishi katika miji hiyo hivi sasa wameshindwa kuondosha uovu huo, na wala hawawezi kuishi katika miji hiyo bila ya kuona qurah hizo. Kwa sababu hali ambayo wanaoishi na aina ya majumba ambazo wanazo keti yalazimisha kuona

mwanamume aurah ya mwanamke, na haiwezekani kwa mtu yoyote kujiepusha kuona qurah ya wanawake, katka mikono yao na vifua vyao na migongo yao na miundi yao na nyele zao kwa hali yoyote ile atakavo jaribu kugeuza macho isipokua akiwa amekaa katika nyumba yake na kutotoka humo. Na hili haliwezekani kabisa. Kwani yeye anamahitajio ya kuweka mahusiano na watu katika kuuza na kununua na kuajiri na kazi nay ale ambayo ni dharura katika maisha yake. Na hawezi kutekeleza hayoo katika kujiepusha kuona hizi aurah. Na uharamu wa kuangalia hivyo iko wazi katika Qur'an na Sunnah, basi afanye nini? Na kutoka katika matatizo haya inakua kwa namna mbili:-

Ya kwanza: Mtazamo wa ghafla (nadharatul fujjah) ni yale anaoyashuhudia katika barabara na hiyo husamehewa mtazamo wa kwanza na ni makosa juu yake kutizama mara ya pili, kwa yaliopokewa kutoka kwa Jarir bin Abdallah amesema: Nilimuuliza mtume (saaw) kuhusu mtazamo wa ghafla, akaniamrisha nigeuze macho yangu na imepokewa kutoka kwa Ali (raa) amesema: “aliniambia mimi Mtume (saaw) “Usifuutilize mtazamo moja kwa moja kwa mtazamo mwengine utasamehewa wa kwanza na itakua juu yako wa pili”

Ama kwa namna ya pili: ni kuzungumza na mwanamke huyo ambae anadhihirisha kichwa chake na mikono yake na ambayo ni kawaida kwake kudhihirisha. Kwa hivyo huyu ni wajibu kumgeuza macho, na kumuinamisha macho, kwa alioyapokea Abu Daudi: “Fadhl bin Abbas alikua ameandamana na mtume (saaw) akaja mwanamke wa khatha’miyah (kabila) kuuliza maswali, n akawa Fadhi bin Abbas anamuagalia mwanamke na mwanamke anamuangularila Fadhl, Mtume (saaw) akageuza uso wa Fadhl. Na amesema Allah (swt):

﴿قُلْ لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغْضُبُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فِرْوَجَهُمْ﴾ (النور - 30)

“Waambie wauminin wanaume waainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao” (Nur-30) Na Muradi wake ni kuinamisha. Kwa hivyo uislamu umetibu mushkila huu kwa kuinamisha macho kwa upande wa mwanamume pamoja na kudumu

kuendelea kufanya kazi zake ambayo huifanya kwa mazungumzo ya dharura pamoja nae akipanda katika gari lake au kukaa katika balkoni yake kwa sababu ya joto jingi au mifano yake. Kwani ni katika mahitaji ya dharura ya maisha amah kwa mwanamume na wala hawezi kujiepusha na mtihani huu wa kudhihirisha aurah, basi ni juu yake kuinamisha macho na kutekeleza nass ya aya na wala sio halali kwake yasiokua hayo kabisa.

Na wala haifai kusemwa kua matatizo haya yamekithiri na ni vigumu kujiepusha nazo. Kwa msingi huu inagongana na uislamu. Kwa hivyo haramu haiwi halali hata kama itaenea na halali haiwi haramu hata lau kama imekithiri. Na wala haifai kusemwa kua wanawake hawa makafiri wanaamiliwa mvamala wa vijakazi, na aurah zao ni kama vijakazi, haifai kusemwa hayo kwa sababu hadithi ni amm kwa killa mwanamke, na haikusema mwanamke muislamu, amesema (saaw) “Ewe Asmaa mwanamke anapoleghe haifai kwake kuonekanwa illa hii nah ii na akaashiriya uso wake na viganja vyake” hadithi hii yaonesha uharamu wa kuangalia mwanamke, awe muislamu au asiwe muislamu ni imekuja amma katika kila hali ikiwemo hali hii. Na wala hafanyiwi Qiyas mwnamke kafiri kwa vija kazi kwa sababu hamna ya kufanyia Qiyaas.

Juu ya hayo ni wajibu juu ya wanaozuru majumba zisizokua zao na zina wanawake wasio mahram, ni juu yao wainamishe macho yao katika kutizama zaidi ya uso na viganja viwili, na ni wajibu juu yao wanaoishi katika miji na wanalozimika kuingia katika mujtama au kuamiliana na wanawake makafiri wanaodhihirisha aurah au kuajiriwa na wao au kuwaajiri wao au kuwauzia na mengineo, ni juu yao wainamishe macho yaowakati wa hayo, na wajifunge kiasi kinachowezekana kwa wanaoyahitja katika yale wasio na budi nayo.

Huu ni upande wa kuangalia ama kuhusiana na kuumpa mkono, inajuzu kwa mwanamke kuumpa mkono mwanamke bila ya kizuizi baina yao kama ilivyothubutu katika Swahili

Bukhari kutoka kwa Umm Atiyah “Tulimbaiyisha mtume (saaw) na akatusomea sisi tusimshirikishe Allah na chochote na akatukataza kuomboleza, mwanamke mmoja kati yetu azuial mkono wake “na bay’ah ilikua kwa kupeana mikono, na maana ya kuuzuia mkono wake ni aliurudisha mkono wake baada ya kua ni zamu yake ya kutoa bay’ah. Na uhakika wake ni alizuia mkono wake ni kua atoe bayah kwa kutoa mkono na mafhum yake “akazuia mwanamke kati yetu mkono wake” ni kua wengineo hawakuzuia mikono yao ni hii yamaanisha wengine walitoa byah kwa kutoa mikono. Na pia kwa mafhum ya gauli yake Allah (swt):

... أَوْ لَمْسُتُمُ النِّسَاءَ ... } (النساء: 43)

“*Au munapowashika wanawake*” kwa lafdhii ya amm kwa kila mwanamke ni kushika inatagua udhu. Yaonesha kufungika kwa hukm ya kutanguka udhu katika kumshika mwanamke na juu kushika iwe ni billa ya matamanio sio haramu kwa kuwapa wao mikonio pia sio haramu na juu ya hayo mkono wa mwanamke sio aurah na sio haramu kuangalia bila ya matamanio kwa hivyo si haramu kumpa mkono.

Na hii ni tofauti na busu. Kwa hivyo mwanamume kumbusu mwanamke ajnabi anaemtaka na mwanamke kumbusu mwanamume ajnabi anaemtaka hiyo ni haramu, kwa sababu ni utangulizi wa kuzini, na kwa kua busu hizi kwa kawaida ni mwanzo wa zinaa kiada, hata lau kama bila ya matamanio na hata lau kama haikupelekea katika zinaa, hata lau kama haikupatikana zinaa, kwa sababu gavili ya Mtume (saaw) kumuambia Ma’az alipokuja kwake na akataka asfishwe kwa sababu alizini “pengine ulimbusu” yaonesha kua busu kama hizi ni mwanzo wa zinaa, na kwa sababu aya na hadithi zinazoharamisha zinaa zimekusanya uharamu wa killa yanaopelekea zinaa hata lau kama ni kushika iwapo ni katika yaliozoeleka katika chanzo cha zinaa, mfano mtu kumtongoza mwanamke au mwanamke kujipeleka mwenyewe kwa mwanamume, au kumbusu mwanamke au kumhamasisha au kwa matamanio au kwa kumkumbatia au mengineo, kama wale

ambao wasio na tabia katika mabarobaro na wanawali, kwa hivyo busu hiyo ni haramu hata lau kama ni kumpokea na kumsalimia anaetoka safari kwa sababu busu kama hizi kati ya mabarobaro na wanawali ni chanzo cha zinaa.

### Sio Wajibu Juu Ya Wanawake Muislamu Kufinika Uso Wake

Kauli kua hijab iliofadharadhiswa juu ya wanawake katika uislamu wasitiri nyuzo zao isipokua macho yao ni rai ya kiislamu, wameseman baadhi ya Maimamu mujtahidin mionganini mwa wenyewe madhheb. Na qauli kua hijab haikufaradhiswa juu ya wanawake katika uislamu kwa hivyo sio wajibu juu ya mwanamke muislamu kusitiri uso wake kabisa kwa sababu sio aurah, hiyo pia ni rai ya kiislamu, wamesema baadhi ya muimamu mujtahidin wenyewe madhhab. Na kwa kua ni tatizo sugu katika matatizo ya kijamii na kufafanua yaani rai ya kiislamu kuhusiana na rai hizi mbili inaathiri njia ya maisha ya kiislamu, kwa hivyo hamna budi kuangalia kikamilifu dalili za kisheria kuhusianan na tatizo hilo kwa kulielewa na kufuatalizia na utabikishaji wake juu ya tatizo ili watabanni waislamu rai yenye nguvu zaidi na ili tabanni serikali ya kiislamu rai yenye nguvu zaidi kwa kuzirudia dalili.

Naam zaidi ya nusu karne imesimama majadiliano kuhusu mwanamke, yalioanzishwa na makafiri wakolono katika nafsi za waliofitiniwa na umagharibi, waliotekwa na thagafa yake na mtazamo wao katika misha. Na wakajaribu kufungamanisha na uislamu rai zisizo za kiislamu, na wakzusha fikra ya hijab na kutenga, na maulama mufakirun hawakua ni wenyewe fifra finyo wa kufanya rai za waliotekwa kuzidi kumakinika. Na wakafanya fikra zao ni chimbuko la utafiti na majadiliano hayo nabado yapatikana mabaki yake na athari zake yaendelea, lakini haustahiki utafiti, au kufika daraja ya utafiti katika hukmu za kisheria waliota mujdahidun na waliotengemea dalili, au dalili ya shubha (inaofanana), na haifai kufanya utafiti katika rai za waandishi, au haifai kufanya utafiti katika rai za waandishi, au kupewa majina na walioajiriwa na ubaya wa waliohadaiwa au urongo wa waliotekwa. Kwa hivyo yale ambayo husemwa na

mujtahidini kuhusiana na dalili ya kisharia ndiyo ambayo hufanyiwa utafiti na ndio hujadiliwa kulingana na sharia pamoja na hayo gauli za mujtahidin na gauli ya baadhi ya mafagiji na gauli ya baadhi ya mashekhe na walioshika mkao wa hijab ndio huwekwa katika meza ya majadiliano na kujadiliwa ili kuondosha shubha katika nafsi zao. Kwa hivyo tutaelezea gauli za mujtahidin na dalili zao ili ipate kubainika gauli yenye nguvu na ajilazimishe killa moja lile ambalo analiona lina nguvu kwa kuifanyia kazi na kufanya bidii utabikishaji wake.

Hakika wale wanaosema kua hijab ni faradhi kwa mwanamke ni kua mwili wake wote ni aurah illa uso wake na viganja vyake ni katika swalah peke yake, ama nje ya swalah wamesema mwili wake woteh ni aurah ikiwemo uso wake na viganja vyake. Na kauli yao hii wakategemea kitab (Qur'an) na Sunnah (hadith)

Ama Qur'an ni kwa sababu Allah (swt) anasema:

{ وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَاسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ } (الأحزاب: 53)

“Na munapo waomba bidhaa waomeni nyuma ya hijab”(Ahzab – 53) hii iko wazi katika kulazimisha hijabu juu yaona anasema Allah (swt):

{ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَا زَوْاجَكَ وَبَنَاتَكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَبِيهِنَّ ذَلِكَ أَذْنِى أَنْ يُعْرَفَنَ فَلَا يُؤْذِنُ... } (الأحزاب: 59)

“Ewe mjumbe waambie wakezo na mabanati wako na wanawake waumini wavae juu ya majalbab yao hilo litawafanya wao watambuliwe ili wasioudhiwe” (Ahzab-59) wakasema maana yake ni wajivishe juu ya jilbab wajisitiri juu yao na wafinike nazo nyuson zao na vidole vyao. Na wanaona kua wanawake wakati wa mwanzo wa uislamu bado wakiwa na ada ya kijahiliyyah wanatoka na nguo za nyumbani na mwanamke hutoka akiwa amevaa deraa na khimar (kitambara cha kichwa) hamna tofauti baina mhuru na mtumwa na walikua maborobaro wa Madina wakiwatongoza watumwa wanapotoka usiku kukidhi

haja zao katika mitende, na mara nyengine wantongoza mhuru, wakisema tulidhani ni watumwa, kwa hivyo waliamrisha wavae tofauti na vile wanavovaa watumwa kwa kuva vazi la juu (ardiya na malahif) na kusitiri vichwa na nyuso, ili wahishimike na asiwe na matumaini nao. Na hili lililkua kwao ni bora ili wasi tongonzwe, na wasifikasiwe na yakuwaudhi wao. Na mionganoni mwao wanasema “hilo ni bora kuna neon “LA” limeondolewa yaani hilo ni bora ili wasikulikane wazuri na wasio wazuri ili wasiudhiwe. Na amesema:

{ وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى } (الأحزاب: 33)

“Na mukae katika majumba yenu na musijipambe kama mulivyokua mukijipamba nyakati za mwanzo wa kijahiliya” (Ahzaab 33) na wanasema Allah amewaamrisha wanawake wake katika majumba ni dalili ya ufaradhi wa hijab.

Ama sunah ni kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (saaw) kua alisema “Mwanamke ni aurah” na kwa qauli ya Mtume (saaw)” iwapo kuna mmoja wenu (mwanamke) ana mtumwa (mwanamume) anataka kujikomboa na akaweza kumiliki kima cha kujikomboa basi ajisitiri nae” na kama ilivyopokewa kutoka kwa umm Salamat amesema “Nilikua nimeketi kwa Mtume (saaw) mimi na Hafswah akaomba ruhusa ya kuingia Ibn Umm Maktum na akasema Mtume (saaw): Jisitirini nae. Nikasema: Ewe Mtume wa Allah yeye ni kipatu hawezi kutuona, akasema: Jee nyinyi pia ni vipofu hamumuoni? Na kama alivyopokea Abu Daud “Fadhl bin Abbas alikua na mtume (saaw) katika safari, akaja mwanamke wa khathami (kabila) akiulizia maswali, akawa fadhl anamuangalia mwanamke na mwanamke anamuangalia Fadhl, Mtume (saaw) akageuza uso wa Fadhl” na imepokewa kutoka Larir bn Abdullah “Nilimuuliza Mtume (saaw) kuhusu mtazamo wa ghaflah akaniamrisha nigeuze macho yangu.” Na imepokewa kutoka kwa Ali (raa) amesema: ameniambia mimi mtume (saaw): “Usifwatizie kutizama utasemehewa ya kwanza lakini sio la pili”.

Hizi ndizo dalili za wanaosema juu ya ufaradhi wa hijab, na wanosema kua mwili wote wa mwanamke ni aurah. Lakini dalili hizi haziambatani na matatizo yaliodokezewa, kwa sababu zote hizi hazihusiani na suala hili. Ama aya ya Hijab na aya:

﴿وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ﴾

“*Na mukae katika majumbi yenu*” haina uhusiano kabisa na wanawake waislamu, na hizi ni khassa kwa wake wa mtume (saaw) kwa uwazi wa aya itakapo somwa yote, na ikiwa ni aya moja ilioshikamana kwa lafdhi na maana. Na aya yenyewe ni:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَى طَعَامٍ غَيْرَ نَاظِرِينَ إِنَّهُ وَلَكُنْ إِذَا دُعِيْتُمْ فَادْخُلُوا فَإِذَا طَعَمْتُمْ فَانْتَشِرُوا وَلَا مُسْتَأْنِسِينَ لِحَدِيثٍ إِنَّ ذَلِكُمْ كَانَ يُؤْذِي النَّبِيَّ فَيُسْتَحْيِي مِنْكُمْ وَاللهُ لَا يَسْتَحْيِي مِنِ الْحَقِّ وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَاسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ذَلِكُمْ أَطْهَرُ لِقْلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذِنُوا رَسُولُ اللهِ وَلَا أَنْ تُنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَدًا إِنَّ ذَلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللهِ عَظِيمًا ﴾  
الأحزاب: 53

“Enyi mulioamini musiingie katika nyumba ya mtume illa munapopewa ualishi wa chakula billa kungoja, na munapoalikwa basi ingieni na munapomaliza kula mutawanyike na wala musianzishe mazungumzo, kwani hayo yanamuudhi Mtume na anawaonea haya nyinyi na Allah haonei haya haki, na munapowaomba wao (wakeza za mtume) kitu basi muwaombe nyuma ya pazia, hilo ni bora kwa nyoyo zenu na nyoyo zao, na haifai kwenu kumuudhi mtume wa Allah, na haifai kwenu kuuowa wake zake baada yake milele, hakika hili mbele ya Allah ni kubwa” (Ahzab-53), kwa hivyo aya imetaja wake za mtume (S.a.a.w) na imekuja khassa kwao, na haina uhusiano na wanawake wowote wasiokua wake za mtume (saaw). Na asili ya ayah ii inatilia nguvu ukhususa wa wake za mtume (saaw) kwa yaliopokewa na Aisha (raa) amesema: “Nilikua nikila Hais (chakula) katika bakuli, akapita Umar akamuita na akala, vidole vyake vikagusna na vidole vyangu, akasema nyinyi (wake za Mtume), na ikateremaka aya ya hijab “Na kama ilivyopokewa kutoka kwa Umar (raa) amesema: “Nilisema ewe mjumbe wa Allah, huingia kwaki mwema na muovu lau ungekua ni mwenye kuwatenga mama wa waumini, Allah akateremsha aya ya hijab. “Na kama ilivyopokewa kutoka kwa Umar (raa) amesema:

Nilisema ewe mjambe wa Allah, huingia kwako mwema na muovu lau ungekua ni mwenye kuwatenga mama na waumini, Allah akateremsha aya ya hijab. Na kama ilivyopokewa kua alipita Umar kwa wake za Mtume (saaw) wakiwa na wanawake wengine katika msikiti akasema: “Mungejisitiri kwani nyinyi ni bora kuliko wanawake wengine, kama alivyo bora mume wenu juu ya wanaume wengine, akasema Zeiynab (raa.): Ewe Inb Khattab wewe unaghera na sisi na wahyi unateremka katika majumba yetu, na hawakukaa muda na ikateremka aya “ Kwa hivyo imetaja aya na hadithi hizi kwa dalili ya kukatikiwa (Qutii Dalil) kua iliteremka kuhusiana na wake za Mtume (saaw) na haikuteremka kwa wasiokua hao.

Ama aya:

{ وَقُرْنَ فِي بُيُوتِكُنَ }

“Na mukae katika majumba yenu (ahzab-33) hiyo pia kamili ni:  
 يَانِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَ كَاحِدٌ مِنَ النِّسَاءِ إِنْ اتَّقَيْتُنَ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقُولِ فَيَطْمَعُ الَّذِي فِي  
 قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَعْرُوفًا - وَقُرْنَ فِي بُيُوتِكُنَ وَلَا تَبَرْجَنَ تَبَرْجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى  
 وَأَقْمَنَ الصَّلَاةَ وَأَتَيْنَ الزَّكَاةَ وَأَطْعَنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ  
 أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُظَهِّرُكُمْ تَطْهِيرًا (الأحزاب: 32-33)

“Enyi wake za mtume nyinyi sio kama wanawake wengine wowote, iwapo munamcha Allah, kwa hivyo musilegeze sauti, ili asiweke tamaa yule ambae katika moto wake muna maradhi, na muzungumze maneno mazuri – Na mukae katika majumba yenu na musijipambe kama mulivyokua mukijipamba wakati wa mwanzo wa jahiliya, na musimamishe swala, na mutoe zakah, na mumtii Allah na Mtume wake, na hakika kile anacho watachia nyinyi Allah ni kuwaondolea uchafu watu wa nyumba (ya mtume) na kuwatakaza kabisa “Kwa hivyo aya imetaja kwa uwazi kabisa kua imeteremka juu ya wake za Mtume (S.a.a.w) na kwa sababu ni khassa kwa “Enyi wake za mtume nyinyi hamna mfano na wanawake wowote wengine” (Ahzab-32/33) kwa hivyo mwanzo wa aya ni kwa wake za Mtume kwa sababu wanazungumiwa wake za Mtume, na kwa sababu ni khassa kwa,

{ يَانِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَ كَاحِدٌ مِنَ النِّسَاءِ }

"Enyi wake za Mtume nyinyi sio kama wanawake wengine wowote" na wala hamna aya fasaha na iliwazi kuliko ayah hii na kua ayah ii imeteremka juu ya wake za mtume (saaw) na ni khassa tu kwao. Na inatiliwa nguvu maoni haya kwa mwisho wake katika gauli katika mwisho wa aya hiyo hiyo.

**{...إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا }** {الأحزاب: 33}

"Hakika anachotaka Allah ni kuwaondolea nyinyi ucha wetu wa nyumba (ya mtume) na awasafisha kabisa" (ahzab-33) haiku wazi kua sifa hii ni khassa kwa wake za mtume (saaw) na kua Allah (swt) amewaaamrisha hayo ili kuwandolea wao uchafu na kuwasafisha kwani wao ni katika watu wa nyumba (ya mtume). Na pia inatiliwa nguvu hayo katika aya ambayo iliopo baada yake moja kwa moja, kwani baada ya haya akasema:

**{... وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا }** {الأحزاب: 33}

"Na awasafisha kabisa" (ahzab-33) na badala y haya akasema:  
**{وَأذْكُرْنَ مَا يُتْلَى فِي بُيُوتِنَ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَيْرًا }**  
**{الأحزاب: 34}**

"Na mudhukuru yale yanaosomwa katika majumba yenu katika aya za Allah na hikmah, kwa hakika Allah ni mpole na mulewa" (Ahzab- 34) na akwakumbusha kua majumbani mwao kunateremka wahya, na akawaamrisha wasisahau yanaosomwa humo katika Qur'an.

Kwa hivyo aya hizi mbili ziko wazi na kua ni kwa wake za Mtume (saaw) na pia ni khassa kwa wake za mtume (saaw). Na pia ni khassa kwa wake za mtume (saaw), kwa hivyo hamna dalili yoyote katika hizo mbili hukmu ya wanawake waislamu wasio kua wake za mtume (saaw). na pia kuna aya nyengine ambayo ni khassa kwa wake za mtume (saaw) mfano wa gauli ya Allah (swt):

**{... وَلَا أَنْ تُنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَدًا...}** {الأحزاب: 53}

"Na haifai kwenu kuowa wake zake baada yake" (ahzab-53) kwa hivyo haifai kwa wake za mtume (saaw) kuolewa baada yake, kinyume na wanawake waislamu inafaa kwao kuolewa baada yake, kinyume na wanawake waislamu inafaa kwao

kuolewa baada ya waume zao, na aya hizo mbili za hijab ni khasa kwa wake za mtume (saaw) kama aya ya uharamu wa kuolewa wao baada yake.

Wala haifai kusemwa – Al-Ibratu bin umumi lafdhi la bikhusus sabab-kwani sababu ya kurermka aya ni wake za mtume (saaw) ni amah kwao na wasiokua wao, haifai kusemwa hivyo kwani sababu ya kuteremka ni tukio lililotokea, na ndio ikawa sababu ya kuteremka. Ama hapa wake za mtume (saaw) sio tukio lililotokea, bali ni aya khasa iliokuja kwa watu maalum, na ikataja ukhusuia wake juu ya wake zake na akasema:

{ يَأْنِسَاءُ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَاحِدٍ مِنَ النِّسَاءِ... } (الأحزاب: 32)

“Enyi wake za mtume nyinyi sio kama wake wengine wowote” (Ahzab-32) na akasema “na munapowauliza” na lengo (Dhamiri) ni kwa wake za mtume (saaw) na ni maalum kwao wao, sio wengine na akaendeleza hayo kwa kauli yake:

{ وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذِنُوا رَسُولَ اللَّهِ }

“Na haifai kwenu nyinyi kumuudhi mtume wa Allah (ahzab-53) na yaeleweka illa (sababu ya kisheria) ya kujiitiri kwao (hijab), na killa ambacho inatafautisha katika hayo kua aya mbili zimekuja maalum kwa wake za mtume (saaw) haifwati qaidah humo ya “Al-ibratu bi umumi lafdhi la bi khusus asabab”.

Na hivyo hivyo haifai kusemwa kua uzungumzi kwa wake za mtume (saaw) ni uzungumzi kwa waawake waislamu, kwa sababu asli ya uzungumzi maalum kwa mtu maalum ni uzungumzi kwa waumini bali ni khassa kwa mtume Mohammad (saaw), na walo haijumishi uzungumzi huo wake zake, kwa hivyo uzungumzi kwa Mtume (saaw) ni uzungumzi kwa waumini, ama uzungumzi, au kitendo au au kunyamazia iwapo haitakua ni khususia yake (saaw). Ama wake za mtume (S.a.aw) sio kiigizo kwa sababu Allah (swt) anasema:

{ لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ... } (الأحزاب: 21)

*“Hakika nyinyi munao katika mtume wa Allah kiigizo chema”* (ahzab-21). Na haifai kufanywa wake za Mtume (saaw) kiigizo, kwa maana kufanya kitendo kwa sababu wao wanaifanya au kujipamba na sifa kwa sababu wao walisifika nazo, bali ni khassa kwa mtume (saaw) kwani yeche hafuati illa wahyi.

Na vile vile haifai kusemwa iwapo wake za mtume (saaw) nao ni wasfi ambao husomwa wahyi katika majumba yao na wantakiwa wawe na hijab, basi wasia kua ha katika wanwake waislamu ni awla (bora) watakiwa wao pia, haifai hayo kwa sababu mbili:

La kwanza: - Kua hayo haya linganishwi na upande wa awla (bora) kwani bora ni kukanywa na itakua ni kukomeka na kikubwa ni bora zaidi (bab-awla) kama kauli yake (swt)

{...فَلَا تَقْنُ لَهُمَا أَفِ...}(الإسراء: 23)

“Usiwaambie wao ufi” (Al-isra – 23) kwa ivyo itaku bora zaidi asiwadhuru. Na bora (Awlah) hufahamika kwa yalivyokuja maneno kwa mfano kauli yake (swt):

{وَمِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِقِطْرَارٍ يُؤَدِّهِ إِلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِدِينَارٍ لَا يُؤَدِّهِ  
إِلَيْكَ} {آل عمران: 75}

“Na katika ahlul kitab wapo ukimwamini ni qintar anakulipa na kati yao ukiwaamini ka dinar hawakulipi” (Al-imran- 75). Kwa hivyo kulipa kichache ya qintar ni katika bab aulah na kutolipa zaidi ya dinar ni katika babawlah na kutolipa zaidi ya dinar ni katika bab aulah. Na aya ya hijab haikuja kwa muelekeo huo, kwa sababu yalivyokuja maneno haimaanishi illa juu ya wake za Mtume (saaw) aulah. Bali jina la kitu maalum (Ism jamid) kwa hivyo yatakua maneno ni khassa kwa kitu Fulani ambayo ‘imetajwa katika aya, hivyo basi haiongezewi chengine au mathum nyengine. Wala haingii katika aya sual la bab-awla kabisa sio upande wa lafdhi ya aya wala katika kufuatana kwake.

La pili: - Aya hizi mbili ni amri ya watu maalum, waliotajwa katika aya wawe na sifa maalum, kwa hivyo haiwi kabisa amri

hiyo kwa wengine, sio wale walio juu zaidi yao au duni yao kwa sababu ni sifa maalum. Nao ni khassa kwa watu Fulani, kwa hivyo ni amri kwa wake za Mtume (saaw) kwa sifa ya kua ni wake za mtume (saaw) kwa sababu wao sio kama wanawake wengine wowote na kwa sababu pambo hilo linamuudhi mtume (saaw).

Na ikianguka qaida ya al-Ibratu bi umum lafdh la bi khusus asabab) itanguka suala la kufuata wake za mtume (saaw) na pia itaanguka sual la bab-awlal kwa wasiokua hao, na imethubutu kua aya ni Qatii katiak asili yake ni ya wake za mtume (saaw), na imethubutu kua aya hizi mbili ni khassa tu kwa wake za mtume (saaw), wala hawajumulishwi kabisa wanawake wengine waislamu, kwa hamna yoyote ile. Kwa hayo yathubutu kua hijab ni khassa kwa wake za Mtume (saaw), na kukaa majumbani ni khasa kwa wake za mtume (saaw), na yaanguka dalili kwa aya hizi mbili juu ya asili yake kua hijab imefaradhishwa kwa wanawake waislamu.

Ama aya **ya** pili nao ni kauli ake (swt):

{ يُذْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَبِيَّهِنَّ }

“Watiririshe juu yao majalbab zao”(ahzab-59) hiyo haimanishi kufinika uso kwa namna yoyote ile, sio kwa matamshi (Mantuq) au ufahamu (mafhum), na hamna katika aya hiyo lafdhi yoyoe inammnishi hayo, sio kipekee wala sio kuwepo katika ujumla wake, juu ya ufaradhi wa usahihi wa sababu ya kuteremka aya. Na aya inasema:

{ يُذْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَبِيَّهِنَّ }

“watiririshe juu yao majalbab yao” na maana yke ni wanninginishe juu yo majalbab yao, na (Min) hapa sio ya sehemu (tabiidh) bali ni ya ufanuzi (Baya) yaani watiririshe juu yao majalbab yao. Na maana (Adna) ametiririsha na maana ya Yudnina ni watiririshe na jalbab ni (milhafah) sitara, na kila ambacho hutumiwa kusitiri katika vazi na mengineo, au ni nguo ambayo husitiri mwili mzima. Amesema katika Qamus A-Muhit” na jalbab ni kama Sirdab na Sinmar “Vazi na nguo pana ya mwanamke inaositiri mpaka chini au ni vazi na nguo pana ya

mwanamke inaositiri mpaka chini au nivazi atakositiri nao nguo zake kama Milhafah". Na amesema Al-Jawhari katika swahah "Jalbab ni Milhafah na yasemekana Mulaah" n aimepokewa katika hadithi jalbab kwa maana ya Milhafa (sitara) ambayo hujisitiri nayo mwanamke juu ya nguo zake. Imepokewa na Umm atiyyah (raa) amesema: "Ametuamrisha Mume (saaw) tuwe tukiwatowa katika Idul-fitri na Iddul-Adh-ha vijakazi na walioko kwenye heidhi na wasichana, ama walioko kwenye heidhi wajitenge na swalah na washuhudie mazuri na ulingnaizi wa waislamu. Nikasema: ewe mtume (saaw) ikiwa mmoja wetu hana jalbab, akasema: atavaa jalbab la dadake" na maana yake ikiwa hana vazi atakalo vaa juu ya nguo zake ili apate kutokea nalo, na akumarisha kuazima kwa dadake vazi ambalo atalivaa juu ya nguo zake, hivyo basi itakua maana ya aya: Allah amemtaka Mume (saaw) awaambie wakeze na banati zake na wanawake waumini watiririshe juu yao vazi ambalo alivaaa juu ya nguo mpaka chini, kwa dalili iliopokewa kutoka Ibn Abbas kua alisema: Jalbaba ni vazi kutoka juu mpaka chini. Kwa hivyo aya yamaanisha juu ya kutiririsha jalbab – no ni vazi kubwa – mpaka chini, wala, haimaanishi jengine lolote. Kwa hivyo yawezekana vipi kufamika kua maana ya "Yudnina Alaiyhinna Min jalabiibihinna" (Watiririshe juu yao majilbab yao) kwa wazianye mavazi yao juu ya nyuso zao? Vovote itakvyofasiriwa neno jalbab, katika mipaka ya kilugha na maana ya kisheria? Bali aya imetaja kutiririsha nguo, na kutiririsha ni mpaka chini na sio kuinyanya mpaka juu. Kwa hivyo hamna katika ayah ii dalili yoyote juu ya ufaradhi wa hijab bali hata dalili iliofanana (Shubhat dalil) sio kwa karibu wala mbala mbali. Na qura'an hufasiriwa vilma vyake na maneno yake kwa maana ya kulugha na kisheria na wala haifai kufasiriwa vengine, na kwa maana ya kulugha ni wazi kua ni amri kwa wanawake watiririshe juu yao mahalbab yao yaani waziteremshe na wasitiri juu ya mavazi yao majalbab yao ambayo wanayoyavaa mpaka chini mpaka ifinike nyayo mbili. Na imekuja maani hii kaitka kutiririsha vazi mpaka chini katika hadithi tukufu (shariff), imepokewa na ibn Umar amesema: amesema mtume (saaw): "Yoyote atakae tiririsha nguo yake kwa kiburi, Allah (swt) hatamuangalia yeye

siku ya Qiyama, akasema umm Salamah: vipi wafanye wanawake na kutiririsha kwao, akaseman: watiririshe shibiri akasema: itadhihiri nyayo zao, akasema watirirshe dhira'a na wazidishe”.

Huu ni upande wa ayah ambazo wanazitegemea kwa madai yao ya hijab na Allah (swt) amewafaradhishia wanawake waislamu, ama kwa upande wa hadithi ambazo wanazitegemea juu ya ufaradhi wa hijab haziowi dalili hiyo, hadithi ya mtumwa anaetaka kujikomboa (mukatib) akimiliki kinachowenza kujikomboa hujitenfa ni khassa kwa wake za mtume (saaw), na haya yatiliwa nguvu na hadithi nyengine, imepokewa na Abi Qalabah amesema: “Walikua wake zake Mtume (saaw) wakiweka hijab kwa mukatilo anapobakisha dinari hamna dalili yoyote katika hadithi juu ya mwanamke muislamu awe na hijab. Ama hadithi ya Umm Salamah na mtume (saaw) kumtaka yeye na Hafswah watisitiri (hijab) hadithi hiyo ni dhaifu haitegemewi, na juu ya hayo hiyo ni khassa kwa wake zza mtume (saaw) na hadithi ametaja Umm Salamh na Hafswah. Ama yale yaliopo kewa kutoka Aisha amesema “Waendeshaji wa farasi walikua wakipita mbele yetu na sisi tulikua na mtume (saaw) katika hali ya ihram wanpokaribia kwa mmoja wetu tunajisiriri na jalbab kutoka kichwani juu ya uso wake na wanpopita tunayavua” hii inagongana na yaliopokewa na Bukhari kutoka kwa ibn Umar kua mtume (saaw) amesema: “Asivae hijab (kitambaa cha uso) mwanamke na aisivae sitara ya mikono (glovu) katika halie ya ihram” amesema katika kitabu Fathul – Baari: na niqaab ni khimar ambayo hufungwa juu ya pua au chini ya macho. Na hadithi ya Aisha yaeleza kua wanawake katiak hali ya ihram walikua wasitiri nyuso zao wakte waendeshaji farasi wapopita karibu yao. Na hadithi ya Ibn umar yaonyesha kukataza kuva ni qaaba nao haisitiri illa kipande cha chini cha uso kwa hivyo vipi itakubaliana na kusitiri uso mzima kwa nguo. Na kuzirudia hadithi mbili yabainika kua hadithi ya Aisha kwa kutiwa dosari kua ni riwayah ya muhahid kutoka kwa Aisha. Na ameeleza yahaya kuhusu udhaifu wa hadithi ya Aisha na kugongana kwake na

hadithi sahih kwa hivyo haitegemewi. Ama hadithi ya Fadhl bin haionesin ufaradhi wowote wa hijab bali ni kinyume na hivyo kwa sababu khathamiyah alikua akimuuliza mtume (saaw) hali ya kua amedhihirisha uso wake kwa dalili ya kua fadhl alikua anamuangalia na kwa dalili ya kua fadhl alikua anamuangalia na kwa dalili kama ilivyopokewa katika riwayah nyengine kwa hadithi hiyo “Mtume (saaw) akageuza uso wake upande mwengine”. Na amekisumulia kissa hiki Ali bini Abi Talib (raa) na akaongeza “akamuambia yeye Ibn Abbas “ewe Mtume wa Allah kwa nini umegeuza shingo ya mtoto wa Ammi yako?akasema: niliona barobaro na msichana na sikumuamini shaitani juu yao” kwa hivyo hadithi ya khathamiyali ni dalili ya kutokuwepo utaradhi wa hijab na sio ufaradhi wa hijab na sio ufaradhi wa hijab. Kwa sababu alikua anamuona hali ya kua uso uko wazi. Ama kumgeuza fadhl ni kwa sababu alimuona anamuangalia kwa matamanio na msichana anamuangalia yaeye kwa dalili ya mapokezi ya Ali “sikumuamini sheitani juu yao “Na kwa ajili hizo alimgeuza kwa sababu alimuangalia kwa matamanio na sioi kwa kuangalia na kuangalia kwa matamaniio hata lau kama ni uso na viganja viwili ni haramu. Ama mtazamo wa ghaflali mtume (saaw) alimuamrisha Jarir aageuza macho yake yaani ainamishe nao ni kama ilivyokuja kuinamisha macho ilivyopokewa katiak Qur'an kwa qauli yake (swt):

... قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغْضُبُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ ... {النور: 30}

“waambie waumini wanaume wainamishe macho yao” (Nur-30) na muradi wake hapa ni kuona kwa ghaflah kwa zaidi ya uso na viganja vile ambavyo ni aurah, na sio kuangalia uso na viganja viwili kwa sababu kuangalia uso na viganja viwili inajuzu billa ya kua ni mtazamo wa ghaflah, kwa dalili ya kuruhusiwa kuangalia katika hadithi ya khathamia iliotangulia, na kwa dalili ya kua mtume (saaw) alikua anaangalia nyuso za wanawake wakati wa kumbayiisha yeye, na wakati alipokua akiwapa mawaidha, yote hayo yanonesha kutahadhari kutizama ghaflah zaidi ya uso na viganja viwili. Ama hadithi ya Ali “Usifuutilize mtazamo kwa mtazamo mwengine” hilo na katazo la kuendelea kuangalia na sio kwa kuona tu.

Na kwa hayo hamna katika ambayo wanaoitegemea wanaodai kua Allah (swt) amefaradhisha hijab na dalili ya ufaradhi wa hijab, na kwa hayo yabainika kuan hamna dalili inaoonesha kua Allah (swt) amejibisha hijab kwa wanawake waislmu, au inaoonesha kua uso na viganja viwili na aurah, sio katika swalah wale nje ya swalha. Na dalili wanazozitegemea hamna nguvu ya kuoneha hayo nazo pia ni dhaifu katika mapokezi yake na dhaifu katika dalili.

Ama asli ya uso na viganja viwili sio aurah na asli ya mwanamke kua inafaa kwake kutoka kwenda sokono na barabara killa mahli anadhihirisha uso wake na viganja vyake hayo yamethubutu katika Qur'an na hadithi.

Ama Qur'an amesema Allah (swt)  
 { وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلَيَضْرِبُنَّ بِخُمُرِهِنَّ عَلَى جِيُوبِهِنَّ } (النور: 31)

*"Na wasidhahirisho mapambo yao illa yaliodhiri na wavae khimar zao mpaka juu ya vifua vyao"* (Nur-31) kwa hivyo Allah (S.w.t) amewakataze wanawake waumini kudhihirisha mapambo yao, yaani amewakataza kudhihirisha sehemu za mapambo yao kwani hayo ndio malengo ya kukatazwa na akachuja sehemu za mapambo yaliodhiri na muhujo uko wazi, na hayo yamaanisha kuna sehemu za mapambo katika mwanamke yadhihiri na hayaiingii katika yaliokatazwa kudhihirisha, na hayo hayahitajii maneno zaidi, kwa hivyo Allah (swt) anawakataza wanawake waumini kudhihirisha sehemu za mapambo illa yale yaliodhiri, ama ni vioungo gani ambavyo vimeelezewa na qauli yake

{ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا }

*"Illa yaliodhiri"* tafsiri yake huregewa mambo mawili ya kwanza ni tafsiri ilionukuliwa (Tafsir-manqul) na ya pili yanaofahamika katika neno:

{ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا }

*"Illa yaliodhiri"* utabikishaji wake wakati juu ya yale waliokua wakidhihirisha wanawake waislamu mble ya mtume (saaw) na katika zama zake, zama za kuteremka ayah hii.

Ama ya kunukuliwa imepokewa kutoka kwa ibn Abbas katika tafsiri ya ayah ii kua “yaliodhihiri” yamaanisha “uso na viganja viwili” na wakafuata hayo mutafassirun, amesema Imam ibn Jarir Tabarri” Na qauli lililo sawa ni na akasema Qurtubi “Na kwa kuna mara nyingi uso na viganja viwili kudhihirisha kwakw ada na ibada kama katika Hajj na Swalah kwa hivyo inafaa kuchujwa kwake inaregelea viwili hivyo “ Na amesema Imam zamakhshari “Hakika mwanamke hana budi kutekeleza shughuli kwa mikono yake na ana haja ya kudhihirisha uso wake na viganja vyake khassa katika ushahidi na mahakama na ndoa na hana budi kutembea katiak mabarabara na kudhihirisha nyayo zake, na khassa wanawake makafiri mionganoni mwao nah ii ni maana ya kauli:

{ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا }

“*illa yaliodhihiri*”.

Ama yanaofahamika katika neno “yaliodhihiri” ni kua yabainika yale yaliokua yakidhihir wakati wa kuteremka ayah ni uso viganja viwili. Na walikua wanawake wanadhihirisha nyuso zao na mikono yao katika soko na mabarabara, na matukio katiak hto ni mengi yasiohisabika, mionganoni mwake ni:-

1:- Imepokea kutoka kwa Jabir bin Abdalla amesema: Nilikua pamoja na mtume (saaw) siku ya Idd, akanza na swala kabla ya khutah billa ya dhanan na iqamah, kisha akasimama hali amejitegemeza na Bila akaamrisha kuumcha Allah, na akasisitiza atiiwe na akaidhi watu na kuwakumbusha, kisha akaondoka kwenda mpaka kwa wanawake na kuwakubusha akasema: “Toeni sadaqah kwani wengi wenu ni kuni za motoni, akasimama mwanamke katikati ya wanawake mwenye matavu meusi, akasema: kwa nini hayo ewe Mtume wa allah? Akasema: kwa sababu mun mashtaka mengi na munakufuru fadhila za waume zenu” akaseman: wakawa wanatoa sadaqah katika madhehebu yao wakizitia katiak nguo ya Bilal.

2:- Imepokewa kutoka Ataa bin Abi Rabah amesem: Aliniambia mimi Ibn Abbas: Jee sikuoneshi wewe mwanamke wa peponi, ni kasema: kwa nini? Akasema: mimi hushikwa n akifafa n apia hua uchi basi niombee mimi Allah, akamuambia yeye: ukitaka nikuombee Allah akuondolee, akasema: “Ninatasubiri akasema: mimi hua uchi basi niombee Allah nisiwe uchi, akamuombea.

3:- Imepokewa kutoka kwa Fatima bint Qais kua Aba Amru bin Hafs alimuacha kwa hasira akiwa safari, akaja kwa mtume (saaw) akamuelwzea hayo na (mtume) akamuamrisha akae enda kaitka nyumba ya Umm Sharik kisha akasema: “Huyo ni mwanamke anaetembelewa na maswahaba wangu, kaa enda yako katika nyumba ya Umm Maktum, kwa sababu yeye ni kipofu na unaweza kuvua nguo zako na asikuone “kwa hivyo akakubali bint wa Qais aonekanwe na wanaume wakti alipomuarisha ake eda katika nyumba ya Umm Sharik, lakina hakumkubalia kuvua nguo zake katika nyumba ya umm Sharik anapotembelewa na wanaume, na ataonekanwa yale ambayo ni haramu, na akamuamrisha kuhama na akae eda katika nyumba ya Umm Maktum.

4:- Amepokea Abu Bakr kutoka kwa Ibn Jureij amesema: amesema Aisha: aliquja kwangu mtoto wa kakangu akiwa amejipamba na akaingia mtume (saaw) na akageuza uso wake na nikaema: ewe myumr wa Allah ni mtoto wa kakangu na mtumishi. Akasema: “Anapo baleghe mwanamke haifai kwake kuonesha illa uso wake na illa chini yah ii, na akshika dhiraa zake na akawacha kati ya aliposhika na kati ya utumbo wa mkono mfano wa mshiko mwengine na mfano wake”

5:- Na katika yanaoonesha kua mkono sio aurah ni mtume (saaw) kuwapatia mkono wanawake katika bayah. Imepokewa kutoka kwa Umm Atiyah amesema: “Tulimbayiisha mtume (saaw) na katusomea tusimshirikishe Allah na kitu chochote na akatukataza kuomboleza, mwanamke moja katiak sisi akazuia mkono wake na aksema: Mwanamke Fulani amenifurahisha na

mimi nataka mimlipe. Na hakusema kitu akondoka na baadae akaregea” na hadithi hii yaonesha kua wanawake walikua wakibatiisha kwa mikono, kwa sababu mwanamke huyu alizuia mkono wake wakati ilipokua ni zamu yake ya kubajiisha kwa hivyo asli ya hadithi yaeleza kua mwanamke alizuia mkono wake wakati aliposikia maneno ya bayah yalo wazi kua bayah ilikua kwa mkono, na kua mtume (saaw) alikua anabaiisha wanawake kwa mkono wake mtukufu. Ama yalei talipokewa kutoka kwa Aisha kua alisema: “Haukugusa mkono wa mtume (saaw) mkono wa mwanamke illa mwanamke anaemiliki”. Hiyo ni rai ya Aisha juu ya upeo wa ilimu yake, na ikilinganishwa qauli yaAisha na hadithi ya hii ya umm Atiyah, hadithi ya Umm Atiyah ina uzito, kwa sababu imeelezea kitendo kilichopatikan mbele ya mtume (saaw). na yaonesha kua kitendo cha mtume (saaw) ina nguvu zaidi kuliko rai ya Aisha nyepesi. Kwa hivyo wapokezi wa hadithi wanairegelea hadithi ya Umm Atiyah na wanaichukua na wanaruhusu mwanamume kumpa mkono mwanamke.

Kwa hivyo matukio hayo matano yaliothubutu katika hadithi ni dalili wazi kua yaliokua yakidhihirika kutoka kwa mwanamke ni uso na viganja viwili na hadithi ya nne yaonyesha juu ya kugeuka mtume (saaw) kuangalia mwanamke aliejipamba kwa sababu laikua anadhihirisha zaidi ya yanaofaa kudhihiri, na kisha akelezea kua haifai kwake kudhihirisha illa uso na viganja na hii ni dalili inaonesha wazi kua kilichochujwa katika aya ni uso na viganja viwili. Na yaonyesha kua viwili hivyo sio Aurah si katika swalah wala nje ya swalah kwa sababu aya ni jumla (amah):

{ وَلَا يُبَدِّيْنَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا } (النور: 31)

“*Na wala wasidhihirishe mapambo yao illa yaliodhiihiri*” (Nur-31).

Ama aya ilioko baada yake mafhum yake yaonyesha kua uso na viganja viwili sio aurahm an Allah (swt) anasema:

{ ... وَلَيَضْرِبُنَّ بِخُمُرِهِنَّ عَلَى جُبُوبِهِنَّ ... } (النور: 31)

*“Na wavae khimar zao juu ya vifua vyao”* (Nur-31). Na khami ni uwingi wa khimar nao knachofinika kichwa, Tuyub ni uwingi wa teiyab, na ni sehemu za uwazi kaitka shati na kanzu, kwa hivyo Alah (swt) ameamrisha kua wateremsha khimar juu ya shingo na vifua na yaonyesha uwajibu wa kusitiri viwili hivyo, na hakumuamrisha kuivaa usoni, na yaonyesha kua sio aurah. Na sio maana ya neno jeib kifua kwa inavodhaniwa bali jeib ni katika kanzu mpasuko wake na uwazi wake ambayo inakua kando ya shingo na juu ya kifua, na kuvaahimmar juu ya jeib ni kuitirisha katika ufunuo wa kanzu ikiwemo shingo na kifua. Kwa hivyo amri ya kuvaahimmar sitara ya kichwa inaotirirka juu ya shingo na kifua na kuchuja uso yaonyesha kua sio aurah. Na kwa haya hijab haipo na Allah (swt) hakufaradhisha.

Huu ni upande wa dalili kuhusiana na Qura'n, ama dalili zinazohusiana na hadithi na kua hijaba Allah (swt) hajavifaradhisha, na kua uso na viganja viwili sio aurah ni kwa yalie alioyapokea Abu Daud kutoka kwa Aisha (raa) kua Asmaa bint Abi Bakr (raa) aliingia kwa mtume (saaw) akamgeuza uso wake akamuambiam mtume (saaw) akamgeuza uso wake akamuambia “Ewe Asmaa mwanamke anapo baleghe haifai kwake kuoneknwa illa hiii ni hii na akashiria uso wak na viganja vyake”, na amepokea Abu Daud kutoka kwa qtatadah kua mtume (saaw) alisema: “Msichana anapoaleghe haifai kwake kuonekanwa illa uso wake na moikono yake isipokus isipokua mfupa (sehemu ya kuvalia saa) na ameipokea Baihaqi kutoka kwa Asmaa bint Amis kuaamesema: Aliingia mtume (saaw) kwa Aisha bint Abi Bakar akiwa na dadake Asmaa bint Bakr akiwa na dadake Asmaa bint Abu Bakr akiwa mevaa nguo ya shamiya (Syria) yenye mikono mipana, alipomuona mtume (saaw) alisimama na akatoka, akasema Aisha (raa) ondoka kwani mtume (saaw) ameona jambo la kumuudhi, akaondoka, akaingia mtume (saaw) na Aisha akamuuliza (raa) kwanini aliondoka? Akasema: jee hukuona mapambo yake hakika haifai kwa mwanamke muilsmu kudhihirisha illa hii na hii, na akachukua kitambara chake na akafinika mikono yake mpaka

ikaonekana vidole vyake kisha akaweka vidole vyake usoni na mpaka akaonekana uso pekee”

Kwa hivyo hadithi hizi ziko wazi kua uso na viganja viwili sio aurah, na ziko wazi kua Allah hakufaradhisha kusitiri uso na viganja viwili, na hakufaradhisha hijab. Kwani lau anagefaradhisha chochote katiak hayo kitu zingeligongana hizi hadithi mabazohazina tafsiri nyengine wala maelezo, bali ni dalili wazi kua mwanamke muislamu anatoka kwenda sokono hali ya kua anaonekana uso wake na viganja vyake na kuzungumza na wanaume Ajnabi hali ya kua anaonekana uso wake na viganja vyake, na ameamiliana na watu killa aina ya muamalah inaokubalika na sharia, kama kununua na kuuza na kukodisha na kuajiri na kuwakilisha na mengineo hali ya kua anaonekana uso wake na vignja vyake. Na kua hijab Allah hakuifaradhishiwa illa wake za Mtume (saaw). na hata lau kama ni rai ya kiislamu kwa sababu iko na mfanano wa dalili (shubhat-dalil) na wameisema maimamu mujtahidun mionganoni mwa wenyewe madhababu ill shubhat dalili ambazo wanazo zitegemea hizo ni dhaifu hazija weza kutoa dalili humo.

Limebakia suala la wanaosema baadhi ya mujtahidin nao ni kua ifarahdishwe kwa mwanamke kwa kuogopea fitna, na wanasema azuiwe mwanamke kudhihirisha uso wake mbele ya wanume sio kwa sababu ni aurah bali kwa kuogopa fitnah, na qauli hii ni batil kwa namn kadha:-

Ya kwanza – Ni kua hazipokewa uharamu wa kudhihirisha uso kwa kuogopea fitna nass ya kisheria. Sio katika Qur'an wala katiaksunnah wala kutoka kwa mjumuiko wa maswahaba (Ijmaa swahahah) wala katiak sababu za kisheria (illah) inaweza kupimiwa, kwa hivyo hayo hayoni thamni kwa sheira na haya zingatiwi ni hukmu ya kisheria kwa sababu hukm sheria ni mazungumzo ya mteremsha sheria, na uharamu wa kudhihirisha uso kwa kuogopea fitna haikuja katika mazungumzo ya mteremsha sheria, na yajulikana kua dalili za kisheria zimekuja kinyume na hayo moja kwa moja, na aya na hadithi zikaruhusu

kudhihirisha uso na mikono miwili kuruhusu wazi wazi na haikufungwa na kitu, na haikufanywa na makhusus kaitka hali yoyote ile. Kwa hivyo qauli ya uharamu wa kudhihirisha uso na ufaradhi wa kusitiri ni kuhamisha alichohalalisha Allah (swt) na kulazimisha jambo ambalo halikulamishwa na Bwana wa viumbe. Kwa hivyo ni zaidi ya kutoizingatia ni hukm ya kisheria, nao inabatilisha hukm za kisheria zilizothubutu kwa uwazi katika nass.

Ya pili:- Kuifanya kuogopea fitna ndio sababu ya kisheria (illha) ya kuhamisha kudhihirisha uso na kulazimisha kusitiri haikupokewa kuhusiana na hayo nass yoyote ya kisheria sio kwa uwazi wala kidalili wala kwa kuitoa (istinbaat) wala kwa kipimo (Qiyaas) kwa hivyo haitakua ni illa ya kisheria kabisa, bali ni illa ya kiakili, na illa ya kiakili haina uzito wowote katika hukm sharii, bali kinachozingtiwa ni illah ya kisheria na sio nyengine. Kwa hivyo hatana uzito maneno ya kuogopea fitnah katika sheria na kuhamamaisha hudhihirisha uso na kufaradhisha kusitiri kwa sababu hiakupokewa katika sharia.

Ya tatu:- Qaida ya Al-wasilatu ilal haram muhramah (Kinachopelekea katika haramu ni haramu) hayainginoni katika kuhamisha uso kwa kuigopea fitnah, kwa sababu qaida hiyo hamna budi yapatikane mambo mawili: La kwanza kua wasila yenyewe inafikisha katiak haramu billah ya shaka na kua ni sababu ya haramu kwa nama sababu itazalisha bila ya shaka ni haina tofauti nayo. Na ya pili yanaoregelewa ni yale yaliotajwa katika Nass uharamu wake na sio yalioharmishwa kuitia akili. Na hili hamna katika kudhihirisha uso kwa kuogopa fitna. Iwapo watasema kusitiri uso kwa kuogopa fitna na wasiseme kwa kupatikan fitna, kwa hivyo haifwatwi kudhihirisha uso kwa kuogopea fitna juu ya msingi kuhamisha kwa kiel kinachokua ni sababu ya yale ambayo ni haram juu ya ulazima kua fitna imeharamishwa kisheria juu ya jule aliefitinishwa kwa sababu silo jammbo lisilo na shaka. Na pia kuogopea fitna haikuja katika Nass kuifanya ni haram bali mteremsha sheria hakuifanya fitna yenyewe kua ni haramu kwa yale yanaowafitinisha watu,

bali amemharmishia aneangalia kua mwangalio wa fitna na asiharamishe hayo juu ya anaengalia, imepokewa na Abu Daud: “Fadhl bin Abbas aikua pamoja na Mtume (saaw) katika safari akaja mwanamke wa khathamiyah kuuliza maswali, fadhi akawa na muagalia mwanamke anamuangalia fadhi, mtume (saaw) akageuza uso wa Fadhl” yaani akgaeuza uso wa fadhi kando nae, kwa dalili ya mapokezi mengine kuhusina na hadithi hii “mtume (saaw) akaushika uso wa Fadhl na kuugaeuza upande mwengine” A na amekipokea kisa hiki Ali bin Abi Talib (raa) na akonageza “Akasema Abbas : Ewe Mtume wa Allah kwanini umeigeuza shingo ya mtoto wa ammi yako? Akasema: Nimemuona barobaro wa kiume na msichana na sikuamini sheitani juu yao”. Na kwa hayo yabainika kua mtume (saaw) aliugeuza uso wa fadhl mbali na khathamiya kusitiri uso wake, na ilikua unaonekana kwake, na lau kama fitna ni haramu juu ya yule anefitinisha, mtume (saaw) angaemuamrisha khathamia kusitiri uso wake baada ya kuhakikisha mwangalio wa fadhl kua ni muangalio wa fitna. Lakini hakumuamrisha bali aliigeuza shingo ya fadhl, yote hayo yaonesha kua ni haramu juu ya anaeangalia na sio anaeangaliwa. Kwa hivyo kuharamisha kufitinishwa watu na mwanamke haikupokewa na nass iliyo muharamishia mwanamke analo fitirisha nalo, bali nass iliopokewa ni ya kutomuharamishia yeye. Kwa hivyo haitakua ni haramu, hata lau kama ni jambo ambalo linapelekea katika haramu. Na ni juu ya serikali kusimamia mambo ya ummah na kuwaondosha wat maalum ambao watu wengine wanaofitishwa nao ili wanafitinisha wasiwe karibu na wanafitinishwa. Iwapo fitna ya imeenea kwa watu amah, kama alivyofanya Umar bin Al-Khattab kwa Nasr bin Hajjaj alipomsafirisha mpaka Basra kwa kuwafitinisha wanawake kwa uzuri wake. Na hili ni jambo limeenea katika wanume na wanawake kwa haifai kuharamishwa juu ya wanawake kudhihirisha uso kwa kuogopea fitna, hata lau kama itapatikana fitna, kwa hivyo hayawi hayo kwa upande wa – “wasila ilal haram muharram”.

### Mwanamke na mwanamume mbele ya majukumu ya kisharia

Wakati uislamu ulipokuja na majukumu ya kisharia ambayo amekalifisha nayo mwanamke na mwanamume, na wakati ukabainisha hukmu za kisheria ambayo husuluhisha vitendo nya killa mmoja kati yao, haukuangalia suala la usawa au ubora kati yao mtazamo wowote, wala kuchunga kwa namna yoyote ile. Bali uliona kama kuna tatizo maalum linlotaka kutatuliwa, na kutatua kwa mzingatio wa tatiozo maalum billa ya kungalia asili yake ni la mwanamke au ni tatizo la mwanamume. Kwa hivyo ukatibu kwa kua ni kitendo cha mwanadamu yaani kwa tatizo lilolotokeza, na sio tatizo la mwanamume au mwanamke. Kwa hivyo halikuwepo suala la usawa kutokua sawa baina ya mwanamume na mwanamke ni suala la utafiti. Na neno hili halipo katiak sharia ya Kiislamu, bali liliopo ni hukm ya sheria la tukio lililotokeza kutoka kwa mwanadamu fulani, sawa awe ni mwanamume au mwanamke.

Kwa hivyo hamna usawa baina ya mwanmume na mwanamke ni suala la utafiti, wala sio suala lina mlango katika nidhamu ya kijamii, kwa sababu asli ya mwanamke ni sawa na mwanamume au asli ya mwanamume ni sawa na mwanamke na sio jambo ambalo lin aathari kwa mwenye akili katika maisha ya kihjamii, na sio tatizo linalotarajiwa kutokea kati ya maisha ya kiislamu, na hayakua maneno haya illa ni maneno yaliopo katiak umagharibi, wala hakuamiongo mwa waislamu anayasema hayo isipo kua anaiga wamagharibi, ambao walikua wanamnyima mwanamke haki zake za kimaumbile kwakumzingatia ni mwanadamu, kwa hivyo akaanza kupigania haki hizo na ikachukua mkondo wa utafiti wa usawa kua ndio njia ya kupata haki hiyo. Ama uislamu haua kitu na vilma hivi kwa sababu umesimamisha nidhamu yake juu ya msingi thabiti inaodhamini kushikamana kwa jamaa na mujtamaa na kunyanya, na kumpatia mwanamke na mwanamume mafanikio ya kihakika anaostahiki kwa utukufu wa uwandamu ambayo Allah (swt) amemtukuza nayo kwa qauli yake:

{...وَلَقَدْ كَرِمَنَا بْنَيَ آدَمَ ...}(الإِسْرَاءُ: 70)

"Kwa hakika tumemtukuza mwanadamu" (Isra-70).

Kwa hivyo uislamu wakati ulipompatia mwanamke haki na kumpatia yeye majukumu, na kumpatia mwanamume haki na kukmpatia yeye majukumu, uliweka haki na majukumu yanaohusiana na maslahi yao kama vile alivyoonelea mteremsha sharia, na utatuzi wa matendo yao kwa mzingatio ni kitendo maalum ya mwanadamu maalum. Na ukaifanya ni moja wakati ilipohitajika kwa umbile la mwanadamu, na kuifanya ni maalum wakati ilipohitajika na killa moja kati yao kwa tafauti hiyo. Na usawa huu katika haki na majukum haiambiwi kua ni usawa, vile vile haimbiwi kutokua sawa, vile vile tafauti hiyo katika haki na majukumu haikusudiwi hayo kutokua sawa au usawa, kwa sababu wakati unapoangalia jamaa wawe ni wanaume au wanawake kakika huuangalia kwa mzingatio wa kikundi cha wanadamu na sio mwangalio mwengine, na katiak umbile la kikundi cha wanadamu uta jumuisha wanaume na wanawake amesema Allah (swt):

{ يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ... } (النساء: 1)

*“Enyi watu mcheni mola wenu ambae amewaumbeni kutokamana na nafsi moja, na akaamumba kutokamana haya mkewe na akatoa kutokomana nao wawili wanaume wengi na wanawke” (Nsia – 1)*

Na kwa mtazamo huu akafaradhisha majukumu ya kisheria, na kwa mujibu wa mtazamo huu ukweka haki na majukumu kwa wanaume na wanawake. Kwa hivyo wakati zinapokua haki hizi na majukumu hiyo ya kibinadamu, yaani wakati yanoapokuja majukumu ni majukumu yanayohusiana na mwanadamu kama mwanadamu utapata kuna usawa katika haki hizi na majukumu, yaani utakuta usawa katika majukum, zitakua haki na majukumu ya killa moja na juu ya killa moja katika mwanamke na mwanamume ni moja hamna tofauti wa upambanuzi, yaani yanakua majukumu ni moja kwa wanaume na wanawake sawa sawa. Na mpaka hapa utakua uislamu haukutafautisha katika kumlingania mwanadamu katika iman baina ya mwanamume na mwanamke, na haukutafautisha katika

mjukumu ya kubeba ulinganizi wa uislamu baina ya mwanamume na mwanamke. Na kufanywa majukumu yanayohusiana na ibadati kama swalah na saumu na Hajj na zakah ni sawa kwa upande wa majukumu na kulazimisha na kujipamba na mazuri ambayo yamekuja kupitia Ahkam za sheria tabia njema kwa wanaume na wanawake kwa usawa na kuwekwa hukm za muamalat kama kuuza na kuajiri na kuwakilisha na ulezi na mengineo katika muamalat yanaohusiana na mwanadamu sawa kwa wanaume na wanawake, na kuweka adhabu kwa anahalifu hukm za Allah (swt) kama adhabu (hudud) uhalifu (Jinayaat) kuanzirisha (Ta'azeer) kwa mwanamume na mwanamke bila ya tafauti baina yao kwa kuwazingatia ni wanadamu na ukawajibisha kusoma na kusomesha juu ya wasilamu bila ya tofauti baina yao kwa kuwazingatia ni wanawadmu na ukawajibisha kusoma na kusomesha juu ya waislamu billa ya tofauti baina ya wanaume na wanawake. Na hivi ndivyo Allah (swt) amefaradhisha hukm zote zinazohusiana na mwanadamu kama mwanadamu ni sawa kwa mwanamume na mwanamke. Kwa hivyo yamekua majukumu kwa upande huu ni sawa na zimekua haki na majukumu ni sawa. Na pamoja na hayo aya na hadithi ambazo zimetaja mfano wa hikm hizi zimekuja amah zimejumuisha wanadamu kama mwanadamu, na mumini kama mumini kwani nyangi katika aya zimetaja majukumau ni ya mwanamume na mwanamke, amesema Allah (swt):

**{إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَالْقَانِتِينَ وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ وَالصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَاسِعِينَ وَالْخَاسِعَاتِ وَالْمُتَصَدِّقِينَ وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّائِمِينَ وَالصَّائِمَاتِ وَالْحَافِظِينَ فَرُوْجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا} (الأحزاب: 35)**

*“Hakika waislamu wanaume na waislamu wanawake na waumini wanaume na waumini wanawake na wanyenyekemu wanaume na wanyekemu wanawake na wakweli wanaume na wakweli wanawake na wasubirivu wanaume na wasubirivu wanawake a wanaogopa wanaume na wanogopa wanawake na wanaotoa sadaqa wanaume na wanotoa sadaqa waawake na wanaofunga wanume na wanofunga wanawake na wanohifadhi*

*tupu wanaume na wanahifadhi tupu wanawake na wanomtaja Allah kwa uwingi wanaume na wanaomkumbuka Allah wanawake. Allah amewaandalia wao msamaha na maliapo makubwa”* (Az-hab – 35) na amesema Allah (swt):

{ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ... } (الأحزاب: 36)

“*Haifai kwa mumin mwanmume wala mumin mwanamke Allah na Mtume wake wanpoamua jambo wawe na khiyari katika jambo lao*” (Ahzab-36) na amesema Allah (swt):

{ مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ اُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُنْجِينَهُ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ } (النحل: 97)

“*Yoyote akakae tendo mema awe ni mume au mke hali ya kua nimumini tukampa yeye maisha mazuri na kwa hakika tutawalipa wao mazuri zaidi nay ale waliokua wakiyatenda*” (Nahl-97) na amesema Allah (swt):

{ وَمَنْ يَعْمَلْ مِنْ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ اُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُونَ نَقِيرًا } (النساء: 124)

“*Na yoyote atake tendo mema awe ni mume au mke hali ya kua ni mumin, hao ndio waakao ingia peopni wala hawatadhumiwa chochote*” (Nisa-124) na akasema Allah (swt):

{ فَاسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيقُ عَمَلَ عَامِلٍ مِنْكُمْ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ اُنْثَى بَعْضُكُمْ مِنْ بَعْضٍ } (آل عمران: 195)

“*Akawaitikia wao mola wao hakika mimi sitapoteza kitendo cha anaetenda mionganii mwenu awe ni mume au mke nyinyi kwa nyini*” (Imran-195) na akasema

{ لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ نَصِيبًا مَفْرُوضًا } (النساء: 7)

“*Wanaume wana fungu kaitka walioachia wazee wawili na jamii na wanawake wana fungu katika walioacha wazee wawili n ajamii, iwe ni kidodogo au kingi fungu lilolofaradhishwa*” (Nisa-7) na akasema

{ لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبُوا وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبْنَ ... } (النساء: 32)

*“Wanaume wana fungu katika walilolituma na wanawake wana fungu kaitka walilotituma”* (Nisa-32) hivi ndivyo tunakuta hukm zote za kisheria zinazohusiana na mwanadamu kama mwandamu vovote ziwazo hukm hizo na namana zinavotafautiana na kua uwingi Allah amezifaradhisha sawa kwa mwanamume na mwanamke sawa kwa sawa, isipokuwa haya haya hayachukuliwi ni usawa naina ya mwanamume na mwanamke, bali hizo ni hukm zimefaradhiwa mwanadamu, ni za mwanamume na mwanamke kwa usawa, kwa sababu wote wao ni wanadamu. Na hukm hizi ni uzungumzi kutoka kwa Allah (swt) zinzohusiana na matendo ya mwanadamu.

Na wakati yanapokua haki hizi na wajibati na majukumu haya ya kisheria zinahusiana na mwanamke kwa umbile lake la kike na kwa asli ya mahli pake kati mujtamaa, au zinahusiana na mwanamume kwa umbile lake la uume na asili ya mahli pake katika mujtam'a, zitakua haki hizi na wajibaat yaani majukumu haya tafauti kati ya mume na mke, kwa sababu sio utatuzi wa mwanadamu kabisa, bali ni utatuzi wa aina hiyo katika mwanadamu ambae ana aina ya umbile la uwandamu tafauti na aina nyengine, kwa hivyo hamna budi iwe ni tiba ya aina hii katiak mwandamu, na sio killa mwandamu, kwa hivyo ikawekwa wa wanawake wawili kwa ushahidi wa mwanmume mmoja katika shughuli ambazo huwa na kikundi cha wanaume na katiak maisha jumla katiak ushahidi wake juu ya haki na mualmalat amesema Allah (swt):

{وَاسْتَشْهُدُوا شَهِيدَيْنِ مِنْ رِجَالٍ كُمْ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَامْرَأَتَانِ مِمَّنْ تَرْضَوْنَ  
مِنْ الشُّهَدَاءِ أَنْ تَضْلِلَ إِحْدَاهُمَا فَتَذَكَّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى } (البقرة: 282)

*“Na watoe ushahidi mashahidi wawili katika wanume wenu na wasipo kuwepo wanume wawili basi mume mmoja na wanawake wawili katiak munaowaridhia katiak ushahidi akisahau mmoja wa pili wao atamkumbuksha mwengine”* (Baqrah – 282). Na hukubaliwa ushahidi wa wanawake pekee katiak mabo ambayo hupatikana katika kikundi cha wanawake pekee bila ya kuwepo wanaume humo, kama makosa yaliofanyika katika sehemu za kuoga (hammam) za wanawake na hutosheleza ushahidi wa

mwanamke mmoja ambaye hayaeleweki illa na wanawake, kama ushahidi wa ubikira na ukekuu ya kunyonyesha, kwa sababu Mtume (saaw) alikubali ushahidi wa mwanmke mmoja katika kunyonyesha, na uislamu ukamuekea fungu mwanmake katiak mirathi nusu ya fungu la mwanamume katika baadhi ya hali amesema Allah (swt):

**{ يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِذِكْرِ مِثْنَ حَظِ الْأَنْثَيْنِ ... } (النساء: 11)**

“Anawausia Allah katika watoto wenu kwa mwanamume mara mbili ya mwanmke” (Nisa-11) na haya kwa familia (Asaba) kama watoto wa ndugu na ndugu kwa baba kwa sababu ukweli wa mwanamke katika hayo usimamizi wake ni juu ya kakake iwapo ni faqiri hata lau kama ni mweza wa kazi, na pia ikawekwa fungu la mwanamke kama fungu la mwanamume kaitka hli nyengine, amesema Alah (swt):

**{ وَإِنْ كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ كَلَالَةً أَوْ امْرَأَةٌ وَلَهُ أَخٌ أَوْ أُخْتٌ فَلِكُلٍِّ وَاحِدٍ مِنْهُمَا السُّدُسُ فَإِنْ كَانُوا أَكْثَرُ مِنْ ذَلِكَ فَهُمْ شُرَكَاءٌ فِي الْثُلُثِ } (النساء: 12)**

“Na iwapo mwanamume au mwanamke hana kalala (mtoto au mzazi) lakini ana ndugu wakiume au ndugu wa kike basi killa mmoja kati yao apate sudus (1/6) na iwapo ni zaidi ya hao basi watashirikiana katrak thuluth (1/3). (Baqarah: 12) Na hili ni katika ndugu wa mama kwa sababu kaklah ni yule aliekatikiwa hana msingi wala mitagaa wala ndugu au ndugu wa baba, kwa hivyo yaeleweka kua muradi wa kaka au dada ni ndugu wa upande wa mama. Na ukweli mwanamke katiak hali hiyo usimamizi wake sio wajibu juu ya ndugu wa mama, kwa sababu hata kama ni mahram lakini sio wajibu usimamizi kua juu yake.

Na uislamu ukaamrisha vazi la mwanamke kua tofauti na vazi la mwanamke, vile vile ukaamrisha kua vazi la mwanamume liwe tofauti na vazi la mwanamke. Na akakatazwa mmoja wao kushabihiana na mwengine katiak vazi, kulingana linavomhusu na kumtafautisha na mwengine, kama kurembesha baadhi vingu vya mwili. Imepokwea kutoka Abu Hurairah (raa) amesema “Mtume (saaw) amemlaani mwanamume anevaa vazi la mwanamke na mwanamke anevaa vazi la mwanaume”. Na

imepokewa kutoka kwa Ibn Abi Muleikah amesema: aliulizwa Aisha (raa) “Mwanamke kuva viatu (boots)? Akasema: amewalaani Mtume (saaw) wanawake wanojifananisha na wanume” Na imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Amru amesema: Nilimsikia Mtume (saaw) akisema “Sio katika sisi wanawake wanaejifananisha na wanaume” Na imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas “Mtume (saaw) amewalaani makhanithi katika wanaume na wanake wanao jifananisha na wanaume”. Na akasema “Watowni wao kaitka majumba yenu” akasema Mtume (saaw) akamtoa Fulani na Umar akamtoa fualni “na katika maneno mengine “Mtume (saaw) amewalaani wanaume wanjifananisha na wanawake na wanawake wanajifananisha na wanaume”.

Na uislamu ukaweka sadaq yaani mahari ya mwanmke juu ya mwanamume, na kuifanya ni haki yake juu ya mtume, pamoja na kwamba starehe ni yao wao wote na sio ya mwanamume pekee. Na amesema Allah (swt):

{ وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدَقَاتِهِنَّ نِحْلَةً فَإِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِيَّا مَرِينَا }  
(النساء: 4)

“Na wapatiensi wanawake mahari yao na wakiwapatia kitu katika hicho basi kuleni kwa furaha na utulivu” (Nsa-4) na maana ya nihlan ni Tunu kwa hivyo sadaq yao. Na amesema (saaw) kumuambia yule aliemuozesha: “Jee una kitu umpatie mahari? Atafuta tafuta na hakupata, akasema: angalia angalia hata lau kama ni pee ya chuma na hakupata kitu na akmuozesha kwa alichonacho katika Qur'an”.

Na Allah (swt) akaifanya kazi ya kutuma mali ni faradhi juu ya wanaume, na hakuifanya faradhi juu ya wanawake bali ni mubah kwakw, akitaka atafanya kazi na ikiwa hataki hatafanya. Amesema Allah (swt):

{ لِيُنْفِقْ ذُو سَعَةٍ مِّنْ سَعَتِهِ ... } (الطلاق: 7)

“Na atoe killa mwenye uwezo kulingana na uwezo wake”. (Talaq – 7) na neno DHU haitumiwi illa kwa wanaume na aksema:

{ وَعَلَى الْمُولُودِ لَهُ رِزْقٌ هُنَّ وَكُسُوتُهُنَّ } (البقرة 230)

“Na ni juu ya mzazi riziqi yao na mavazi yao” (Baqarah-230 na ikafanywa usimamizi ni juu ya mume.

Na uslamu ukaweka suala la usimamizi wa wanawake juu ya wanaume, na wakapewa wao uongozi na kuamrisha na kukataza, amesema Allah (swt)

{ الرِّجَالُ قَوَامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ وَبِمَا أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ فَالصَّالِحَاتُ قَانِتَاتٍ حَافِظَاتٍ لِلْغَيْبِ بِمَا حَفَظَ اللَّهُ وَاللَّاتِي تَحْافُونَ نُشُورُهُنَّ فَعَظُوْهُنَّ وَاهْجُرُوهُنَّ فِي الْمَضَاجِعِ وَاضْرِبُوهُنَّ فَإِنْ أَطَعْنَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْهَا كَبِيرًا } (النساء: 34)

“Wanaume ni wasimamizi juu ya wanawake, na kwa vile alivywafanya baadhi yao kua bora kuliko baadhi na kwa kile wanachotoa katika mali yalo, kwa hivyo wanawake wema ni wanyenyeketu na watiifu na wanajihifadhi katika siri kua Allah Amewaaamrisha wahihifadhi, na ambao mnachelea kutoka katiak utiifu wapeni mawaidha, muwaguse katika malazi na wapiaeni, na wakiwatii basi musiwatafutei njia hakika Allah ndie alie juu na mkubwa” (Nisa-34) Na ameeleza kua usimamizi ni wa wanaume kwa yale majukumu ya ziada kam utawala na uimam wa Swlah, na wali (usimimizi) katika ndoa na ikawekwa talaqa katika mkono wake amesema Allah (swt):

{... بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ... } (النساء: 34)

“Kwa vile alivyowafanya baadhi yao bora juu ya baadhi” (Nisa-34) na imekua usimamizi huu pia kwa wa hupewa katika majukumu ya matumizi kama mchari, na matumizi na akasema Allah (swt):

{... وَبِمَا أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ... } (النساء: 34)

“Na kwa kile wanachotoa katika mali yao” (Nisa-34) vile vile mume amepewa haki ya kumrekebisha mkewe kwa kumpa mawaidha na kumgura katika malazi na kumpiga bila ta kumjeruhi kwa kiwango cha dhambi aliotenda, na akiasi. Na akapewa mwanamke haki ya ulezi wa mtoto awe wa kiume au wa kike na kunyimwa haki hiyo mwanamume. Na akapewa mwanamke moja moja kutuia juu ya mtoto, iwapo atadharau babake au kuwakhini wao, na kunyimwa haki hiyo katika hali

hiyo, alikuja Hind kwa Mtume (saaw) na akasema “Ewe Mtume wa Allah hakika Abu Sufyan ni mtu bakhili, hanipati mimi n watoto wangu matumizi ya kutosha, akasema: chuku kinachokutosha wewe na watoto waki kwa uzuri” na hakimu atamlazimisha yeye kutoa matumizi ya kutosha na kumpa mwanamke kusimamia moja kwa moja, na hakubaliwi yeye kufanya hivyo.

Na hivyo ndivyo uislamu ukaja na hukmu tofauti baadhi ni makhus za wanaume na baadhi ni makhsus za wanawake na akatafautisha baina ya wanaume na wanawake katika sehemu zake, na akaamrisha killa mmoja wao aridhike na yale aliofanyiwa takhsees katika hukmu za Allah, na akawakataza kuhusudiana na kutamani yale ambayo Allah (swt) aliyoafadhilisha nayo baadhi yao juu ya baadhi nyengine:

﴿ وَلَا تَتَمَنُوا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبُوا وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبْنَ ... ﴾ (النساء: 32)

“*Na wala musitamani yale ambayo Allah amewafadhilisha nayo baadhi yenu juu ya baadhi, wanaume wana fungu katika walioyatuma*” (Nisa-32). Na takhsees hii katika hukm haimaanishi ukiosefu wa usawa, bali ni utatuzi wa matendo ya mwanamke kwa umbile lake la uuke, na ni uttuzi wa viedo vya mwanameume kwa umbile lake la uume, na yote yametatuliwa kwa uzungumzi inaohusiana na matendo ya waja, na zikiangaliwa uhakika wake yabainika kua ni tutauzi wa tatizo wa aina ya mwanadamu kwa aina yake, na hamna budi itafautiane na utatuzi wa mwanadamu kama mwanadamu. Na heri kutiliwa maanani suala la usawa au ubora kwa sababu si pahali wa kufanya utafiti, bali imetiliwa maanani kuwa ni utatuzi maalum, la tiatizo maalum, la mwanadamu maalum. Huu ni upande wa tofauti katika hukmu kati ya mwanamume na mwanamke katika zilizopokewa katiak hukmu tofauti, na kwa namna yoyote ni utatuzi wa tatizo la mwanadamu, iwe ni utatuzi moja kwa killa mmoja mwanamume au mwanamke kama kutafuta ilimu ama iwe tafauti yake baina yao kwao upande wa mwanamume na kwa upande wa mwanamke, na haya maanishi

tafauti ya ubora na usawa au kutokua sawa. Ama yaliopokewa katika maneno (Athaar) kua wanawake ni wapugufu wa akili na dini, hayo hukusudiwa kwa kuzingatia athari inaotokamana kwa munasaba wa akili na dini, na sio maana yake, wana upungufu wa akili au upungufu wa dini. Kwa sababu akili ni moja kwa mujibu wa asili ya killa moja mwanamume na mwanamke, na dini ni moja kwa mujibu wa iman na matendo ya killah moja mwanamume na mwanamke. Na muradi wa maneno hayo ni upungufu kwa mujibu wa ushahidi wa mwanamke, kwa kufanywa ushahidi wa wanawake wawili kua ushahidi wa mwanamume moja, na upungufu wa masiku ya swalah kwa mwanamke kwa kutoswali katika siku ya heidhi katika killa mwezi na masiku ya heidhi na nifas katika mwezi wa ramadhani.

Hayo ndio maudhui ya haki na majukumu, yaani majukumu ya kisheria alioyafaradhishe Allah (swt) juu ya mwanadamu kwa umbile lake la uwanadamu, na ya killa aina katika aina mbili ya mwanadamu: mume na mke, lakini kwa mzingatio wa aina katika aina ya mwanadamu alie na sifa za uwanadamu na sifa ya aina katika sheria, na wala haikukusudiwa kumtafautisha moja wao na mwengine wala kutiliwa umuhimu wowote kuhusu suala la usawa kutokua na usawa.

### Kazi za mwanamke

Asli ya mtazamo wa Kiislamu wa kisheria inafanya vitendo ambayo anavitekeleza mwanadamu kwa umbile lake la uwanadamu ni mubari kwa killa mmoja wao kwa mwanamume na mwanamke sawa sawa, billa ya tafauti baina yao, au kumpambanua mmoja wao na mwengine na kuyafanya matendo hayo kua ni faradhi au haramu au ya kuchukiza au kupendekeza (Mandub) billa ya tafauti yoyote au upambanufu kati yao. Ama vitendo ambavyo anavyovitekeleza mwanamume kwa sifa yake ya uume mwenye sifa ya uwanadamu na anavovitekeleza mwanamke kwa sifa ya uuve mwenye sifa ya uwanadamu. Kwa sababu shraa amewatafautisha baina yao ni kwa upande uwajibu au uharamu au uchukivu au kupendekeza au kuruhusu. Na

mpaka hapa tunapata kua utawala na uongozi shoraa imewapatia wanaume na sio wanawake, tunaipata kua ulezi wa watoto wawe ni wa kiume au wa kike wameptiwa wanawake na sio wanaume. Kwa hivyo hamna budi yawakilishwe matendo yanaohusiana na mwanamke kwa sifa za uu ke kwa wanawake, na pia yawa kilishwe matendo yanaohusiana na mwanamume kwa sifa za uume kwa mwanamume. Kwa kua ndie alieuumba mume na mke ni muelewe zaidi, kwa yale ambayo ni katika mambo ya mwanamume au mambo ya mwanamke, kwa hivyo hamna budi kusimama katika mipaka ya hukmu ambayo imefaradhishwa billa yakuivuka, iwe ni kwa wanaume pekee yao au kwa wanawake peke yao au kwa wanadamu billa ya kujali asli yake mume au mke, kwa sababu yeye ni muelewa yalio na maslahi kwa mwanadamu. Kwa hivyo kutumia akili kunyimwa mwanamke katiak amali kwa hujja sio katika mambo yake, au kupewa amali zinazohusu mwanamume kwa mzingatio kua mgawanyo huo ni uadilifu kwa mwanamke, na kuleta uadilifu baina yake na mwanamume, yote hayo ni kukeuka sharaa, na makosa makubwa na sababu ya ufisidifu.

Na sheria imemfanya mwanamke ni mama na msimamizi wa nyumba, na hukmu zinazohusiana na mamba na hukmu zinazohusiana na mazazi na hukmy zinazohusiana na kunyonyesha na hukmu zinazohusiana na ulezi na hukmu zinazohusiana na eda. Na mwanamume hakuhushishwa katika hayo na kitu chochote kwa sababu hukmu hizi zahusiana na mwanamke kwa umbile lake la uu ke, kw ahivyo akapewa majukumu ya mtoto kama mamba na kuzaa na kunyonyesha na ulezi. Na yakawa majukumu yake muhimu na majukumu makubwa. Na mpaka yavezekana kusemwa kasi asli ya mwanamke ni kua yeye ni mama na mke nyumbani, kwa sababu katika shughuli hizi ni kuendeleza kizazi cha mwanadamu na kwa sababu ni makhsusi kwake billa ya mwanamume kwa hivyo ni wajibu iwe wazi kwa vovote itakavolekezwa kwa mwanamke katika shughuli na vovote itavobandikizwa juu yake katika majukumu, ni wajibu ibakie shughuli zake za asli kama mama na mlezi wa watoto. Na kwa hivyo tunapata kua mteremsha

sheria amemruhusu yeye kula katika ramadhani hali ya kua amebeba mamba au ananyonyesha na kumsamehe swalah katika hali ya hedhi na nifas, na kumkataza mwanamume kusafiri mji mwengine na mtoto wake madamu mama anamlea, yote hayo ni kwa ajili ya kumkamilisha kazi yake ya asli nao ni mama na mlezi wa nyumba.

Isipokuwa haimaanishi kwa asli ya kazi ni mama na mke nyumbani basi atafungika katika kazi hizo, na amekatazwa kujishughulisha kati kazi zisizo kua hizo, bali maana yake ni kua Allah (swt) amemuumba wanawake ili mume apate utulivu kwake na ili apate kuleta kuzaa na watoto, amesema Allah (swt):

﴿ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَجَعَلَ لَكُم مِنْ أَزْوَاجِكُمْ بَنِينَ وَحَدَّةً . ﴾ {النحل: 72}

“Na Allah amewaekea nyinyi wake kutokamana na nafsi zenu, na akawajaalia nyinyi kutokamana na wake zenu watoto wa wajukuu” (Nahl-72) na akasema:

﴿ مِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا... ﴾ {روم: 21}

“Na ni katika alama zake amewaumbia nyinyi kutokamana na nafsi zenu wake ili mupate utulivu kwao” (Rum-21) lakini wakati huo huo amemuumba ili ashughulike katika maisha jumla, kama anavoshughulika katika maisha yake. Na akamruhusu yeye kuuza, na kukodisha na kuwakilisha. Na akamharamishia yeye urongio na ulaghai na khiyanah. Kama yule yaliofaradhishwa hayo juu ya mwanamume na kuruhusiwa kujishughulisha na ukulima na usanii kama kujishughulisha na biashara na kusimamia mikataba n akumiliki killa aina ya umilikaji na kukuza mali yake, na kutekeleza mambo yake katika maisha yaye binafsi na kua mshirika au muajiriwa na pia kuajiri watu na kukodisha mali isohama (nyumba au ardhi) na vitu na kutekeleza killa aina ya muamatat. Na hiyo ni kwa ujumla wa uzungumzi wa mteremsha sheria na billa ya takhsees ya kumkataza mwanamke; isipokuwa haifai kwa mwanamke kusimamia utawala, haifai kua ni kiongozi wa serikali au

msaidizi (Muawin) wala walii (Mkuu wa wilaya) wa Meya (Amil) au shughuli yoyote ambayo inatambuliwa ni za utawala, kulinana na yaliopokewa na Abi Bakrah amesema: “Zilipomfikia Mtume (saaw) khabari kua watu wa fursi wamemtawalisha juu yao bint ya Kisra, alisema: “hawatafaulu watu watakao simamiwa mambo yao na mwanamke”. Na hili lipo katika kukataza mwanamke kusimamia utawala kwa kuwakemea ambao wanegemezq mambo yao kwa wanawake. Na waliyul-Amir ni mtawala amesema Allah (S.w.t)

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ لِمَنْ كُنْتُمْ } (النساء: 59)

“Enyi mulioamini mtiini Allah na mumtii Mtume na watawala mionganii mwenu” (Nisa-59) kwa hivyo kusimamia utawala haifai kwa mwanamke, ama kisicho kua utawala yafaa kwa mwanamke kusimamia. Kwa hivyo inafaa kwa mwanamke kusaidia katika kazi za serikali, kwa sababu si katika utawala lakini inaingia katika mlango wa kuajiriwa, kwa hivyo muajiriwa ni muajiriwa maalum wa serikali na ni kuajirwa na mtu yoyote au shirika, na inafaa kwake kusimamia uhakimu (qadhi) kwa sababu hakimu sio mtawala bali ni mtatuzi wa matesi baina ya watu, na kuwalazimisha watesi kushikamana na hukm sharii kwa namna ya ufaradhi. Kwa hivyo inajulikana kua uhakimu ni kuelezea hukumu kwa njia ya kuilazimisha. Kwa hivyo hakimu ni muajiriwa wala sio mtawala basi yeye ni muajiriwa wa serikali kama kuanjiriwa vengine. Na imepokewa kutoka kwa Umar bin Al-Khattab kua yeye alimweka shotaa – mwanamke katika jamii yake – sokoni yaani qadhi hisbah ambae anatatua juu ya matatizo yote. Na suala la mwanamke kufaa kua hakimu linafungamano na nass ya hadithi na utabikishaji wake juu ya jukumu la hakimu, na ikichukua hadithi muelekeo wa kukataa mwanamke kua hakimu itakua haifai, na isipochukua mwelekeo huo basi hadithi haitakua ni dalili ya kumkataza yeye kua hakimu. Na tukiangalia hadithi tutakua Mtume (saaw) amewakemea watu ambao mambo yao wanasihamiwa na mwanamke, na ni jawabu ya yaliomfikia kua watu wa fursi wamemtawalisha juu yao mwanamke, kwa hivyo ni maelezo juu ya khabari, na ni jawabu juu ya suala. Kwa hivyo ilikua ni khassa katika sual la khabari ilikua ni utawala yaani

uongozi wa serikali na maelezo yalikua ni juu ya hayo, kwa hivyoo ni khassa kuhusiana na uongozi wa serikali na kwa maana ya utawala. Huu ni upande moja na kwa upande mwengine ni kua ukataza imejengwa juu ya utawala jumla (amah) kwa sababu ni usimamizi wa mabo. Haya ndio maana ya hadithi yale amayo yaelezea. Ama suala la uhakimu hiyo ni kazi inafautiana na kazi ya khalifa na kazi ya meya. Kwani kazi ya khalifah na kazi ya meya ni kutekeleza hukmu moja kwa moja kwa upande wake liwe suala limepelekwa kwake, au kupelekwa hukmu ya hakimu kwake au asipelekewe na yoyote suala, ambalo ameliona ni kinyume na sheria, kwa hivyo atahukumu dhidi ya mhalifu bila y mlalamishi n aktoka hukmu juu yake na ni yenye kutekelezwa. Ama hakimu yeye hawezi kutoa hukumu isipokuwa yapelekwe ulalamishi, yaani mtu apelike malalamishi yake kwake, na kuwe na walalamishi kwa hivyo atahukumu iwatio itapatikana ulalamishi, na neno lake jambo iwapo hatakua na mlalamishi. Na uchunguzi wake juu ya sual na kelezea hukmu ya Allah kusiana na suala hilo kwa njia ya kuvilazimisha na hana uwezo wa kuitekeleza kabisa, isipokua lau atawekwa kama mtawala na hakimu na wakati huo ataitekeleza kama mtawala na hakimu na wakati huo ataitekeleza kama mtawala na kuhukumu kama hakimu. Kwa hivyo uhakika wa uhakimu ni tafauti na uhakika wa utawala, na hadithi haingii katika hakimu. Na juu ya hayo uhakimu sio usimamizi juu ya mtu yoyote katika watu wan chi ambayo yeye amewekwa kama hakimu, wala hana usimamizi wowote hata juu ya walalamishi. Wala si wajibu kumtii yeye, bali ni wajibu kuitekeleza hukmu yake wakati anapohukumu katika sual kwa sababu ni hukmu ya Allah, na sio kwa sababu ni amri ya hakimu na haizingatiwi kua ni hukmu yake ni hukmu ya hakimu isipokua anapohukumu katika baraza la mahakimu. Kwa hivyo haizingatiwi kushuhudia kwake kwa tukio, au kusikia kwake kua na uzito nje ya Baraza la mahakimu kufaa kuhukumu kulingana aliyashuhudia au alioyasikia, madam hayataku hayo katika baraza la mahakimu. Tafauti na kiongozi ni wajibu kutiiwa katika killa hali na hana baraza maalum la hukumu. Bali atasimamia utawala katika nyumba yake na katika barabara

katiak makao makuu ya serikali na killa mahali, na ni wajibu kumtii, amesema (saaw) "Yoyote anaemtii kiongozi (Amir) basi amenitii mimi" Kwa hivyo hadithi ya kukataza kumtawalisha mwanamke haingiliani na kazi ya hakimu kabisa, hivyo basi uhakimu haukukatzwa juu ya mwanamke kupitia hadithi hii. Na uhakika wa hakimu yeye ni muajiriwa na mtawala, aliemuajiri kwa mshahara maalum juu ya kazi maalum, na neno Ajir (ajira) limekuka katika hadithi sahihi linakusnaya killah ajira yaani kazi, na iwapo mwalimu wa qur'an Mtume (saaw) alimzingatia kama muajiriwa na akasema (saaw) "Bora wa munyoyachukulia ujira juu yake ni kitab cha Allah (Kusomesha Qur'an)" basi hakimu pia kuzingatiwa ni muajiriwa na kile anachokichukua kutoka Bait-ul-Maal ni ujira wake. Na pia haisemwi kua hakumu ni msaidizi wa mtawala na atashirikiana nae katika utawala kwa sababu hakimu ni muajiriwa wa mtawala, na sio msaidizi wake, na wadhifa wake ni kufahamu uhakika wa tatizo baina ya watesi wawili, na kuelewa utabikishaji wa vifungu vyakununi katiak hali ya kutabani hukm ya kisheria au hukmu ya kisheria wazi katika hali ya kutabani, juu ya watakopatikana na hatia na wale ambao hawatapatikana na hatia, kwa hivyo yeye ni muajiriwa kwa ujira maalum juu ya kazi maalum.

Huu ni upande wa hakimu na muhtasib. Ama kwa upande wa hakimu wa maonevu (Qadhi al-madhalim) hiyo haifai Kwa mwanamke, kwa hivyo hajuzu kwake kwa mwanamke kusimamia mahakimu wa maonevu kwa sababu ni uatwala, au inaingia katika hadithi. Kwa sababu hupelekwa maonevu ambayo hupatikana kutoka kwa kiongozi ivu ya watu yawe malalamishi yamepelekwa au watu au yasipelekwe. Na hahitajii ulalamishi wa mlalamishi ivu ya mtwawala iwapo atamshtaki yoyote maonevu ni yake, bali inajuzu kwake kumuita akae mbele yake na pia inajuzu kwa asimuite. Kwa sababu sio suala la kueleza hukmu katika suala, bali ni kupelekwa mashtaka ambayo yanapatikana kutokamana na watawala juu ya watu. Kwa hivyo kiuhakika linafanana na kuondosha dhulma kua ni utawala, na kwa hayo hajuzu kwa mwanamke kusimamia.

Limebaki – suala la kufaa kwa mwanamke kua ni kiungo katika baraza la ummah katika hali ya kuwepo baraza la ummah au kutokuwepo, hilo huenda likafishika kwa baadhi yao, au kuhudhuria haifai kwa kulinganisha baraza la Ummah katika Uislamu juu ya baraza la wabunge katika demokrasia. Na kiukweli kuna tofauti kati ya baraza la wabunge katika nidhamu ya demokrasia na baraza la ummah katika Uislamu. Kwa hivyo baraza la wabunge ni katika utawala, kwa sababu katika milah ya demokrasia ia maana ya utawala kwani yeye ndie anaechagua kiongozi wa serikali na kumuuzulisha na ndio wanatoa kura ya imani, na kutoka kwao imani na kumuangusha kutoka utawala papo hapo. Na ukweli wa baraza la wabunge husimamia mambo matatus: la kwanza ni kuihisabu serikali na kuirekebisha, ya pili ni kutunga sheria, na yatatu kusimamisha watawala na kuwaangusha. Ama upande wa kuihisabu serika na kuikosoa sio katika utawala lakini kwa upande wa kutunga sheria na kuuzungusha watawala na kuwasimamisha yanazingatiwa na katika utawala na hayo ni tofauti na baraza la Ummah uhakika wake ni kumhisabu kiongozi na umkosoa na kudhihirisha ubaya kwa yaaohitajika kudhihirishwa, kama upungufu wa kusimamia mambo na kama ulegevu katika kutabikisha Uislamu au kuregea nyuma na kubeba ulinganizi wa kiislamu wa yanaofanyika na hayo. Lakini hatungi sheria wala kumsimamisha kiongozi wala kumuuzulisha kiongozi nao ni kinyume barza la wabunge, kwa hivyo haijuzu kwa mwanamke kua ni kiungo katika baraza la wabunge madamu huzigatiwa ni katika baraza la Ummah, kwa sababu sio katika utawala. Isipokuwa haimaanishi kua kutofaa kwa mwanamke kua kiungo baraza la wabunge basi haufai kwake kumchagua mtawala, kwa asliya kua ni kiungo katika baraza la wabunge yamfanya yeye kuwa katika utawala yaani miongoni mwawenye viongozi, na hili halifai, kwa usaraha wa kukataza hayo katika qauli yako (saaw) “hawatofaulu watu wanaosimamiwa mambo yao na Mwanamke” na hili ni kinyume na kuchagua kwake kiongozi kwani halimfanyi yeye kuwa katika watawala bali linamfanya yeye kuwa na haki ya kuchagua atakaemtawala. Na sharia imemruhusu mwanamke kumchagua kiongozi, na kumchagua mtu ye yeyote kwa kazi

yejote katika kazi za utawala, kwa sababu inafaa kwake kumbayiisha khalifah na kumpigia kwa. Imepokewa kutoka kwa Umm Atiyah amesema. “Tulimbayiishe Mtume (saaw) na akatusomea kua tusimshirikishe Allah na chochote na akatukataza kuomboleza, akazuia mwanamke mkono wake kati yetu na akasema; Fulani alinifurahisha na mimi nataka kumplipa. Na hakusema chochote akaondoka na kisha akarudi “na kumbayiisha Mtume (saaw) haikua ya Utume bali ilikuwa juu ya utiifu kwa utawala. Na hii yaonyesha kuwa infaa kwa mwanamke kumbayiisha kiongozi na kumchagua. Huu ni upande wa baraza la wabunge. Ama baraza la Ummah ni kinyume na hivyo kwa sababu ni baraza la kuchukua rain a kutoa rain a hana uwezo wa utawala, kwa hivyo hatachagua kiongozi illa Umma watakapo wakilisha nalo katika hayo na wala hatumuuzulisha kiongozi, na wala kutunga sheria na kazi yake yote yahusiana na rai. Kwa hivyo kazi ya baraza la Ummah ni kua serikali inairegelea kuchukua rai yake katika yanao itaka kutekeleza katika kazi za kindani na kuihisabu katika kinachoteklezwa katika kazi za kindani na zakiinje, au yeye mwenyewe kwa nafsi yake kuipatia rai katika mambo ya kindani au ya kiinje, na pia katika kazi zake ni kutoa rai yake kwa wagombezi wa cheo cha khilafah, na kudhihirisha uovu wa mawali na muawin, nao pia ni kupeona rai, na yote hayo yanaingia chii ya kutoa ushauri pekee, na halazimiziki khalifah kuifuata, kutoa rai yake katika atakayotabai khalifah katika hukmu. Na yote hayo ni rain a sio utawala. Kwa hivyo itakua kazi yake yahusiana na rai na si jengine.

Na viungo vya baraza la Ummah ni wawakilishi wa watu kwa rain a si jengine ni sio wawakilishi wao katika utawala sio katika kumsimamisha kiongozi illa Ummah watakapowakilisha wao alo katika hayo wala katika kumuuzulisha. Mpaka wakati wa watakapodhihirisha uovu wao kama wasaidizi na mawali hawawezi kuuzulishwa kwa rai yao pekee, lakini watauzulishwa na khalifah kwa rai yao, tofauti na baraza la wabunge kwani mawaziri wanauzulishwa hapo hapo wakati baraza la wabunge

watakapo kua hawana imani nao bila ya umuhimu wa kiongozi wa serikali kuuzulisha.

Na madamu vuingo vya baraza la Ummah ni wawakilishi katika rai basi mwanamke ana haki kutoa rai yake katika yote yale ambayo ni uweza wa baraza la Ummah, basi anaweza kutoa rai yake ya kisiasa nay a kiuchumi nay a kisheria na mengineo. Na pia ana haki ya kuwakilishwa na anemtaka ili kutoa rain a yeye kumuakilisha anaetaka ili yeye atoe rai hiyo. Na Uislamu umempatia yeye haki ya kutoa rai kama alivyopewa Mwanamume sawa kwa sawa, kwa hivyo shura katika Uislamu ni haki kwa mwanamume na mwanamke sawa sawa amesema (swt):

... وَشَاءُرْهُمْ فِي ... {آل عمران: 159}

“*Na uwashauri wao katika mambo*” (Imran – 159) na amemsema:

} وَأَمْرُهُمْ شُورَى بَيْنَهُمْ ... {الشورى: 38}

“*Na mambo yao hushauriana baina yao*” (Shura – 38) na hoyo ni maneno jumla (amm) yamejumuisha mwanamume na mwanamke. Na kuamrisha mema na kukataza maovu ni wajibu juu ya mwanamume na mwanamke sawa kwa sawa amesema (swt):

{ وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ } {آل عمران: 104}

“*Na kipatikane mionganini mwenu kikundi watakao lingania katika kheri (Uislamu) wa waamrishe mema na wakataze maovu*” (Imran-104) na amesema (saaw) “Yoyote atakae ona munkar na aondoshe “mpaka mwisho wa hadithi pia ni maneno jumla (amm) inajumlisha mwanamume na mwanamke – na kuwalisabu viongozi ni faradhi juu ya mwanamume na mwanamke, na Mtume (saaw) wakati aliposema “Dini ni nasaha, akaulizwa kwa nini ewe Mtume wa Allah, akasema ni kwa ajili ya Allah na Mtume wake na viongozi wa Waislamu na kwa wote wao (Ammah) “hakuifunga nasaha kwa wanaume bali kwa Waislamu kutoa nasaha kwa viongozi wa waislamu na kwa jumla yao (amah) ni sawa anaetoa awe ni Mwanamume au

mwanamke. Na ikiwa wanawake walimjadili Mtume na walimuuliza, ina maana wanaweza kumjadili au kuuliza Khalifah na wengineo wale ambao wana utawala mikononi mwao. Na imepokewa kuwa Mtume (saaw) baada ya kutoa waadhi kwa wanaume siku ya idi “Alikwenda mpaka kwa wanawake na akawa waadhi na kuwakumbusha na akasema toeni sadaqa kwani wangi wenu ni kuni za moto, akasimama mwanamke kati kati ya wanawake alien a matavu meusi, kwanini ewe Mtume wa Allah “mpaka mwisho wa hadithi,” pia yaonyeshwa kuwa mwanamke alimjadili Mtume na kumuuliza sababu ya kusema hayo kuhusu wao. Na kissa cha Khaulah bin Thaalabah ambae alikuja kwa Mtume (saaw) kumuuliza kuhusu dhihar (kumfananisha mke kama mama) na Mtume akamuambia sina la kukujibu kuhusiana na jambo lako na mwanamke akamjadili Mtume, kissa mashuhuri kilishatajwa katika Quran na akasema:

{ قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا } (المجادلة: 1)

“Ameshasikia Allah neno la anaekujadili kuhusiana na mumewe na amemshtakia Allah na Allah anasikia malumbano yanu” (Mujadala-1) na hili lipo saraha kuhusiana na mwanamke kumjadili Mtume, kwa hivyo hamna haja ya maneno ya ziada ya kumruhusu mwanamke kwa kutoa rai yake katika killa jambo, na kujadili, na hamna shubha kwa yoyote kuhusiana na hayo na walikwabaliana wote Ijmaa juu ya hayo.

Ama asli ya mwanamke inafaa kwake kuwakilishwa na anaemtaka au yeye kumwakilisha amtakae katika kutoa rai hamna haja ya kusema zaidi, kwa sababu mwanamke huwakilishwa katika ndoa, na kuuza na kukodisha na mengineo na pia ye kuwakilisha mwengine katika hayo. Na hiyo si maalum katika mambo Fulani na sio mengine, bali ni amm kwa killa jambo ikiwemo rai. Na kwa hayo inajuzu kwa mwanamke kuwakilishwa anaemtaka katika kutoa rain a yeye kuwakilishwa na anaemtaka katika kutoa rai.

Na kwa kua barza la Ummah ni baraza la kutoa rain a viungo vyake ni wawakilishi wa wengine katika kutoa rai, kwa hivyo inajuzu kwa mwanamke kuchagua na kuchaguliwa katika baraza la Ummah, yaani yajuzu kwake awe ni mwakilishi wa wengine, nay eye kuwakilishwa na mwengine katika kutoa rai. Na Mtume (saaw) katika mwaka wa kumi na tatu wa Utume aliiendewa na wanaume sabiini na tatu na wanawake wawili wakiwa ni Umm Ammarah bint Kalb mwanamke wa bani Mazin, na Asmaa bin Amru bin Adi mwanamke wa bani Salamah na Mtume (saaw) akaagana nawo wakutane Aqabah- na wakaenda usiku wa manane na wote wakajificha katika vichaka na wanawake pia waliandamana nao na Mtume (saaw) aliwaambia. “Nawabaiisha juu ya mutanihifadhi mimi kama munavyo wahifadhi wake zenu na watotot wenu “na ilikuwa bayana aya hii walisema “Tulimbayiisha juu ya kusikia na kutii katika mazito yetu na mepesi yetu na yakutuchangamsha na yakutuudhi, na tuzungumze haki popote tunapokuwepo, tusiogope katika Allah lawama za mwenye kulaumu “na hii ni bayan ya kisiasa. Na iwapo yafaa kwa mwanamke kutoa bayah, bayah ya kisiasa yafaa kwake kuchagua na kuchaguliwa kwa sababu bayan na kuchagua ni suala moja nalo ni kumchagua mtawala na mumtii, na dalili ya kua bayan na kuchagua ni swala moja ni kua khalifa asipabaiishiwe hafai kuwa khalifah kisharia. Kile kinachomfanya awe khalifah na ahadi ya kumsikiza na kumtii. Na haisemwi kua bayah ni ahadi ya kusikia na kutii pekee basi inakua pia kwa ambao hawakubaiishiwa isipokuwa baada ya kuchaguliwa khalifah ama bayah ya kwanza nib ayah ya kumchagua na baadae ahadi ya kusikia na kumtii. Na sharit iwe uridhiano kwa sababu ni mkataba wa marishiano, kwa hivyo hiyo au kuchagua ni suala moja. Na kumchagua ataemuakilisha mwanamke katika kutoa rai katika baraza la Ummah ni bora zaidi (min bab awlah), kwa sababu ikiwa inafaa kwa mwanamke kuchagua khalifah nao ni cheo cha juu katika utawala kwa hivyo kufaa kumchagua wa chini yake ni ubora zaidi (min bab awlah). Na kwa hayo yabainika kua kumchagua mwanamke kua ni kiungo cha baraza la Ummah yafaa kisheria.

Huu ni upande wa dalili ya bayah ya aqabah ya pili kua yafaa kwa mwanamke kuchagua mwengine katika baraza la Ummah. Na upande wa dalili yenyewe kua yafaa kwake kumchagua mwengine kua ni kiungo katika baraza la Ummah kwani Mtume (saaw) baada ya kumaliza bayah aliwaambia wote waume na wake “Nitoleeni mionganoni mwenu wasimamizi kumi na mbili ambao ni wasimamizi wa watu wao “na hii ni amri kutoka kwake kwa wote, yaani wote wachague, nao ni amm, na Mtume hakuifanya makhsus kwa wanaume na hakuchuja wanawake sio kwa watakaochagua wala katika kuchaguliwa. Amm (jumla) hufuata ujumla wake na haikupokewa dalili ya kuifanya makhsus. Na kwa kua haikufanywa ni makhsus basi inajumuisha wanaume na wanawake wote ni sawa kuchagua au kuchaguliwa.

Kwa hivyo kufaa kwa mwanamke kua kiungo katika baraza la Ummah na pia kuchagua kiungo, imethubutu kwa upande wa asli yake ni mwakilishi wa wengine katika rai na pia yeye kuwakilishwa na wengine katika rai. Na imethubutu katika hadithi ya bayah ya pili.

Na hamna shubha kwa yoyote kwa shura ni haki ya mwanamume na mwanamke, na kumhisabu kiongozi ni faradhi juu ya mwanamume na mwanamke na kua kuamrisha mema na kukanya maovu ni wajibu juu ya mwanamume na mwanamke na nasaha ni amri kwa mwanamume na mwanamke, na kuwakilishwa kwa rai yajuzu kwa mwanamume na mwanamke, na kwa mwanamke ana haki pia ya kua na rain a kutoa rai hiyo, hamna tofauti kati ya rai ya kisiasa au ya sheria au mengineo kuhusiaana na rai. Na kwa kua baraza la Ummah kazi yake imefungika katika shura na kumhisabu kiongozi na kuamrisha mema na kukanya maovu na nasaha ni kwa viongozi wa waislamu. Na killa linalohusiana na rai, na sio katika kazi yake ni utawala jambo ambalo hamna budi kusiwe na shubha katika kumruhuru mwanamke kua kiungo katika baraza la Ummah na pia kumruhusu yeye kuchagua viungo vyataga la Ummah.

Isipokuwa baadhi wamechanganyikiwa juu yao ya kumruhusu mwanamke kuchagua viungo vya baraza la Ummah kua bayah ya ahadi ya kusikia na kutii na sio kuchagua na wasione dalili ya kumruhusu kuchagua. Isipokuwa ilipothubutu kua baraza la Ummah ni kwa ajili ya rain a mwanamke kuwakilishwa na amtakue kwa rai kwa hivyo hamna budi kusiwe na shubha yoyote katika kumruhusu mwanamke kuchagua viungo vya baraza la Ummah, juu ya hayo bayah mwanzo ni makubaliano ya kuridhiana nao ni kuchagua khalifah kwa maridhiano ya wanaokubaliana na sio tu ahadi ya utiifu, kwa hivyo itakuwa hayo na uchaguzi ni suala moja nao ni kumchagua khalifah. Kwa hivyo mwanamke ana haki katika kuchagua kiongozi na kumchagua ni kama yanavyoonesha hayo na hadithi ya bayah ya wanawake iliothubutu ni ubora zaidi (min babi awlah) kua yafaa kumchagua yeye kua ni baraza la Ummah. Na pia baadhi wamemchanganyikiwa katika kumruhusu mwanamke kua ni kiungo katika baraza la ummah kwa kuifananisha baraza la ummah na baraza la wabunge, isipokuwa ilipothubutu kua baraza la Ummah sio baraza la wabunge, kwani baraza la Ummah ni la rai, na baraza la wabunge ni la utawala, kwa hivyo isifananishwe moja na jengine, basi hamna budi kusiwe na shubha yoyote katika kumruhusu mwanamke kua ni kiungo katika baraza la Ummah kwa kuondosha mfano wa baraza la Ummah na baraza la wabunge. Kwa hivyo isibakie shubha katika kumruhusu mwanamke kua kiungo katika baraza la Ummah, na pia yeye kuchagua baraza la Ummah illa katika killa la kusumbua.

### Jamii ya kiislamu

Huenda kwa baadhi ikatokeza suali na kuuliza: vipi yawezekana kwa mwanamke kutekeleza shughuli zake ambayo ameruhusiwa na sheria? Kama kua nimuajiriwa katika serikali na hakimu wa kutatua utesi na kiungo katika baraza la Ummah akiwajadili watawala na kuwashabu pamoja na vizuizi hivi alivyo wekewa ya kutokuwa faragha (khulwa) na kutojirembesha (tabarujj) na kuishi kwake katika maisha khassa akiwa na wanawake na maharim.

Na pia huenda kwa baadhi kuuliza: vipi itahifadhika tabia na kuhifadhiwa utukufu? Iwapo ataruhusiwa mwanamke kuingia masokoni na kuwajadili wanaume na kutekeleza shughuli zake katika maisha amah na katika mujtamaa?

Na jawabu ya maswali haya ni: nidhamu ya kijamii ya kiislamu ni hukmu tofauti za kisheria moja imeshikamana na nyengine, na wala haimaanishi kujifunga na baadhi ya humku na kuacha kujifunga na nyengine, bali hamna budi kwa muislmau mwanamume na muislamu mwanamke kujifunga na hukmu za kisheria zote, mpaka isipatikane mgongano katika mtu mmoja, na kuonekana mgongano katika hukmu. Kwa hivyo uislamu haumaanishi katika kumruhusu mwanamke kuenda katika maafisi za serikali akifanya kazi au hata lau kama ni muuguzi katika hopitali, baada ya kujipamba, na amejitengeza kama bibi arusi, na kutoka akihidhihirisha kwa wanaume mapambo hayo ya kushwawishi, na kuchemsha matamanio yao kwake. Wala hamuonisho kwenda dukani katika mapambo hayo, akifanya biashara katika hali ya kushwawishi, na kwa mbinu kulegeza sauti ya kumshawishi mnunuzi na kumfanya kufurahia sauti yake wakati wa maelewano na kwa mbinu ya kuwapendishia bei ya bidhaa au kuwashawishi wanunue wala haimaanishi kufanya kazi maka katibu kwa wakili au katibu kwa tajiri yake kwa kumuacha kukaa nae faragha killa kazi inapohitajia kua faragha, na kumvalia mavazi ambayo yatadhihirisha nyele zake na kifua chake na mgongo wake na mikono yake na miundi yake na kumdhahirishia kitakacho mvutia katika kiwiliwili chake ambaco ni uchi..

Vile vile Uislamu haumaanishi chochote katika hayo au mfano wake katika yanaopatikana katika jamii hii ambayo anayoishi katika mujtamaa isiso ya kiislamu, unaotawaliwa na njia ya kimagharibi katika maisha. Bali Uislamu wamaanisha muislamu atabikishe hukmu za uislamu zote juu ya nafsi yake kwa hivyo wakati Uislamu ulipomruhusu mwanamke kushughilika na kuuza na kununua katika soko umemkataza

kutoka amejipamba (tabarujj) na ukamuamrisha atoke na hukmu zote pamoja. Kwa hivyo itiqadi ya kiislamu yalazimisha juu ya muislamu kutabikisha hukmu zote juu ya nafsi yake. Na Uislamu utafarashisha hukmu inajumuisha vitendo vyta kutekelezwa na vitendo vyta kuepukwa, zitamuhifadhi muislamu awe ni mwanamume au mwanamke kujitoa na mpaka wa tabia bora, na kua kinga kwake kuingia katika mtazamo wa kijinsia wakati wanapokuwa katika jamii.

Na hukmu hizi ni nyingi, na mionganini mwa hukmu ambazo zinajumuisha juu ya kutekeleza vitendo vyta kutekeleza kama ifuatavyo:

1:- Amewaaamrisha wote mwanamume na mwanamke wainamishe macho yao, na wahifadhi tupu zao na amesema (swt):

{ قُلْ لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغْضُبُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَلِكَ أَزْكَى لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَيْرٌ  
بِمَا يَصْنَعُونَ - وَقُلْ لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُبْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ }  
(النور: 30-31)

“Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao hayo ni bora kwa hakika Allah ni muelewa kwa wanayoyatenda – nia waambie waumini wanawake wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao”(Nur-30-31) na kuinamisha macho ni kwa wote mwanamume na mwanamke ni hifadhi ya kihakika kwa killa mmoja wao. Hiyo hifadhi ya kidhati ambayo ni kizuizi baina yake na kuingia katika ya haramu, kwa sababu macho ndio mbinu ya kikweli kufikia hayo. Na wakati atainamisha macho basi atajiepusha na maovu.

2:- Amemuamrisha mwanamume na mwanamke kumcha Allah na akasema (swt):

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا } (الأحزاب: 70)

“Enyi Mulioamini mcheni Allah na museme maneno ya sawa “(Ahzab-70) na akasema:

{ وَاتَّقِينَ اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا } (الأحزاب: 55)

*“Na mumche Allah hakika Allah hakika Allah ni shahidi wa killa jambo”*(Ahzab-55) na akasema

وَالْعَاقِبَةُ لِلتَّقْوَىٰ ... ﴿١٣٢﴾

*“Na mwisho mwema ni kwa wachaji”* (Taha-102) na wakati muislmau atakaposifika kwa uchaji Allah na kuogopa adhabu yake na mutumaini kuingia katika pepo yake na kupata radhi zake kwani uchaji huo utamuepusha yeye na maovu na kumhifadhi yeye na kumuasi Allah. Na hii ni kizuizi cha kidhati ambalo hamna kizuizi chengine baada yake. Na akijipamba muislamu na kumcha Allah hakika amejipamba kwa sifa bora ya iliokamili.

3:- Ameamrisha mwanamume na mwanamke wajiepushe na sehemu shaka, na wakae mbali na hayo ili wasiingie katika kumuasi Allah (swt) na wasiingie sehemu yoyte au wasitende kitendo chochote na wasitumbukie kwa namna yoyote kwenye shaka ili wasiingie katika haramu. Amesema Mtume (saaw) “Halali iko wazi na haramu iko wazi na baina yake kuna mambo ya shaka watu wengi hawayajui, basi atakae jiepusha nay a shaka ameihifadhi dini yake na hishma yake na atakae tumbukia kwenye shaka atatumbukia kwenye haramu, nikama mchungaji anaechunga karibu na mpaka na yaogopewa kuingia ndani yake, na mujue ya Allah ni alioyaharamisha “na shaka (shubha).

Ya kwanza: kua na shaka na jambo Fulani jee ni haramu au mubah au katika kitendo jee ni faradhi au haramu au makhruh au mandob au mubah. Na kuwepo kwa shaka hii katika sifa ya kitu au katika hukmu ya kitendo, na haifai kwake kutenda mpaka imbainikinie yeye hukmu ya Allah kuhusiana nalo, na atatekeleza akiwa mtulivu kwa ameivuka dhanna yake (ghalabat – dhann) kuhusu hukmu ya Allah kuhusiana nalo. Iwe ni baada ya ijtihami yake au baada ya kujua hukmu ya Allah kuhusiana nalo imam kutoka kwa mujtahid au mjuzi wa hukmu hata lau kama ni mugalid au Ammi madam ana imani na uchaji wake wa Allah na ujuzi wake katika hukmu ambayo yeye hana ujuzi nalo kabisa.

Ya pili: kuwa na shaka nalo asije akatumbukia katika haramu katika kutenda mubah kwa kua karibu na haramu, na kwa asli yake lina dhanna kua linaweza kumpelekea kama kuweka mali katika benki na inaamiliana na riba au kuuza zabibu kwa mfanyi biashara anaemiliki kiwanda cha mvinyo au kufundisha wasichana kwa wiki au killa siku na mfano wake. Kwa sababu mfano wa vitendo hivi ni mubah na yafaa kwake kuvitekeleza lakini ni bora asivifanye kwa kujiepusha kwa kumuogopa Allah.

Ya tatu: watu kua na shaka nakitendo cha mubah kua ni kitendo kilichokatazwa kwa kuogopea kudhaniwa na watu dhanna mbaya, na hayo nikama pupita sehemu iliyojaa maovu, na watadhania watu kua yeye ni muovu, kwa kuogopea watu wasizungumze kwa uovu juu yake na ajiepushe na mubah. Na kama kua mkali (tashid ) kwa mkewe na mahami wake wasitir nyuso zao nay eye anajua uso sio aurah lakini ni mkali kwa kuogopea watu wasiseme kua mke wa Fulani au dadake hajisitiri, nah ii ina maana kwa pande mbili.:

Ya kwanza: kiwe ni kitu ambacho watu wanakifananisha na haramu au makruh au ni kitendo cha haramu au makruh kisheria. Na katika kutekeleza mtu kitendo cha mubah watu watafahamu kua ametekeleza kitendo kilichokatazwa. Na katika hali hiyo ajiepushe mtu na kitendo cha mubah watu wasimdhanie mabaya ay awaelezee wao “imepokewa kutoka kwa Ali bin Hussein kwa Swafiyah bint Huyyein mke wa Mtume (saaw) alimulezea kua alikwenda kumzuru mtume (saaw) akiwa katika itikafu katika msikiti katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhan na wakazungumza muda wa saa baada ya isha kisha akasema kutaka kwenda na mtume (saaw) akasimama kumsindikiza mpaka walipofika mlangoni wa msikiti amba ni karibu na mlangano wa umm Salamah mke wa Mtume (saaw) wakapia wanaume wawili katika Ansar, wakamsalimia Mtume (saaw) na wakapita na Mtume (saaw) akawaambia ngojeni kidogo huyu ni Swafiyah Bint Huyeiy, wakasema: Subhana Allah ewe Mtu (saaw) na kapiga takbira (Allahu Akbar) kwa walioyayema: akasema: Hakika shetani

anatembea katika mwanadam inapofika damu. Na mimi niliogopa asije sheitani akawatia mawazo mabaya katika nyoyo zenu.” Na yafahamika katika hadithi hii kua Mtume (saaw) alitoa wasi wasi ambao huenda ikaja kwa swahaba wake pamoja na kua Mtume (saaw) hana wasiwasi.

Ya pili: kiwe kitu ambacho wana shaka nacho kua kimetazwa na kihakika hakikukatazwa, lakini kwa kupgopea wasiwasi watu kuhusu yeye kuwa ametenda kilicho katazwa, na akajiepusha nacho kwa maneno ya watu sio kwa sababu kimekatazwa.

Na mfano wa aina hii ya shakla haijuzu kujiepusha nacho bali atatekeleza kwa namna ambayo ameamrishwa na sharia na wala watu asiwatie kwenye hisabu. Na Allah (swt)

...وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَى...} (الأحزاب: 37)

“*Na un-waogopa watu na Allah ana haki zaidi ya kuogopewa*” (Ahzab-37) yaonesha kua muislamu anapoona kua sharia haikukataza kitu basi atekeleza hata lau kama watu wote watasema kua kimekatazwa.

Kwa hivyo shaka hizi ambazo sharia imekataza wakijiepusha nazo mwanamume na wanamke watajiepusha na maasiyah na zitawafanya wasifike na tabia bora.

4:- Uislamu umehimiza kuoa mapema ili ianze hifadhi ya mahusiano ya kijinsia kwa mwanamume na mwanamke kwa ndoa katika miaka ya mwanzo. Na yapatikana kwa hayo na ili kuizunguka katika kuifunga mtazamo huu wa kijinsia kwa ndoa, wakatio inapo anza kuchemka ghasiza ya kijinsia. Amesema (saaw) “Enyi mkusanyiko wa mabarobaro yoyote kati yenu anaeweza kuoa basi basi awe na alisahalisha suala la kuoa kikamilifu kwa kuhimiza kupunguza mahari, amesema (saaw) “Mchache wenu wa mahari ni mwingi wenu wa baraka”.

5:- Uislamu umewaaamrisha wale ambao hawawezi kuoa kwa sabau Fulani wajilazimishe na kujihifadhi (iffah) na wazuie nafsi amesema (swt):

**{... وَلَيْسَتْعِفُ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّىٰ يُغْنِيهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ } (النور: 33)**

“Na wajihifadhi wale ambao hawawezi kuoa mpaka Allah awatajirishe au fadhla zake” (Nur-33) au ukawaamrisha wafunge kama suluhisho la ghariza ya kijinsi ili ajishughulishen ibada ya Saum kwa kuishinda, na kuishughulisha nafsi kwa ambayo ni bora na mtukufu, na pia kutilia nguvu mahusiano ya mwanadamu na Allah kwa kumtii, amesema (saaw) “Enyi mkusanyiko wa mabarobaro yoyote anaeweza kuoa basi aowe kwani ni hifadhi ya macho na hifadhi ya tupu na asieweza basi ni juu yake afunge kwani ndio kinga kwake “Na saumu sio kuikandamiza ghariza ya kijinsia bali ni kuleta ufahamu unauhusiano na ghariza ya kuabudu itakaomshughulisha mwanadamu na ghariza ya kuendeleza kizazi, kwa hivyo haitochemka ili ikamtia wasiwasi na dhiki. Na sio maradi wa saumu kudhofisha mwili kwa sababu kula usiku yatosheleza kula mchana, kwa hivyo kudhofisha katika saumu sio ukweli lakini uhakika ni kuleta ufahamu wa kiroho kwa saumu za sunnah.

6:- Uislamu umewaaamrisha wanawake wajisitiri kwa kuva vazi kamili katika maisha jumla. Na kuyafanya maisa khassa yamefungika kwa wanawake wa maharim. Na hamna shaka kuonekanwa mwanamke aliejisitiri uzuri itakua kinga baina yake na wanaotizama katika wasomogopa Allah. na Quran imeeleza wazi vili kwa uzuri na ukamilifu wan a ujumla. Na mwanamke wakati atakapo vua vazi hilo kamili na kuvaakhimori yake katika ufunuo wake na kuteremsha sitara ya kichwa chake juu ya shingo yake na kifua chake na wakati atakapovaa juu yake jilbabblake na kuva sitara yake au lufadhi yake mpaka chini ili asitiri mwili wake wote mpaka uyayo zake,atkua amevaa vazi kamili na kuzungu kwana vazi lake na kudhihirika hishma yake na kwa vazi hili kamili itamuezesha yeze kotoka kwenda katika maisha ya ammah kutekeleza shughulizake,nao ni kilele cha hishma na utulivu itakao kua kizuizi baina yake na wanaoangalia waovu wasiomuogopa Allah.

Hizi ndizo hukmu za kisheria ambazo zimekusanya vitendo ambavyo ni vya kutekelezwa ama hukm za kisharia ambazo zimekusanya vitendo vya kuepukwa ni kama ifuatavyo;

1:- Wamekatazwa wote mwanamume na mwanamke kua faragha moja na mwengine na faragha na kujumuika mwonamume na mwanamke katika sehemu ambayo haiwezekani kwa mtu kuwaingilia illa kwa ruhusa yao, kama kukutana katika nyumba au faragha mbali na barabara na mabali na watu. Amesema katika qamus muhit ( ----- alitaka wakutane faragha na akafanya) na faragha na akafanya) na faragha (khawlah) ni kukutana baina ya wawili kanda wao wawili peke yao, na kuamini kua mbali na wao wawili hakuna mwengine. Na hii faragha ndio kiini cha uharibifu uislamu ukakataza kwa ukatozo wazi killa aina ya faragha baina ya mwanamme na mwanamke wasioku maharim .wowote watakua watu hao na faragha yoyote iwayo Amesema (saaw) “yoyote anaemuomini Allah na siku ya mwisho basi asikae faragha na mwanamke ambae hayuko na mahram wake, kwani wa tatu wao ni sheitani, “Na kwa kukatazwa faragha sheria ilichukua vizuizi baina ya mwanamume na mwanamke. Na ukweli wa faragha nikuwa mwanamume hamjui mwanamke illa kwa uu ke na mwanamke hamjui mwanamume illa kwa uume kwa kukataza faragha hii ya kivyao nikufunga mbinu za uharibifu, kwa sababu faragha ni njia wazi wazi ya uharibifu.

2:- Amekatazwa mwanamke kutoka nje na nguo za nyumbani (Tabarruj) amesema Allah (swt):

{... وَالْقَوَاعِدُ مِنِ النِّسَاءِ الَّتِي لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ أَنْ يَضَعْنَ ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ مُتَبَرِّجَاتٍ بِزِينَةٍ ...} (النور: 60)

“Na watu wazima katika wanawake ambao hawana matarajio ya kuolewa sio makosa juu yao kuvalaa mavazi zisizo za mapambo“(Nur-60) kwa hivyo aliwakataza kutabarruj wakati alipomshurutisha kuvalaa mavazi ambayo alimruhusu kuzivaa yaani kuzivaa, na kwa namna ambayo haitakuwa ni tabarruj na

mafhum yake amewakataza tabarruj. Na iwapo wazee wamekatazwa tabarruj kwa hivyo ina maana wasiokua hao katika wanawake ni bora zaidi (bin bab awlah) amesema Allah (swt):

... وَلَا يَضْرِبُنَّ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِيَ مِنْ زِينَتِهِنَّ ... {النور: 31}

“Na wala wasipige miguu yao ili ipate kujulikana mapambo yao” (Nur-31) kwani hayo na mfano wake huzingatiwa ni tabarruj. Na tabarruj ni kudhihirisha mapambo na mazuri kwa ajnabi, na husemwa tabarruj: Ni amedhihirisha mapambo yake mazuri yake kwa ajnabi. Na zilipokewa hadithi kadha zinazokataza yale ambayo yanaozingatiwa ni tabarruj. Imepokewa kutoka Abi Musa Al-Ashari amesema: amesema Mtume (saaw) “Mwanamke aliejitia manukato na akapita mbele ya watu ili wasikie harufu yake basi amezini, “yaani yeye ni kama mzinifu katika madhambi. Na amesema (saaw) “watu aina mbili sitawaona, watu walio na mijeledi kama mikia ya ng’ombe wakichapia watu, na wanawake waliovaa waliouchi wananaoinamisha (miili) mbele ya wanaume vichwa vyao kama nundu ya ngamia ilionanguka, hawataingia peponi na wala hawatasikia harufu yake, na harufu yake hupatikana masafa ya kadha na kadha (Fulani na Fulani) kwa hivyo dalili hizo zote ziko wazi katika kukataza tabarruj kwa hivyo tabarruj ni haramu. Kwa hivyo killa pambo isio ya kawaida itakao shawishi macho ya wanaume, na kudhihirisha mapambo ya mwanamke itakua ni tabarruiwapo atadhahirisha mwanamke katika maisha amah, au adhahirishe katika maisha khassa mbele ya wanaume ajnabi. Kama manukato na kuweko rangi katika uso na kuva skafu (barukah) na sio khimar na kuva surwali billa ya jalbab wakati anapotoka katika hadharani.

Na ukweli wa tabarruj ni kua kuchemka ghariza ya kuendeleza kizazi cha kutaka kukutana kijinsia kwa wanaume na wanawake. Na kuwa changamsha wanaume kwa wanawake kwa namna ambayo itawaletea uhusiano baina yao juu ya msingi wa uume na uukena kufanya mahusiano kati yao ni ya kijinsia, na kufisidi ushikiano baina yao kwa namna ambayo

huvunja umoja wa jamii yao, na sio kuijenga na kua kizuizi baina ya mkurubiano wa kihakika ambayo msingi wake ni usafi na uchaMungu. Na tabarruj hiyo itajaa faragha ya maisha kuchemsha ghariza ya kuendeleza maisha, na haitakua katika maisha illa majukumu makubwa, na mambo makubwa na hamu kubwa ili kushibisha mahitio ya kiwiliwili kwa kuchemshwa kwake na tabarruj kutoka mwao na mahitaji hayo. Na kua vingamizi baina ya Muislamu mume au mke na baina ya kutekeleza ujumbe wake katika maisha nao ni kubeba ulinganizi wa kiislamu, na jihad katika njia ya kunyanya neno la Allah-kwa hivyo hamna budi kujua khatari ya tabarruj juu ya jamii ya kiislamu na kujua kua katika tabarruj hujidhihirisha mwanamke kwa mwanamume na kumchemsha, na ni khatari juu ya jamii na juu ya mahusiano yao. Hii ndio tabarruj ambayo uislamu umeiharamisha na huu ndio ukweli wake na khatari iliyopo juu ya jamii ya kiislamu. Ama kudhihirisha mazuri na mapambo katika nyumba na katika maisha khassah haizingatiwi na tabarruj wala haingii katika neno la tabarruj.

3:- Uislamu umewakataza wote mwanamume na mwanamke kushughulika na kazi yoyote ambayo ni khatari juu ya tabia au uharibifu kwa jamii. Kwa mwanamke amekatazwa kujishughulisha katika killa kazi ambayo yakusudiwa kuonyesha uu ke wake. Naimepokewa kutoka kwa Rafii bin Rufaa'h amesema "Alitukataza (saaw) na tumo la vijakazi illa kwa kila alichokifanya kwa mikono yake. Na akasema: Hivi kwa vidole vyake kumaanisha kupika mikate, kufuma na kuchonga naqshi "kwa hivyo amekatazwa mwanamke kufanya kazi katika duka kwa ajili ya kuleta wateja na kufanya kazi katika mabalozi na wawakilishi na mfano wake inakusudiwa kutumia uu ke wake ili kufikia malengo ya kisiasa, na pia amekatazwa kufanya kazi ya kupokea wasafiri katika ndege na inao fanana na hayo katika kazi ambazo atafanya mwanamke kwa kukusudia uke wake.

4:- Uislamu umekataza kusingizia wanawake wema yaani kuwasengizia kwa uzinifu, amesema Allah (swt)

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَزْبَعَةٍ شُهَدَاءَ فَاجْلُدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدًا وَلَا  
تَقْبِلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ {النور: 4}

“Na wale ambao wanawasingizia wanawake wema na wasilete mashahidi wane basi wachapeni wao mijeledi thamanini na wala musikubali ushahidi wao milele, na hao ndio mafasiqi “Nur-4) na akasema (swt):

إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لَعِنُوا فِي الدُّنْيَا وَالآخِرَةِ وَلَهُمْ  
عَذَابٌ عَظِيمٌ... {النور: 22}

”Hakika wale ambao wanawasingizia wanawake wema walioghalika waumini wamelaaniwa katika dunia na akhera na watakuwa na adhabu kubwa “(Nur-22) na akasema Mtume wa Allah (saaw) “Jiepusheni na saba yanaoangamiza wakasema ni yapi hayo ewe Mtume wa Allah? Akasmea: kumshirikisha Allah na uchawi na kuuwa nafsi ambayo Allah ameharamisha na kulla riba na kula mali ya mayatima na kukimbia siku ya mapambano (Jihad) na kusingizia wanawake wema waumini walioghalika “na muradi wa wema hapa ni waliojihifadhi kwa hivyo imeharamishwa kumsingizia killa aliejihifadhi. Na katika kukataza huku kuwasingizia wema sharia imezuia ulimi kuzoea kuzungumza maovu na kuhitadhi heshima ya watu ili isienee maneno maovu katika jamii ya kiislamu, wala isienee masingizio za batili. Na kwa hili itahifadhika jamii ya kiislamu.

Hizi ndizo hukmu za kisherai ambazo zimejumuisha vitendo vya kuepukwa itafanya jamii ya kiislamu vovote itakao patikana mahusiano baina yao yatakwenda juu ya mipaka usafi na uchaji Mungu.

Na kwa yote hayo yawezekana mwanadamu kuufahamu jamii ya kiislamu ni upi, na kumuelewa mwanamke wa kiislamu na yupi, na yawezekana kumuona mwanamke akitekeleza shughuli zake alizoruhuiswa na sheria katika maisha amah billa ya kupatikana ufisadi wowote na haipelekei katika madhara yoyote bali ni dharura kwa maisha amah na kuinyanyua jamii. Na kwa hayo hamna budi kwa waislamu wajifunge na hukmu za sharia wawe wako katika Darul-Islam au katika nchi ya ukafiri

katika biladi ya kiislamu au katika biladi isiokuwa ya kiislamu katika jamii ya kiislamu au nyengineo na matekelezo vitendo ambavyo sharia imemruhusu mwanamke kuvitekeleza, na wala wasiogope katika haya mazito, kwani katika kutekeleza hukmu za sharia ni kumhifadhi mwanamke, na kuinyanya jamii, na kutii maamrisha ya Allah na makalazo yake. Kwa mteremsha sharia ni muelewa zaidid kwa yaliona maslahi kwa mwanadamu awe ni pekee au jamii katika maisha khassa ana amah.

Huu ndio mukhosari wa nidhamu ambayo uslamu umeitibu makutano ambayo hupatikana nayo matatizo, nao ni kukutana wanaume na wanawake. Na kupitia nidhamu hii yapainika kua alikuwa za kisharia ambazo zimekuja nazo ni dhamana katika kuzui uharibifu, ambayo huenda yakapatikana kutokamana na makutano hayo na katika kuleta mafanikio ambayo itaeneza usafi na ucha Mungu na bidii na kazi. Na wakati huo huo ikidhamini maisha khassa anayoishi mwanadamu na kutulia nafsi na kumfurahisha, na kudhamini maisha amah iliyo na bidii na kuzalisha, na kuzidisha katika jamii wanayoyahitajia katika maisha yao katika mafanikio na furaha. Na hukmu hizi ni sehemu ya nidhamu ya kijamii, kwa sababu inapanga makutano ya mwanamume na mwanamke. Ama yale mahusiano yanaopatikana na makutano hayo katika mahusiano na matanzu ya matatizo hayo, kwani ni sehemu ya pili katika nidhamu ya kijamii nao ni ndoa na talaka na utoto na utoaji (nafaqah) na mengineo. Na ijapo kua hukmu hizo – hukmu za kijamii – hukmu za ndoa na takala na mengineo – ni nidhamu za mujtamaa kwa sababu zinapangilia mahusiano mtu moja na mtu mwengine, isipokua kwa upande wa asli yake hupatikana kwa makutano ambayo hupatikana baina ya mwanamume na mwanamke, kwa hivyo hufanyiwa urafiki kwa msingi wake na kupatikana kwake katika nidhamu ya kijamii. Ama kwa upande wa ufanuzi wake wa mitagaa yake kwani ni sehemu ya nidhamu ya mujtamaa na kufanyiwa utafiti katika mlango wa Muamalat.

## Ndoa

Hupatikana kwa makutano ya jamii ambayo wanaoishi undani yake, nao ni tafauti ua mutatizo ambayo hupatikana kutomana na makutano katika mujtamaa katika kuza na kukodisha na uwakala na mifano yake. Na huenda ikaingia katika mabongo kua mahusiano hayo ni ndoa pekee, na uhakika kua ndoa ni moja wapo na pia inajumuisha yasiokua ndoa, kwa kwa hivyo makutano ya kiwiliwili sio dhihirisho pekee ya ghariza ya kuendeleza kizazi bali ni moja wapo wa madhihirisho yake, kwani madhihirisho mengine yasiokuwa makutano ya kiwiliwili sio dhihirisho pekee ya ghajariza ya kuendeleza kizazi bali ni moja wapo wa madhihirisho yake. Kwani madhihirisho mangeni yasiokuwa makutano ya kiwiliwili. Kwa umama au ubaba na undugu na uotot na ujomba na uammi yote ni dhihirisho la ghariza ya kuendeleza kizazi. Na mpaka hapa mahusiano yanayopatikana na makutano ya wanaume na wanawake inajumuisha umama na ubaba..... mpaka mwisho. Kama inavyojumuisha ndoa. Na nidhamu ya kijamii inajumuisha kama inavyo jumuisha ndoa. Na sharia imekuja na hukmu na utoto na ubaba na umama kama ilivyokuja na hukmu za ndoa.

Isipokuwa ndoa ndio msingi wa mahusiano hayo na mengineo yote ni matagaa yake, na pasipopatikana ndoa hayatopatikana ubaba wa utoto wala umama wala mengineo. Na mpaka hapa imekua ndoa ndio msingi wake na mengineo yote mitagaa yake kwa upande wa kuipangilia, hata kama hisia ya kuhitajia hayo kama inavosukuma kuhitaji makutano ya kiwiliwili. Na ghariza hutaka kushibishwa husukuma kwa msikuma wa dhihirisho la umama na utoto, kama inavotaka kushibishwa kwa msukumo wa dhihirisho la makutano ya kiwiliwili sawa sawa. Kwa sababu ndoa na umama na mengineo yote ni dhihirisho la ghariza ya kuendeleza kizazi, ha hisia zake zote ni hisia za kuendeleza kizazi, na huchukua mwelekeo kwa waqiah wake pamoja na ufahamu wa killa moja kati yake kama inavyokuwa mwelekeo katika jengine.

Na ndoa ni kupangilia mahusiano ya uume na uukenyaani makutano ya viwiliwili kati ya mwanamume na mwanamke kwa nidhamu maalum, au nidhamu hii maalum ndio ambayo yawajibisha kupangilia mahusiano ya uume na uukenya kwa muundo maalum, amabyo ndio wajibu pekee kufuatwa kuendeleza kizazi, na ndio ambayo hupatikana nayo kuongezeka kwa wanadamu. Na kwayo hupatikana familia na juu ya msingi wake huchukua mpangilio wa maisha maalum.

Na uislamu umehimiza ndoa na kujamrisha, imepokewa kutoka kwa Ibn Masoud (raa) amesema: amesema mtume (saaw) “Enyi mkusanyiko wa mabarobaro yeyote katika nyinyi anaeweza kuowa, basi aowe kwani ni hifadhi ya macho na hifadhi ya tupu na asieweza ni juu yake afunge kwani ni kinga kwake” na imepokewa kutoka kwa qatadah kutoka kwa Hassan kutoka kwa Samurah alisoma:

} وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً ... { (الرعد: 38)

“Hakika tuliwatuma Mitume kabla yako na tukawajaaliya wao wake na watoto” (rad-38). Na maana ya ukasisi/utawa ni kujiepusha na ndoa na yanofuata katika ladha kwa kuabudu. Na imepokewa kutoka kwa Abi Hureira kutoka kwa Mtume (saaw) kua alisema” watatu wana haki mbele ya Allah kusiadiwa, anaepigana jihad katika njia ya Allah na anacowanaetaka kujihifadhi Mtumwa (Mukatib) abaetaka kujikombowa” na akasema (saaw) “Hamna ukasisi katika Uislamu na ukasisi na upapa ni kujiepusha na wanawake, na kuacha kuowa na kujishughulisha na kumuabudu Allah. Na Qur'an imekuja wazi katika kuamrisha kuowa amesema (swt):

}...فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِّنَ النِّسَاءِ مَتْنَى وَثُلَاثَ وَرُبَاعٍ.{ (النساء: 3)

“Oweni munaowapenda nyinyi katika wanawake wawili wawili na watatu watatu na wane wanne: (Nisa – 3).

} وَأَنكِحُوا الْأَيَامَى مِنْكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عَبَادِكُمْ وَإِمَائِكُمْ { (النور: 32)

“Na waozesheni wepweke mionganini mwenu na wema katika watumwa wenu na vijakazi vyenu “Nur-32)

Na Uislamu ukasisitiza kuowa wanawali/wasichana na wazazi na wenyе dini. Imepokewa kutoka kwa Anas kuwa Mtume (saaw) alikuwa akiamrisha kuowa na akikataza vikali ukasisi, na alikuwa akisema “Oweni wazuri wanaozaa kwani mimi nitajifakhiri kwa uwingi wenu kwa Mitume siku ya qiyamah” na imepokewa kutoka kwa Maa’qal bin Yassar alisema: “Alikuja mtu kwa Mtume (saaw) na akasema: mimi nimempenda mwanamke aliye na kabilia bora na usuzi lakini hazai, jee nimuowe? Alisema: La. Kisha akaja mara ya pili, akamkanya, kisha akaja mara ya tatu, akasema: oweni wazuri wanaozaa kwani mimi nitajifakhiri kwa uwingi wenu.” Na Alimuombia yeye “Ewe Jabir umeowa mwanamwali au mke mkuu? Akasema : mke mkuu, akasema “ kwanini haukuowa mwanamwali umchezeshe na akuchezeshe “Na imepokewa kutoka kwa Abu Hureira kutoka kwa Mtume (saaw) akasema “ “Huolewa mwanamke kwa sababu nne, kwa ajili ya mali yake na ukoo wake na uzuri wake na dini yake, owa mwenye dini habariki mikono yako” kwa hivyo imependekewa kwa mwanamume achague katika wanawake mwanamwali na anaejulikana kua ni mzazi kwa kumjua mamake na anti yake na shangazi yake na achague mwenye dini na achague mzuri ili aihibadhi nafsi yake na awe mwenye ukoa mzuri na nasaba, yaani amealelewa na tabia bora na ucha Mungu na utukufu, lakini haimaanishi hayo ni masharti, bali ni kuvutia na kupendekeza, illa ni juu ya mwanamume achague mke yeye anaemridhia na mwanamke achague mume ambae yeye anaemridhia.

Ama kulinganisha (kuff) baina mume na mke haina msingi katika sharia. Hazikupokewa hadithi illa za urongo. Na Qura’n tukufu ina kwenda kinyume nayo. Vile vile na hadithi sahihi, kwa hivyo killa muislamu mwanamke anamtosheleza muislamu mwanamume yoyote, na killa muislamu mwanamume ni sawa na muislamu mwanamke yoyote, na hamna thamani iliyopo kati ya Mume na Mke katika mali au kazi au ukoo au mengineo. Kwa kuokotaji taka ni sawa na binti wa Amirul mumineen, na binti wa kinyozi ni sawa na mtoto wa kiume wa Amirul

Mumineen, na hivi ndivyo wanavyokuwa waislamu ni sawa. Amesema Allah (swt):

... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَانُكُمْ ... } (الحجرات: 13)

"*Hakika mbora wenu mbele ya Allah ni mchaji Mungu zaidi*" (Hujrat – 13. Na Mtume (saaw) alimuonyesha binti ya shangazi yake Zainab bint Jahsh ambae ni kutoka qabila la Qureish na Ziyy bin Harith aliekua ni mtumwa wake aliemuacha huru. Na imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Bureiydah kutoka kwa babake amesema: "Alikuja msichana kwa Mtume (saaw) na akasema: Babangu ameniozesha mtoto wa kakake ili anyanyue hadhi yake. Akasema: akamuachia uamuzi yeye akasema (msichana) nimeyakubalia alioyafanya babangu, lakini nilikuwa nataka niwajulishe wanawake kuwa mababa hawana lolote kuhusiana na jambo hili "Na maana ya qauli yake ili anyanyue hadhi yake yaani kunyanya hadhi ya mtoto wa kakake kwa kuniozesha mimi. Na hili lamaanisha kuwa alimuozesha billa ya marishia yake, kwa sababu hakumuona ni sawa kumuowa yeye, na sio halinganinae kwani ni mtoto wa Ammi yake lakini kwa kutoridhia. Na imepokewa kutoka kwa Abi Hatim Al-Muzniy amesema: amesema Mtume (saaw) "Anaewajieni munaemridhia dini yake na tabia basi muozesheni, na mukitofanya hivyo itakuwa mchafuko katika ardhi na uharibifu mkubwa, wakasema ewe Mtume wa Allah hata kama ana kasoro Fulani? Akasema : Akiwajieni munaemridhia dini yake na tabia yake muozesheni maratatu "Na ameileta Tirmidhi pia hadithi hii kutoka kwa hadithi ya Abu Hureira na lafdhi akasema : "Anapokuja kuposa kwenu munaemridhia dini yake na tabia yake basi muozesheni, na kukitofanya hivyo kutakuwa na mchafuko katika ardhi na uharibifu mkubwa" na pia imepokewa kutoka kwa Abi Hureira kuwa babake Hindu alimuumika Mtume (saaw) katika kichwa akasema Mtume (saaw) "ewe mtoto wa Bayadhah muozesheni babake Hindu na nyinyi muowe kwake "Na imepokewa kutoka kwa Handhala bin Abi Sufya Al-Humhiy kutoka kwa mamake amesema " Nilimuona dadake Abdulrahman bin Auf kua ni mke wa Bilal." Kwa hivyo dalili zote hizi ziko wazi kuwa kulinganisha baina ya mume na mke haizingatiwi na haina

thamani, kwa hivyo, (mwanamke) akiridhia mwanamume yoyote kama mumewe basi ataoleta na maridhia yake billa ya kujali suala la kulinganisha. Ama kwa yaliopokewa kutoka kwa ibn Umar kuwa Mtume (saaw) amesema: “Waarabu wanalingana baadhi yao kwa baadhi kabila kwa kabila ukoo kwa ukoo na mume kwa mume isipokuwa mshonaji na muumikaji.” Hadithi hii ni urongo isio na msingi na ni batili amesema ibn Abi Hatim nilimuuliza babangu kuhusu hadithi hii akasema : imekanushwa. Na akasema ibn Abdul Barr hadithi hii imekanushwa na imezuliwa. Ama alioyaeleza Bazzar kutoka hadithi ya Mua’dh “Waarabu baadhi yao wanalingana na baadhi na walioachwa huru waadhi yao wanalingana na baadhi, “Mapokezi yake ni dhaifu. Ama hadithi ya Bureirah “kuwa Mtume (saaw) alimuambia Bureirah alipaachwa huru, umeshachwa huru chagua umtakae.” Hapa haimaanishi kulinganisha. Kwa sababu mumewe alikuwa mtumwa na kijakazi alioleta na mtumwa anapokua huru anakhiyarishwa kubakia chini dhimma ya mtumwa au avunje ndoa yake. Wala haioneshi humo juu ya kulinganisha. Na dalili ya kuonesha kuwa mume wa Bureirah alikuwa mtumwa ni ile iliopokewa kutoka kwa Qasim kutoka kwa Aisha kuwa Bureira alikuwa chini ya mtumwa alipoachwa huru Mtume (saaw) alimuambia “chagua ukitaka kubakia chini ya Mtumwa huyu au ukitaka utengane nae.” Ama kwa yaliosimuliwa katika Muslim kutoka kwa Urwah kutoka kwa Aisha “Kua Bureira aliachwa huru na mumewe alikuwa mtumwa akam khiyarusha Mtume (saaw) angelikuwa ni huru asingemkhiyarisha.” Ama kwa yaliosimuliwa kuwa Mtume (saaw) alisema: “musiowe wanawake illa munaolingana nao na wala musiwooowe illa kwa wasimamizi (Awliyah).” Hiyo ni dhaifu na haina msingi. Na kwa haya yabainika kuwa hamna nass yaonesha juu ya kulingana na kuwa nass walizozitaja wanaosema kuhusu kulinganisha ni nass za batili au hamu upande wa kuzitegemea. Na sharti la kulinganisha ina gongana na qawli ya Mtume (saaw) “Hamna ubora kwa mwaarabu juu ya asie kuwa muarabu (ajami) illa kwa ucha Mungu “Na inagongana na aya ya Qur'an iliokatikiwa:

{... إِنَّ أَكْرَمُكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَانُكُمْ ...} (الحجـرات: 13)

“Hakika mbora wenu mbele ya Allah ni mcha Mungu zaidi”  
(Hujrat-13).

Ama tafauti ya dini sio suala la utafiti wa kulinganisha bali ni suala la kuwaozesha waislamu kwa wasio kuwa waislamu na huo ni utafiti mwengine. Na maelezo yake ni kuwa Allah (swt) amemruhusu muislamu kumuowa mwanamke wa kitabiyah: yahudi au mnasara, kwa sababu Allah (swt) anasema:

{ الْيَوْمَ أَحْلَّ لَكُمُ الطَّيَّبَاتُ وَطَعَامُ الدِّينِ أُوتُوا الْكِتَابَ حَلٌّ لَكُمْ وَطَعَامُكُمْ حَلٌّ لَهُمْ وَالْمُحْسَنَاتُ مِنْ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُحْسَنَاتُ مِنْ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ مُحْسِنِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ وَلَا مُتَخَذِّي أَخْدَانٍ ...} (المائدة: 5)

“Leo mumehalishiwa nyinyi vizuri, na chakula ambacho cha waliopewa vitabu ni halali kwenu na chakula ni halali kwa, wanawake wema katika wanawake waumini, na wanawake katika waliopewa vitabu kabla yenu mutakapo wapa mahari yao na kuwaowa billa ya kufanya uasharati au kuwaweka kinyumba.” (Maidah – 5) kwa hivyo aya iko wazi kuwa wanawake wema katika waliopewa vitabu ni halali kwa waislamu, na ujira wao ni mahari yao, na inajuzu kwa mwanamume muislamu kuowa mwanamke wa kitabiya kwa mujibu wa ayah ii. Kwani imetaja kkuwa wanawake wema miongoni mwa waliopewa vitabu ni halali kwa waislamu, yaani kuwaowa ni halali kwenu. Ama mwanamke muislamu kuolewa na mwanamume wa vitabu ni haramu kisharia wala haifai kabisa, na ikipatikana basi ni ndoa batili na haikufungika. Na uharamu wa kuolewa mwanamke muislamu na mwanamume wa vitabu imethubutu wazi katika Qur'an amesema Allah (swt):

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا جَاءَكُمُ الْمُؤْمَنَاتُ مُهَاجِرَاتٍ فَامْتَحِنُوهُنَّ اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ فَإِنْ عِلِّمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ لَا هُنَّ حِلٌّ لَهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ } (...المتحنة: 10)

“Enyi mulioamini wakiwajieni nyinyi wanawake waumini waliogura basi wajaribuni wao, na Allah ni muelewa kwa Imani yao, na mukiwajua kuwa ni waumini basi musiwaregeshe kwa makafiri, wao (wanawake waumini) sio halali kwa (wanaume

*makafiri) na wao (wanaume makafiri) sio halali kwao (wanawake waumini)* (Mumtahinah – 10). Na ayah ii haiwezekani kuwa na maana illa moja tu na sio nyengine, nao ni mwanamke muislamu si halali kwa makafiri na makafiri si halali kwa wanawake waislamu. Na ndoa ya kaffiri kumuoia mwanamke muislamu ndo haifungiki, amesema Allah (swt):

﴿فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ لَا هُنَّ حِلٌّ لَهُمْ وَلَا هُنْ يَحْلُونَ لَهُنَّ﴾ (المتحنة: 10)

“*Mukiwajua ni waumini basi musiwaregeshe wao kwa makafiri wao (wanawake waislamu) si halali kwao (wanawake waislamu)*” (Mumtahinah – 10) na akatumia neno makafiri (kuffar), na hakutumia neno washirikina. (Mushrikin), kwa kujumuisha killa alie kafiri, awe mushrikina au ahlul-kitab. Ama asli ya ahlul kitab manasara na mayahudi ni makafiri imethubutu kwa aya ya Qur'an amesema Allah (swt):

﴿مَا يَوْدُ الدِّينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الْمُشْرِكِينَ أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِنْ خَيْرٍ مِنْ رَبِّكُمْ ...﴾ (البقرة: 105)

“*Hawapendei makafiri katika ahlul kitab na mushrikin muteremshiwe nyinyi kheri yoyote kutoka kwa Mola wenu*” (Baqarah-105) na (min) hapa ni ufanuzi na sio ya baadhi (tabiidh) na amesema Allah (swt):

إِنَّ الَّذِينَ يَكُفِّرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُغَرِّفُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَخَذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا - أُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَقًا وَأَعْنَدُنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا﴾ (النساء: 150 - 151)

“*Hakika wanaomkufuru Allah na Mtume wake, na wanataka kutenganisha baina ya Allah na Mtume wake, na wanasema tunaamini baadhi na tunakufuru baadhi na wanataka kuweka njia katika hayo – hao ndio makafiri wa kihakika, na tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha*” (Nisa-150 – 151). Na ahlul-kitab haawamini ujumbe wa Muhammad (saaw) kwa hivyo ni makafiri. Na amesema Allah (swt):

﴿لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ ...﴾ (المائدة: 17)

“*Hakika wamekufuru ambao wanasema kuwa Allah ni mosihi mtoto wa Maryam*” (Maidah-17) na akasema (swt):

{ لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ ... } (المائدة: 73)

“wamekufuru waliosema Allah ni watatu katika watatu”  
(Maidah-73) na akasema (swr):

{ لَمْ يَكُنْ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ ... } (البينة: 1)

“Hawakuwa ambao waliokufuru katika ahlul-kitab na mushrkina “Bayyinah-1) na (min) hapa ni ya ufanuzi na sio ya badhi. Na amesema: (swt):

{ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ ... } (البينة: 6)

“Hakika waliokufuru katika ahlul-kitab na mushrikina“Al-Bayyinah – 6) na (min) hapa pia ni ufanuzi na sio ya baadhi. Na akasema:

{ هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ مَيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ... } (الحشر: 2)

“Ni yeye amabe amewatoa waliokufuru katika ahlul-kitab kutoka majumbani mwao kwa mjumuiko wa kwanza “(Hushr – 2) na akasema (swt):

{ أَلَمْ تَرَى إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِأَخْوَانِهِمْ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ } (الحشر: 11)

“Hukuwaona walio fanya unafiki wanasema kuwaambia nduguzao walio kufuru katika ahlul-kitab” (Hashr-11). Na kupitia aya hizi yabainika kuwa ahlul kitab ni makafiri kwa uwazi wa ayah, na neno makafiri (kuffar) linawakusanya. Na kwa hivyo qauli yake (swt):

{...فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ لَا هُنَّ حِلٌّ لَهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ...} (المتحنة: 10)

“Na mukiwajua ni waumini basi musiwaregeshe wao kwa makafiri, wao (wanawake waislamu) sio halali kwao (wanaume makafiri) na wao (wanaume makafiri) sio halali kwa (wanawake waislamu)” (Mumtahinah -10) ipo wazi katika kukataza mwanamke muislamu kuolewa na ahlul-kitab kabisa, kwa sabau ahlul – kitab ni makafiri wazi.

Ama mushrikina nao ni wasiokuwa watu wa kitab, kama majusi na masabaj na mabuda na wanaoabudu masanamu na

mifano yao, kwani haijuzu kuowa kwao kabisa, kwa hivyo haifai kabisa kwa muislamu kuowa mwanamke mushrikina, na pia haifai kabisa kwa mwanamke muislamu kuolewa na mushrikina na hili limekuja wazi katika aya ya Quran iliokatikiwa, amesema Allah (swt):

{ وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكَاتِ حَتَّىٰ يُؤْمِنَنَّ وَلَا مُؤْمِنَةً خَيْرٌ مِّنْ مُشْرِكَةٍ وَلَوْ أَعْجَبْتُمُوهُنَّا  
تُنْكِحُوا الْمُشْرِكِينَ حَتَّىٰ يُؤْمِنُوا وَلَعَذْدُ مُؤْمِنٍ خَيْرٌ مِّنْ مُشْرِكٍ وَلَوْ أَعْجَبْتُمُوهُنَّا } (البقرة: 221)

“Na musiwaowe mushrikina mpaka waamini na kijakazi muimini ni bora kuliko mushrikina hata lau kama amewapendezea na musiwaizeshe mushrikina mpaka waamini na mtumwa muumini ni bora kuliko mushrikina hata lau kama amewapendezea” (Baaqarah -221) na aya hii haiwezekani kuwa imebeba maana nyenghine illa maana moja nao ni uharamu wa kumuowa mushrikina na mushrikina kumuowa muislamu uharamu kata kata, na ikipatikana mfano wa ndoa hiyo itakua ni batili na haitafungika. Imepokewa kutoka Hassan bin Mohamed amesema: “Aliwaandikia Mtume (saaw) majus wa Hajar akiwalingania katika Uislamu na atakae silimu atapolekewa na atakae kataa atawekewa jizyah na kisiliwe kichinjo chake na mwanamke wao asiolewe”.

Na kwa hayo sharia haikuacha tu kuhimiza kuowa na kulipendekeza bali alibainisha pia ni yupi anaefaa kuolewa na mwanamume muislamu na yupi anaefaa kumuowa mwanamke muislamu na wale ambao ni haramu juu yao wao wawili kuowa na kuolewa, na akabainisha sifa ambazo zitakazompendeza kwa anae taka kuowa kuzingatia katika mkewe. Isipokuwa ni sharti mwanamke asiwe ni mke wa mwengine au alie na eda, kwa sababu ni sharti ya ndoa ni mwanamke kua faragha na ndoa na eda.

Ama alieposwa ambae ndoa yake haijafungwa, itaangaliwa iwapo amekubali mwenye kuposa kwa posa yake yeye au msimamizi wake, au amemudhinisha msimamizi wake katika kumjibu au kumuozesha, iwe ni wai au ishara, kwa hivyo ni

haramu kwa mwengine kumposa yeye, kwa yaliopokewa kutoka kwa Uqbah bin Amir kua Mtume (saaw) alisema: “mumin ni ndugu wa mumin, kwa hivyo si halali kuvunja bei ya ndugu yake, wala asipose juu ya posa yake mpaka awache” Na imepokewa kutoka kwa Abu Hureirah kutoka kwa Mtume (saaw) alisema; “Mtu asipose juu ya posa ya ndugu yake mpaka aowe au awache”. Ama bado anafanya utafiti juu yake wakati huo inafaa kwa mwanamume mwengine kumposa na hatazingatiwa kua ameposwa na yoyote, kama ilivyopokewa na Fatimah bin Qeysi kua yeye alikuaja kwa Mtume (saaw) na akaeleza kua Maawiyah na Aba Taham wamekuja kumposa yeye, akasema Mtume (saaw): “Ama Muawiyah ni masikini na hana mali, ama Aba Jaham haiondoshi fimbo yake kutoka shingo yake, olewa na Usama bin Zeid” na Mtume (saaw) alamposea Usama baada ya kumueleza yeye kuhusu posa ya Muawiyah na Aba Taham.

Na anaposwa mwanamke basi ni yeye tu alie na haki kukubali ndoa au kukataa na wala sio kwa yoyote katika wasimamizi wake wala kwa wengine kumuozesha yeye billa ya idhini yake au kumkatalia kuolewa. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas amesema; Mtume (saaw) “Mke mkuu ana haki zaidi kwa nafsi yake kuliko msimamizi wake, na bikra hatakwa idhini yeye mwenyewe na idhini yake ni kimya chake” yaani kunyamaa. Na imepokewa kutoka kwa Abi Hureirah amesema: Mtume (saaw) “Asiozwe mke mkuu mpaka ashauriwe, wala bikra mpaka atakwe idhini yake? Akasema ni kunyamaa”. Na imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas “kua msichana bikra alikuaja kwa Mtume (saaw) na akaeleza kua babake amemuozesha nae anachukia, basi Mtume (saaw) akakhiyarisha”. na imepokewa kutoka kwa Khansaa binti Khudhaam A-ansaria “kua babake alimuozesha akiwa bikra nae aalichukia hilo na akaja kwa Mtume (saaw) akavunja ndoa yake”. Kwa hivyo hadithi hizi ziko wazi kua mwanamke ambae hakutakwa idhini katika ndoa yake, basi ndoa yake haikamiliki, na akikataa ndoa hiyo au kuozeshwa kwa nguvu haitafaa illa arudi au aridhike.

Ama ukatazo wa kumzuia mwanamke kuolewa anapokuja mwenye kumposa imethubutu katika Qur'an amesema Allah (swt):

{ فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَنْكِحُنَّ أَزْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضُوا بَيْنَهُمْ بِالْمَعْرُوفِ } (البقرة: 232)

"*Musiwazuie wao kuolewa na waume zao (wa kale) iwapo wataridhiana baina yao kwa uzuri*" (Baqrah-232) na imethubutu kwa hadithi sahihi iliopokewa kutoka kwa Ma'aqat bin Yassar amesema: " Nilimuozesha dadanu kwa mtu na kisha akampa talaqa, ilipomalizika eda yake akaja tena kumposa na nikamuambia; Nilikuozesha na nikamfanya yeye kua kitendo chako na kukukirimu na kisha ukamuacha, kisha waja kumpsa, haiwezekani naapa na Allah hataregea tena kwako milele, na alikua ni mtu asie na ubaya, na mwanamke alikua anataka kuregea tena kwake. Na Allah akateremsha aya hii:

{ فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ } (البقرة: 232)

"*Musiwazuie*" (Baqarah – 232) nikasema sasa nitafanya ewe Mtume wa Allah, akasema: akamuozesha yeye". Na katika riwayah nyengine akasema: "Nikatoa kaffarah kwa kiapo changu na nikamuozesha yeye". Na maana ya ADHL ni kumzuia mwanamke kuolewa anapotaka, nao ni haramu na anaefanya haya ni fasiqi, kwa hivyo killa anaemzua mwanamke kuolewa hua fasiqi kwa kitendo chiae hicho. Na wameelezea wana Vyuoi kua mtu hua fasiqi kwa kuzuia. Na wakati mwanamke anapoposwa kwa ajili ya ndoa au akitaka kuolewa basi yeye pekee ataamua au kukubali au kukataa.

Na wakati yanapokamilika maafikiano baina ya mwanamume na mwanamke juu ya ndoaa basi ni juu yao waendeleze kwa kufunga ndoa kwani haitakamilika ndoa illa kwa kuifunga kisheria. Na ndoa hiyo haitkua ni ndoa illa kwa kuifunga na sharia ambazo zimefuatwa kwa mujibu hukmu za kisheria, ili iwe ni halali kwa mmoja wao kustarehe na mwengine, na ili ipangiliwe juu yake hukmu ambazo zinapagilia juu ya ndoa. Na madam hayajapatikana mafungamano hayo haitkua ni ndoa, hata lau kama ameishi mwanamume na mwanamke kwa muda mrefu. Na mpaka hapa maingiliano ya

wapenzi wawili kama wanavyoingiliana walioowana wawili haizingatiwi kua ni ndoa. Bali huzigatiwa ni zinaa na maaingiliano ya wanaume wawili kwa makubaliano ya mapenzi, haizingatiwi kua ni ndoa bali inazingatiwa ni uliwati.

Ama ndoa za kiinchi ni makubaliano yanaofungwa baina ya mwanamume na mwanamke juu ya maaingiliano na talaka na juu ya yaliopagwa kuhusiana na hayo kama usimamizi (nafaqa) na matumizi na kutoka nje ya nyumba na mke kumtii mume na mume kumtii mke na mengineo kama utoto na mtoto wa kiume ni wa nani na mtoto wa kike ni wa nani na mengineo kama kurithi na nasaba na mengineo kwa yaliopangwa juu ya maaingiliano au kuacha maaingiliano. Kwa mujibu wa sharuti watakzo kubaliana juu yake na kujilazimisha kutekeleza. Kwa hivyo ndoa za kiinchi sio makubaliano ya ndoa pekee bali ni makubaliano kamili ya ndoa, na yaliopangwa juu ya ndoa hiyo kuhusu nasaba na nafaqah na urathi na mengineo, na imejumuisha killa hali ambazo inawafaa kwao au kwa yoyote kati yao kumuacha mwengine, yaani imekusanya talaka, na juu ya hayo hufuata kwa killa mwanamume kuoa mwanamke yoyote na mwanamke kuolewa a mwanamume yoyote, kwa mujib wa makubaliano ambayo watakubaliana nayo katika killa kitu wanachotaka kwa mujibu wa makubaliano yao wao wawili. Na wala haingaliwi kwa sifa ya makubaliano ya ndoa kabisa, wala hazingatiwi kua kufunfa ndoa kwa sababu haina thamani mbele ya sharia.

Na ikifungwa ndoa ya kiinchi baina muislamu mwaameme na muislamu mwanamke au baina ya muislamu mwanamume na mwanamke wa kitabiyah, huangaliwa matamshi ambayo yamepatikana baina ya mwanamume na mwanamke kuyatamka au kuyaandika, iwapo yamepatikana baina yao matamshi ya tazwij na inkhah na yamepatikana kupendekeza (ijaab) na kukubali (qabul) kutoka kwao wao wawili, na wakatekeleza yale ambayo ni wajibu katika ijaab na qabul kisharia na kupatikana msimamizi (wali) na kupatikana mashahidi wawili wakati wa ndoa hiyo itakua ni ndoa, kwa matamshi hayo kwa

namna hiyo, kwa sababu ni ndoa iliokamilisha sifa za ndoa kwa sharia a masharti yake. Kwa hivyo ni ndoa iliofungwa kisheria, wala sio kwa sharia za nchi. Na yasipopatikana baina yao yale ambayo ni wajibu yapatikanae katika ndoa ya kisharia haitazingatiwa ni ndoa. Ama masharti ambayo yamekusanywa na mkataba wa ndoa za kiinchi hazina thamani kabisa. Lau kama zinaafikiana na sharia. Kwani uwajibu wa kutekeleza hukmu ambazo zimekuja na sharia hazikuelezwa kwa makubaliano juu yake baina ya mume, bali hutekelezwaw kwa kufunga ndoa na kwa hukmu za sharia ambayo imezifafanua. Kwa hivyo hayazingatiwi masharti ambayo yamekusanywa na mkataba wa kiinchi katika ndoa. Ama ikiwa ni kinyume na sharia basi ubatili wake ni dhahiri. Na iwapo masharti hayo ni yale aliyoyaruhusu na sharia kwa mmoja wa maharusi wawili amezishurutishahaziendi kinyume na sharia wala kugongana na yanayohitajika katika kufunga ndoa, hiyo itazingatiwa iwapo itazingatiwa kufunga ndoa baina yao, ama iwapo hayatazingatiwa kwa yaliopita baina yao kufunga ndoa basi hazina thamani kabisa, hiyo iwapo itaptikana kufunga ndoa za kiinchi baina ya Muislamu mwanamume na muislamu mwanamke wa ahlul-kitab, ama ikifungwa ndoa ya kiinchi baina ya muislamu mwanamume na mwanamke asie muislamu basi ndoa wakati huo itakua ni batili wala haitafungika. Na kwa hayo ni wajibu ikamilike ndoa kwa kuifunga kwa njia sahih ya kisheria itakao kamilisha masharti yote ya kisheria, na iwapo hayatakamilishwa kwa hayo haitakua ni ndoa kabisa.

Na itafungika ndoa kwa ijaab na qabul ya kisheria, wa hivyo kupendekeza (ijaab) ni ile inaotoka mwanzo katika mazungumzo kwa mmoja wa wanafunga ndoa, na qabul (kukubali) ni yale yanaopatikana ya pili katika mazungumzo ya anaefunga wa pili. Ni kusema alieposwa kumuambia alieposa. Nimejiozesha nafisi yangu kwako. Na atasema alieposa: Nimekubali. Au aseme tafauti. Na kama ijaab na qabul baina ya waposi wawili moja kwa moja wao wenyewe vile vile inafaa kwa wawakilishi wao, au baina ya mmoja wao na mwakilishi wa mwenyewe. Na ni sharuti katika ijnaab iwe kwa lafdhi ya

tazwiji na nikah, na wala si sharti yawe hayo katika qabul, bali ni sharti kuridhika kwa mwengine kwa ijaab hiyo, kwa lafdhi yoyote itakaoeleweka kuridhika na qabuli kwa ndoa, na hamna budi ijaab na qabul iwe kwa matamshi ya kale (kitendo kishapita) kama niliowa na nilikubali au moja wa kwa matamshi ya kale na la pili kwa tamshi ya mustaqbal, kwani ndoa ni mkataba, kwa hivyo hamna budi yatumike matamshi yanamaanisha kishapatikana nao ni kale. Na imeshurutishwa katika kufunga ndoa masharti manne:-

Ya kwanza:- Kupatikana ijaab na qabul katika kikao kimoja, kiwe ni kikao ambacho imepatika ijaab ndicho kikao hicho hicho ambacho itapatikana qabul. Na hili iwapo wanakubaliana wamehuduria, na iwapo mmoja wao yuko katika nchi moja na mwengine yuko nyengine, na mmoja wao amuandikie barua mwengine ya kumpendezea ndoa, na mwengine kumkubalia, ndoa itafungika. Lakini ni sharti katika hali hiyo aisome au isomwe barua kwa mashahidi na wawasikilizishie matamshi au awaambie mashahidi fulani amenitumia ujumbe wa kuniposa na awashuhushe mashahidi katika kikao hicho kua ameshajiozesha nafsi yake kwake.

Na sharti la pili:- katika masharti ya ndoa anaefunga ndoa asikie maneno ya mwengine na ayafahamu na ijulikane kua anataka kufunga ndoa kwa matamshi hayo. Na iwapo haikujulikana hayo yaani hayakusikika au kufahamika, kama atamke mwanamke kumuambia mwanamke nimeizoeshe nafsi yangu kwa mfano kwa lugha ya kifaransa na mwanamke haifahamu, na akasema matamshi ambayo mwanamume alioyatamka billa ya kufahamu na ye ye akakubali billa ya kuelewa lengo la yale yanayotamkwa katika kuifunga ndoa, basi ndoa haitafungika. Na iwapo anaelewa lengo la yale anayotamka katika kufunga ndoa basi inasihi.

Sharti la tatu:- Kutogongana qabul kwa ijaab iwe kugongana kiujumla au sehemu yake.

Sharti la nne:- Sharia imeruhusu au ahlu-kitab, na mume ni kua mwanamke awe muislamu au ahlu-kitab, na mume awe muislamu wala sio dini nyengine.

Na iwapo ndoa itakamilisha masharti hayo manne ndoa imefungika, na iwapo moja wapo itafungwa katika hizo basi ndoa haitafungika, na itakua ni batili kutoka msingi wake. Na ikiwa ndoa itafungwa basi hamna budi ili kusihi kwake ikamilishe masharti ya ushahihi wake nayo ni masharti matatu:-

Kwanza:- Awe mwanamke ni halali kuolewa.

Pili:- Ni kua nikah haitasihi illa kwa msimamizi, kwa hivyo hawezি mwanamke kujiozesha yeye mwenyewe, wala kumuozesha mwengine vile vile hawezی kumwakilisha mwengine msimamizi wake (wal) katika kumuozesha, na iwapo atafanya basi nikah yake haitasihi.

Tatu:- Kuwepo mashahidi wawili waislamu walio baleghe walio na akili watakao sikia maneno ya wanaofunga ndoa wanaofahamu lengo la matamshi ambayo yaliopatikana nayo ijaab na qabul ni kufunga ndoa. Ikikamilisha ndoa masharti hayo itakua ni shahihi na ikipungua moja wapo itakua ni nikah fasidi. Isipokuwa si sharti kaitka kufunga ndoa iwe ni yenye kuandikwa au kusajiliwa kama kumbu kumbu, bali ni kupatikana ijaab na qabul kutoka kwa mwanamke na mwanamume watakayotamka au kuandika na yeye kukamilisha masharti yote itakaoifanya ndoa kua ni sahihi iwe itasajiliwa au isisajiliwe. Ama asli ya ndoa haitatimia illa kwa ijaab na qabul kwa ni makubaliano kati ya wawili.

Na ukweli na ndoa ua haikamiliki wala kua ni ndoa illa kwa ijaab na qabul, ama asli y sharti katika ijaab ni lafadhi ya ndoa (zawaj) na nikah ni kwa sababu yametumika hayo amesema Allah (swt)

... زَوْجَنَاكُمْ {الْأَحْزَابِ: 37}

“Tulikuozesha” (Ahzab-37) na akasema:

**{ وَلَا تَكْحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ } (النساء: 22)**

“wala musioowe wliowaowa mababu zenu katika wanawake” (Nisa-22) na kwa kua ijmaa ya mashwahaba walifunga ndoa hivyo. Ama sharti ya kupatikana kaitka kikao kimoja, ijaab na qabul kwani hukmu ya kikao ni hukmu ya hli ya ndoa, iwapo watatengana kabla ya qabul ijaab itabatirika, kwani hakutakuwa na maaana ya kukubali kwa kutengana kwa hivyo haitakua ni kkukubali kwani kupuza ndoa pia kwa kushughulisha na kukubali kwake. Ama sharti ya moja kumsikia mwengine katika wanaofunga ndoa na kumfahamu yeye yaani kuuelewa kua anataka kufunga ndoa kwa matamshi hayo, ni kwa sababu hilo litakua ni jawabu ya kile alichopendekezewa, na kwa sababu ijaab ni mazungumzo ya moja wa wanaofunga ndoa kumkubalia mwengine, na iwapo hakuelewa hatakua amezungmziwa yeye, wala kupatikana qabul juu ya mazungumzo, kwa hivyo ukweli wake sio ijaab na qabu illa ikiwa yafahamiks juu ya kujisalimisha na ijaab yote, kwa hivyo ikitafautiana na asijisalimishe kwa yaliokuja katika ijaab basi haitakua ni qabuli. Ama asli ya sharia hamna budi iwe imeruhusu moja kumuowa mwengine kwai ikiwa imekuja katika sheria ukatzo wa kufunga haituzu kutekeleza ndoa hiyo.

Huu ni upande wa kufungika ndoa, ama kwa upande wa kusihi kwake kwani sheria ikiwa haikueleza kukataza kwa ndoa itakamilika ndoa, lakini itakuja kukataza kuindeleza ndoa juu ya sababu fulani ndoa itakua ni ni fasid lakini haitakua batili. Ama asli ya sharti mwanamke kua ni halali kwa kufugwa ndoa kwa sababu sharia imeharamisha kuowa baadhi ya wanawake a k kuharmaisha kukusanya kati ya baadhi ya wanawake, kwa hivyo ikipatikana ndoa kwa mwanamke ambae ni haramu kupatikana kwa ndoa kwa mwanamke ambae ni haramu kupatikana kwa ndoa juu yake, basi ndoa hatisihi. Ama asli ya ndoa haitasihi illa kuitia kwa Mtume (saaw) qauli yake “Hamna nikah illa kwa msimamizi (wali) “Ama asli ya mwanamke hamiliki kujoozesha nafsi yake wala mwengine wal hamiliki uwezo wa kuwakilisha bila ya wali wake katika

kumuozesha ni kama ilivyopokewa kutoka kwa Aisha kua Mtume (saaw) amesema: “Mwanamke yoyote atakae olewa bila ya idhini ya msimamizi wake basi nikah yake ni batil nikaha yake ni batil” na kama alivyopokewa Abu Hureirah kutoka kwa Mtume (saaw) amesema: “Mwanamke hamuozeshi mwanamke wala mwanamke hajiozeshi nafsi yake kwani mzinifu ndie ambae anajiozesha nafsi yake” Ama sharti la kuepo mashahidi wawili waislamu ni kwa sababu Qur'an imeshurutisha mashahidi wawili waislamu katika kutmregea alieachwa talaka regea kwa mke aliemuowa amesema Allah (swt):

{ فَإِذَا بَلَغُنَ أَجْلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا ذَوِي عَدْلٍ  
مِنْكُمْ... } (الطلاق: 2)

“Na wanapofika muda wao basi wazuieni kwa wema au watengeni kwa wema na washuhudie mashahidi wawili waadilifu mionganoni mwenu” (Talaq-2) amesema Hassan yaai waislamu wawili. Na iwapo regera ua ni kuendeleza mkataba wa nikah imeshurutishwa kuwe na mashahidi wawili waislamu, basi kuanzisha ndoa yaai kuazisha mkataba wa nikah ni awlah kuwepo mashahidi wawili na juu ya hayo asli ya kufunga ndoa na kuiendeleza ndoa yote hayo ni mmoja na hukm yake ni hukmu moja.

### Walioharamishwa katika wanawake

Na walioharamishwa kuwaowa katika wanawake imetajwa uharamu wake wazi katika Qur'an na Sunnah. Na asli katika hayo katika Qur'an na Sunnah, ama Qur'an ni qauli ya Allah (swt):

{ وَلَا تَتَكَحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنْ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَمَقْتاً وَسَاءَ سَبِيلًا } (النساء: 22)

“Na wala muisoowe walioolewa na mababa zenu katika wanawake illa yale ambayo yashapita hakika hayo ni machafu na la kuchukiza na njia mbaya” na akasema:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخْوَاتُكُمْ وَعَمَاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخْتِ وَأَمَّهَاتُكُمُ الَّتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخْوَاتُكُمُ مِنْ الرَّضَاعَةِ وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَّاتُكُمُ الَّتِي فِي حُجُورِكُمْ مِنْ نِسَائِكُمُ الَّتِي دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأَخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُورًا رَّحِيمًا - وَالْمُحْصَنَاتُ مِنِ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ كِتَابُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَأَحِلٌ لَّكُمْ مَا وَرَأَءَ ذَلِكُمْ .} (النساء: 23 - 24)

“Mumeharamishiwa niyinyi mama zenu na mabanati zenu na madada zenu na mashangazi zenu na na madada wa mama zenu na mabanati wa ndugu zenu na mabanati wa madada katika kunyonya mama wa wake zenu na watoto wa kambo kutoka kwa wanawake muliowaingilia na ikiwa hamujawaingilia basi hamna makosa juu yenu na wake wa watoto wenu wanaotoka katika migongo yenu na kujumuisha madada wawili illa yale ambayo yashapita hakika Allah ni mwingi wa kushamehe na mwingi huruma” – Na wanawake walioolewa illa wale ambao mumewamiliki na mikono ya kulia (watumwa) Allah amewalazimishia hayo juu yenu na mumehalalishiwa wasio kua hao (Nisa 23/24). Ama katika sunnah imepokewa na Abu Hureirah kutoka kwa Mtume (saaw) kua amesema: “Mtu asijumuushe baina ya mwanamke na shangazi yake na baina yake na khalati yake (dada wa mama)” Na ameipokea Muslim kutoka kwa Aisha (R.a.a) amesema: amesema Mtume (saaw) “Yameharamishwa katika kunyonyesha kama yalivyooharamishwa katika kizazi”

Imeharamishwa kabisa kuwaowa mamama, na ni killa wanaonasibiana nae katika kizazi, iwe inaingia kwake jina la mama la kihakika nae ni yule aliekuzaa au kwa majazi na ni yule aliemzaa aliekuzaa wewe na kuendea juu. Na katika hao nyanya zako mama wa mamako na mama wa babako na manyanya wawili wa mamako na manyanya wawili wa babako na nyanya wa nyanyako na manyanya wa mababu zako na kuenda juu wanaorithi au wasiorithi wote ni mamama waliharamishwa.

Na ni haramu kabisa kuwaowa mabanati nao ni killa mwanamke anenasibiana na wewe kwa kizazi kama mabanati wa mgongo na mabanati wa watoto wa kiume na mabanati wa watoto wa kike na hata wakashuka daraza zao wanaorithi au wasiorithi wote hao ni mabanati walioharamishwa.

Na imeharamishwa kabisa kuwaowa madada kwa namna tatu kwa upande wa wazazi wawili au kwa baba au kwa mama.

Na imeharamishwa kuwaowa mashangazi madada wa baba kwa upande tatu, na madada wa mababu kwa upande wa baba na kwa upande wa mama wa karibu awe babu au mbali, anae rithi au asierithi.

Na imeharimishwa kuwaowa makhalati madada wa mama kwa namna tatu na madada wa nyanya hata kwa juu kwa sababu kila nyanya ni mama kwa hivyo killa dada wa nyanya ni khalati alieharamishwa.

Na imeharamishwa kuwaowa mabanati wa ndugu wa kiume, na killa mwanamke anaenasibiana na kaka kwa kizazi hiyo ni binti wa kaka alieharamishwa, kwa namna yoyote yule awe kaka na mabanati wa madada pia ni haramu.

Na imeharamishwa kuwaowa mamama wa kuwanyonyesha ni ni wale waliokunyonyesha wewe na mama zao na nyanya zao hata wakiwa juu kwa daraja, kwa namna iliotajwa katika nasaba. Na mwanamke mamake aliekunyonyesha au mamako alemyonyesha au aliekunyonyesha wewe na yeye mwanamke moja kwa aliekunyonyesha wewe na yeye kutoka kwa maziwa ya mwanamume moja hata lau kama wakiwa wengi walionyonyesha huyo ni dadako ni haramu juu yako.

Na imeharamishwa kuwaowa mamama wa wake, kwa hivyo yoyote atakae owa mwanamke ni haramu juu yake kila mamake kwa nasaba au kunyonyesha wa karibu au mbali kwa kufungika tu ndoa amuingilie au asimuingilie kama alivypokea Amru bin Shueb kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake kua Mtume (saaw) amesema: “Yoyote atakae owa mwanamke na akampa talaka kabla hajamuingilila hamna makosa kumuowa mtoto wake wa kambo na wala si halali kwake kumuowa mamake”

Na imeharamishwa kuwowa mabanati wa wake ambao amewaingilia nao ni watoto wakambo kwani sio haramu illa kwa kuwaingili mama zao nao ni killa binti wa mke kwa nasaba au knyonya kwa karibu au wa mbali anaerithi au asie rithi kwa mujib wa ilivyotajwa katika mabanati ikiwa amemuingilia mama ni haramu juu yake awe yuko chini ya ulezi wake au asiwe kwa sababu imetajwa:

{ الَّتِي فِي حُجُورٍ كُمْ } (النساء: 23)

“*Ambao wako chini ya usimamizi wenu*” ameeleza kwa zaidi ilivyo hali yake wala haikuletwa kwa masharti, ama kueleza:

{ مِنْ نِسَائِكُمُ الَّتِي دَخَلْتُمْ بِهِنَّ } (النساء: 23)

“*kutoka kwa wake zenu ambao mumewaingilia*” (Nisa-23) hiyo imeajwa kwa sharti kwa uwazi wa yaliokuja baada yake:

{... فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ ...} (النساء: 23)

“*Iwapo hamuwaingilia basi hamna makosa kweu*” (Nisa-23) na kwa hivyo ikiwa hajamuingilia mwanamke basi sio haramu kumuowa binti yake.

Na ni haramu kabisa kuowa mabibi wa watoto wa kiume, yaani ni haramu kwa mtu wake wa watoto wake wa kiume na wtoto wa mabinti wake kwa nasaba au kunyonyesha wa karibu au mbali kwa kufunga ndoa ni sawa awe amemuingilia au hajamuingilia.

Na ni haramu kuowa wake wa baba, imeharamishwa juu ya mtu wake wa babake wa karibu au anae rithi au asie rithi wa nasaba ua kunyonyesha. Ameiopkea Naai kua Barra bin Azib amesema: “Nilikutana na mjombangu na amebeba bendera, nikamuuliza waenda wapi? Akasema; Mtume (saaw) amenituma kwa mtu alieoowa mke wa babake baada yake niikate shingo yake au nimuuwe.”

Na imeharamishwa kuwajumuisha madada wawili, iwe kwa nasaba au kunyonyesha, kwa upande wa baba na mama au kwa

baba au kwa mama iwe ni kabla ya kumuingilia au baada yake na ikiwa atawaowa kwa ndoa moja ndoa itafisidika.

Na imeharamishwa kujumuisha baina ya mwamke na shangazi yake na baina ya mwanamke na khalati yake. Kama alivypokea Abu Hureirah amesema: amesema Mtume (saaw) “Asijumuushe mtu baina ya mwanamke na shangazi yake wala baina ya mwanamke na khalati yake” Na katika mapokezi ya Abu Daud” Asioolewa mwanamke juu ya shangazi yake wala shananzi juu ya binti ya kakake, wala mwanamke juu ya khalati yake wala khalati juu ya binti ya dadake, asiolewe mkumbwa kwa mdogo wala mdogo kwa mkubwa.”

Na imeharamishwa kuwaowa walio na waume, Allah (swt) akawaita wema kwa sababu wamezihifadhi tupu zao kwa kuolewa.

Na yameharamishwa katika kunyonyesha kama yalioharamishwa katika nasaba, kwa hivyo killa alieharamishwa kwa nasaba vile vile imeharmishwa katiak kunyonyesha, nao ni mamama na mabanati na madada na mashangazi na makhalati, na mabanati wa kaka na mabanati wa madada kwa namna ilivyoelezwa katika kuharamisha nasaba kwa qauli yake Mtume (saaw) “Yameharamishwa katika kunyonyesha yale yalioharmishwa katika nasaba” Na katika mapokezi ya Muslim “kunyonyesha inaharamisha yalioharmishwa na kizazi” na amepokea Aisha (raa) “Aflah kaka wa Abi Al-qabiis alitaka idhini kuingia kwangu baada ya kuteremka aya ya hijab, nikasema naapa na Allah sitakurusu mpaka nilombe ruhusa kwa Mtume (saaw) kwa kaka wa Abi Al-qa’ais sie alieninyonyesha lakini alieninyonyesha ni mke wa Abi Al-qa’s, akaja kwangu Mtume (saaw) nikasema: Ewe Mtume wa Allah, mtu huyu sie alieni nyonyesha lakini mkewe ndie alieninyonyesha akasema: Mruhusu kwani yeye ni Ammi yako, unge angamia au kupotea usingeli uliza” na kilichoharamishwa katika kunyonyesha ni maziwa, kwa hivyo mwenye maziwa ambayo mtu amenyonyesha anakua ni haramu yeye na yule ambae

amenyonya kwake awe mwenye maziwa ni mwanamume au mwanamke iwe yule alienyonya ni mtoto wa aliemnyonyesha au asiwe ni mtoto wake, na mpaka hapa ni halali kwa mtu dada wa kakake wa kunyonya na si halali kwake kaka wa kunyony wala dada wa kunyonya, na ikiwa mtu amenyonya kwa mwanamke basi huyo mwanamke atakua mamake wa kumyonyesha na mumewe ni baba wa kunyonyesha na watoto wao ni ndugu zake wa kunyonya, lakini madada wa mtu alienyonya sio ndugu wa ndugu za wa kunyonya, kwa hivyo inajuzu kwao kuowa madada wa ndugu yao wa kunyonya, kw hivyo kilicho haramishwa ni maziwa yao wala sio jengine.

Hawa ndio wanawake ambao ni haramu kuwowa, na wasio kua hao si haramu kuwaowa kwa qauli yake (swt):

...وَأَحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذِكْرِنَا {النِّسَاءُ: 24}

“*Na mumehalalishiwa nyinyi wasioi kua hao*” (Nisa-24) illa walioagilia amelezo ya kuhamishwa kwao wakiwa ni washiriki na walioolewa.

### Wake wengi

Amesema Allah (swt) katika kitabu chake tukufu:

...فَكُحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَثْنَىٰ وَثُلَاثَةٍ وَرُبَاعَ فَإِنْ خِفْتُمُ أَلَا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً  
أَوْ مَا مَلَكْتُ أَيْمَانُكُمْ... {النِّسَاءُ: 3}

“*Oweni munaowapenda nyinyi katika wanawake wawili wawili na watatu watatu na wane wanne, na iwapo mutaogopea kutofanya uadilifu basi mmoja au walioamilikia na mikono yenu ya kulia (watumwa) hilo ni bora ili musivuke mipaka:* (Nisa – 3). Aya hii ilimteremka bwana Mtume (saaw) katika mwaka wa nane wa hijrahi. Na kuteremka kwake ilikua kuifungia mipaka idadi ya wanawake kwa nne, na ilikua mpaka kuteremka kwake haina mipaka. Na katika kuisoma na kuifahamu yabaininka kua iliteremka kuiwekea mipaka idadi ya wake kwa nne. Na maana ya ayah oweni ambao ni halali kwenu na wanaowapendezeeni katika wanawake wawili au watatu au wane. Na wawili na watatu na wane ni sawa na kukariri, yaani oweni munaowapenda nyinyi kwa idadi hii wawili wawili na watatu watatu na wane wane, na imezungumziwa wote. Kwa hivyo

ilibidi ikaririwe ili ieleteke kwa kile anaeowa wake kadha anaowataka yeye katika idadi iwe ni sharti kwa kukusanya kwa yoyote imefungika katika idadi hiyo. Ili ieleteke kwa killa aneowa anaetaka kujumuisha anaotoka kwa idadi aliotamkiwa yeye, kama tunavowaambia watu gaweni mali hii. Na kwa mfano iwe ni dinari elfu moja. Tunasema gaweni dinari mbili mbili na dinari tatu tatu na dinari nne nne. Na ukiitaja mara moja haitakua na maana kwa hivyo hamna shaka kwa kueleza mbili mbili na tatu tatu na nne nne ili apate killa mmoja anachotaka kwa idadi maalum katika kueleza. Kwa hivyo Allah (swt) anasema:

.. فَانْكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَثْنَى وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ . {النساء: 3}

"Aowe killa mmoja wenu munaowapenda nyinyi katika wanawake wawili na watatu na wane. Na hii yamaanisha nyoteni nyinyi oweni wawili wawili na watatu watatu na wanne wanne. Yaani aowe killa mmoja katika nyinyi wawili na watatu na wanne. Na maana ya auli yake:

فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً { النساء: 3}

"Na iwapo munaogopea kutofanya uadilifu basi mmoja tu" (Nisa-3). Na iwapo munaogopa hamutafanya uadilifu katika idadi hiyo basi oweni mmoja na muwachie kujumuisha. Kwa hivyo basi oweni mmoja na muwache kujumuisha. Kwa hivyo suala zima linazunguka pamoja na uadilifu, kwa hivyo popote munapo weza uadilifu basi ni juu yenu nalo, na asli ni kua muowe mmoja ni ubora kwa kutofanya dhulma. Kwa hivyo maana ya Alla taulu yaani musifanye dhulma kwa sababu ya hapa ni dhulma, husemwa A'la hakim anapo dhulumu. Na amepokea Aisha (raa) kutoka kwa Mtume (saaw) "Musivuke mipaka: Musidhulumu".

Na aya inaruhusu wake wengi na kuifunga kwa wanne lakini pia inaanrisha uadilifu kati yao, na kupekeza katika kujifunga na mmoja katika hali ya kuogopea kutofanya uadilifu, kwa sababu kujizua kwa mmoja katika hali ya kuogopea kutofanya uadilifu ni karibu na kutofanya dhulma nalo ni wajibu kuwa nalo muislamu.

Isipokua ni wajibu ieleweke kua uadilifu hapa sio sharti katika kuruhusu wake wengi bali ni hukmu ya kumueka mtu ambae anaowa idadi ya wanawake. Katika kumwajibisha yeye katika hali ya kuzidisha na mapendekezo katiak kujizuia kwa mmoja katika hali ya kuogopea katika kufanya uadilifu, na haya maana ya maneno yamekamilishwa katika ayah katika qauli yake:

فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَتْنَى وَثُلَاثَ وَرِبَاعَ .. {النساء: 3}

*“Oweni munaowapenda nyinyi katika wanawake wawili wawili na watatu watatu na wanne wanne”* (Nisa-3) nah ii maana yake ni kuwepo wazi ruhusa ya wengi, na ikakamilisha maana ya maneno na baadae kuandi maneno mengine

فِإِنْ خَفْتُمْ { (النساء: 3)

“Na iwapo mutaogopea” (Nisa-3) na wala haiwezi kua:

فِإِنْ خَفْتُمْ { (النساء: 3)

“Na iwapo mutaogopea” (Nisa-3) kua ni sharti kwa sababu hayakuungana na maneno ya kwanza kwa muungo wa sharti, bali ni maneno yaliofuatia, na lau angetaka kua ni sharti angelisema oweni wanawake munaowapenda nyinyi wawili wawili na watatu watatu na wanne wanne iwapo mutafanya uadilifu. Na hayakua hayo kwa hivyo imethubutu kua uadilifu sio sharti, bali ni hukmu imethubutu kua uadilifu sio sharti, bali ni hukmu ya sharia nyengine na sio hukmu ya kwanza. Kwa hivyo mwazo yeye aliruhusu wake wengi mpaka wanne na baada kuja na hukmu nyengine nao ni bora kujizuia na mmoja iwapo ataonelea kuowa kwake wengi zaidi ya mmoja iwapo ataonelea kuowa kwake wengi zaidi ya mmoja itamfanya yeye asifanye uadilifu kati yao.

Na kwa hayo yabainika kua Allah (swt) ameruhusu wengi (wake) bila ya kizuizi wala sharti na bila ya sababu yoyote, bali kila Muislamu aowe wawili na watatu na wanne wale anaowapenda yeye katika wanawake. Na kwa sababu hiyo tunapata Allah (swt) anasema

مَا طَابَ لَكُمْ { (النساء: 3)

“Wanawake munaowapenda nyinyi” (Nisa-3) yaani wale munaowapata katika munaowapenda nyinyi na yabainika kua Allah ametuamrisha sisi kufanya uadilifu kati ya wake, na kutupendekezeshea sisi katika hali ya kuogopea kutumbukia katika kudhulumu kati ya wake tujifunge na mmoja, kwa sababu kujizuia na mmoja ni karibu zaidi na kutofanya dhulma.

Ama uadilifu unaotakiwa baina ya wake sio uadilifu kamili, bali ni uadilifu katika ndoa kati ya wanawake ambaa unaingia katika uweza wa mwanadamu kuyatekeleza, kwa sababu Allah (swt):

{... لَا يُكِلُّ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ...} (البقرة: 286)

“Allah haikalifishi nafsi illa katika uweza wake” (Baqara-286) ndio neno uadilifu limekuja katika aya ni jumla (Ammah) na akasema:

{... فَإِنْ خِفْتُمُ الَّذِينَ تَعْدِلُوا ...} (النساء: 3)

“Iwapo mutaogopea hamutafanya uadilifu” (Nisa-3) kwani imejumuisha killa aina ya uadilifu lakini ujumla huu akaifanyia maalum kwa anayoweza mwanadamu kwa aya nyengine na akasema Ta'ala:

{ وَلَنْ تَسْتَطِعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمَيْلِ فَتَذَرُوهَا كَالْمُعْلَقَةِ ...} (النساء: 129)

“Na kamwe hamutaweza kufanya uadilifu baina ya wanawake hata mukajipindana, basi musilemee wazima na mukamwacha mmoja kama alietundikwa” (Nisa-129) hakika Allah anabainisha katika aya kua ni muhali kuweza kufanya uadilifu na usawa baina ya wanawake, 1 na ili isipatikane kupendelea kamili wala ziada wa pungwani kwa yale ambayo ni wajibu kwao, na kwa hayoo kuondoshwa juu yenu uadilifu kamili na upeo wake, na hamukukalifishwa illa munayoweza, kwa sharti mutumie uweza wenu na juhudi zenu, kwa sababu kukalifishwa yasiowezekana huingia katika mipaka ya dhulma

{... وَلَا يُظْلِمْ رَبَّكَ أَحَدًا} (الكهف - 49)

“Na Mola wako hamdhulumu yoyote” (Kahf-49) na qaulu yake Ta'ala:

**{ فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمَيْلِ...} (النساء: 129)**

“*Kwa hivyo musilemee kikamilifu*” (Nisa-129) ni maelezo ya qauli yake “Na kamwe hamutaweza kufanya uadilifu na marudio yake, na ni dalilli juu ya maana yake hamutaweza kufanya uadilifu katika mapenzi, na ufahamu wake ni uwezekanaao wa uadilifu katika yasiokua mapenzi. Nao ni yale ya wajibu katika aya iliotangulia na itakua ni makhsus ya uadilifu unaotakiwa katika aya iliotangulia na itakua ni makhsus ya uadilifu unaotakiwa katika yasiokua mapenzi na kuchujwa katika uadilifu mapenzi na kumuingilia kwani sio wajibu uadilifu katika hayo kwa sababu mwanadamu hawezi kufanya uadilifu katika mapenzi yake na maana hii yatiliwa nguvu na yaliopokewa kutoka kwa Aisha (raa) kua alisema “Mtume (saaw) alikua akigawa na akifanya uadilifu na anasema : Ewe Mola huu ni mgawanyo wangu kwa kile ninachokimiliki na usinilaumu kwa kile unachokiliki wewe wala similiki mimi “yaani moyo wake. Na imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas (raa) katika qauli yake Taala:

**{ وَلَنْ تَسْتَطِعُوا أَنْ تَعْدِلُوا...} (النساء: 129)**

“*Wala hamutaweza kufanya uadilifu baina ya wanawake*” (Nisa-129) alisema katika mapenzi na kumuingilia. Na Allah (swt) ameamrisha kujiепusha kupendelea kamili, na maana yake ni kua ameruhusu kupendelea, kwa sababu yafahamika kilichokatazwa na kupende kamili katika qauli yake Ta’ala:

**{ وَلَا تَبْسُطُهَا كُلَّ الْبَسْطِ } (الإسراء: 29)**

“*Wala usitumie kamili*” (Isra-29) maana yake ni ruhusa ya kutumia. Na kwa hivyo itakua Allah amemruhusu mume kupendelea baadhi ya wake zake kuliko wengine, kwa hivyo itakua maana ya aya jiepusheni kupendelea kamili, kwa sababu kupendele kamili likipatikana kwenu humfanya mwanamke kama alietundikwa, ambae sie aliena mume wala alieachwa. Na imepokewa kutoka kwa Abu Hureirah (raa) kutoka kwa Mtume (saaw) kua alisema “Yoyote alie na wake wawili na anapendelea mmoja wao kuliko mwengine atakuja siku ya qiyama anakokota nusu ya mwili wake umeanguka au umepeta”.

Na kwa hayo imekua uadilifu ni wajibu juu ya mume ni usawa kati ya wakeze juu ya anaoyaweza kama kulala usiku na katika chakula na mavazi na makao na yanaofanana na hayo. Ama yale yanaoingia katika maana ya kupendelea ni mapenzi na kuvutiwa kwani sio wajibu kufanya uadilifu ndani yake kwa sababu haliwezekani nao pia imechujwa kwa aya ya Quran.

Hii ndio maudhi ya wake wengi kama ilivyo kuja na nusus za kisheria, na kwa kuzisoma nusus hizi na kusimama katika mipaka ya maana ya kilugha na kisheria na yanaodokezwa na kuvuliwa humo, yabaininka kwa Allah alietukuka ameruhusu wake wengi kuruhusu kiujumla billa ya kizuizi au sharti na imepokewa nass humo isio na illah yoyote, bali Allah ameeleza kile ambacho kincho kanusha kuifanyia illah akasema:

{ مَا طَابَ لِكُمْ } (النساء: 3)

“*Wanawake munaowapenda nyinyi*” (Nisa-3) na kwa hivyo ni wajibu kusimama katika mipaka ya nass ya kisharia, na pindi inpowuliwa kutoka kwake hukmu ya kisharia, na wala haijuzu kupewa illah hukmu hiyo kwa illah yoyote, si illa ya kulinganishwa waya haja, na wala kwa yasiokua hayo, kwa sababu nass kaikuja na illah ya hukmu, na wala haikuja illah yake katika nass yoyote ya kisharia. Na ni wajibu illah ya hukmu iwe ni ya kisharia, yaani ni wajibu iwe nass imekuja nayo ili iwe inafaa kua hukmu iliovuliwa kupitia kwake hukmu ya kisheria. Na iwapa illah ya kiakili au haikuja nao nass ya kisheria haitakua ni hukmu iliovuliwa kwa wasita wake hukmu ya kisheria bali itakua ni hukmu iliowekwa na ni haramu kuichukua wala haijuzu kuitabikisha kwa sababu itakua ni hukmu ya ukafiri. Kwani killa hukmu isio ya kisheria ni hukmu ya ukafiri kwa utambuzi wa hukmu ya kisheria kua ni “*Uzungumzi wa mteremsha sheria*” (Khitab Al-sharii) inaolazimisha kua hukmu ichukuliwe kutoka kwa uzungumzi wa mteremsha sheria imma ni nass au ufahamu (Mafhum) au udokezi (dalalah) au kwa kuwepo alama (Amarah) katika nass inaodokeza juu ya hukm ya kisheria, kwa namna ambayo itakua killa hukmu iliopatikana kwa alama hiyo (Amarah) ni hukmu ya kisheria. Na alama hiyo ndio illah ya kisheria ambayo itakua

imekuja katika nass imam kwa usaraha au kwa udokezi au kwa kuvuliwa au kwa kukisia (qiyas) na iwapo haikuja alama (Amarah) hiyo yaani illah hiyo katika nass basi haina thamani. Na mpaka yabainika kua haijuzu kuifanya sababu ya wake wengi kwa sababu yoyote, kwa sababu haikuja katika uzungumzi wa mteremsha sheria illah yoyote, wala thamani kwa illah yoyote katika kuifanfa hukmu ni hukmu ya kisheria illa itakapo kuja katika uzungumzi wa mteremsha sharia.

Isipokua kutokuja sababu ya sharia katika hukmu ya kisheria kwa illah haimanishi kua haijuzu kuelezea waqiala wa athari yanaopatikana katika athari ya hukm hii ya kisheria na uhakika wa matatizo yanaotatuliwa. Lakini hayo ni maelezo ya waqiah na sio kuelezea illah ya hukmu. Na tofauti baina ya maelezo ya waqiah na kuelezea illahi ya hukmu, ni kua kuelezea illha ya hukmu kwa illah yalazimisha iwe diama ipo ndani yake, na kukisiwa (qiyas) lengine juu yake katika killa yanaopatikana ndani yake. Ama maelezo ya waqiah hua ni bayana wa yalio juu yake waqiah huu wakati wa kuelezea. Na huenda isiendelee kwa yalio juu yake humo, na wala haifai kufanyia qiyas lengine. Na kwa hayo yabainika athari katika wake wengi kua watu wanaruhusiwa wake wengi ni kua hakupatikani wapenzi wengi na watu ambao hukatazwa wake wengi huptikana humo wapenzi wengi. Mbali na hayo wake wengi hutatua matatizo mengi ambayo hupatikana katiak jama'ah (watu) ya kiuwanadamu kwa asili yao jama'a Iwat) ya kiuwanadamu, na wahitajia kutatuliwa na wake wengi. Na yafuatayo ni mfano wa matatizo hayo.

1:- Hupatikana maumbile yasioya kawaida kwa wanaume wengine ya kua hawezi tosheka na (mke) moja, kwa hivyo huenda wakawaumiza wake zao na kuwadhuru, au kudundia mwengine au mwengine iwapo watakuta mlango wa kuoa mke wa pili na watatu na wane ulioko mbele yao umefungwa. Na katika hayo kuna madhara ya kuenea uovu machafu kati ya watu na kuenea madhanna na shaka katika jamii. Na kwa ajili ya hilo imekua ni lazima mtu alie na maumbile kama hayo apate nafasi

wazi mbele yake ili aweze kushibisha njaa yake ya kiwiliwili. Ni halali katika alioyahalalisha Allah.

2:- Mwanamke huenda akawa ni tasa asiezaa, lakini ana mapenzi ya mumewe katika moyo, na mume nae ana mapenzi ya mkewe moyoni mwake, yale yatakowafanya wao kufanya bidii ya kuendeleza maisha yao ya ndoa baina yao kwa amani, na mume kua na hamu ya kuzaa na kupenda watoto, kwa hivyo iwapo hatarushusiwa yeye kuowa mwengine, na akakuta mbele yake nafasi ni finyo, basi hana jengine illa kumuacha mkewe wa kwanza na hayo yataapelekea kuvunjika kwa nyumba na amani yake, na kuangamiza maisha ya ndoa yilio na utulivu, au kumharamishia yeye kujiliwaza na kuzaa na watoto. Na hayo ni katika kukandamiza dhihirisho la ubaba katika ghariza ya kuendeleza kizazi. Na kwa hayo imekua ni lazima apate mume huyu nafasi wazi mbele yake ya kuowa mke mwengine ili apate kuzaa kama anavotaka.

3:- Huenda mwanamke akawa na maradhi ambayo hawezi kukutana kiwiliwili, au kusimamia huduma ya nyumbani na mume na watoto. Na huenda akawa ni kipenzi kwa mumewe na hataki kumuacha na wala kuishi nae pekee billa ya kuowa mke mwengine. Kwa hivyo katika hali hii ni lazima ufunguliwe mlango wa ndoa kwa mke zaidi ya mmoja.

4:- Huenda kukapatikana vita au mapenduzi na kuangamia maelefu bali mamilioni katika wanaume na kupotea usawa katika idadi ya wanaume na wanawake, kama yalivyopatikana katika vita vya kiulimwengu vya kwanza na vya pili kivitendo katika ulimwengu, na ziadi bora la uropa. Na iwapo mwanamume hataweza kuowa zaidi ya mmoja, watafanya nini katika wanawake wengi waliosalia? Hakika ataishi akiwa amenyimwa maisha familia, na utulivu wa nyumba na raha ya mume mbali na hayo yatakayo letwa na ghariza ya kuendeleza maisha inapo chemka katika khatari ya kuharibu akhlaqi.

5:- Huenda ikawa kuzaana katika ummah au taifa au sehemu Fulani idadi ya wanaume na wanawake humo haipo swawa, na huenda idadi ya wanawake kua ni nyingi kuliko idadi ya wanaume na kupotea usawa kati ya wanaume na wanawake, na yakaribia hayo ndio uhakika katika mataifa mengi ummah nyingi. Na katika hali hiyo hamna suluhisho la kutatua tatizo hilo illa kuruhusu wake wengi.

Hayo ndio matatizo ya kihakika katika jamii za wanadamu katika mataifa. Na iwapo likakatazwa kuowa wake wengi litakuwepo tatizo hilo billa ya suluhisho. Kwani hamna suluhisho illa kwa wake wengi. Na mpaka hapa ni wajibu liruhusiwe ili lisisuluhishe matatizo ambayo hupatikana kwa mwanadamu. Na uislam umekuja ukaruhusu wake wengi wala haikuelezwa ufaradhi wake. Na wajibu ijulikane kua hali hizi na mifano yake katika yale yanaompata mwanadamu na jamii za wanadamu ni matatizo ya kiuhakika yanayopatikana, wala sio illali ya kuowa wake wengi na wala sio sharti ya kuruhusu wake wengi. Bali inafaa kabisa kwa mwanamume kuowa wa pili na wa tatu na wane, iwe yapo matatizo yanaohitajia wake wengi au yasiwepo. Kwa sababu Allah Ta'ala anasema:

{ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مُثْنَى وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ ... } (النساء: 3)

“Oweni wanawke munaowapenda nyinyi wawili wawili na watatu watatu na wane wane” (Nisa-3) na akasema:

{ مَا طَابَ } (النساء: 3)

“*Munawapenda*” (Nisa-3) na akajumuisha haya bila ya kizuizi au sharti. Ama kujifunga na mmoja sharia imependekeza humo katika hali ya moja pekee, katika hali ya kuogopa kutofanya uadilifu ama katika mengineo hakupokewa mapendekezo yoyote katika mke mmoja wala nass katika nusus zozote. Na pamoja na hayo wake wengi ni hukmu ya kishria iliokuja katika aya ya Qur'an kwa swaraha, kwani thaqafah ya kirasilimali na propanganda za kimaghari dhidi ya uislamu ni za kidhati wala sio dini zote zilizosalia, na wakalifanya hukmu ya wake wengi kwa ubaya na walifanya upungufu na kukashifu dini, na yakawapelekea hayo osio kuaibisha hukmu ya Allah bali

kukashifu uislamu. Na diaya hizi ziliwaathiri waislamu na ziadi kipote cha watawala na mabarobaro wasomi, na kiliwafanya wengi wale ambao bado zipo hisia za kiislamu zinatembea ndani yao juu ya kuuhami uislamu. Na kuwafanya wao kujaribu kuweka tawili za batili kwa kukataza wake wengi, kwa mwelekeo ule ule wao walivyothiri nayo katika diayah za batili ambazo wameziweka maadui wa uislamu. Kwa hivyo hamna budi kuwatanabahisha waislamu kua mazuri (Hassan) ni yale ambayo sheria imeyafanya mazuri, na mabaya (Qabihi) ni yale sheria imefanya ni mabaya. Na yale sheria imeyaruhusu hayo ndio mazuri nayale sharia imeyaruhusu hayo ndio mazuri nay ale yalioharamishwa ni mabaya. Na wake wengi iwe kuna athari inaoonekana ni nzuri au isionekana sawa sawa itatue matitizo yaliotokea au yasitatue, kwa sheria imeruhusu na Quran imeeleza hayo kwa hivyo hicho ni kitendo kizuri na kukataza wake wengi ni uovu, kwa sababu ni hukmu ya ukafiri. Na hamna budi iwe wazi kua uislamu haukufanya suala la wake wengi ni faradhi juu ya waislamu wala la mandub kwao wao bali limeruhusiwa ambalo yajuzu kwa kulitenda wanapoonelea hayo. Na asli ya kuruhusiwa yamaanisha suluhisho limewekwa katika mikono ya watu waitumie killa wanapoona ni lazima litumike. Na wakaruhusiwa wao wasijiharmishie nafsi zao wanawake wanaowapenda wao na kulemea kwa hayo maono yao. Kwa hivyo kurushusiwa wake wengi na kutoi faradhisha ndilo linalofanya wake wengi ni suluhisho la kiuhakika la kutatua matatizo ya watu na mujtama'a za wanadamu.

### Ndoa za Mume (saaw)

Aliteremsha qauli yake Ta'ala:

فَإِنْ كُحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَتْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ فَإِنْ خِفْتُمُ الَّذِي تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ  
مَا مَلَكْتُ أَيْمَانُكُمْ } (النساء: 3)

“Oweni munaowapenda nyinyi wanawake wawili wawili na watatu watatu na wanne wanne na iwapo mutaogopea kutofanya uadilifu basi mmoja pekee au waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia” (Nisa-3). Katika mwisho mwisho wa mwaka wa nane wa Hirah, baada ya Mtume (saaw) amekwisha owa ndoa zake zote, na wakati wa kushuka kwake Mtume

(saaw) amekwisha owa wake zaidi ya wanne, lakini hakuwacha hata mmoja katika hao, bali aliendelea hivyo hivyo kuishi nao wake zake wote. Na hayo ni kwa sababu ni katika khususia zake Mtume (saaw) kuowa wake zaidi ya wanne pasi na waislamu wengineo. Na yabainika kua ni katika khususia zake kwa asli yake kuowa zaidi ya wanne na kuendelea kuishi nao baada ya kuteremka aya kwa kuweka mipaka kwa wake wanne. Kwa sababu Mtume (saaw) kitendo chake hakiendi kinyume na maneno anayoyasema, kwa hivyo ikipatikana mgongano kitendo kitakua ni katika khususia yake na qauli yake ni kwa ummah wote kwa ujumla. Kama iliyokuja katika usul Fiqh kua kitendo chake hakigongani na kauli ambayo ni khassah kwa ummah, bali itakua ni khassah kwake. Kwa sababu amri yake (saaw) kwa umma ni amri kahassa kwao wao yeye ameifanya kua ni khassa kwao kupitia dalili ya kumuiga yeye kwa maneno na matendo, na kujengwa Amm kwa khass, na kwa hivyo haijuzu kumuiga yeye katika kitendo hicho ambayo imekuja amri kwa ummah kinyume na hivyo. Juu ya hayo kuowa kwake (saaw) zaidi ya wanne na mwanamke kujipeleka kwake (Hiba) na mengineo yalioelezwa na aya ya Qur'an tukufu, amesema (swt):

{ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَحْلَنَا لَكَ أَزْوَاجَكَ الْأَتْيَتِ أَجُورَهُنَّ وَمَا مَلَكْتُ يَمِينُكَ مِمَّا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَيْكَ وَبَنَاتٍ عَمَّكَ وَبَنَاتٍ خَالِكَ وَبَنَاتٍ خَالِاتِكَ الْأَتْيَتِ هَاجِرْنَ مَعَكَ وَامْرَأَةً مُؤْمِنَةً إِنْ وَهَبْتَ نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنْ أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا خَالِصَةً لَكَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَنِيهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ وَمَا مَلَكْتُ أَيْمَانُهُمْ لَكِيلًا يَكُونَ عَلَيْكَ حَرْجٌ } (الأحزاب: 50)

*"Ewe mjumbe sisi tumekuhalalishia wewe wake zaki uliowapa mahari yao na wote uliowamiliki na mikono yako ya kulia katika alio kupa Allah, na mabinti wa ma'mmi zako na mabi mashangazi zako na mabinti wa wajomba zako na mbinti wa makhalati zako walio hama pamoja nawe na mwanamke mumini akijitoa mwenyewe kwa Mtume iwapo Mtume atataka kumuowa ni maalum (Khassah) kwako wewe billa ya waumini, tumekwisha kuyajua tuliwafaradhishia wao juu yao wake zao na waliowailiki wao na mikono yao ya kulia, ili yasiwe ni mazito juu yako (Ah-zab -50). Kwa hivyo ayah ii inasema:*

{ خَالِصَةً لَكَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ } (الأحزاب: 50)

“Ni khassa kwako wewe tu billa ya waumini” (Al-ahzab-50). Na khalisa ni chimbuko (la neno) linalotilia mkazo wa yalio tangulia yaani khalas ni halali kwako, yale tulikuhalalishia wewe khalisa, na dalili iliopokewa kua imuejumuisha yote yaliokabla yake, na ni makhush kwa Mtume (saaw), ni kwa asli yake imekuja baada kuhalalishiwa wanne, na ikiwa ni halali wake, na waliomilikiwa na mikono ya kulia (fay) moja kwa moja na mabanati wa familia yake (Aqarib) katika walio hama nae na kujitolea mwanamke moja kwa moja, ana asli yake imekuija kwa njia ya kutia mkazo. Na yanatiliwa nguvu hayo kwa asli yake imekuja kukamilisha maana hii na baada ya kauli yake:

{مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ}

“Billa ya waumini”(ah-zab-50) imekuja kauli yake:

{ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ وَمَا مَلَكُتْ أَيْمَانُهُمْ } (الأحزاب: 50)

“Tumekwisha kuwajulisha tuliowafaradhishia juu yao kwa wake zao na waliowamiliki mikono yao ya kulia (ahzab-50) kwa hivyo maana yake kua hayo sio tuliwafaradhishia juu yao, na kwa ajili ya hilo akasema baada ya yote hayo

{ ... لِكِيلًا يَكُونَ عَلَيْكَ حَرْجٌ ... } (الأحزاب: 50)

“Ili yasiwe ni uzito juu yako” (Ahzab-50) yaani ili isiwe ni dhiki juu yako.

Kwa hivyo hatafanywi ni kiigizo ndoa za Mtume (saaw) katiak matendo wala kua ni sehemu ya utafiti katiak sheria kwa sababu ni katiak khususia zake (saaw) juu ya kwamba uhakika wa ndoa zake (saaw) yaonesha kwamba zilikua ni ndoa za Mtume (saaw), na hazikua ni ndoa za mtu yoyote anaeowa kwa ajili ya maingiliano ya kijinsia na kushibisha ghariza kuendelza kizazi kwa upande wa uume na uuken. Kwani kwa kuiregelea waqiah wa tarikh tanapata kua yeye (saaw) alimuowa Khadija akiwa na umri wa miaka ishirini na nane, kwani alikufa katiak mwaka wa kumi na moja ya utume, yaani kabla ya hihra kwa miaka miwili, baada yakuvunjwa mkataba (vikwazo) kwa miezi kadhaaa na kabla ya kuenda Taif na hapo ilikua ni mwaka mia sita na ishirini miladia (620) na uri wake ulikua ni miaka khamisni (50). Na tangu kumuoa Khadija hakufiria kuoa zaidi

ya mmoja mpaka kufa kwake (Khadija), na wkti huo wake wengi ilikua ni jambo lililoenea katika waarabu katiak wakti huo. Na aliihi na Khadija miaka kumi na saba kabal ya kutumilizwa na ujumbe katika maisha matulivu yaliojaa neema, na pia aliihi nae miaka kumi na moja baada ya utume katika maisha ya kiulinganizi na kupambana na fikra za makafiri, pamoja na hayo hakufikiria kuowa, na haikuwahi kutoka kwake (saaw) katika maisha ya Khadija wala haikuwahi kutoka kwake, kua aliwahi kughurika na fitina za wanawake, na katika wakti ilikua tabarruj ya kijahiliya inawaghuri watu. Kwa hivyo si jambo la kawaida kua tunamuona yeye ameshapindukia miaka khamsini na ghafla kupatikana mabadiliko ambayo yanaomfany yeye asitosheke na mmoja bali anaowa na kuawa mpaka kufika wanawake kumi na moja kuwajumuisha kwa muda wa miaka mitano katika kumi la sita ya umri wake zaidi ya wake saba na kujumuisha katika miaka sabini katika kumi la saba umri iliobakia wake tisa. Na jee yawezekana hayoo katika umri huo ni kwa ajili ya kupenda wanawake na kwa ajili ya kushibisha ghariza ya kuendelza kizazi kwa upande wa maingiliano ya kiwiliwili? Ama kwa ajili ya msukumo mwengine aliolazimisha yeye na maisha aliokua akiishi yeye (saaw) hayo ni maisha ya utume ambayo aliamrishwa yeye awafikishie watu? Ili tuweze kuyafahamu hayo tutaeleza matukio ya ndoa zake (saaw).

Katika mwaka wa kumi na moja ya utume yaaani katiak mwaka aliokufa Khadija (raa) alifikiria kuowa, na ilikua ni katiak miaka ya khamsini. Na akamposa Aisha bint Abu Bakar, rafikiye na wa kwana kuamini katiak wanaume, kua kwa kua alikua bado ni mdogo katika mwaka wa sita wa umri wake (Aisha) alifnga ndoa nae wala hakumuingilia illa bada ya miaka mitatu na ilikua baada ya hijra wakati alipokua na miaka tisa, lakini wakati huo huo ambaa alifunga ndoa na Aisha pia alifunga ndoa na Sauda bint Zama'a. na Sauda alikua ni mjane wa Sukran bin Amru bin Abd Shams mmoja katika waislamu waliogura kuenda Habash na kuregea tena Makah na kufikia huko. Na Sauda alikua maesililmu yeye na mumewe na kugura nae na kupambana na misukosuko kama alivyopambana na

misukosuko (mumewe) na kukutana na dhiki kama alivyokutana na (mumewe). Na baada ya kufa mumewe Mtume (saaw) alimuowa. Wala haikupokelewa kua Sauda huyu alikua mzuri au tajiri au kua na hadhi katika yale yanaomvutia mtu katiak mambo ya kidunia yallo mvutia kumuowa. Kwani Mtume (saaw) baada ya kufiliwa na mumewe, na yafahamika kwa hayo kua alimuowa ili kumsimamia na kumnyanya hadhi yake na kumfanya ni mama wa waumini. Kisha baada kugura aliyoafanya makao yake karibu na msikiti, na ndio makao ya kwanza kujajenga katika makao ya wakeze.

Kisha katika mwaka wa kwanza ha hijra baada ya kukamilisha suala la kuwangularisha kiundugu kati ya Ansaar na muhajirina ndipo Mtume (saaw) alimuingilia Aisha na kukmemea makao yake ubavuni ya makao ya Sauda karibu na msikiti. Na kumuekea msaidizi wake na rafiki yake Abu Bakr awe akija nyumbani kwake kwa binti yake.

Kisha katika mwaka wa pili wa hijra baada ya vita vya Badr na kabla ya vita vya Uhud akamuowa Hafswa binti Umar bin Al-Khattab, na Hafswa alilkua ni mke wa Hanish mmoja katika wliotangulia katika uislamu, na akafiliwa kabla ya kuolewa na Mtume (saaw) kwa miezi saba, na kwa kumuowa Hafswa akamuelkea msaidizi wake wa pili na rafiki yake Umar bin Al-Khattab awe akimjia yeye nyumbani kwake katika nyumba ya binti yake, kwa hivyo ndoa yake kwa Aisha na Hafswa ni ndoa kwa mabinti wawili wa mawaziri wake na wasaidizi wake, mabinti wa marafiki zake waliokua nae katika ulinganizi na utawala na vita na mengineo. Kwa haikua kwa ajili ya kuowa tu. Na iwapo Aisha alikua ni mzuri na kipenzi cha Mtume (saaw) lakini hayo hayokuwepo kwa Hafswa. Kwa hayo yanaonesha kua kuwaowa wao silo lengo la kushibisha kiwiliwili.

Kisha katika mwaka wa tano wa hijra katika vita vya Bani Mustaliq alimuowa Juweiriyah bint Harith bin Abi Dharar, na sababu ya kumuowa ilikuwa ni kwa ajili yakumkurubisha babake na kunyanya hadhi yake. Kwani Juweiriya alikua ni

mateka wa Bani Mustaliq, na alikua ameangukia katika fungu la mmoja katika Ansaar na alikua ni binti wa bwenyenyenye wa bani Mustaliq. Na babake alikuja kwa Mtume (saaw) kumkomboa na akamkomboa, na baadaye akasilimu baada ya kuamini ujumbe wa Mtume (saaw). kisha akamchukua bint yake Juweiriya mpaka kwa Mtume (saaw) na akasilimu kama alivysilimu babake na Mtume (saaw) akamposa kwa babake na akamuowa, kwa hivyo ilikua ndoa yake kwa binti ya bwenyenyenye na kabilia alioliweka chini ya utiifu wake kwa hivyo alitaka kuyaleta mapenzi ya bwenyenyenye wao kwa kumuowa binti yake.

Kisha katika mwaka wa saba wa hijrah baada ya ushindi wa Khaibar alimuowa Swafiyah bint Huyeiy bin Akhtab mmoja katika wakubwa wa mayahudi. Na kisa cha kumuowa ni kua alichuliwa mataeka ambaao walitekwa na waislamu kwa kuizinguka Khaibar, baadhi ya waislamu wakamuambi Mtume (saaw): Swafiya ni bibie wa bani Qureidhar na Nadhir hafai mwengine illa wewe. Mtume (saaw) akamuacha huru na akamuowa, na hili ilikua ni kumhifadhi na kumuach huru katiak mateka na kunyanya hadhi yake. Na imepokewa na Aba Ayyub Khalid Al-ansari aliogopa kuwa Swafiya aweke chuki juu ya Mtume (saaw) kwa sababu ya kumulia babake na mumewe na watu wake, kwa ajili ya hilo alilala na amshikilie upanmga karibu na hema aliokua amelala Mtume (saaw) pamoja na Swafiya wakati wa kurudi kutoka Khaibar, kulipo pambazuka alimuona na kumuuliza: una nini? Akasema: nilikuogopea wewe na mwanamke huyu, amae ameua babake na mumewe na watu wake na hivi karibuni anatoka kwenye ukafiri, na Mtume (saaw) akamtuliza na akaishi Swafiyah kwa Mtume (saaw) kwa uaminifu mpaka Allah alipoichukua roho yake.

Na katika mwak wa nane wa hijrah alimuowa Maimuna dadake Umm Fadhil mke wa Abbas bin Abdul Muttalib na ilikua ndoa yake katiak mwisho mwisho umra ya qatha. Na kisa cha kumuowa ni kua Maimuna alikua na miaka ishirini na sita na anaemff. Alipoona Maimuna mambo ya waislamu katiak umra ya qadha aliukubali uislamu ye ye umetayarisha chakula

kwa hivyo muhudhurie, na jawabu yao ilikua: hatuna haja na chakula chako, wewe toka, kwa hivyo Mtume (saaw) hakusita na akatoka na waislamu wakiwa nyuma yake.

Ama ndoa zake za kuwaowa Zeinab bin Khuzeima na Uum Salama, walikua ni wake wa wanaume wawili katika maswahaba wkae waliouwawa katika vita. Zeinab alikua ni mke wa Ubeid bin Harith bin Mutlib ambae aliuwawa shahidi katiak vita vya Badr na alikua hana uzuri, lakini alijulikanwa kwa wema wake na ihsani yake mpaka akaitwa mama wa maskini na alikua ashapita ujana wake, na Mtume (saaw) akamuowa katiak mwaka wa pili wa hijra, baada ya vita vya Badr na baada ya kufiliwa na mumewe. Na hakukaa nae illa kwa miaka miwili kisha Allah akaichukua roho yake kwa hivyo baada ya Khadija yeye ndie wapekee aliekufa kabla ya (Mtume). Ama Umm Salama alikua ni mke wa Abi Salama katika Uhud na baadae akapona jaraha lake na Mtume (saaw) akamruhusu kuenda vita vya Badr Asad na akawashinda na akaregea Madina na gharima, na jaraha la Uhud likamregea mpaka akata nalo na Mtume (saaw) alimtembelea akiwa katika kitanda cha mauti na akakaa ubavuni mwkae akimuombea mema mpaka akafa na kamfunga macho yake. Na baada ya miezi mine kutoka kufa kwake Mtume (saaw) alimposa Umm Salama kisha yeye akatoa sababu ya watoto wengi na kua ujana wake ushapita. Na Mtume (saaw) akasisitiza mapka akmuowa na akamsaidia kulea watoto kwa hivyo Mtume (saaw) aliwaowa kwa kuwasimamia watu na marafiki zake wawili baada ya kufa kwao.

Ama ndoa yake kwa Umm Habiba bint Sufyan ilikua ni kumuowa mumini aliegura kwenda habasha kwa kuihfadhi dini yake na akasubrira uislamu wake wakati mumewe aliporitadi kutoka uislamu mumewe. Na Umm Habiba ni Ramal bint Abi Sufyan bwenyenye wa Makka na kiongozi wa washirkina. Na alikua ni mke wa mtoto wa shangazi ya Mtume (saaw) Ubeid Allah bin Tahsh Al-asadi. Aliposilimu Ubeidu Allah Ramla pia alisilimu nae babake na akagura pamoja na mumewe kwenda Habasha akiwa ni mja mzito. Na akazaa uhumishoni binti yake

Habiba bint ubeid Allah jina ambalo aliitwa nalo na akawa anaitwa Umm Habiba, isipokua mumewe Ubeid Allah bin Jahsh hakuchukua muda na akatoka uislamu na kuingia unasara dini ya Mahabashi na akajaribu kumtoa mkewe katika uislamu lakini aliusuria uislamu wake. Mtume (saaw) akamtumia ujumbe Najashi amwakilishe kimuoga Umm-habiba, Najashi akamulezea umm Habiba na Umm Habiba, Najashi akamuelezea Ummu habiba na Umm Habiba akawakilishwa na Khalid bin Said Al-aas na ndoa ikafungwa baina yao na Khalid akamsimama Umm Habiba katika ndoa kwa kumwakilisha. Na Najashi akamsimamia Mtume (saaw) katika ndoa. Na wakati wakimbizi wa habash kuhama kwenda Madina baada ya vita vya Khaibar Umm Habiba aliregea pamoja nao na akaingia nyumbani kwa Mtume (saaw), na wakasherekewa watu wa Madina kwa harusi ya Mtume (saaw) kwa kumuoa Umm Habiba na akaishi katika nyumba yake.

Ama ndoa yake kumuowa Zeinab bint Jahsh na ilikua ni Kisheria kwa mambo kadha, ilikua ya kisheria kwa kuvunja yanajulikana kama kulinganisha baina ya mwanamke na mwanamume katika kumuozesha binti ya shangazi yake na pia alikua ni kiongozi wa maquraish na kmuozesha aliekua mtume wake na kisha kumuacha huru, na pia ilikua ni ya kisheria ya kuvunja ada hiyo. Na kisa cha Mtume (saaw) kumuowa Zeinab bint Jahsh ilikua Zeinab bint Jahsh huyu ndie binti wa Umeimah binti Abdul-Muttalib, shangazi yke Mtume (saaw) ambae alimlea yeye na alikua kama binti yake au dadake mdogo. Na alikua anamjua kama ni mzuri au sio mzuri, kabla ya kuolewa na Zeid. Na alishuhudia kukua kwake kuanzia kutambaa katiak utoto wake usichana wake na mpaka uwanawali wake, na sio eti alikua hajulikani na Mtume (saaw) alimposea ili aolewe na Mtumwa wake Zeid lakini kakake Abdallah bin Jahsh akakataa dadake ambae ni maquraish Hashimiy juu ya hayo ni bint ya shangazi ya Mtume (saaw) aolewe na mtumwa alienunuliwa na Khadija na kuachwa huru. Na Mtume (saaw), na pia alionelea kua ni aibu kubwa juu ya Zeinab. Na pia ilikua ni aibu kubwa sana kwa waarabu, na haikua mabanati wa watukufu kuolewa na

watumwa hata kama wameachwa huru. Lakini Muhammad alitaka kuondosha mtazamo huo ulikuwepo katika nafsi zilozosimama juu ya uasabiyah pekee na watu watambue kua hamna ubora kwa mwaarabu juu ya asiekua muarabu illa kwa uchaji Mungu, na waifahamu kauli yake Ta'ala:

{... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْأَكُمْ ...} (الحجرات: 13)

“Mbora wenu mbele ya Allah ni mchaji Mungu Zaidi” (Hujraat-13). Na ye ye hakupendelea kumlazimisha mwanamke mwengine hilo asie kua ni watu wake, na kumtweka jukumu hilo Zeinab bint Jahsh binti ya shangazi yake aondosha desturi hiyo ya waarabu, na hilil ndio kuvunda ada yao, na kutojali watakaoyasema yale ambayo tunayaogopa kuyasikia, na akawa ni Zeid mtumwa wake ambae alimbatiza, na ambayo yakawa kwa hukm ya warabu na dasturi zao kua na haki ya kumrithi ye ye sawa na watoto wake wengine, na ndie alieandaliwa na mteremsha sheria kwa watumwa waliokua wamewafanya watoto. Na alisisitiza Mtume (saaw) ili akubali Zeinab na akubali kakake Abdalla mtumwa wake (Mtume) amuowe Zeinab, lakini Zeinab aliendelea kukataa. Na Allah (swt) akateremsha kauli yake:

{ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةً إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا } (الأحزاب: 36)

“Na haifai kwa mumin mwanamume wala mumini wa kike. Allah na Mtume wake wanapoamrishaa jambo kua na khiyari katika amri yao, na yoyote anaemuasi Allah na Mtume wake hakika amepotea upotofu wa wazi” (Ahzab-36) Na wakati haikubakia mbele ya Abdalla na mbele Zeinab illa kukubali, na wakasema: “Tumeridhika ewe mjumbe wa Allah”. Na ikafungwa ndoa kati ya Zeid na Zeinab baada ya Mtume (saaw) kutuma mahari kwa Zeinab ye ye mwenyewe hakuiridhia ndoa bali alikubali kwa kua ni amri ya Allah an Mtume wake. Na hakua ni mwenye kujisalimisha na amri za mumewe wala hakua laini kujisalimisha na amri za mumewe wala hakua laini mbele yake, bali alikua anajifakhirisha juu ya Zeid kwa kua hakuwahi kua mtumwa na kuya fanya maisha ya Zeid kua magumu, na Zeid alimshtakia Mtume (saaw) mara kadha, na kumueleza

ubaya wa mamiliano ya Zeinab juu yake. Na alitaka idhini mara kadha ya kumuacha, na Mtume (saaw) alikua akimjibu mzuie mkeo. Na Allah alimfunulia (wahy) Mtume (saaw) kua Zeinab huyu atakua ni mkewe, na yakawa mazito hayo kwa Mtume (saaw) na kuogopea watu wasije wakasema kua Muhammad ameowa mke wa mtoto wake na hakuna koso a kwa hayo na Mtume (saaw) alikua amembatiza Zeinab, lakini Zeid alimstisitiza Mtume (saaw) pamoja na kujua Mtume (saaw) kua Zeinab atakua mmoja katika wakeze kama alivyojulishwa na Allah hayo kwa njia ya wahy na alikua akimwambia Zeid:

{...أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتْقِ اللَّهَ...} (الأحزاب: 37)

“Mzuiie mkeo na mche Allah” (Ahzab-37). Na Allah akamrudi kwa hayo, wakati alipomuambia hakika nimekuelezea kua mimi nitakuozesha, na ikawa unayaficha katika nafsi yako na Allah hatayaficha na haya ni maana ya kauli yake:

وَتُخْفِي فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ...} (الأحزاب: 37)

“Na unayaficha katika nafis yaki yatakadhlilishwa na Allah” (Ahzab-37) atakua ni mkewe pamoja na kua ni mke wa mtoto aliembatiza. Na sababu ya Mtume (saaw) kuficha ndoa hio ambayo Allah aliidhihirisha baadae, ni kua waarabu ililkua ni katika ada yao ni kuaweka walio wabatia watoto majumbani na kuwaniganisha na nasha zao, na walikua wakimpatia mtu aliebatizwa haki zote za mtoto. Na kupidishwa sharia za mtoto, mpaka katika mirathi na uharamu wa nasaba, na wakati Allah alipomjulisha Mtume kua Zeinab mke wa mtoto wa kubatizwa atakua ni mkewe baada ya hapo, alikua akificha alioyojua na kumkazania Zeid amzuie mkewe na asimpe talaka pamoja na kusitisizwa na Zeid na kumshtakia na kwa kukosekana uhusiano na ushirikiano katiak maisha ya kindoa kati yao tangu kuowana kwao, Zeid aliendelea kutaka kumuacha na Mtume (saaw) akampa ruhusa Zeid ya kumuacha na bila ya kujua Zeid kua Mtume (saaw) atamuowa. Kwa dalili kama walivyopokea Ahmad na Muslim na Nasai kupitia Suleiman bin Mughira kutoka kwa Thabit kutoka kwa Anas amesema: “Ilipomalizika eda ya Zeinab Mtume (saaw) alimuambia Zeid nitaje mimi kwa

Zeinab akasema (Zeid): Nikaondoka na nikamuambia Zeinab furahi amenituma Mtume anakutaja, akasema sitafanya kitu au mpaka Allah aniamrishe, akasima sehemu anaofanya ibada na Qur'an ikateremka na akaja Mtume (saaw) akaingia kwake bial ya idhini wakati Allah alipoitemremsha kauli yake:

﴿فَلَمَّا قَضَى رَيْدٌ مِنْهَا وَطَرَا زَوْجَنَاكُهَا لَكِنْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرْجٌ فِي أَرْوَاحِ أَذْعَانِهِمْ...﴾ (الأحزاب: 37)

"*Na Zeid alipokamilisha matamanio yake tulikuozesha wewe ili yasiwe ni mazito juu ya waumini katika wake wa watoto wa kubatizwa*" (Ahzab-37) lau kama Zeinab alijua au Zeid anajua asine muambia furahi na asingelisema Zeinab au Allah aniamrishe au nimtake usharui katika ndoa hii. Na illha (sababu ya kisharia) ya ndoa hii ni yasiwe mazito juu ya waumini katika kuwaowa wake wa walio wa batiza.

Hivi ni visa vyta Mtume (saaw) kwa wake zake, na killa mmoja katika wao yabainika kisa cha kuwaowa kua ilikua sio lengo la kuowa. Na kupitia hayo yadhihirika maana ya ndoa zake kwa zaidi ya waume, na maana ya khususia yake (saaw) kwa idadi hiyo billa ya ummah. Na hayo sio kuchemka ghariza ya kuendleza kizazi kwa mtu ambae ameshavuka umri wa miaka khamsini na kwa mtu anaejishughulisha na ulinganizi na serikali anaejishughulisha na ujumbe wa mola wake aufikishe kwa ulimwengu, awanyanyue watu ili awafanye ni ummah, na kua malengo yake katika maisha kubaeba ujumbe wa Allah katika ulimwengu na kuujengwa mujtamaa upya baada ya kuvunjika uliotangulia, na kusimamisha serikali itakao sukuma ulimwengu mblele yake ili kubebwa ujumbe kwa watu. Na kila anejishughulisha akili yake kunyanyua ummah na kusimamisha serikali na kujenga mujtamaa, na kubeba ujumbe kwa ulimwengu haikiniki kushurghulishwa na wanawake wa kuwaeleke wao, anaowa killa mwaka, bali watabebwa wao na ulinganizi, na kuyafurahikia maisha ya ndoa kikawaida kama atakavyofurahikia maisha ya ndoa kikawaida kama atakavyofurahikia mwanadamu yoyote.

## Maisha ya ndoa

Mke sio mshirika wa mume katika maisha bali ni swahiba wake, kwa hivyo mahusiano baina yao sio mahusiano ya ushirika na wala sio wenyewe kulazimishwa juu yke maisha yote, bali mahusiano kati yao ni mahusiano ya urafiki, killa mmoja atamsuhubu mwengine kwa usuhuba kamili kwa killa sura, urafiki utakao mtuliza nao killa mmoja mwengine, kwa Allah ameifanya ndoa hii ni sehemu ya utulivu kwa wawili (mke na mume). Amesema Allah (swt):

{ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجًا لِيُسْكُنَ إِلَيْهَا } (الأعراف:  
189)

“Ni yeye aliewaumbeni nyinyi kutokana na nafsi moja na akajaalia kutokamana nayo mkewe ili apate utulivu kwake” (Arafat-189) na amesema Allah (swt):

{ وَمَنْ آتَيْتَهُ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً }... (الروم: 21)

“Na katika Alama zake amewaambieni nyinyi kutokamana na nfsi za wanawake ili mupate utulivu kwa na akajaalia baina yenu mapenzi na huruma” (Rum-21), na sakan ni utulivu, yaani ili atulie mume kwa mkewe na mke kwa mumewe, na kumtegemea killa mmoja wao kwa mwengine na asimtoroke. Na asli ya ndoa ni utulivu, na asli ya maisha ya ndoa ni utulivu, na ili yawe mahusiano hayo baina ya mke na mume ni mahusiano ya makini na utulivu, sharia imeelezea yale ya mke ambayo ni haki juu ya mume, na ambayo kwa mume ni haki juu ya mke. Na zimekuja ayah na hadithi wazi kuhusiana na mlango huu. Amesema Allah (swt):

{ ... وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ... } (البقرة: 228)

“Na wanawake wana haki juu ya waume zao sawa na za waume zao kwa wema juu yao” (Baqarah-228) yaani wanawake wana haki za ndoa juu ya waume mfano wa waume juu ya wanawake. Na kwa ajili ya hayo ibn Abbas alisema: “Mimi hujirembesha kwa ajili ya mke wangu kama anavyojirembesha yeye kwa ajili yangu napendelea kutekeleza haki zake zote zilizoko juu yangu

ili apate kuwajibika yeye kutekeleza haki zangu zilioko juu yake kwa sababu Allah (s.w.t) anasema:

... وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ... } (البقرة: 228)

“Na wanawake wana haki juu ya waume zao kama waume zao wana haki juu yao kwa wema” (Baqarah-228) katika mapambo yasio ya madhambi” na imepokewa kutoka kwake pia “Wana haki ya usuhuba mzuri na mahusiano mfano wa yale ambayo ni juu yao katika utiifu kwa yale ambayo ni wajibu wao kuwatekeleza waume zao.”

Na ameusia Allah Ta’ala mahusiano mazuri kati ya wawili walioowana amesema Taala “na mukae nao kwa wema” (Nisa-19) na akasema:

... وَعَاشُرُو هُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ... } (النساء: 19)

“Mukae nao kwa wema” (Baqara-229) na akasema:

... فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ ... } (البقرة: 229)

“Mukae nao kwa wema” Na mahusiano ni matangamano na maingiliano na mahusiano. Kwa hivyo Allah (swt) ameamrisha mahusiano mazuri kwa wanawake wanapo funga mana na ndoa nay awe matangamano yalio kati yao na usuhuba wao baina yao kwa ukamilifu, kwani ndio yanatuliza nafsi na maisha yaliotulia, na mahusiano ya wanaume kwa wanawake ni zaidi ya uwajibu wa kutekeleza haki zake kama mahari na lishe (nafaka) na asimkunjie uso billa ya kosa na awe ni mlaini wa maneno katika maneno wala sio lafadhi wala mkali wala kudhihirisha kulemea kwa mwengine.

Na aliusia Mtume (saaw) wanaume kwa wake zao, ameipokea muslim katika swalih yake kutoka kwa Jabir kua Mtume (saaw) amesema kati khutba yake ya hijjah yakuoga (Hijjatu) widaa “Mcheni Allah katika wanawake hakika nyinyi mumewachukua kwa amana ya Allah nyinyi muna haki juu ya kutowa karibisha katika matandiko yenu yoyote munaemchukia wakifanya hayo basi wachapeni kichapo kisicho umiza na wao wanaume ni juu yao lishe yao mavazi yao kwa wema”

Na imepokewa kutoka kwa Mtume (saaw) kua lisema “mbora wenu ni mbora wenu kwa watu wake na mimi ni mbora wenu kwa watu wangu. Na imepokewa kutoka kwake (saaw) kua alikua ni mzuri wa mahusiano alikua akicheza na wakezee, na kua mpole kwao na akiwachekesha wakeze mpaka alikua aksshindana mbio na mkewe Aisha mama wa waumini (raa) na akikupendekesa kwake kwa hilo.alisema (Aisha) Mtume (saaw) alishindana na mimi na nikamshinda na ilikua kabla sija pata mwili na nikashindana nae tena baada ya kupata mwili na akanishinda na aksema “Hili ni kwa lile”. Na Mtume (saaw) alkua amesali isha anaingia kwake anakaa pamoja na wakeze kidogo kabla ya kulala na kuwapumbaza, na imepoklewa Ibn Majah kua Mtume (saaw) alisema “Mbora wenu ni mbora wenu kwa wakeze”.

Na yote haya yaonesha kua ni juu ya waume watengeze mahusiano ya wake zao. Na kwa kua maisha ndoa huenda yakawa na misukosuko ambayo itaitoa kwenye mipaka yake, Allah akaiweka uongozi wa nyumba kwa mume juu ya mke, na akafanywa mume ni msimamizi wa mke. Amesema Ta’ala:

{ الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ ... } (النساء: 34)

“*Wanaume ni wasimamizi juu ya wanawake*” (NIsa-34) na akasema:

{ وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ } (البقرة: 228)

“*Na wao pia mfano wa wema juu yao, na waume wana daraja juu yao*” (Baqarah-228) na akausiwa mwanamke kumtii mumewe amesema (saaw) “Akilala mwanamke malaika mpaka atakaporegea.” Na akasema (saaw) kumuombia mwanamke: “Una mume wewe”? akasema: ndio, akasema (saaw) “Basi yeye ni pepo yako na moto wako” Na imepokewa Bukhari kua Mtume (saaw) “Sio halali kwa mwanamke kufunga na mumewe yupo illa kwa idhini yake, wala asiruhusu mtu katika nyumba yake illa kwa idhini ya mumewe na chochote atakacho towa katika sadaqah billa ya idhini yake basi nusu yake itakwenda

kwake” na imepokewa Ibn Batlah kati ahkam annisai kutoka kwa Anas kua mtu alisafiri na akamtakataza mkewe kutoka. Akawa mgonjwa babake akaomba idhini kwa Mtume (saaw) kumtembelea babake, Mtume (saaw) akamuambia “Mche Allah na usimkhalifu mumeo” akafa babake akaomba ruhusa Mtume (saaw) kuhudhuria mazishi ya babake, na Mtume (saaw) akamuambia “Mche Allah na usimkhalifu mumeo” Allah akamfunutia (wahy) Mtume (saaw) “Mimi nimemsamehe kwa kumtii mumewe” sharia ikamjaalia mme haki ya kumkataza mumewe kutoka katika nyumba sawa na kuwatemblea wazee wake au kuwazuru au kutoka kwa yasio na budi au kimatembezi, wala haifai kwake kutoka illa kwa idhini yake, lakini haifai kwa mume kumkataza kuwatembleza wazazi wake na kuwzuru kwa sababu itakua ni kua kata, na kumpeleka mke kumkhalifu mumewe, na Allah ameamrisha matangamano mazuri, na kumkataza kuwatemblea wazee wake na kuwazuru sio matangamano mazuri na pia haifai kwa mume kumkataza mkewe kwenda msikitini, kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (saaw) kua alisema “Musiwakataze vija kazi wa Allah msikihi ya Allah” na akiasi mke amri ya mumewe basi Allah amempa mume haki ya kumtia adabu, amesema Allah ta’ala:

{... وَاللَّاتِي تَخَافُونَ شُوْرَهُنَّ فَعَظُوهُنَّ وَاهْجُرُوهُنَّ فِي الْمَضَاجِعِ وَاضْرِبُوهُنَّ فَإِنْ أَطْعَنْتُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا ...} (النساء: 34)

“Na wale munaowaogopea katika malazi na muwapige wao na wanapo watiini basi musiwatafutie sababu” (Nisa-34) na kipigo hapa ni wajibu kiwe ni kipigo khafifu, yaani kipigo kisicho umiza. Kama alivyoeleza Mtume (saaw) kwenye khutba yake katiak hijra na kuaga (Hijaratul-widaa) wakati aliposema “Wanapofanya hayo wapigeni kipigo kisicho umiza” na akapewa Mtume uweza wa kumuadhibu mke anapo kosa kwa sababu yeye ni msimamizi na mchungaji wa mambo ya nyumbani, na kutekeleza yasiokua ni ya kukhalifu kama sharia ilivyoamrisha basi haifai kabisa kwa mume kumsumbuu nalo kwa chochote. Amesema Ta’ala na wanapo wafitini basi musiwatafutei sababu”. Amesema Ta’ala:

{... فَإِنْ أَطْعَنْتُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا ...} (النساء: 34)

*“Na wanapo watiini basi musiwatafutie sababu”* (Nisa-34) bali ni wajibu awe mpole na e mpole anapotaka chochote kutoka kwake hata lau kama anamtaka yeye basi inatakiwa aangalie namna bora inaonasibiana nae. Amesema (saaw) “Musiwabishie wake usiku mpaka amchane na anyoe sehemu za siri”. Na haimaanishi usimamizi wa mume juu ya mke na uongozi wake wa mume wa nyumba na uchungaji wa mambo na kuyasimamia, wala sio mtawala au utawala, kwa hivyo mwanamke anaweza kurudisha maneno ya mumewe na kuyajadili, na yeye kuyarudi anaoyasema kwa sababu ni marafiki wala sio mtawala na mtawaliwa au kiongozi na raia. Bali ni marafiki wawili na mmoja wao kupewa usimamizi juu ya mwengine kwa upande wa kuendesha mambo ya nyumba hiyo, na alikua Mtume (saaw) katika nyumba yake ni rafiki kwa wakeze na wala sio kiongozi wa serikali mbali na kwamba ni Mtume amesema Umar bin Al-Khatib katika hadithi yke “Naapa na Allah hatukua tukiwaona wanawake ni chochote wakati wa Jahiliya, mpaka Allah alipoteremsha Allah kuhusu wao alioyateremsha, na akawagawia wao aliowagawia, mpaka nikafirkiria kufanya jambo fulani na akaniambia mimi mke wangu lau ungelifanya hivi na hivi, na nikamuambia una nini wewe haya hayakuhusu wewe usiingilie ninayokusudia, akaniambia mimi mke wangu ni ajabu kwako wewe mtoto wa Khattab hutaku kurudiwa na wakati bint yako anamrudi Mtume (saaw) mpaka akakasirika Mtume (saaw) siku hiyo. Akasema Umar itachukua shuka langu na nikatoka kwangu mpaka nikaingia kwa Hafswah na ni kamwambia ewe binti yangu wewe unamrudi Mtume (saaw) mpaka anakua na hasira siku hiyo. Akasema Hafswa sisi humrudi nikamuambia, jua kwani nakutahadharisha na adhabu ya Allah na ghadhabu .w) na akaingia baada ya kuruhusiwa kisha akaomba idhini Umar na akaingia baada ya kuruhusiwa na akamkuta Mtume (saaw) amekaa na wakeze na ana huzuni amenyamaa akasema Umar : Nisemae kitu nimchekeshe Mtume (saaw) baada akasema : Ewe Mtume wa Allah natamani ungelimuona bint Kharijah alipotoka kwangu nafaqah na nikamsimamia na kumpiga kofi la shingo, akacheka Mtume (saaw) “Ndio hawa

wamenizunguka wanataka kwangu nafaqa". Na kwa hayo yabainika usimamizi wa mume juu ya mke ni kua uongozi ni kwake lakini kwa namna ya urafiki wala sio wa kulazimisha na kumtawala, basi anarudiwa na kujadiliwa.

Huu ni upande wa matangamano, ama katika upande wa kutekeleza kazi za nyumba, ni wajibu juu ya mwanamke kumhudumia mumewe kama kukanda unga na mikate na kupika na kufagia nyumba na kuisafisha na ni wajibu juu yake kumywesha anapotaka kunywa na kumuandalia chakula ili ale, na kutekeleza huduma zote za nyumbani yanaojulikana ni katika mambo ya kimaisha ya nyumba killa kitu bila mipaka yoyote. Na ni wajibu juu yake (mume) kumletea anaoyahitaji (mke) yalioko nje ya nyumba kama kumletea maji na yanaohitajika ili kuondosha uchafu na kukata kucha nay a kujirembesha nayo na mifano yake na mengineo.

Kwa ufupi killa kazi ambayo inahitaji kutekelezwa ndani ya nyumba ni wajibu juu ya mwanamke kuzitekeleza, kazi yoyote iwayo, na killa kazi inaohitajiwa kutokelezwa nje ya nyumba basi ni wajibu juu ya mwanaume kutekeleza. Kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (saaw) katiak kissa cha Ali na Fatima (raa) "Alimuamrisha binti yake na kazi za nyumbani na Ali ni juu yake yalio nje ya nyumba" na alikua Mtume (saaw) akiwaamrisha wakeze kumtumikia yeye na akasema: "Ewe Aisha tunyweshe ewe Aisha niletee wembe na kinoa na jiwe" na imepokewa "Fatima alikuja kwa Mtume (saaw) akimlalamikia anayo kumbana nayo katika kusaga kwa mkono na akataka mtumishi atakemfanyia hayo". Na yote hayo yaonesha kumhudumia mwanamume ndani ya nyumba na kuihudumia nyumba ni wajibu mionganoni mwa wajibu za mke na ni wajibu kutekeleza, isipokua kutekeleza kwake ni kwa qadri ya uweza wake, na iwapo kazi ni nyingi kwa namna itampa yeye taabu itakua ni juu ya mume ameletee mtumishi atakae msaidia kutekeleza kazi hizo, na ni juu yake (mke) kutakaa hilo, na iwapo kazi sio nyingi na yeye anaweza kutekeleza basi sio wajibu nyingi na yeye anaweza kutekeleza basi siio wajibu

kupata mtumishi yeye bali ni wajibu juu yake kutekeleza yeye kwa dalili kama alivyoamua Mtume (saaw) kwa bint yake Fatima kuitumikia nyumba. Na ndio hivyo ilivyo wajibu juu ya mume mfano wa wajibu kwake kwa uzuri, ili yawe maisha ya ndoa yaliotulia na yanaopatikana ndani yake qauli yake Ta’ala:

} وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَرْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً {  
الروم: 21}

“Ni katika alama zake amewaumieni nyinyi kutokamana na nafsi zenu wake, ili mupate utulivu kutoka kwa o na akawajaalia baina yenu mapenzi na huruma (Rum-21).

### Kumuaga nje (azl)

Azl ni mwanamume kutoa anapo karibia kumwaga ili amwage nje ya tupu. Na azl imeruhusiwa kisheria, kwa hivyo yajuzu kwa mwanamume anapomuingilia mkewe na akikaribia kumwaga, awe ni mwenye kumwaga maji yake nje ya tupu, ameipokea Bukhari kutoka Ataa kutoka Jabir amesem “Tulikua tunafanya azi katika zama za Mtume (saaw) na Qur'an inateremka” na pia imepokewa kutoka Ataa kua alimsikia Jabir (raa) anasema “Tulikua tunafanya azi zama za Mtume (saaw) na yalimfikia yeye haya na asitukanye”. Na hili ni kukubali kua Mtume (saaw) juu ya azl, na inaonesha juu ya kuruhusiwa kwake, kwa sababu lau kama azl ni haramu asingelinyamazia. Na juu ya kwamba hukmu ya azl hili linahusiana na maswahaba kuanzia zama za Mtume (saaw), na sahabi anapohusika na hukmu katika zama za Mtume (saaw) basi ni juu yake uamuzi wa kuiondosha, kwa sababu kidhahiri lilipelekwa suala hilo kwa Mtume (saaw) na kali kubali, kwa kua mara nyingi wakipeleka maswali yao kwake ili kujua hukm zake. Na zimepokewa hadithi swahijihi kadha katika kuruhusu azl. Wamepokea Ahmad na Muslim na Abu Dau kutoka kwa Jabir “Alikuja mtu kwa Mtume (saaw) na akasema mimi nina kija kazi yeye ni mtumishi wetu na mwenye kutunywesha sisi katika miteule na mimi humuingilia na sipendi abebe mamba, akasema fanya azl ukitaka kwani yatampata yeye alioqadiriwa yeye “Na ameipokea Muslim kutoka kwa Abi Said amesema : “Tulitoka na Mtume (saaw) kuenda katiak vita vya Bani Mustaliq

tukapata watumwa katika waarabu, na tukatamani wanawake na ubarobaro ukawa mzito kwetu na kukapendelea kufanya azl na tukamuulizia Mtume (S.a.a.w) kuhusiana nalo na akasema ni lipi linawazuia kuyafanya hayo, kwani Allah alietukuka ameshaandika kile atakakiumba mpaka siku ya kiyama. Na ameipokea Abu Daud kutoka kwa Jabir amesema: alikuja mtu miongoni wam Ansaar kwa Mtume (saaw) na akasema; “Mimi nini kijakazi na humuingilia na nachukia abebe mamba, akasema fanya azl ukitaka kwani atayapata yale yalioqadirwa yeye” Na azl inajuzu wazi wazi iwe ni lengo lolote liwalo kwa anaefanya azl, ni sawa amekusudia kutozaa au watoto wachache au kwa lengo la kumsikitikia mke kwa udhaifu wake wa kubeba mamba au kwa lengo la kutomzeesha na abakie msichana astarehe nale au kwa lengo lolote jengine kwani mume ameruhusiwa afanye azl kwa lengo lolote liwalo n ahayo ni kwa sababu dalili zilizo kuja kuhusiana nayoo ni wazi kabisa, na wala haikufunwa na namna Fulani na pia ni kwa ujumla bila ya takhsis yoyote, kwa hivyo itaendelea kubakia kwa uwake wake na ujumla wake. Wala haiambiwi kua azl ni kuuwa mtoto kabla ya kuumbwa kwake kwani zimekuja hadithi kuyarudi hayo. Kwani ameipokea Abu Daud kutoka kwa Abi Said “Alisema mtu: Ewe Mtume wa Allah mimi nina kijakazi na humfanyia azl na nachukia abebe mamba na mimi nataka wanayo yataka wanaume na mayahudi wanasema kua azl ni kuzika watoto wachanga akasema wamedanganya mayahudi lau Allah angelitaka kumuumba hungeliweza kumzuia “Na zimepokewa nass ya kuruhusu azl kwa lengo la kutozaa. Kwa amepokea Ahmad na Muslim kutoka kwa Usama bin Zeid “Alikuja mtu kwa Mtume (saaw) na akasema mimi hufanya azl kwa mke wangu akamwambia kwanini unafanya hayo, akasema mtu namsikitikia mtoto wake” akasema Mtume (saaw) lau kama ni madhara lingewadhuru mafursi na warumi “Na hapa alisema Mtume : “Kwa nini unafanya” na haumuambia usifanye. Na yafahamika kupitia hadithi kua alikubali lakini akamjulisha kua kuzaliwa watoto baada ya watoto haidhuru kwa dalili iliopokewa na Muslim katika hadithi ya Usama bin Zeid, alikuja mtu kwa Mtume (saaw) na akasema “Mimi hufanya azl kua

mke wangu kwa kumsikitikia mtoto wake, akasema Mtume (saaw) ikiwa ni kwa ajili ya hilo usifanye, hilo hlikuwadhu wafursi na warumi.” Na katika Muslim kwa njia ya Abdulrahman bin Bashir kutoka kwa Abi Said “Kwa kuogopea mamba kumdhuru mtoto wa kunyonya “Na iwapo Mtume alikubali azl kwa kuzuia mamba ili asidhurike mtoto anaenyonya basi yakubaliwa azl kwa kwa kukimbia watoto wengi au kikimbia kupata watoto asli au mengineo. Na iwapo Allah anajua kua mtoto atakuja basi hamna budi aje afanye azla au asifanye azl. Na kwa hiloo amepokea Ibn Hibban kutoka hadithi ya Anas kwa mtu aliulizia kuhusu azl, akasema Mtume (saaw) “Lau maji ambayo yatapatikana nayo mtu ukimwaga kwenye jiwe basi litatoa mtoto” Na pia haisemwi kupunguza kuzaa inakwenda kinyume na aliosisitiza (saaw) katika uwingi wa kuzaa wakati aliposema “Oweni muzaane muwe wengi” na akasema “Mweusi anaezaa ni bora kuliko wazuri tasa”. Hayo hayafai kusemwa kwa sababu kuruhusiwa azl haiendi kinyume na himizo la uwingi wa kuzaa, kwani hilo ni himizo la kuzaa sana, na hili ni ruhusa ya azl. Ama alioyapokea Ahmad kutoka Tudhmalli bin Wahab Al-asadiyah amesema: Nilihudhuria kwa Mtume (saaw) akiwa na watu na alikua anasema “Napenda sana nikataze kuingilia wanawake wanaonyonyesha (ghilali) na nikiangalia warumi na wafuasi na wao wanawaingilia wanawake wanaonyonyesha na watoto hawaridhiki na chochote, kisha wakamuuliza kuhusu azl, akasema Mtume (saaw) hiyo ni kumzika mtoto aliehai iliofichika hiyo.

} وَإِذَا الْمَوْعُودَةُ سُئِلَتْ { (التكوير: 8 - 9)

“Na pindi atakapo ulizwa aliezikwa hai.” Hadithi yagongana na hadithi zilizo sahihi zilizowazi katika kuruhusu azl, na iwapo itagongana hadithi na hadithi nyengine zilizo kuja kwa njia nyingi zitachukuliwa hadithi zilizo kuja kwa njia nyingi na kuacha hadithi nyengine. Na kwa msingi huo hurudishwa hadithi kwa kugongona na hadithi yenye nguvu na kwa njia katika mapokezi.

Wala haifai kusemwa kujumuisha baina ya hadithi hii na hadithi za kuruhusu azl na o ni kubebwa hadithi hiyo juu ya kuchukia azl, kwa sababu lawezekana lau isinge kuwepo mgongamano katika kukataza Mtume katika hadithi nyengine kwa maona hiyo hiyo ambayo iliokuja hayo hadithi hiyo. Kwani hadithi iliopokewa na Ahmad na Abu Daud kutoka kwa Abi Said “Na mayahudi wanasema azl ni kuzika watoto walio hai, akasema: Wamedanganya mayahudi” na hadithi ya Tudheimah inasema “Hilo ni kuzika mtoto alile hai, hilo ni

} وَإِذَا الْمَوْعِدَةُ سُئِلَتْ { (التکویر: 8 - 9)

*“Na pindi watakapoulizwa watoto waliozikwa hai”* (Takwir-8) kwa hivyo haimkiniki kujumuisha baina ya hadithi hizi mbili, na ima mmoja wapo itakua imefutwa (masukh) au nyengine ni yenye nguvu zaidi kuliko nyengine kwa hivyo itaachwa hadithi dhaifu, na kwa kua tarikh ya hadithi hizo mbili haijulikani na hadithi ya Abi Said inatiliwa nguvu na hadithi kadha na kwa njia kadha. Na hadithi ya Hudheimah imekuja pekee na haikutiliwa nguvu na chochote kwa hivyo itaachwa na itachukuliwa yenye nguvu zaidi. Na kwa hayo azl inafaa kaisa billa ya uchukivu wowote, lolote liwalo lengo la anaefanya azl katiak azl kwa ujumla wa dalili. Na wala mtu hahitaji idhini ya mkewe ili afanye azl kwani lamhusu yeye (mume) wala halimhusu mke. Wala haisemwi kumuingilia ni haki yake (mke) na maji pia ni haki yake kwa asiya mwage nje ya tupu ya yake illa kwa ruhusa yake, kwani hyo ni illah (sababu ya kisheria) ya kiakili na sio ya kisheria wala haina thamani, na hili hutupwa kwani kumuingilia ni haki yake wala sio kumwaga maji, kwa dalilikumuingilia mwanamke umemtekelezea haki yake hata kama hakumwaga (mume), kwa hivyo hana haki ya kuvunja ndoa (faskh). Ama yaliopokewa na Ibn Majah kutoka kwa Umar bin Al-Khatab amesema “Alikataza Mtume (saaw) kufanya azl kwa muungwana illa kwa idhini yake” kwnai hiyo ni hadithi dhaifu na katiak wapokezi wake kuna Ibn Lahia’h na kuna yalio semwa kuhusu yeye. Kwa hivyo zinabakia hadithi wazi katika kuruhusu azl.

Na hukmu ya hii azl yaingia pia juu ya utumiaji wa madawa na utumiaji wa mipira au utumiaji wa koili ya kuzuia mamba kwani yote hayo ni yanaingia mlango mmoja, kwa sababu dalili ya kuruhusiwa azla inalingana nazo kiukamilifu, nao ni suala katiak masuala yake, kwani hukmu ni kuruhusiwa mtu kufanya kitendo cha kuzuia mamba, iwe ni kumwaga nje au nyenginezo, na alicho ruhusiwa mume ameruhusiwa mwanamke, kwa njia yoyote iwayo.

Na ruhusa hii ya kuzuia mamba ni maalum kuizua kwa muda, ama kuzuizua mamba daima na kuleta utasa ni haramu, kwa hivyo kutumia madawa ambayo yatazuia mamba milele na kukat uzazi ni haramu, haifai kuyafanya hayo, kwa sababu ni aina ya kuvunja (Khasaa) na inaingia chini yake na inachukua hukm yake kwani hayo, na imekuja ukatazo wazi wa khasaa. Imepokewa kutoka Saad bin abi Waqqas amesema: “Mtume (saaw) alimrudi Athman bin Madhu’ui juu ya utasa, lau angeliruhusiwa tungelivunja” Na Athman bin Madhuin alikua amekuja kwa Mtume (saaw) na akasema: “Ewe Mtume wa Allah limekua uzito juu yangu mimi ubaro baro, niruhusu nijivunje, akasema: La, lakini funa” na katika maneno mengine alisema “Ewe Mtume wa Allah ametubadilishia ukasisi kwa ilio safi iliotukufu”. Na imepokewa kutoka kwa Anas amesema: “Mtume (saaw) alikua anatuamrisha kuowa, na akitukataza vikali na utawa, ana alikua anasema: oweni wazuri wanao zaa lakini mimi nitakua na wengi katika umma siku ya qiyama.”

Kama inavyo gongana kukata uzazi milele pamoja na kwamba mteremsha sharia amejaalia kizazi na ulezi ndio asli ya ndoa, kwa ajili ya hayo amesema Ta’ala katika kuelezea neema yake juu ya watu

{وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَرْوَاحِكُمْ بَنِينَ وَحَدَّةً} (النحل: 72)

“*Na akawajaalia nyinyi kutokamana na wake zenu watoto na vijukuu*” (Nahl-72). Na amejaalia mteremsha sharia kuzaa wengi ni jambo la kupendeza (Mandub) na kulisisitiza na kupongezwa anaelifanya. Imepokewa kutoka kwa Anas kua Mtume (saaw) amesema: “Oweni wazuri wanaozaa kwa mimi nitakua ummah

mkubwa kuliko Mitume mingine siku ya kiyama". Na imepokewa kutoka kwa Abdalla bin Umar amesema Mtume (saaw) "Oweni wanawake wanaozaa hakika mimi nitajigamba na nyinyi siku ya kiyama" Na kutoka kwa Ma'aqal bin Yassar amesema "Alikuja mtu kwa Mtume (saaw) na akasema: Mimi nampenda mke alien a hadhi na uzuri lakini hazai, Je nimuowe? Akasema: La, kisha akaja mara ya pili, akamkataza, kisha akaja mara ya tatu, na akasema: Oweni wazuri wanaozaa hakika mimi nitakua na wengi kupitia nyinyi".

Ruhusa ya kuzuia mamba kwa muda kupitia azl na njia nyenginezo zinazotumika, inamaanisha kuharibu mimba, kwani kuharibu mamba baada ya kupulizwa roho ni haramu, sawa na kuiharibu kwa kunywa dawa au kujisumbua au kwa uapsuaji na ni sawa yamepatikana kwa upande wa mama au baba au daktari, kwani ni uadui kwa nafsi ya mwanadamu asie na madhambi. Na ni hatia na ni wajibu itolewe fidia (diyya) na kiwnago chake kuacha mtumwa huru meme au mke, na thamani yake ni fungu la kumi 1/10 la fidia ya mwanadamu kamili. Amesema Ta'ala:

{... وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ...} (الأنعام: 151)

"*Na wala musivuwe nafsi ambayo Allah ameharamisha illa kwa haki*" (Anaam-151) na wameileta Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Hureirah amesema: "Alihukumu Mtume (saaw) katika mtoto alietumboni wa Bani Lahyan alieuwawa awache huru mtumwa mume au mke "Na uchache wa inavyo kua wa kuharibu mamba ambayo hutolewa fidia ni kua ibainike kutoka kwa umbile la kitu na umble la uanadamu kama vidole au mkono au mguu au kichwa au macho mawili au kucha.

Ama ikiwa kuharibu mimba kabla ya kupulizwa roho. Iwapo ni kuharibu baada ya masiku arubaini kuanzia kubeba mamba, na kua mwanzo wa kuumbwa mtoto basi itakua ni haramu pia na inachukua hukmu ya kuharibu mimba baada ya kupulizwa roho kwa uharamu, na inawajibika fidia ambayo ni kuacha mtumwa huru mume au mke. Na hilo ni kua iwapo ameanza kuumbika mtoto na kutokeza baadhi ya viungo na hupatikana

uhakika kua ni mtoto alieua uhai akielekea kua ni mwanadamu kamili. Kwa hivyo kumfanyia uadui yeye ni kuifanyia uadui nafsi ya mwanadamu asiena dhambi, na itaku ni kumzika alie hai na hayo Allah ameharamisha amesema Ta'ala:

وَإِذَا الْمُؤْعُودَةُ سُئِلَتْ - بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ { (التكوير: 8 - 9)

“Na pindi aliezikwa hai ataulizwa ni kwa kosa gani umewauwa” (Takwir-8/9).

Kwa hivyo ni haramu kwa mama na baba na daktari kuharibu mamba baada ya kupita siku arubaini kuanzia siku ya kwanza ya kubeba mimba, na anaefanya hayo amefanya hatia na madhambi na yamlazimu yeye kutoa fidia ya kuharibu mamba nao ni kuacha mtumwa huru mume au mke maka ilivyokuja katika hadithi ambayo imepokelewa na Bukahri na Muslim.

Na wala hairuhusiwi kuharibu mimba sawa iwe katika mzunguko wa kuchukua umbile au baada ya kupulizwa roho illa watakapo eleza madaktari waadilifu kubakia mtoto katika tumbo la mama itasababisha kifo cha mama na mauti ya mtoto pia. Basi katika hali hiyo kutoa mimba kwa kuyahifi maisha ya mama.

### Talaka

Kama Allah alivyoweka sheria ya ndoa vile ameweke sharia ya talaka. Na asli ya kulazimishwa kwake ni kupitia Qur'an na sunnah na ijmaa sahaba. Ama Quran anasema Allah (swt):

الطلاقُ مَرْتَانٌ فِإِمْسَاكٍ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ { (البقرة: 229)

“Talaka ni mara mbili kushikamana kwa wema au kuachana kwa wema” (Baqarah-229) na akasema

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ فَطْلَقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ...} (الطلاق: 1)

“Ewe Mtume munapowaacha wanawake basi waacheni wakati wa eda zao” (Talak-1) Ama sunna imepokewa kutoka kwa Umar bin Khattab “Mtume (saaw) alimuacha Hafsa kisha akmregea na imepoklewa kutoka kwa Abdallah bin Umar amesema: “Nilikua nimemuowa mwanamke na likua nampenda

na babangu alikua anamchukia na akaniamrisha ni muache na nikakataa akamuelezea hay Mtume (saaw) na akasema: ewe Abdalla bin Umar muache mke” na wamekubaliana jumla ya maswahaba juu ya kuwepo talaka.

Na talaka ni suluhisho la mkataba wa ndoa, yaani ni suluhisho la fundo la ndoa, na kuruhusiwa kwa talaka haina illah yoyote ya kisharia, kwani nusus zilizokuja kuishuluhisha haziambatani na illah yoyote sio kwa aya ya Quran wala hadithi. Kwa hivyo ni halali iliohalalishwa na sharia imehalalisha na sio kwa sababu yoyote nyenginezo. Na talaka ya kisheria ni talaka tatu, Talaka baada ya talaka kwa hivyo akiwacha moja basi inaanguki talaka moja na ameruhusiwa kumregelea wakati wa eda billa ya ndoa mpya, na akimuacha talaka ya pili basi inaangukia talaka ya pili, na ameruhusiwa kumregelea wakati wa eda billa ya ndoa mpya. Na ikimalizika eda katika hali nzuri mbili na asimrudie atakua ni Bain mdogo (Baynuna – sughra) na sio halali kumrudia illa kwa ndoa mpya na mapya. Na akimuacha ya tatu basi itangukia talaka tatu, na atakua ni Baynuna kubra, na haijuzu kwake kumregea illa baada ya kuolewa na mtu mwengine na amuingilie (amuache) na amalize eda yake amesema Allah (swt):

الظَّلَاقُ مَرَّتَانِ فَامْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيْحٌ بِإِحْسَانٍ وَلَا يَحْلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْنَمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافُوا أَلَا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَإِنْ خَفْتُمْ أَلَا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ تُلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ - فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا تَحْلُّ لَهُ مِنْ بَعْدِ حَتَّىٰ تَنكِحَ رَوْجًا غَيْرَهُ فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا إِنْ ظَنَّا أَنْ يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ وَتُلْكَ حُدُودُ اللَّهِ يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ (البَقْرَةُ: 229 - 230)

“Talaka ni mara mbili kushikamana kwa wema na kuachana kwa wema, na wala si halali kwenu (waume) kuchukua chochote mulichowapatia wao (wake), illa kwa kuogopea (wao wawili) wasisimame katika mipaka ya Allah, basi mukiogopea musisimame katika mipaka ya Allah basi hamna makosa juu yao katika watakacho toa fidia, hiyo ni mipaka ya Allah basi musiivuke, na yoyote anaevuka mipaka ya Allah basi musiivuke, na yoyote anaevuka mipaka ya Allah basi hao ndio madhalimu. \*Na iwapo atamuacha si halali kwake baada ya hapo mpaka

*aoewe na mume mwengine, an akimuacha si makosa juu yao wakidhania wataweza kusimama katika mipaka ya Allah, na hiyo ni mipaka ya Allah anafafanua kwa watu wanaolewa* (Baqarah-229-230) Kwa hivyo Allah (swt) amewafundisha waislamu katika ayah vipi wataacha na akasema:

{الطلاقُ مرتانٌ }

“*Talaka ni mara mbili*” (Baqarah-229), na hakika akawa khiyarisha baada ya kuwaelimisha kati ya kuwashika wanawake kwa matangamano mazuri na kutekeleza wajibu wao nia kati ya kuachana nao kw auzuri ambao ni juu yao. Kisha akasema:

{فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا تَحْلُّ لَهُ مِنْ بَعْدِ حَتَّىٰ شَكَحَ زَوْجًا غَيْرَهُ } (البقرة: 230)

“*Na iwapo atamuacha basi si halili kwake baada ya hapo mpaka aolewe na mume mwengine*” (Baqara-229) yaani akimuacha ya tatu baada ya mara mbili iliotangulia si halali kwa kumuacha huku mpaka aolewe na mwengine, kisha akasema:

{...فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجِعَا... } (البقرة: 230)

“*Na iwapo atamuata basi hamna kosa kwao kurudiana*” yaani iwapo mume wa pili atamuta basi wakati huo itafaa kwa mume wa kwanza kumrudia kwa ndoa na mahari mapya. Na tamko la tallqaha la linamrudilia alie tajwa wa karibu zaidi nalo ni tamko:

{ زَوْجًا غَيْرَهُ } (البقرة: 230)

“*Mume mwengine*” yaani mume wa pili na tamko la kurudiana la pili linamrudilia mume wa kwanza. Yaani hamna pingamizi kwa kila mmoa wao kurudia mwenzake kwa ndoa. Kwa hivyo mwanamume anamiliki juu ya mwanamke talaka tatu, mbili kati mwake inajuzu kwake kumrudilia, na ya tatu haifai kumrudilia mpaka aolewe na mume mwengine.

Na Talaka ipo katika mikono ya wanaume wala sio katika mikono ya mwanamke, mume ndie anaemiliki na wala sio mwanamume, ni kwa sababu Allah ta’ala ameijalia katika mikono yake, na haikuelezwa katika sharia illah ya hayo, kwa hivyo haifanyiwi illah. Naam kua ndoa ni chanzo cha maisha mapya ya ndoa, na anakua mume na mke wanashirikiana killa mmoja wao kuchagua swahibu amtakae, na killa mmoja ana

haki ya kufunga ndoa na anaemtaka, na kukata ndoa na asiemtaka, lakini baada ya kupatikana ndoa kivitendo, uongozi wa familia kupewa mume, kufanywa mume ndie msimamizi juu yake, imekua hamna shaka iwe talaka mikono ya mwanamume na inakua ni katika haki ya mwanamume kwa sababu yeye ni kichwa cha familia na mlezi wa familia. Kwa hivyo ni juu yake yeye pekee kubandikwa majukumu ya nyumba na takilifu zake, kwa hivyo imekua ni wajibu wake yeye pekee suluhisho ni kulingana na majukumu, na utengano kati ya walioowana ni katika mikono ya msimaizi ya mmoja wao juu ya mwengine. Lakini haya ni kwa kulilngana na ukweli uliopo na wala sio illah ya hukm ya kisheria, kwa sababu illah ya hukmu haijuzu kuwa illah ya kisharia isipokuja katika nass ya sharia.

Isipokua sio maana yake kwa kua talaka iko katika mikono ya mwanamume, na ni yeye pekee, basi haifai kwa mwanamke kujiachisha na kuleta utengano na mwanamume, bali asli ya haki ni kwake yeye mume, na kuwacha, billa ya pingamizi yoyote katiak hali yoyote, bali ana haki ya kuwacha hata lau kama bila ya sababu. Lakini mke pia ana haki ya kujiachisha, na kuleta ufarakano kati yake na mume katiak hali maalum, ilitajwa na sharia, kwani sheria imeruhusu mwanamke kuvunja (faskh) ndoa katika halizifuatazo:-

1:- Wakati mume atakapo iweka talaka mikononi mwa mke. Basi yeye mke atakua na haki ya kujiachisha kulingana na alichomilikishjwa yeye. Na atasema naiachisha nafsi yangu kwa mume wangu Fulani, au amuelezee najiachisha nafsi yangu na wewe wala asiseme nimemuacha au wewe umeachwa, kwa sababu talaka humuangukia mwanamke na sio juu ya mume, hata lau kama talaka yatoka kwa mke. Bali imeruhusiwa kwa mume kuiweka talaka katiak mikono ya mke, kwa sababu Mtume (saaw) aliwa khigarisha wakezee na jumal ya maswahaba wamekubaliana huu ya hayo.

2:- Anapoju mke kua ana kasoro ambayo ni kizuizi ya kumuingilia kukosa matamanio au kujivunja (Khasaa) na

mwanamke amesalamika na mifano yake. Kwa katika hali hiyo ataweba kuvunja ndoa yake, na kiongozi akihakikisha kuwepo ksw kasoro atapewa muda wa mwaka mmoja na asipo tibu yatatekelezwa matakwa ya mke na ndoa itavunjwa. Na Umar akamuambia ulimuelezea hayo mke, akasema: La, akasema: Mueleze na umkhiyarishe. Na imepokewa kua Umar alimpa muda mwaka. Na iwapo mwanamke atampata mumewe amekatwa uume au kupoza basi hapo hapo ana khiyari wala hapewi muda kwa sababu amekatiwa tama ya kumuilingilia wala hamna haja ya kungonjea.

3:- kimbainikia mke kabla ya kuingiliwa au baada yake kua mume ni mgonjwa wa maradhi ambayo hawezi kuishi nae billa ya kudhurika kama mbalanga au kisonono au kifua kikuu (T.B) au ana magonjwa mengine mifano yke, basi mke ana haki ya kumrudia kadha na kutaka atenganishwe na mumewe, na yatatekelezwa matakwa yake yatakapo thubutu maradhi muda maalum. Na khiyari yake ni ya daima na sio ya muda. Na hayo ni kulingana yalivyo kuja katika muata kutoka Malik kua ameyapokea kutoka Said bin Musayyih kua amesema: “Mtu yoyote atakae owa mke na ana wazimu au kasoro basi mke ana khiyarishwa imam akubali au atengane”

4:- Ashikwe na wazimu mume baada ya kufunga ndoa basi mke ana haki ya kwenda kwa kadhi na kutaka kutenganishwa nae. Na iwapo hakupona wazimu kwa muda huo na mke akaendelea na mashtaka, kadhi ataamua kutenganishwa na hayo ni kupitia hadithi iliotangulia katika Muata.

5:- Mume asfiri iwe mbali au karibu, na kisha khabari za mume zikatike na kua uzito juu ya mke kupata nafaqah, basi ana haki ya kutaka kutenganishwa nae baada ya kutumia juhudii katika kumtafuta na kumuulizia, na hayo ni kupitia qauli ya Mtume (S.a.a.w) kuhusu mwanamke akimuambia mumewe “Nilishe au niache” kwa hivyo ikafanywa kutolisha ni illa ya kutengansishwa.

6:- Akigoam muem kumtumilia mkewe nae ni mweza, na inakua ni uzito juu ya mke kufika mali ya mume kwa namna yoyote ili aweze kujitumilia, basi mke ana haki ya kutaka talaka na ni juu ya kadhi kumuachisha papo hapo bila ya kumchelewesha mke kwa sababu Mtume (saaw) aliwaandikia barua wanaume walioko mbali na wkae zao na akawaamrisha wawasimamie au wawape talaka, na maswahaba walijua hayo na hakuna yoyote aliemkatakaza kwa hivyo hiyo ni ijmaa.

7:- Kupatikana utesi na mizozo kati ya mke na mume, basi mke ana haki ya kutaka utengano, na ni juu ya kadhi aweke mtu kwa upande wa familia ya mke na mtu katika familia ya mume. Na kikao hicho kitasikiza mashtaka ya killa upande, na kufanya bidii ya kusuluuhisha, na ikiwa si majaliwa (taufiq) kati yao kikao kitatoa uamuzi wa kutenganishwa kama wata kavyoonelea, ambayo yatapatikana na kuyafikia qauli yake Ta'ala:

وَإِنْ خَفِتُمْ شِقَاقَ بَيْنَهُمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِنْ أَهْلِهَا إِنْ يُرِيدَا إِصْلَاحًا  
يُوَفِّقُ اللَّهُ بَيْنَهُمَا. {النساء: 35}

“Na iwapo munaogopea utesi kati ya basi wekeni mtu kutoka watu wa mume na mtu kutoka watu wa mke, iwapo wanataka suluhu Allah atawajaalia taufiq kati yao” (NIsa-35).

Kwa hivyo katika hali hizi sharia imempatia mwanamke haki ya kutaka kutenganishwa baina yao katiak hali zilizobakia. Na uhakika wa hali hizi yaonekana zilizobakia. Na uhakika wa hali hizi yaonekana kua mteremsha sharia inamuangalia mwanamke kua ni rafiki wa mume katika misha ya ndoa, na killa balaa na misukosuko inaopatikana ndani ya nyumba humsibu yeye kama inavyo msibu mume, kwa hivyo imekua hamna budi adhaminiwe yeye kujikomboa kutokamana na aibu itakapo isibu katiaka nyumba, kwa kufungua fundo la ndoa kwa upande wake, na kwa hivyo mteremsha shria hakumuacha mwanamke ni mwenye kulazimishwa kubaki na mume iwapo imekua ni uzito kupaa utulivu wa ndoa. Kwa hivyo sharia imemruhusu

avunje ndoa katika hali ambazo yatapatikana kwake ukosefu wa matangamano, au kukosa kupatikana utulivu wa ndoa.

Na kupitia hayo yabainika kua Allah ameweka talaka katika mikono ya mwanamume, kwa sababu ndie msimamizi wa mwanamke na ndie masuul wa nyumba, na akapewa mwnamke haki ya kuvunja (faskh) ili asiteseke katika ndoa yake, wala haiwi nyumba aliomo mume kua ni sehemu utulivu na amani na kua ni mateso na dhiki kwa mke.

Ama ni kwa illah gani imewekwa sharia ya talaka, ni kama tulivyosema kua nusus za kisheria haikutaja illah ya talaka kwa hivyo haina illah lakini yawezekana kueleza uhakika wa kuwepo sharia kulingana na ndoa na yanao fuatia juu yake. Hakika uhakika wa ndoa yaonesha kua imewekwa utulivu katika familia hiyo, na iwapo yatatokea katika maisha haya ya ndoa yatakao tishia utulivu huo, na ikafika hali ngumu kuwepa maisha ya ndoa, basi hamna budi iwepo njia wataitumia walioowana kutengana. Wala haijuzu wateseke kubakia juu ya ndoa hiyo pamoja na kuyashukia wote wawili au mmoja kati yao. Na Allah ameweka talaka. Amesema Allah (Ta’ala):

{ الطَّلاقُ مَرْتَانٌ فِإِمْسَاكٍ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيْحٌ بِإِحْسَانٍ } (البقرة: 229)

“*Talaka ni mara mbili kushikamana kwa wema au kuwachana kwa wema*” (Baqarah-229) ili isiendele kuwepo maafa katiak nyumba na ili ipatikane utulivu wa ndoa wima kati ya watu. Na ikiwa ni vigumu kuwepo baina yao kwa kukosekana makubaliano kati yao au yametokeza katika maisha yao yanowafisidi basi watakua wamepewa nafasi ili afanye bidii killa mmoja wao juu ya kulea utulivu wa ndoa kwa mwengine. Isipokua Uislamu haukufanya kuwepo ugomvi na uchukivu ndio sababu ya talaka. Bala amewaamrisha walioowana matangamano mazuri. Na kusisitiza kustahmili uchukivu huenda ikawa kuna kheri. Amesema Ta’ala:

{ وَعَاشُرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ فَإِنْ كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا } (النساء: 19)

“Na mutangamane nao kwa wema, na iwapo mutawachukia basi huenda kuchukia kitu na Allah akajaalia ndani yake kheri nyingi” (Nisa-19) Na amemwamrisha wanaume watumie mbinu ambayo kwayoo itasahilisha hasira za mwanamke na uasi wao (Nushuz) Na akasema Ta’ala:

{وَاللَّاتِي تَخَافُونَ نُشُوزْهُنَّ وَاهْجُرُوهُنَّ فِي الْمَضَاجِعِ  
وَاضْرِبُوهُنَّ} (النساء: 34)

“Na wale munaowaogopea uasi wao, basi wapeni mawaidha, na muwahame katika malazi na muwapige”(Nisa-34) Na ndio ameamrisha kuchukua mbinu za kutosha za laini na zisizo laini, ya kutatua matatizo ambayo hupatikana baina ya walioowana, suluhisho litakao kua ni kizuizi baina yao na talaka. Hata iwapo matangamano mazuri yasinufaishe, na isifae nyengine katika mbinu kali, na mambo yakavuka uchikivu na balaa na uasi na kuelekea mizozo na migawanyiko basi uislamu haukufanya talaka kua ndio hatua ya pili, pamoja na kwamba ugumu wa misukosuko kati yao. Bali ameamrisha mambo yaingiliwa na wengine kati watu wao, ilil waweze kuleta suluhu mara nyengine, akasema Ta’ala

{ وَإِنْ خَفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِنْ أَهْلِهِ إِنْ يُرِيدَا إِصْلَاحًا  
يُوفِيقُ اللَّهُ بَيْنَهُمَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْمًا خَبِيرًا} (النساء: 35)

“Na mukiogopea mpasuko kati yao basi peleka hakimu katika mtu wa mume na hakimu katika mtu wa mke, iwapo wanataka suluhu Allaha atawaafikia baina yao. Hakika Allah ni mjuzi na muelewa” (Nisa-35). Na iwapo watashindwa mahakimu hawa wawili kusuluhisha kati ya mume na mke kwa wakti huo hamna namna ya kuendeleza maisha ya ndoa kati yao baada ya majaribio yote hayo. Kwani hamna namna ya kuleta uelewano kati yao illa ni kuwatenganisha. Kwa hivyo hamna budi na talaka huenda wakapata utulivu wa ndoa au huenda tatizo hili kusuluhishika kupitia talaka hiyo amesema Ta’ala:

{ وَإِنْ يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللَّهُ كُلُّا مِنْ سَعَتِهِ وَكَانَ اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا} (النساء: 130)

“Na iwapo watatengana Allah atamtosheleza killa mmoja wao kwa uweza wake, na Allah ni mkujufu na mwenye hikima” (Nisa-130).

Isipokua hii talaka imewacha ndani yake nafasi ya mume na mke, na wala sio ufarakano kamili kati yao, bali wamepewa haki ya kurudiana kwa ya kwanza naya pili, kwani talaka ya kwanza au ya pili ikachemsha katika nafsi ya mume au mke hamu mpya ya kurudisha maisha ya ndoa kati yao kwa mara nyengine baada ya talaka ya kwanza na mara ya tatu baada ya pili. Na mpaka hapa tutapata kua sharia imeweka talaka mara tatu na akasema Ta'ala:

**{ الطَّلاقُ مَرَّتَانِ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرِيرٌ بِإِحْسَانٍ } (البقرة: 229)**

"*Talaka ni mara mbili kukaa kwa wema au kuachana kwa wema*" ili liwachwe kwa mume na mke killa mmoja wao airudi nafsi yake na arudi kumcha Allah iliokita katika kifua chake na huenda wao wakajaribu kurudia majaribio ya kurudia maisha ya ndoa mara nyengine, na kupata ululivu wa ndoa na raha na ukamilifu ambayo hawakua wakiyapata mbeleni. Na mpaka hapa tunakuta kua usilamu umemruhusu mume kumrudia mkewe baada ya talaka ya kwanza nay a pili. Vile vile ameweka yatakao wasaidia wao kuzirudi nafsi zao. Na kurudi kufikiria tena, na kumuangalia yeye muangilio wa makini zaidi ya vile walivyo kua wakiangalia. Kwani ameweka kipindi cha eda baada ya talaka kuani hedhi tatu nayo inakurubiana miezi mitatu au kuzaa, na kuifanya kua ni wajibu juu mume kumsimamia mtalaka wake huyu na kumpatia makao kwa muda wa kipindi hicho na mume akakatazwa kumtoa aliena eda mapak akamilisha eda yake, na hayo ni kulainisha nyoyo na kuzisafisha nafis. Na kufunua njia ambayo wataregeana. Na kuanzisha maisha safi mapya, na akausia katika upande huo kuusia wazi katika Quran amesema Allah Ta'ala:

**{ وَإِذَا طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ فَلْيَغْنِ أَجْلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرِحُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَلَا تُمْسِكُوهُنَّ ضِرَارًا لِتَعْتَدُوا وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ... } (البقرة: 231)**

"*Na munapo waacha wanawake na wakakmilisha muda wao basi wazuieni kwa wema au waacheneni kwa wema wala musiwazuie ili muwadhuru anaefanya haya basi ameidhulumu nafsi yake*" (Baqara-231). Na iwapo maamiliano hayo hayo kuathiri au yameathiri baada ya talaka ya kwanza nay a pili

kisha likapatikana ya tatu mbali na yote hayo kwani suala wakati huo ni mzizi uliokita, na gumu zaidi na baya zaidi, wala kuibakisha ndoa. Na imekua hamna budi kutenganisha kikamilifu na kuanzisha mahusiano mapya mengine. Bila ya kuyrudia majaribio yalioshindwa kwa mahusiano hayo hayo, kabla ya kujaribu mahusiano mengine na kwa sababu hiyo imekua talaka ya tatu kua ni uamuzi, na akasema Ta’ala:

**{فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا تَحْلُّ لَهُ مِنْ بَعْدٍ حَتَّىٰ شَكَحَ زَوْجًا غَيْرَهُ} (البقرة: 230)**

“*Na iwapo atamuacha basi sio halali kwake baada ya hapo mpaka aolewe na mume mwengine*” (Baqarah-230). Na akakatazwa mume kumrudia mke aliemuacha talaka ya tatu mpaka atangamane na mume mwengine na amuingilie “mpaka (mke) aonje asali ya mume, na (mume) aonje asali ya mke” ili aonje matangamano ya ndoa kamili. Na iwapo atajaribu matangamano mengine kwa mwengine majaribio ya kikawaida, na asipate raha na utulivu katiak matangamano hayo ya pili, na kukapatikana ufarikiano baina yake na mumewe wa pili, wakati yawezekana kwake kuudia matangamano hayo ya pili, wakati yawezekana kwake kurudia matangamano ya ndoa pamoja na mume wa kwanza, kwani atakua ameshapita katiaka majaribio ya pili ya matangamano ya ndoa pamoja na mume wa kwanza, kwani atakua ameshapita katika majaribio ya pili na kuwapima kati yao (waume). Na wakati huo atachagua kurudi kwa kujua. Na mpaka tunakuta kua mteremsha sharia amemruhusu mwanamke kurudi kwa mume wa kwanza aliemuacha talaka tatu baada ya kuolewa na mume mwengine, amesema Allah (Ta’ala):

**{فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا تَحْلُّ لَهُ مِنْ بَعْدٍ حَتَّىٰ شَكَحَ زَوْجًا غَيْرَهُ} (البقرة: 230)**

“*Na iwapo atamuacha basi sio halali kwake baada ya hapo baada ya hayo akasema “Na iwapo atamuacha”*” (Baqarah-230) yaani mume wa pili ambae sio wa kwanza:

**{فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا}**

“*Sio makosa kwao*” (Baqara-230) yaani mume wa kwanza na alieachwa talaka mbili:

“Kurudiana” (Baqarah-230) yaani killa mmoja wao kumrudia mwezake kwa ndoa.

Hayo ndio yaliodokezwa nayo kwa upande wa kuwepo shariah ya talaka, na kwayo yadhihirika yaliomo katika sharia ya talaka na njia ya kuwepo kwake na hamna na kuwepo katika hikma ilikamilika, na mtazamo wa kindani wa maisha ya kijamii, ili idhamini maisha matulivu. Na ikikosekana utulivu huo na kusiwe na matumaini ya kuyarudisha, basi hamna budi kuwatenganisha walioowana. Na kwa sababu hiyo Allah akaweka sharia ya talaka kwa namna ambayo tumeileza.

### Nasaba (uhusiano)

Kwa Hikma ya uungu ameamua kwa mwanamke kua ndio sehemu ya mamba na kuzaa, na kwa sababu hiyo amewajibisha afungwe mwanamke kwa kuolewa na mwanamume mmoja, na kukatazwa kuolewa na zaidi ya mume mmoja. Na ikaharamishiwa juu yake ili aweze killa mtu kujua anae nasibiana nae. Na sharia imekusudia kwa kuthubutu nasaba na akabainisha hukmu zake ukamili wa bayana.

Na muda mchache wa kuzaa ni miezi sita na uwingi wake ni miezi tisa, na urefu zaidi ni miaka miwili, na mume akimzalisha mkewe mtoto inaweza kua amepaa mtoto kwake kwa miezi sita na zaidi kutoka tarehe ya kumuowa basi ni mtoto wake, kwa qauli yake Mtume (saaw) “Mtoto ni wa kitandani” kwa ufupi: Madamu mke yupo katika ndoa ya mume na akazaa mtoto kwa zaidi ya miezi sita kutoka kuolewa basi atakua ni mtoto wa mume wazi kabisa.

Isipokua mume akizaa mkewe mtoto kwa miezi sita na kuzidi na kuhakikishwa kua mtotoo huyu sio wake basi inafaa amkatae kwa sharuti zisizo na budi zihakikishwe na hamna thamani kukataa kwake bali atabakia kua ni mwanawe atake au akatae na masharti yenyewe ni:-

Ya kwanza:- Awe mtoto anaemkataa sioi wke amezaliwa hai na haikataliwi nasaba ya mtoto iwapo amezaliwa ni maiti kwa sababu haiingiliani kukataa kwake na hukmu ya kisheria.

Ya pili:-nAsiwe ameshalikubali kwa saraha au kwa dalili kua ni mtoto wake, na iwapo alikubali kwa saraha au kwa dalili kua ni mtoto wake basi haifai kukataaa nasaba yake baada ya hapo.

Ya tatu:- Awe amemkataa mtoto katika wakati maalum na hali maalum nao ni wakti wa mazazi au wakati kununua mahitaji yake, au wakati anapojua kua mkewe amezaa na yeye hakuwepo, wala haina uzito kukataa kwake akikataa katika nyakati zisizokua hizo au kwa hali nyenginezo. Kwa hivyo mkewe akizaa mtoto na akanyamaa kumkataa kwake pamoja na kuweza atalazimika nasaba yake na haifai kukata baada ya hapo. Na itakadiriwa khiyari kwa kujua kwake na uwezekano wke kwa kumkataa, kwa hivyo akijua khusu mtoto na akawa anaweza kumkataa na asimkatae itathubutu nasaba yake, kwa sababu Mtume (sssw) amesema: “Mtoto na kitanda” na iwapo atadai kua hajui kuhusu kuzaliwa mtoto basi yawezekana kukubaliwa kwa kua alikua sehemu ambayo yeye hakuijua, mafano alikua kwengine au nchi nyengine, kwa hivyo maneno yatachukuliwa pamoja na kiapo chake, kwa sababu asli ya kutojua. Na iwapo atasema nilijua kuzaliwa kwake lakini sikujua kua nawezaa kumkataa, au aseme niliyojua hayo lakini sikujua kua ni juu yangu kumkataa papo hapo, na kua hakuyajua hayo kama jumla ya watu, basi atakubaliwa, kwa sababau hukmu hiyo ni yale yaliofichika kwa jumla na kushabihiana na yule alieingilia uislamu karibuni. Na hukmu yoyote iwe ni yale yaliofichika kwake ni kwa mfano huo huo atapewa udhuru kwa kutolijua, kama yule ni mgeni katika uislamu. Na iwapo haikufichika mfano wa hukmu hiyo juu ya mfano wa mtu huyo hatapewa udhuru kwa kutolijua.

Ya nne:- Kukataa mtoto yafuatane na laa’na (Liaan) au amekatalika na atakua ni haki ya mwanamke, amepokea Ibn Umar kua mtu alimlaani mkewe katika zama za Mtume (saaw)

na akamkataa mtoto wake na Mtume (saaw) akwa tenganisha, na mtoto akakabidhiwa mwanamke. Na iwapo haakupatikana masharti ya kukataa mtoto basi hatakatalika na itathubutu nasaba ya mume, na kuangukiwa juu yake hukmu zote za utoto. Hayo ikiwa utesi umeletwa juu ya mazazi ka upande wa mume. Ama ikiwa ni utesi baina ya mke na mume umekuja kwa upande wa mke, na mke akadai wakati wa kuishi nae kindoa kua alizaa nae mtoto na mume akapinga hayo, kama aseme mume wewe hukuzaa, basi itaku nijuu ya mke kuthibitisha madai yake kwa ushahidi wa mwanamke mmoja muislamu, na katika hali hiyo inatosha ushahidi wa mwanamke mmoja, kwa sababu nasaba inathubutu kwa kuwepo malazi. Na mazazi inafaa kuthubutu kwa ushahidi wa mwanamke mmoja mwenye kutekeleza masharti ya ushahidi.

### La'ana (lia'an)

Neno laan lilnatoka kutoka laan, kwa sababu killa moja wao (mke na mume) anailaani nafsi yake katika ya tano iwapo ni mrongo. Na asli katika qauli yake Ta'ala:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ أَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شَهَادَةُ إِلَّا أَنفُسُهُمْ فَشَهَادَةُ أَحَدٍ مِنْ أَرْبَعِ شَهَادَاتٍ بِاللَّهِ أَنَّهُ لَمْ يَكُنْ مِنَ الصَّادِقِينَ - وَالْخَامِسَةُ أَنَّ لَعْنَةَ اللَّهِ عَلَيْهِ أَنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ - وَيَدْرِأُ عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ تَشْهَدَ أَرْبَعَ شَهَادَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمْ يَكُنْ مِنَ الْكَاذِبِينَ - وَالْخَامِسَةُ أَنَّ غَضَبَ اللَّهِ عَلَيْهَا إِنْ كَانَ مِنَ الصَّادِقِينَ (النور: 6-9)

“Na wale ambao wanatuhumu wake zao na wasiwe na mashahidi illa nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakua kuapa mara nne kw kiapo cha Allah ya kwenye hakika yeye anasema ukweli – na ya tano ni kua laana ya Allah iwe juu yake iwapo anasema urongo – na mke itamuondokea adhabu kwa kutoa viapo vine ya kwamba mume ni mrongo. Na ya tano ni ghadhabu za Allah iwe juu yake (yeye mke) ikiwa mume ni mkweli“ ( An-Nur) Na ameipokea Abu Daud kupitia isnaad kutoka kwa ibn Abbas (raa) amesema: (Alikuja Hilal bin Ummayah mmoja katika watatu waliotubiwa na Allah aliru;di nyumbani kwake ishaa kutoka ardhi yake na akamkuta mtu kwa mkewe na akaona kwa macho yake na akasikia kwa masikio yake na asimsumbue mpaka kulipopambazuka, na akamuendea Mtume (saaw) na akasema “Ewe mtume wa Allah niliingia kwa

mke wangu na nikamkuta kwake mwanamume na nikaona kwa macho yangu na nikasikia kwa masikio yangu, Mtume (saaw) yakamchukiza aliokuja nayo, na yakawa ni mazito juu yake na aya ikashuka )Na wale wanotuhumu wake zao na wasiwe na mashahidi illa nafsi zao basi kiapo cha mmoja wao) aya mbili . yakawa mepesi haya kwa Mtume (saaw) na akasema : “Fulani ewe Hilal, kwani Allah amekujalia wewe wepesi na sahali. Akasema Hilal: Nilikua nikitarajia hayo kutoka kwa Mola wangu alietukuka. Akasema Mtume (saaw) niitieni yeye (Mke wa Hilal). Akaitwa. Na Mtume (saaw) akaisoma aya na akawakumbusha kua adhabu ya Akhira nikali zaidi kuliko adhabu ya dunia. Akasema Hilal naapa kwa Allah nasema ukweli juu yake. Akasema mke: Amedanganya. Akasema Mtume (saaw): Wapitishieni laani kati yao” Akaambiwa Hilal: aapa, akaaapa mara nne kua yeye ni mkweli. Iliro kua ya tano, akaambiwa, ewe Hilal mche Allah hakika adhabu ya dunia ni ndogo kuliko adhabu ya akhera na hili ni kiwajibisho kitakchowajibisha adhabu juu yako. Akasema: Naapa na Allah, sitaadhibiwa kwa ajili yake kama ambavyo sikupigwa viboko kwa ajili yake. Akaapa ya tano kua laana ya Allah iwe juu yake iwapo ni mrongo. Kisha akaambiwa mke apaa, na akaapa viapo vine kua (Hilal) ni mrongo n ailipokua ya tano akaambia mche Allah kwani adhabu ya dunia ni ndogo kuliko adhabu ya akhera. Na hili ni kiwajibisho kitakachio wajibisha juu yako adhabu. Akasita kwa muda, kisha akasema naapa na Allah, sitowafedhehi watu wangu n akaapa ya tano. Kua ghadhabu za Allah ziwe juu yake iwapo mume ni mkwelil. Na Mtume (saaw) akawatenganisha kati yao na akaamua kua mke hana nyumba wala tongue kwa mume.

Na mume anapomtuhumu mkewe na akamuambia umezini au ewe mzinifu au nilikuona ukizini na asilete ushahidi atalazimika viboko (hadd) iwapo hatalaani. Na iwapo mume atabani na mke asilaani itamlazimu mke viboko kwa qauli yake ta’ala:

{ وَيَدْرُأُ عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ تَشْهَدَ أَرْبَعَ شَهَادَاتٍ ... } (النور: 8)

“Na itaondosha juu yake adhabu kwa kuapa viapo vine” (Nur-8). Na adhabu inaomuondokea yeye ni hadd iliotajwa katika qauli yake ta’ala:

}... وَلِيَشْهُدْ عَذَابَهُمَا طَائِفَةٌ مِّنْ الْمُؤْمِنِينَ { (النور: 2)

“Na washuhudie kuadhibiwa kwa kundi la waumini” (Nur-2). Kwa sababu Hilal bin Umayah alipomtuhumu mkewe na akamuendea Mtume (saaw) na akamuelezea akaitishwa mke na wakalaaniana kati yao. Na hali hii ni maalum mionganoni mwa hali ambazo huthubutu zinaa na in hali ambayo mume anapomtuhumu mkewe kwa zinaa basi itathubutu kwa kulaani mume na kwa kutomlaani mke, na iwapo walaaniana hata thubutu, na iwapo mke atakataa kulaani itathubutu zinaa juu yake na hapasa kupigwa hadd mke kwa kumlaani kwake mumewe.

Na iwapo wote watalaani na kiongozi akawa tenganisha basi hawatakutana milele na mke ataharamisha juu ya mume milele. Kwa sababu Mtume (saaw) aliwatenganisha waliolaaniana. Ameipokea Maliki kutoka kwa Nafii ibn Umar: “Mtu alimlaani mkewe katika zama za Mtume (saaw) na (mume) akamkana mtoto wake (mke) na Mtume (saaw) akawatenganisha kati yao na mtoto akampa mke” Na ameipokea Sahl bin Saad amesema: “Iliendelea Sunnah katika wanaolaaniana watenganishwe kisha wasikutane tena milele” Na mfarakano huu kupidia laana ni faskh kwa sababu huwajibisha uharamu wa milele, kwa hivyo sio halali kwake hata lau kama amedanganya. Isipokua atakapo rudi na akaikadhibisha nafsi yake basi hadd itakua ni wajibu juu yake, na atapewa nasaha itakua ni wajibu juu yake, na atapewa nasaha ya mtoto iwe amedanganya kabla ya kulaani au baada yake. Na kulaani ambayo inamuokoa mume na hadd na kulazimisha hadd juu ya mke iwapo atasita kulaani ni kusema mume mbele ya kiongozi “Namshuhudisha Allah yeye amezini” na atamuelezea kidole mke na iwapo mke hayupo atataja jina la mke na nasaba yake mpaka ikamilike mara nne kisha atasimamishwa na kuambia yeye mche Allah kwnai hili linawajibisha na adhabu ya dunia ni ndogo kuliko adhabu ya

akhera, na iwapo hatosita na aendele basi atasema : laan ya Allah iwe juu yake iwapo ni mrongo kwa anaomtuhumu naye ya zinaa. Na yeye atasema mke: Namshuhudishia Allah kua mume ni mrongo mara nne, kisha atasimamishwa katika ya tano na ataogopeshwa kama alivyo ogopeshwa mwanamume na iwapo hatasita illa akamilishe basi atasema: ghadhabu ya Allah iwe juu yke iwapo mume ni mkweli kwa anaomtuhumu nayo ya zinaa. Na iwapo kati yao kuna mtoto atatajwa mtoto katika lian, na iwapo atasema namshuhudishia Allah kua yeye ni mrongo na mtoto huyu ni wake.

Hii ndio namna ya kulaaniana na hayo ndiyo matamshi yake na maneno yake, na kwa ajili ya hilo mwanamke amezaa na akasema mumewe mtoto huyu sio kutoka kwangu au aseme huyu si mtoto wangu, basi hamna haddi juu yake kwa sababu hiyo si tuhuma lakini ataulizwa iwapo atasema alizini na akamzaa huyu kwa zinaa, basi hiyo ni tuhuma na itapasa kulaani. Na iwapo atasema namaanisha kua hayafanani na mimi umbile au aseme nafikiri ameingiliwa na mtoto ni wa yule aliemuilingilia, au mfano wa maneno hayo basi hamna haddi juu yake, na atachukua nasaba ya mtoto kwa sababu hakumtuhumu. Na hamna kulaani katika hali hiyo kwa sababu sharti ya laana ni tuhuma.

### Usimamizi wa baba (waliy)

Kwa kua baba ndie raisi wa jamii, na kiongozi wake msimamizi juu yake, imekua hamna budi awe ni mlezi (wali) juu yake. Kwa baba ni msimamizi juu ya watoto, yeye ndie msimamizi wa watoto wake wadogo na wakubwa ambao sio mukallaf, waume kwa wake katika nafsi na male hata kama ni mchanga katika hifadhi ya mama au familia yake.

Na mtu imam atakua ni mkubwa au atakua ni mdogo. Na mkubwa imma awe na akili au asiwe nayo. Na iwapo ni mkubwa mwenye akili basi hana juu yake usimamizi wa yoyote kwa upande wa nafsi na mali, bali yeye atosimamia mwenyewe mambo. Lakini itabakia haki ya usimamizi juu ya baba. Na

iwapo ni mdogo au mkubwa aise na akili, kama kua mwandazimu. Kwani usimamizi haiwi juu yake, kwa sababu atashindwa na hayo, bali usimamizi wake ni juu ya baba. Na usimamizi huu utaendelea madamu anacho kinacho wajibisha nao ni utoto au ukosefu wa akili. Na ikiwa atabaleghe mtoto mdogo au apone mtoto mkubwa na uwazimu itakatika usimamizi juu yake, na itabakia kwa baba juu yao usimamizi wa kujitolea (Nadh) na kupendekezwa (istinhab). Kwa sababu yeye ana haki ya usimamizi daima.

### Ulezi wa mtoto (kafalah)

Kumlea mtoto ni faradhi kwa sababu ataangamia kwa kumuacha, na hiyo ni upande wa kuhifadhi nafsi ambayo Allah amewajibisha, kwa hivyo ni wajibu kuihifadhi na maangamivu, na kuikoa na maangamivu. Ijapokua asli ya kulea mtoto ni faradhi lakini inahusiana na qaraba waae kwa sababu ndiio wanastahiki mtoto, kwa hivyo inahusiana na haki kama inavyohusiana na wajibu. Na ulezi ni haki ya killa mtoto na ni wajibu wa killa aliewajibishwa na Allah juu ya ulezi wake. Na inakua ni faradhi ya kumlea juu ya wanao julika kwa aina yao. Ama haki ya waliowajibishwa juu yalo na Allah ya ulezi ni kuchukua uleizi huu ni maalum kwa walei ambao ni wahusika. Wala sio jumla (amm), kwa hivyo haithhubutu ulezi kwa atakae mpoteza mtoto, kwa hivyo hunyimwa moja kwa moja kwa sababu kuangamia. Wala haitathhubutu ulezi wa mtoto kwa mtoto au mwandazimu, kwa sababu killa mmoja wao hawezi hayo, na yeye mwenyewe ahitaji wa kumea yeye, kwa hivyo vipi ataleta mwengine. Vile vile haithhubutu ulezi kwa yule anaejulikana kua mtoto atapotea kwa kutomshughulikia au kutomjali au kwa mashughuli zitakazo mzuia kumleta au kwa kua na tabia mbovu kwa mfano mtoto atamlea na malezi ya ufisadi kwa ufisadi huzingatiwa ni maangamivu. Ama kafiri haiwezekani kua ni baba wa mtoto wa mama muislamu, kwa kutoruhusiwa muislamu kuolewa na kafiri. Kwa hivyo yafahamika kua anaestahiki kumlea mtoto ni mwanamke mama au mwengine. Na katika hali hiyo huangaliwa iwapo mtoto ni mkubwa katika miaka ya kuelewa mambo na anelewa tafauti

maamiliano ya mamake na inaamiliano ya babake, kama awe amepita umri wa kunyonya basi katika umri huo atakhiyarishwa baina ya wazee wake na mtoto atake mchagua baina ya wazee wake na mtoto atake mchagua ataunganishwa nae, kama alivyopokea Abu Daud kutoka kwa Abdulhamid bin Ja'afar kutoka kwa babake kutoka kwa babu ykae rafii bin Sinan "Kua yeye Akakataa kusilimu, akaja mke kwa Mtume (saaw) na akasema : Binti yangu ananyonya au mfano wake. Na rafii akasema: Ni bint yangu. Na akasema Mtume (saaw) kaa upande mmoja na wewe (mke) kaa upande mwengine na akasema muijeni (mtoto) na mtoto akalemea kwa mamake. Akasema Mtume (saaw) Ewe mola muongoze. Na akalemea kwa babake na akamchukua". Na wameipokea hadithi kwa maan hivyo hiyo iliyopo katika riwaya hii.

Na iwapo mtoto ni mdogo katika umri wa kutolewa kitu wala haelewi tofauti ya maamiliano ya mamake na maamiliano ya babake, kama kua kati umri wa kunyonya au chini yake au juu yake lakini karibu yake basi hato khitayarishwa, bali atapewa mama. Na hayo ni kwa mafhum ya hadithi ya rafii bin Sinan iliotangulial kwa sababu imethubutu kua mama ndie mwenye haki yake ya kumlea mtoto, wala haikuja nass kumzuia hayo. Wala haisemwi kua ulezi ni usimamizi basi haithubutu kwa kafiri juu ya muislamu kwani uhakika wake ni ulezi na kumhudumia wala sio usimamizi wala haichukui hukmu za usimamizi.

Na mama ndie mwenye haki zaidi ya kumlea mtoto na mwandazimu aliepewa talaka. Kama alivyopokea Abu Daud kutoka kwa Abdalla bin Amru bin A'as. "Kwa mwanamke alisema ewe Mtume (saaw) wewe una haki nae zaidi kwa muda hujaolewa". Na ameipokea ibn Shaibah kutoka kwa Umar kua yeye alimuacha Umm Asim kisha amjilia na katika mapajani mwake ana Asim, na akataka kumchukua kutoka kwake na wakavutana na mtoto mpaka mtoto akalia, na wakaondoka kwenda kwa Abi Bakr Siddiq na akasema "mpapaso wake (mume) na mapaja yake (mama) na harufu yake (mama) ni bora

kwa mtoto kulikyo yako muache awe mkubwa na achague mwenyewe". Na iwapo mama hafai kulea kwa kukosekana na masharti yaliotajwa au baadhi yake kama ameolewa au wazimu au mifano yake hiyo ni kama hayupo, na huangukia kwa anaemfuata katika kustahiki. Na iwapo wazazi hawafai kulea inahamia kwa wanaowafuata katika kustahiki. Kwani wao ni kama hawapo. Na bora zaidi kulea ni mama kisha mama yake hata kama wajuu hutangulizwa wakaribu na waribu. Kwa sababu wao ni wanawake na wanaujuzi kulea, kwa hivyo wanachukua maana ya mama, kisha ni baba kisha mama zake kuisha babu kisha mama zake kisha babu wa baba, kisha mama zake hata kama sio warithi, kwa sababu wao wanaingia katika watu wanaostahiki kulea. Na iwapo mababa na ma mama wamekuwa huenda ulezi huo kwa madaha na hutangulizwa dada wa wazee wawili, kisha dada kwa upande wa baba kisha dada kwa mama, na hutangulizwa dada kuliko kaka wa wazee wawili ni bora zaidi kisha kaka kwa baba kisha watoto wao, wala hamna kulea kwa kaka kwa mama. Na iwapo hawata kuwepo ulezi ni kwa khalati na wakitoo kuwepo itakua kwa mashangazi na iwapo hawata kuwepo kwa ma'ami kwa wazee wawili, kisha kwa ammi kwa baba, wala hamna kulea kwa ammi kwa mama, na iwapo watakosekana itakua ni kwa makhalati wa mama kisha makhalati wa baba kisha mashangazi wa baba wala hamna kulea kwa mashangazi wa mama kwa sababau wao wanaingia mlango wa mama wala hamna kwake kulea.

Wala haitahama ulezi kwa anaestahiki kwa chini yake illa katika hali ya kukosekana kwake au katika hali ya kutofaa kwake. Ama akiwacha anae stahiki ulezi kumlea mtoto, basi haiangukii kwa anaefuata illa iwapo ulezi wa mtoto litapatikana kwake, kwa sababu ulezi hata kama ni haki ya mlezi na wakati huo huo ni wajibu juu yake na haki ya anaolewa haiwezekani awachwe illa awe ni katika watakao kueleza wajibu huo, na wakati huo utakwenda ulezi kwa mlezi anaefuata ambae amewaacha ulezi wake kwa utaratibu uliotangulia. Na iwapo atataka alie bwaga haki yake ya ulezi kurudia kutekeleza haki

yake, na akawa anafaa kulea basi haki ykae bado imesimama na mtoto atarudushiwa yeye. Vile vile akiolewa mama, na akabwaga haki yake katika kulea, kisha apewe talaka atarudishiwa haki yake ya kumlea mtoto, vile vile qarabah anestahiki ulezi na kunyimwa haki yao ya kulea kwani sababu ipo.

Na wakizozana watu juu ya mtoto kuhusu mwenye haki zaidi ya kulea hurudiwa wala ambao ni mitagaa katika walio na haki ya ulezi. Imepokewa kutoka Barra bin Azib kua Ali na Jaafar na Zeid walizozana juu ya binti wa ammi yangu na khalati yake ni mke wangu na Zeid akasema ni mtoto (Hamza) wa kakangu. Na akaamua Mtume (saaw) kwa khalati yake na akasemaa “Khalati ni daraja ya mama”.

Na hayo yote ni kuhusu mtoto na anaetaka kumlea kwa ajili ya kumhifadhi na maangamivu. Ama mtoto ambae anaweza kujiangalia, basi kwa kujitosheleza hypotea illah ya kumlea, na kwa kuondoka kwa hypotea illah ya kumlea, na kwa kuondoka kwake hypoea hukmu nao ni uwajibu wa kulea na haki ya karibu ya kumlea, na wakati hyuo huangaliwa iwapo alie na haki ya karibu ya kumlea, na wakati huo huangaliwa iwapo alie na haki ya kulea kama mama ni kafiri basi huchukuliwa kutoka kwa na kupewa kwa alie na usimamizi juu yake (wali) kwani uhakika wake ni usimamizi (wali) sio ulezi. Na usimamizi haifai kwa kafiri kwa Qauli yake Ta’ala:

}...وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا { (النساء: 141)

“*Na kamwe Allah hatawapa uweza makafiri juu ya waumin*” (Nisa-141) na kwa Qauli yake (saaw)” uislamu unatawala wala hautawala hivi” na hiyo ni jumla wala hakuja ya kuifanya ni makhsus, kwani hadithi za ulezi makhusus haingii juu yake wakati huo kwa kujitosheleza na ulezi. Na iwapo wanaostahiki kumlea na wale waliona usimamizi juu yake ni waislamu, kama baba na mama na waislamu basi barobaro au msichana yaani mtoto wa kiume au binti atakhiyarishwa kati ya babake na mamake, na yoyote atakae chagua ataunganishwa nae. Kama

ilivyopokewa na Ahmad na ibn Majah na Tirmidhi “kutoka kwa Abu Hureira kua Mtume (saaw) alimkhiyarisha kijana kati ya babake na mamake”. Na katika mapokezi ya Abu Daud “Kua alikuja mwanamke na akasema: Mume wangu anataka kuenda na mtoto na alininywesha maji kutoka kwa kisima cha Abi Habah nao alinifaa, akasema Mtume (s.a.a.w): wapigieni kura kwa hilo, akasema mumewe: Ni nani anashindana na mimi juu ya mtoto wangu, akasema Mtume (saaw): huyo ni babako na hivyo ni mamako, uchukue mkono wa yule amtakae kati yao, akashika mkono wa mamake na akaondoka nae”. Na ameipokea Bayhaqi kutoka kwa Umar kua alimkhiyarisha kijana baina ya babake na mamake. Na pia amepokea kutoka kwa Ali kua alimkhiyarisha Ammarah Al-Judhami kati ya mamake na shanganzi yake na alikua ni mtoto wa miaka saba au minane. Kwa hivyo hadithi hizi ziko wazi na pia muna dalili juu ya wanapo zozana baba na mama juu ya mtoto wao inakua ni wajibu yeye achague na atake mchagua atakwenda nae. Ama ufahamu inaopatika katika mapokezi ya Abi Daud, haikuja katika mapokezi ya Nasai, wala katika mapokezi yaliosalia kwa kufahamika juu ya hali ya kutomkhiyarisha mtoto mmoja kati yao. Wala kuchagua haifungwi kwa umri maalum bali hyo humrudia hakimu vile anavyoonda kwa mujibu wa wajuzi. Iwapo watasema ametosheka na ulezi na akakinai hkumu hayo basi atamkhiyarisha, au sivyo atamuacha kwa aliena na haki ya kumlea. Na hutafautiana hayo katika watoto kwa kutafautika hali zao, kwani huenda mtoto akatosheka na ulezi na umri wake ni miaka mitano, na mtoto mwengine huenda asitosheke na umri wake ni miaka tisa kwa hivyoo cha kuzingatiwa ni uhakika wa mtoto kwa upande wa kutosheka kwake au kutosheka kwake.

### Kunga jamaa (silat ar-rahim)

Hakika Allah (swt) wakati alipokataza uasabiya wa kijahiliya aliyakataza hayo kwa kuifanya uasabiya wa kikabila ndio mafungamano kati ya watoto wa umma wa kiislamu, na akakataza isitawale katiak mahusiano ya waislamu. Lakini ameamrisha kuunga jamaa na kuwfanyia wema. Imepokewa kuwa mtu alimuuliza Mtume (saaw) yupi nimfanyie wema

akasema: “Mamako na dadako na kakako” na katika matamshi “Na anaehusiana (mawla) ambae ni kribu yako ni haki na wajibu, na kisazi cha kuungwa” na imepokewa kutoka Asmaa bint Abi Bakr (raa) amesema: “Alinijia mamangu nay eye ni mushrik kati zama za Qureish wakati waipoweka mkataba na Mtume (saaw) na nikamuuliza Mtume (saaw) na nikasema: Mamangu amekuja na ananitamani. Akasema ndio muunge mamako.”

Na uislamu umeigawanya jamii vigawanyinko viwili cha kwanza ni Aqarib ambao wanaweza kurithi mtu anapokufa. Na la pili ulul-arham. Ama wale walio na haki ya kurithi wao ni watu fungu (furudh) na Asaba, ama wale ulul arham hao ni wengine wasio kua hawa nao wasio na fungu katika urathi wala sio Asaba. Nao ni aina kumi mjomba na khalati na babu kwa mama na mtoto wa kaka upande wa mama na yoyote alie karibu na mmoja wao. Nao hawa hawakuwekewa na Allah fungu katika urathi wa mtu kabisa na wala sio wajibu nafaqah yaani kwa yoyote miongoni mwao juu ya mtu. Lakini Allah ameamrisha kuunga na kufanya wema kwa Aqarib wote. Imepokewa kutoka kwa Jabir (raa) kutoka kwa Mtume (saaw) amesema: “Ikiwa mmoja wenu ni kafiri basi aanze juu ya nafsi yake ikiwa ana zaidi basi kwa jamii yake (familia) ikiwa ana zaidi basi kwa jamaa zake”. Na imepokewa kutoka Abi Ayyub Al-ansari kwa mtu alisema “Ewe Mtume wa Allah nijulishe mimi kitendo kitakacho ni inigiza mimi peponi, watu wakasema, ana nini huyu? Akasema Mtume (saaw) ana jambo anauliza. Akasema Mtume (saaw): Muabudu Allah na usimshirkishe na chochote na usimamishe swalah na utoe zakah na uunge kizazi”. Kwa hivyo haikubanisha wala nyenginezo katika hadithi ambazo zimetaja kuunga jamaa lililokusudiwa ni ulul arham pekee au ni wote wanao nasabiana na kizazi cha mtu. Na kidhahiri katika hadithi ni jumla, kwa hivyo inajumuisha kuunga killa mmoja katika jamaa wawe ni kizazi muhram au ni kizazi wasio mahram katika Asabah au ulul-arham, kwani wao wote huchukuliwa ni ulul-arham, na zimepokewa hadithi kadha katika kuunga kizazi, kwani amesema (saaw) “Haingii peponi

anaekata jamaa”. Na imepokewa kutoka kwa Anas bin Malik amesema Mtume (saaw) “Yoyote anaependa akunjuliwe katika riziki yake na maisha yake yarefushwe basi aungejamaa”. Na kutoka kwa Abu Hureirah kutoka kwa Mtume (saaw) “Allah aliumba viumbe alipokamilisha, ukasimama uzao mionganoni mwao, na akasema: Nataka hifadhi yake na anaekata? Akasema: Naam, Jee huridhiki nimuunge anaekuunga na mimkate anaekukata? Uzao akasema: kwanini, akasema: hivyo hivyo ni yako, kisha akasema Mtume (s.a.a.w) someni ikiwa munataka:

{ فَهُنْ عَسِيُّنَمْ إِنْ تَوَلَّنَمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقْطِعُوا أَرْحَامَكُمْ} (محمد: 22)

(*Basi yanatarahjiwa kutoka kwenu mukitawala ni mufanye uharibifu katika ardhi na mukate kizazi?* (Mohammad – 22). Na akasema (saaw) “Sio anaeunga ni yule inapokatika jamaa anaunganisha”. Na yote hayo yaonesha juu ya umuhimu wa kuunga. Na jamaa kuunga jamaa yaonesha upeo wa aliofaradhisha Allah katika kuunga na mapenzi katika jamii ya Kiislamu, katika kuunga Aqarib baadhi yao kwa baadhi na kushirikiana baina yao na upeo wa msaad wa sharia katika kupangilia makutano ya mwanamke kwa mwanamume na kupangilia yanaotokamana na makutano hayo katika mahusiano na mitaga yanaopatikana nayo kwa hiyo imekua sharia ya Kiislamu kuitia hukmu ambazo zimebekwa kwa upande wa kijamii katika mujtamaa ndio nidhamu bora ya kijamii kwa wanadamu.